

Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 26 Mei, 2014

(Mkutano Ulianiza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tano (15) na Kikao chetu leo ni Kikao cha Kumi na Nane (18).

Katibu tuendelee.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

NAIBU SPIKA: Hati za Kuwasilisha Mezani, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa, ahsante sana, naona Mheshimiwa Naibu Waziri akija. (Makofii)

Basi ametangulia, wakati anajipanga nimwite Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, halafu atafuata Waziri wa Mambo ya Nje. Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi?

Mheshimiwa Simbachawene?
Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Randama ya Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa 2014/2015.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

Na. 120

Mashine ya Kuteketeza Taka za Hospitalini

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC aliuliza:-

Hospitali nyingi za Wilaya na Zahanati zimekuwa zikitupa taka zitokanazo na vifaa vilivytumika na mabaki ya dawa zilizotumika kwenye madampo ya kawaida ambayo huzungukiwa na watoto na watu mbalimbali hali ambayo ni hatari sana kwa afya zao:-

Je, Serikali ipo tayari kupeleka mashine maalum ya kuteketeza taka hizo toka Hospitalini na katika Zahanati, ili kunusuru afya za wale wanaozungukia madampo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Annamarystella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu umuhimu wa kuwa na mashine za kisasa kwa ajili ya kuteketeza taka zinazozalishwa katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati kwa lengo la kunusuru afya za wananchi. Utkelezaji wa suala hili unazingatia Sera ya Afya ya Mwaka 2007 ambayo inasilitiza kulinda afya ya jamii kwa kuboresha usafi wa mazingira ulio endelevu, ikiwa ni pamoa na dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara vilivyoaribika au kuisha muda wake.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya ukosefu wa vichomea taka vyta kisasa katika baadhi ya Vituo vyta kutolea huduma za afya. Kwa mfano, katika Mkoa wa katavi kati ya Vituo 75 vilivyopo, ni 19 tu ndivyo vyenye Vichomeataka.

Kwa kuzingatia hilo Halmashauri zimekuwa zikitenga fedha katika mipango ya bajeti kila mwaka kwa ajili ya ujenzi na ununuvi wa vichomeataka kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa vichomeataka vyta kisasa, Serikali inashirikiana na Taasisi ya Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation (TEMDO) ambayo imeanza kubuni mashine za kisasa za kuteketeza taka zinazokidhi mahitaji ya kiafya na bila kuathiri mazingira. Mashine hizo zimeanza kutumika katika baadhi ya Hospitali za Mikoa ya Mbeya, Iringa na Singida. Serikali inaendelea kushirikiana na Taasisi hiyo ili kuona uwezekano wa kubuni mashine ambazo zitafaa kwa ajili ya matumizi ya Zahanati na Vituo vyta Afya kwa gharama nafuu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhimiza Mikoa na Halmashauri kuhusu kutenga bajeti kwa ajili ya upatikanaji wa vifaa hivyo, ili kunusuru afya za wananchi. Aidha, Serikali itendelea kutoa elimu kwa ajili ya jamii kuhusu hatari za watoto na watu wengine kucheza kwenye maeneo ya vichomeataka, ili kulinda afya zao.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Waziri, napenda kumuuliza swali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, pamoja na kwamba, amejibu, jibu hili ni zuri, lakini naelewa ametambua umuhimu kabisa wa swali langu na madhara yanayowakumba watoto wetu ambavyo ni vizazi vyta kesho, ni taifa la kesho.

Sasa nilikuwa napenda kusema kwamba, kuna Zahanati nyingi ambazo ni za watu binafsi ambazo zimeenea katikati ya miji mijini na zikiwa na maeneo madogo ya kufanya kazi. Pamoja na hizo Hospitali 19 ambazo labda ndio zina uhakika wa vifaa vyta kuchomea taka. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, pamoja na hizo Zahanati nyingine ambazo zimeenea mijini hovyo kila mitaa. Je, Serikali sasa ina mpango gani na mikakati gani ya kuhakikisha usalama wa watoto kwamba, hizo Zahanati zote zinakuwa na vifaa vyta kuteketeza taka hizo? (Makofii)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Annamarystella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tu-appreciate kwamba, Mbunge pia anaona kwamba, sisi tuna-appreciate kwamba, kuna tatizo hili na anachokisema hapa anasema jambo la msingi. Hakuna mahali popote katika swali lake ali-particularise akasema kwamba, nataka eneo hili.

Ninadhani kama Kiongozi wa Kitaifa alikuwa anaangalia broadly na ndio maana tulichukua Katavi kama sample tu ya kueleza na kutoa kielelezo za tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejaribu kuzungumza na watu hawa wote, tumezungumza mpaka na TEMDO, tumetaka kujua ghamama halisi; zile za Zahanati anazosema hapa zinakwenda kwenye shilingi milioni 8, hizi anazosema za Vituo vya Afya zinakwenda kwenye shilingi milioni 22 mpaka milioni 30, inapanda hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo haya ya afya hata kama ingekuwa ni bilioni bado tatizo linabaki palepale kwa sababu, kama hakuna hivi vichomeataka hivi, maana yake ni watu wetu watakufa. Sasa tunafanya nini, hizi zahanati zinazozungumzwa hapa, nimejaribu kuzungumza na Mtesiwa, huyu Daktari wa kwetu ambaye ni Naibu Katibu Mkuu; tunafanyaje katika situation hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanachofanya wanachukua hizi takataka wanazika chini, hiyo nayo bado haikubaliki. Unatakiwa uende deep, uende pale kama mita chini kama unavyotengeneza septic tank.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujibu swali hili; Sisi tutatoa maelekezo kwa maandishi kwenye Zahanati zote na Vituo vyote vya Afya, ni responsibility yao hao watu, viwe vya private, viwe vya Serikali, lazima wawe na hivi vichomeataka (Incinerators).

Hilo jambo tutalifanya Mheshimiwa kwa hiyo, hiyo ndio ahadi tunayoitoa hapa tutafwatilia kwa karibui, lakini wakati huohuo tunataka Halmashauri zetu zote zitenge katika Bajeti yake na ndio maana nimesisitiza jambo hili.

NAIBU SPIKA: Majibu ya nyongeza?

Mheshimiwa Naibu Waziri, Afya na Ustawi wa Jamii? Dkt. Kebwe Stephen Kebwe.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba niongezee katika majibu mazuri ambayo Mheshimiwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ameyatoa kutokana na swali la Mheshimiwa Marystella, Viti Maalum, Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, Wizara ya Afya kuitia Sera ya 2007, Watumishi wa Afya wote nchi nzima wamefundishwa namna ya kutupa taka na kuteketeza. Mathalani sehemu ile ambako taka zinazalishwa kunakuwa na containers za aina tofauti na rangi tofauti kulingana na aina ya taka; tukielewa kwamba, 25% ya taka ambazo zinazalishwa katika huduma ya afya zinakuwa na maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tahadhari hizi, natoa maelekezo kwa nchi nzima taratibu hizo zifuatwe kama mafundisho ambayo yametolewa.

Kwa mfano ma-container yale ya black au nyeupe ni kwa ajili ya taka ambazo hazina maambukizi. Ma-container yale ambayo ni ya rangi ya yellow ni kwa ajili ya sharps zikiwemo sindano, vipande vya chupa na kadhalika, ambavyo huwa vinatupwa kwa utaratibu maalum.

Sehemu ambayo kunakuwa na ma-containers ya rangi nyekundu ni taka zile ambazo zina maambukizi. Kwa hiyo, Mwongozo huu ambao Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeutoa nchi nzima taratibu hizo zifuatwe kupunguza athari ya maambukizi. (Makofij)

Na. 121

Visima Saba vya Maji Kijiji cha Kanondo - Sumbawanga

MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. ABIA M. NYABAKARI) aliuliza:-

(a) Je, Visima saba vya maji vilivyochimbwa katika Kijiji cha Kanondo katika Manispaa ya Sumbawanga, Rukwa, vimefikia wapi?

(b) Je, ni lini maji ya visima hivyo yatatawamywa katika Manispaa ya Sumbawanga?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA

MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, visima 7 vilivyo chimbwa katika Kijiji cha Kanondo, vimekamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 kwa gharama ya shilingi milioni 393,640,200. Kisima kimoja kilibomoka kutokana na athari za tetemeko la ardhi na jithada za kutafuta chanzo kingine zinaendelea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, visima viwili vimeanza kutumika ambapo katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 jumla ya shilingi bilioni 4.9 zimetumika kujenga mtandao mpya wa bomba wenyе urefu wa kilometa 10 kutoka kwenye visima hivyo vipyaa na kuunganisha katika mtandao wa zamani.

Aidha, ukarabati wa mtandao wa bomba wenyе urefu wa kilometa 48 na ujenzi wa tanki la ujazo wa lita 500,000 umefanyika, ili kuboresha huduma za maji katika Manispaa ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumanii kupitia Benki ya Maendeleo ya Watu wa Ujerumanii (KFW) na Jumuiya ya Ulaya inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji kwa gharama ya shilingi bilioni 30 kwa visima 4 vilivyo chimbwa kwa awamu ya kwanza; kwa sasa hali ya utekelezaji imefikia 27%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi wa miundombinu hii ya maji kwa kutumia visima vilivyo chimbwa katika Kijiji cha Kanondo inatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2015. (Makofii)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Nashukuru sana kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lini wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga, mpaka sasa yanatoka ni maji machafu, sio salama. Lini Serikali itajenga chekeche, ili wananchi wa Sumbawanga wapate maji salama na safi kwa matumizi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Miradi ya World Bank katika Wilaya ya Nkasi, yote 10 mpaka sasa iko chini ya 10%. Lini Serikali, kila mara mnakwenda kufungua miradi ya maji, lakini Nkasi naona hakuna hata mradi mmoja wa maji wa World Bank umefumnguliwa. Lini Mheshimiwa Waziri

Nakala ya Mtandao (Online Document)

unatuhakikishia miradi ya Wuilaya ya Nkasi itafunguliwa, Miradi ya World Bank ya maji kwenye Vijiji hivi vya Wilaya ya Nkasi? (Makofi)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kessy, Mbunge wa Nkasi, kaa ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa hili analosema ni *technical*, hili la chekecheke na nini. Tuliondoka hapa na Profesa Jumanne Maghembe tukaenda Sumbawanga pale na tumefanya mukutano mkubwa pale. Na nimekwenda tena mara ya pili nimekwenda na mara ya tatu na Mheshimiwa Kessy anafahamu kwamba, nimekwenda mpaka kule kwake Nkasi; kazi inayofanyika katika Mji wa Sumbawanga na Mheshimiwa Aheshi atakuwa anafahamu jambo hili, ni jambo kubwa la kutukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tume-commit pale bilioni 4.1 tumeongeza visima vingine pale 12, bilioni 1.1 tumetoka tumechukua hivi visima tunavyozungumza hapa ambavyo vimebomoka hapa tumeweka pale. Kazi kubwa inafanyika na KFW hapa tunazungumza Peoples' Bank of German ndio *ime-invest* pale; wale wanaotoka Wilaya ya Hai wanaweza wakaelewa tunazungumza kitu gani hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili analolisema la chekeche, maji yanayozungumza hapa ni maji safi na salama. Na Waziri wa Maji yuko hapa anasikia na Naibu Wziri wake anasikia hapa.

Sisi tutakwenda kuangalia hiyo chekeche ambayo anasema kwamba, chekeche pale kwamba, kuna tataizo hilo, lakini nataka niseme hapa kwamba, kazi hiyo inafanyika; Mheshimiwa Kessy ame pause hiyo, tutaiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Nkasi; Nkasi nimekwenda mimi na anafahamu. Ni kweli, ni kwamba, mpaka sasa hivi hakuna visima pale ambavyo unaona, lakini jitihada zinazofanyika katika Mji wa Nkasi ni kubwa, ukiacha mambo ya umeme na mambo mengine ambayo yanafanyika pale.

Tutawahimiza watu wa Nkasi kuitia hili swali ambalo limeulizwa hapa, ili tuone kwamba, visima vile vyote vinakamilika apatikane Mgeni Rasmi atakayekwenda kuzindua vile visima.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali dogo. Hii miradi ya World Bank ambayo iko Tanzania nzima na kwa umuhimu wa maji, maji ni uhai.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kule Karatu tuna visima 10. Kati ya hivyo 8 vina maji, lakini maji yanaendelea kukaa huko chini ya ardhi wananchi wanayatizama tu kwa hapa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje? Lini watu wataanza kutumia maji ya visima vya World Bank Karatu?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kuna visima vingi ambavyo vimechimbwa maeneo yote nchini kwa ajili ya kujua mifumo ya maji katika mabonde mbalimbali tisa (9) ambayo yako nchini, baadhi ya visima hivyo vya Bonde la Kati viko Karatu.

Katika Mpango wa Water Sector Development Programme au Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Maji na chini ya *Big Results Now*, mpango tulionao katika Bajeti inayokuja ni pamoja na kuvifunua visima hivyo, kuvivekea pump na kwa vile ambavyo vina maji, ili kuwasambazia wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Kazi hiyo itafanywa katika awamu ya pili ya Water Sector Development Programme na tunategemea kwamba, vyote vitatumika kama ilivyopangwa. (Makofisi)

Na. 122

Kitengo cha Physiotherapy Hospitali ya Wilaya ya Masasi

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED (K.n.y. MHE. MARIAM R. KASEMBE
aliuliza:-

Kitengo cha Mazoezi ya Viungo (*Physiotherapy*) ni muhimu sana kwa kutoa huduma kwa wananchi:-

Je, Serikali iko tayari kuipatia Wataalamu na vifaa vya kisasa Hospitali ya Wilaya ya Masasi, ili wananchi wenye matatizo waweze kupata huduma hiyo?

Nakala ya Mtando (Online Document)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuanzisha Kitengo cha Mazoezi ya Viungo katika Hospitali ya Wilaya ya Mkomaindo, iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa katika kuanza kutoa huduma hiyo ni kutenga jengo katika Hospitali ya Mkomaindo kwa ajili ya utoaji wa huduma hiyo na kutengwa kwa fedha za ukarabati wa jengo hilo kwa kiasi cha shilingi milioni 5 kwenye Bajeti ya mwaka 2014/2015. Aidha, Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi 9,073,178/= kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vya Kitengo hicho cha Mazoezi ya Viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Masasi imetenga nafasi moja ya ajira ya Mazoezi Viungo kwenye Bajeti ya mishahara (*Personal Emoluments*) ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo kwa sasa wanapewa rufaa ya kwenda Hospitali ya Mission ya Mtakatifu Benedict, iliyoko Ndanda na Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ya Ligula. (*Makofii*)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hapa swali la msingi linasema. Je, Serikali ipo tayari kuipatia wataalam? Kuna suala la wataalam ambalo bado Mheshimiwa Waziri hajaliongelea, japokuwa suala la upatikanaji wa vifaa pamoja na fedha tayari amelitolea ufanuzi. Naomba majibu katika hili. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hiyo kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Rajabu, kwa niaba ya kufanyakazi kwa pamoja kwa swali ambalo ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kasembe.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri mwezi wa pili nimetembelea Wilaya ya Masasi, Hospitali ya Mkomaindo tulifika. Suala hili tulikutana nalo na tunaomba watupe barua ya maombi kwa wale watumishi ambao wameweza kuwabaini wanaweza kukaa maeneo yale kwa sababu tumepeata uzoefu unapanga mtumishi anakwenda sehemu lakini anakaa muda mfupi anaondoka.

Hiyo ni sehemu ya kwanza. Lakini sehemu ya pili tunashauri kwamba walete barua kuainisha mahitaji mengine ya ziada kwa sababu ya uhalisia wa maeneo ili kusudi tuweze kupanga watumishi pale.

Kwa bahati nzuri mwaka huu kwa rekodi ya historia ya nchi yetu imepata nafasi za ajira 11,221 watumishi wa afya kwa ujumla wake wakiwemo watumishi 940 wa Kada ya Afya, 224 wa Ustawi wa Jamii na 57 katika sehemu ya Lishe. Kwa hiyo, naomba nafasi hiyo tutapanga mtumishi atakwenda kule Masasi Hospitali ya Mkomaindo, nashukuru. (Makofi)

Na. 123

Umeme Unaozalishwa Kwenye Vituo vya Kibondo na Kasulu

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Serikali imeamua kupanua mtando wa umeme kwa kupeleka umeme unaozalishwa katika Vituo vya Kibondo na Kasulu kwenda vijijiini.

(a) Je, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika miji mikuu ya Wilaya mpya za Kakonko, Buhigwe na Uvinza umefikia wapi?

(b) Je, ni vikwazo gani vinavyosababisha kusuasua kwa kuunganishiwa umeme waombaji kwenye miji ya Kibondo na Kasulu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA
KITWANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijijiini REA imeanza kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika Makao Makuu za Wilaya za Kakonko, Buhigwe na Uvinza.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Miradi hii ilianza kutekelezwa tangu mwezi Aprili mwaka huu 2014 chini ya mpango kabambe wa umeme vijiji ni awamu ya pili. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kilovoti 33 zenyе urefu wa kilimota 172.7. Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 zenyе urefu wa kilomita 170, ufungaji wa *transfoma* ishirini na tatu na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 4,594 miradi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015 kwa gharama ya shilingi bilioni 12.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikwazo vinavyosababisha kasi ndogo ya kuunganisha umeme wateja kwenye miji ya Kasulu na Kibondo ni kutokana na kuchelewa kuwasili kwa vifaa vya ujenzi hasa baada ya mkandarasi kuongezewa kazi za ziada. Hata hivyo hivi sasa vifaa vimeshaanza kuwasili na zoezi linaendelea vizuri. (Makofji)

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Wilaya ya Kasulu Serikali kupitia mradi wa umeme vijiji REA iliahidi kupeleka umeme katika vijiji kumi lakini mpaka sasa ninavyozungumza hakuna dalili zozote zinazoonyesha utekelezaji wa mradi huo. Nataka kumwuliza Waziri ni lini sasa vijiji hivyo vilivytajwa vitapatiwa umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili Wilaya ya Kasulu na Wilaya ya Kibondo kwa muda mrefu sana ilikaa bila umeme lakini kwa kupitia sera nzuri ya Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Kasulu na Kibondo ina umeme mwangi wa kutosha lakini wananchi wamekuwa kwa muda mrefu wakiomba kuunganishiwa umeme bila mafaniko yoyote.

TANESCO ikitoa majibu ya kwamba hakuna nguzo wala nyaya za kuunganishiwa umeme. Leo ni mara ya pili nikisimama hapa Bungeni kuuliza ni kwa nini wananchi hawa hawaunganishiwi umeme.

Sasa nataka Waziri aniambie ni lini Serikali itasimamia kuunganishiwa umeme wananchi kuwaondolea matatizo waliyonayo kila siku kuomba kuunganishiwa umeme bila mafanikio yoyote? Nimwombe Waziri afike katika eneo hilo aje kujridhisha mwenyewe.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephine kama ifuatavyo.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia suala hili la umeme katika maeneo hayo. Sasa nimhakikishie tu kwamba vile vijiji kumi viko katika njia ya umeme utakaopelekwa katika miji hii ya Makao makuu ya Wilaya kama nilivyoeleza. Kwa hiyo, mpango huu huu ambao umeshaanza mwezi Aprili vile vile utavihuisha vijiji hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kama nilivyojibu katika swali la msingi sehemu (b) ilikuwa ni matatizo ya kutokuwa na vifaa lakini nimhakikishie tu kwamba sasa hivi vifaa vimefika na tayari wananchi tumeshawaelekeza TANESCO waanze kuwaunganishga wananchi haraka iwezekanavyo. Basi nikubali tu kwamba nitafika huko kujihakikishia mwenyewe, kuhakikisha kwamba ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa. (Makof)

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme ni muhimu sana hasa katika kuondoa umaskini katika vijiji vyetu. Katika Jimbo la Singida Kaskazini, kijiji cha Ipanoda wananchi waliwekewa nguzo yapata miaka zaidi ya sita sasa na hapa ninapozungumza nguzo nyingine zimeshaanguka na kuonza jambo ambalo inaleta pia uharibifu wa maliasili ya Taifa na uharibifu wa rasilimali.

Je, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, anawaambia nini wananchi wale wa jimbo la Singida Kaskazini kuhusu kwenda kuangalia upya zoezi lile la kuweka nguzo nyingine na kuweka nyaya ambapo hilo zoezi halijafanyika zaidi ya miaka sita sasa? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba nijibu swali la Mheshimiwa Christowaja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata hiyo taarifa sasa hivi nitaongea na watendaji wa TANESCO kuhakikisha kwamba matatizo hayo ambayo umeyasema tunayarekebisha haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kuunganishiwa umeme na kuiunga mkono CCM. (Makof)

Na. 124

Fidia kwa Wananchi wa Kata ya Malolo

MHE. ABDULSALAAM S. AMER aliuliza:-

Nakala ya Mtando (Online Document)

Je, ni lini wananchi wa Kata ya Malolo watalipwa fidia ya mazao yao yali oathirika na kupasuka kwa bomba la mafuta la Kampuni ya TAZAMA Pipeline na kupatiwa wananchi hao maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES K. MUHANGWA)
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulsalaam S. Amer, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4 Juni, 2011 bomba la kusarifisha mafuta TAZAMA Pipeline lilipasuka na kusababisha uvujaji wa mafuta ghafi katika kijiji cha Malolo Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro na kusababisha adhari kwa mazao ya wanakijiji, vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla. Mara baada ya tatizo hilo kutokea hatua mbalimbali ikiwemo kushughulikia suala la ulipaji fidia zilichukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia ulipaji wa fidia Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa iliomba TAZAMA Pipeline kuilipa shilingi milioni 5,387,000 kama gharama za tathmini ya fidia ya mazao na utafiti wa mali TAZAMA ilitekeleza ombi hilo mwezi August, 2012 na kazi ya tathimini ilifanyika zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao mazao yao yaliathirika litafanyika baada ya wakazi wa Malolo kukubali offer ya malipo ya shilingi milioni 50 iliyotengwa na TAZAMA kufuatia tathmini hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maji safi na salama kwa wananchi wa Kata ya Malolo TAZAMA ilikubali kuchangia gharama za mradi kama zilivyoombwa. Zoezi hili litaanza rasmi pindi utekelezaji wa mradi huu utakapoanzishwa unaotarajiwu kuanzwa na kusimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na wananchi wa Malolo utakapoanza. (Makofi)

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Malolo wiki ijayo wanatimiza mwaka wa nne hawajalipwa fidia yao nao wananchi wamekubali kupokea hiyo milioni hamsini kama fidia angalau ni chache lakini wameridhika kupokea hiyo fidia.

Je, ni lini watapokea hiyo fidia?

Mhehimiwa Naibu Spika, swali la pili pamoja na kuletewa maji safi na salama ahadi waliyotoa mbele ya Naibu Waziri wakati ule Mheshimiwa Adam

Nakala ya Mtando (Online Document)

Malima na tathmini imeshaenda kwenye ofisi yao Makao Makuu, Dar es Salaam, ni lini wataanza mradi huo wa maji kwa vijiji vya Kata ya Malolo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na madini napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amer, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nafurahi kwamba wananchi sasa wamekubali na nikupongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo umekuwa ukilifuatilia suala hili. Kwa hiyo, kwa sababu wamekubali basi tutawaelekeza wananchi wa kijiji hiki wawasiliane na Halmashauri ya Kilosa ili waweze kutuandikia na TAZAMA Pipeline itatoa hizo hela mara moja.

Mheshimiwa naibu Spika, kuhusu suala la pili kama nilivyojibu katika swali la msingi TAZAMA wamekubali kuhakikisha kwamba wanachangia hizo hela katika huu mradi wa maji. Kwa hiyo, niwaombe tu Mkurugenzi wa Kilosa pamoja na wewe Mheshimiwa Mbunge muweze kufuatilia kuweza kuandikiwa hiyo cheque kama mlivyokuwa mmeomba. (Makofii)

Na. 125

Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria

MHE. SHAFFIN A. SUMAR aliuliza:-

Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Tabora Mjini hadi Urambo uko katika hatua ya upembuzi yakinifu.

(a) Je, ni vijiji vingapi katika Jimbo la Tabora Kaskazini vitapitiwa na mradi huo?

(b) Ahadi ya kuwepo mradi huo iko katika Ilani ya Uchaguzi ya 2010 na sasa tumebakisha mwaka mmoja tu kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu mwingine.

Je, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Tabora. Mjini ukiwa ni utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2010. Mradi huu utahusisha Miji ya Tabora, Nzega, Igunga pamoja na vijiji vyote ambavyo vitakuwa umbali usiozidi kilomita kumi na mbili kila upande wa bomba kuu. Utekelezaji ulianza katika mwaka 2012 wa Kampuni ya serikali ya India WAPCOS kufanya na kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi huo mwaka 2013. Aidha WAPCOS walitumia kazi hiyo kuandaa makisio ya awali ya gharama za mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 Aprili, 2014 Serikali ilisaini mkataba na Mhandisi mshauri Mateferia Engineering ya Ethiopia akishirikiana na G-PES na Don Consult wa Tanzania. Mtaalam mshauri huyo atapitia upembuzi yakinifu uliofanywa awali pamoja na kufanya usanifu wa kina, kuandaa vitabu vyatumbu na kutathmini athari za kimazingira na kijamii. Kazi hiyo itachukua miezi kumi na mbili hadi kukamilika kwa gharama za dola za kimarekani 838,525.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kazi zilizofanywa na WAPCOS Serikali inatafuta fedha ili kujenga mradi huo mara baada ya usanifu wa kina kukamilika. Aidha baada ya kukamilisha kazi za usanifu wa kina tutajua kwa uhakika kuwa bomba kuu litapita wapi toka Shinyanga hadi Tabora hivyo kuweza kuvitambua vijiji vilivyo kilomita kumi na mbili kila upande wa bomba kuu litakalojengwa kwenda tabora kupitia Wilaya ya Kahama, Bukene, Nzega, Igunga, Uyui na Tabora. (Makofu)

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa katika swali la msingi nilitaka kujua vijiji ambavyo vitapitiwa na mradi huu katika jimbo langu la tabora Kaskazini swali ambalo sijapatiwa majibu yake.

Lakini pia naomba nifahamu kwamba kila mara tumekuwa tukizungumzia feasibility study lakini naomba Naibu Waziri atueleze kwamba ni kiasi gani cha fedha kimetengwa katika Bajeti ya mwaka huu tunaoutarajia kuuanza ili tujue kwamba hiyo kazi sasa kweli itatekelezeka kwa sababu ni pamoja na hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sumar Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kujua ni vijiji vingapi na hasa katika jimbo lake ambavyo vitaweza kupata maji. Nimeeleza katika maelezo ya msingi kwamba huyu msanifu ndiyo atakayebaini sasa baada ya kusanifu maana yake bomba litapita wapi na vijiji ambavyo kutoka umbali wa kilomita kumi na mbili kila upande atavibaini yeze baada ya kufanya usanifu na hapo ndiyo tutakuwa katika nafasi ya kuweza kuelewa Igunga ni vijiji vingapi, Nzega vijiji vingapi na hata katika jimbo lake na pale Tabora mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Bajeti ni kwamba hii ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi na lazima tuitekeleze. Kwa hiyo, kwa mwaka huu kwa fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni moja zitatumika kwa ajili ya usanifu huo. (Makofij)

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nilitaka nimwulize Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza mwaka jana wakati swali hili hili linajibiwa Naibu Waziri aliyejewepo wakati ule alitaja vijiji vilivyo ndani ya jimbo la Bukene, Nzega na Igunga na ndani ya Jimbo la Tabora Kaskazini mpaka Tabora ambavyo vitapitiwa na bomba hili na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tathmini ya kwanza imeshafanyika na kubaini gharama za awali.

Kwa hiyo, kwa maana hiyo ni kwamba *at least* vijiji na miji mikubwa ambayo bomba hili litapita vimeshajulikana. Sasa nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufanya ziara kwenye miji hii?

Kwa mfano Nzega, Igunga, Bukene ili kuwaeleza wananchi mpango ulivyo angalau wananchi wetu wajenge matumaini kwamba ahadi hii kweli itatekelezeka?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zedi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu apokee maelezo haya ndiyo rasmi ya Serikali kwamba usanifu utafanyika na tutabaini vijiji vitakavyopitiwa. Hilo suala la kufika Bukene na maeneo mengine niko tayari na juzi nilikuwa Nzega. Kwa hiyo, nitafika na maeneo mengine kutoa elimu hii juu ya mradi huu. (Makofij)

Na. 126

Ruzuku kwa Wafanyakazi wa Hospitali ya Kolandoto

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT aliuliza:-

Serikali ilishapandisha hadhi hospitali ya Kolandoto Manispaa ya Shinyanga kuwa Hospitali Teule lakini hakuna rukuzu, dawa na wafanyakazi kutolipwa mishahara yao:-

(a) Je, ni kiasi gani cha ruzuku kinatakiwa kulipwa kwa mwezi katika hospitali hiyo na fedha kiasi gani kimeshalipwa?

(b) Je, kwa nini fedha za kununulia dawa hazifiki pamoja na kuwa fedha hizo zilitengwa mwaka jana?

(c) Je, ni lini wafanyakazi hao watalipwa malimbikizo yao yote ya mishahara ambayo hawajalipwa kwa muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ruhusa yako naomba nianze kwa kutoa pole kwa Ndugu zangu wa Jimbo la Serengeti kwa mashambulizi ya kundi kubwa la tembo ambalo viko katika vijiji jirani na hifadhi, ikiwemo kuua Ndugu mmoja wiki iliyopita ambaye ni mdogo wake na diwani, Chacha Wangwe wa Kata ya Nyamoko, naomba wawe wastahimilivu, wavumilivu katika kipindi hiki ambacho Serengeti inashughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rahel Mashishanga Robert, Viti Maalum, kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Julai, 2012 hospitali ya Kulandoto ilipandisha hadhi kuwa hospitali teule ya Manispaa ya Shinyanga, ikiwa ni utekelezaji wa sera ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma wa afya nchini. Ruzuku ya uendeshaji wa hospitali ya Kolandoto, hulipwa kila mwezi kulingana na mgao unaopatikana kutoka Hazina.

Julai, 2012 zililipwa shilingi 1,900,000/= Agosti, 2012 zililipwa shilingi 2,500,000/= na Septemba shilingi 2,500,000/. Aidha, Julai, 2013 zililipwa shilingi 3,418,763/=, Agosti 2013 zimelipwa shilingi zipatazo milioni 3,418,763 na Septemba 2013 zimelipwa shilingi milioni 3,418,763.

Pia Februari, 2014 zililipwa shilingi 3,418,763 na Machi, 2014 shilingi 904,774/. Kiasi kinacholipwa kwa mwezi hutegemea kiasi kinachopokelewa kutoka Hazina kwa mwezi unaohusika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa fedha ya kununua dawa vifaa tiba na vitendanishi zimetengwa katika mfuko wa pamoja sekta ya afya yaani *Health*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Basket Fund. Mwaka 2012/2013 asilimia 30 ya mgao wa manispaa ya Shinyanga sawa shilingi milioni 90 zililipwa na mwaka 2013/2014 kufikia Desemba, 2013 zimelipwa shilingi milioni 45. Fedha za kipindi cha Januari hadi Juni, 2014 zimeingia kwenye akaunti ya Halmashauri takriban malipo yote yanaandiliwa yaweze kwenda katika hospitali hii. Aidha, Wizara imetoa mwongozo utakaozingatiwa ili hospitali iingie kwenye orodha ya vituo vinavyopata dawa kutoka bohari ya dawa ya MSD.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya malimbikizo ya mshahara kipindi cha 2008 hadi 2012 yalihakikiwa kwa hospitali zote za Mashirika ya Dini ikiwemo Kolandoto. Uhakiki ulihusisha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Utumishi pamoja na Hazina. Taarifa ya uhakiki ilionyesha kuhitajika uthibitisho wa ziada wa madai hayo kutokana na kuwepo kwa upungufu kadhaa.

Madai wa shilingi zipatazo milioni 25,717,846/= ziliainishwa, Wizara ya Fedha itaanza kulipa madeni ya Serikali ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya mshahara wa watumishi wa Kolandoto kwa awamu kulinga na upatikanaji wa fedha. (Makofii)

MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nilikuwa nataka kujua Serikali ni lini sasa itaisaidia hospitali kuingia katika orodha ya vituo ambavyo vitapata dawa kupitia moja kwa moja MSD kwa sababu ni muda mrefu saa hizi wamekuwa wakihangaika kuingiza kwenye kuingiza kwenye orodha.

Swali la pili, toka hospitali hii imekuwa CDH ilikuwa na wafanyakazi 180 lakini mpaka sasa ni wafanyakazi 61 ndiyo walio kwenye pay roll nini hatma ya hawa wafanyakazi 119?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Dkt. Kebwe Stephen Kebwe.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rachel Viti Maalum, Shinyanga kwa ufuatiliaji wa karibu sana wa suala hili la hospitali teule ya pale Kolandoto. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, sehemu ya kwanza ya swali lake ni lini kwamba hospitali itaingizwa katika mgao wa dawa.

Kwa utaratibu naomba kutoa maelezo na nchi nzima naomba utaratibu huo ufuatwe pale ambapo hospitali husika imeingia mkataba na Halmashauri husika inapaswa kusaini mkataba kulingana na mwongozo wa mkataba wa ule

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kipengele namba tano hospitali hizi teule zitaendeshwa kama ilivyo hospitali ya Serikali.

Kwa hiyo, naomba ombi hilo lije likainisha vizuri wamesaini lini mkataba na halmashauri na hospitali ili kusudi waweze kupatiwa mgao wa dawa kulingana na idadi ya wagonjwa wale ambao wanaohudumiwa waweze kupangiwa dawa kutokea MSD kama mwongozo ulivyo.

Sehemu ya (b) wafanyakazi hawa 180 ambao wako katika orodha ni 61 ambao wako katika mgao wa kupata mishahara. Naomba kwa maelekezo hayo ya swalî lake la kwanza na jibu la nyongeza sehemu (a) naomba orodha hiyo ije ipitiwe vizuri iweze kuhakikiwa na utumishi, pamoja na Hazina kuitia liaison waweze kupata stahili zao kwa sababu kama nilivyosema kipengele kile cha tano cha mkataba kinaainisha vizuri hospitali hizi zitafanya kazi kama ilivyo hospitali ya Serikali.

MHE. SELEMAN MASOUD NCHAMBI SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Sika, nakushukuru sana kwa kuwa mkoa wa Shinyanga unatekeleza mpango kabambe wa ujenzi wa hospitali ya rufaa, itakayogharimu takriban bilioni 86 mpaka 100 katika kipindi hiki na na kwa kuwa Serikali inatutengea shilingi bilioni 1 kila mwaka katika Bajeti. Kwa hiyo, ni dhahiri hospitali hiyo ya rufaa ya Mkoa wa Shinyanga itachukua miaka 86 mpaka kukamilika.

Je, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Serikali sikuvi ya Chama cha Mapinduzi kwanini isiangalie uwezakano wa kuongea na taasisi kama PSPF, NSSF na mashirika mengine ili wananchi milioni 2 wa Mkoa wa Shinyanga waweze kuipata huduma hii ndani ya miaka mitatu mpaka mitano? Waweja sana.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumpongeza sana kufuatilia suala hili la kuimarisha huduma ya afya katika mkoa wa Shinyanga ni kati ya mikoa ambayo imedhamiria kwa dhati kujenga kulingana na sera ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hospitali za rufaa za mkoa nawapongeza sana kwa hili.

Lakini kama ushauri unavyotolewa na pia kufuatilia maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu *government guarantee* ni jambo ambalo litatazamwa upya ni kweli kwa bilioni moja ambayo inatolewa kulingana na ukomo wa bajeti. Bajeti hiyo ya shilingi zipatazo shilingi 86 mpaka bilioni 100 ni kazi ambayo ni kubwa.

Kwa hiyo, kuitia mazungumzo na juhudzi za Serikali pamoja na mkoa tunajua wanafanya kazi kubwa sana ni vizuri kushirikisha wadau mbalimbali ikiwemo mchango wa Serikali suala hili la hopitali ya rufaa ya mkoa kama ilivyo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

sera ya nchi iweze kujengwa. Wafuate mfano kama ilivyokuwa hospitali ya Singida ya rufaa ya mkoa, hospitali ya Mkoa wa Manyara ya rufaa ya mkoa, mkoa wa Pwani pamoja na Mkoa wa Mara kwa juhudii kubwa ambazo zimeanza.

MHE. MAGRETH AGNES MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kufanya marekebisho kidogo hii sheria ilipitishwa mwaka 2010, baada ya marekebisho hayo naomba swali namba 127 lijibiwe.

Na. 127

Kuundwa kwa Baraza la Ushauri wa Huduma kwa Watu wenyewe Ulemavu

MHE. MARGARETH AGNES MKANGA aliuliza:-

Sheria ya watu wenyewe ulemavu ilikwishatungwa Aprili, 2004.

Je, ni kwanini Baraza la Watu wenyewe ulemavu halijaundwa mpaka leo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magreth Agness Mkanga, Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Julai, 2004 Serikali ilitunga sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa watu wenyewe ulemavu kwa lengo la kuchochea maendeleo kwa watu wenyewe ulemavu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendana na mahitaji yaliyo katika mkataba wa kimataifa kwa haki za Watu wenyewe ulemavu ambao Tanzania ili saini tarehe 30 Machi, 2007 na kuridhia mnamo tarehe 10 Novemba, 2009.

Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria Namba 9 ya Mwaka 2010 ya watu wenyewe ulemavu. Aidha, mnamo tarehe 3 Februari, 2014 Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Dkt. Edward Tikamanyile Bagandanshwa Mlemavu asiyeona ambaye pia ni mhadhiri katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Utoaji wa Huduma kwa watu wenyewe ulemavu hapa nchini. Kwa kuzingatia sheria hiyo, uteuzi huu ni miaka mitatu yaani kuanzia tarehe 3 Februari, 2014 hadi tarehe 2 Februari, 2017.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Aidha, wajumbe wengine wa Baraza hilo ambao uteuzi wao uko ndani ya mamlaka ya Wizara ya Afya na Ustawi na Jamii pia wamekwisha teuliwa uzinduzi wa Baraza hili utafanyika baada ya maandalizi kukamilika.

MHE. MARGARETH AGNES MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi tunashukuru kwamba mambo yanaendelea lakini napenda kufahamu kwa kuzingatia kwamba watu wenyewe ulemavu bado wana matatizo na changamoto nyingi angalau katika kupata huduma mbalimbali zinazowahu.

Je, uzinduzi huu utakamilika lini kwa sababu katika kuendelea kuchelewesha ndivyo hivyo ambavyo Serikali itaendelea kuchelewesha kutoa huduma kwa watu hawa kama sheria inavyotaka?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, mazungumzo ambayo tumefanya jana Mwenyekiti mteule Dkt. Tikamanyile Bagandanshwa, tulikubaliana kwa ruhusa yake ipatapo wiki ya pili ya mwezi wa saba bada ya Bunge hili la Bajeti tutafanya uzinduzi huo kulingana na nafasi na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pale ambapo kazi itakuwa imekamilika.

Ni matarajio kwamba Baraza hili likamilike mapema kwa sababu ni daraja zuri kuwakilisha hawa wenyewe ulemavu ambao kwa idadi ya Watanzania ni takriban asilimia 13. Baraza hili ni muhimu sana. (Makofisi)

Na. 128

Ujenzi wa Barabara ya Lami Toka Njombe Ludewa Mjini

MHE. RITA E. KABATI (K.n.y. MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE) aliuliza:-

Tatizo la miundombinu ya barabara limedumu katika nchi tangu tupate uhuru hadi sasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara kutoka Njombe hadi Ludewa Mjini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi kuptitia Wakala wa Barabara TANROADS imeanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni hatua muhimu ya maandalizi ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Kampuni ya Crown Tech Consult ndiyo iliyopewa kazi hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanda makabrasha ya zabuni kwa barabara yote kutoka Itoni – Ludewa hadi Manda kilomita 211.4.

Wakati kazi hii ya usanifu ikiendelea, Serikali kwa upande wake inaendelea kutafuta fedha za kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa sasa Serikali katika Bajeti ya 2013/2014 inaendelea na ujenzi wa kilomita 6.7 za barabara kwa kiwango katika eneo la mji wa Ludewa kwa gharama ya shilingi milioni 3,779.25.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inafanya maandalizi ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe katika barabara za Itoni hadi Ludewa Mkomang'ombe kilomita 168.5, Mchuchuma Access kilomta 7.0 na Mkiu – Liganga kilometra 46.0 ili kurahisisha usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo ikiwa ni pamoja na usafirishaji wa mitambo mikubwa kwenda kwenye machimbo ya makaa ya mawe na chuma Mchuchuma na Liganga. Zaidi ya shilingi bilioni 8 zimetengwa kwa kazi hii na makandarasi wamepatikana.

MHE. RITA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya Mheshimiwa Deo Filikunjombe. Kwa kuwa mwekezaji wa mradi wa makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Liganga ameshapatikana.

Je, Serikali haioni kuchelewesha kwa ujenzi wa barabara ni kuchelewesha kwa mradi huu ambao ni muhimu sana kwa nchi yetu?

Katika jibu lake Mheshimiwa hajaweka *time frame* ya kuanza mradi huu. Kwa faida ya wananchi wa Ludewa ni vizuri angeweka wazi kwamba mradi huu sasa utaanza lini na utaisha lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rita Kabati, pamoja na Mheshimiwa Filikunjombe kwa namna wanavyosukuma ujenzi wa barabara hii. Serikali inatambua kabisa umuhimu wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

barabara hii na ndiyo maana nimesema hizo ni hatua za awali tunaanza kwanza na upembuzi yakinifu na kazi hiyo imeshaanza.

Lakini kwenye hotuba yangu ya bajeti nimesema kwamba zile kilomita 50 za mwanzo katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kuanza kujenga barabara ile ni ikiwa pamoja na barabara nyingine ya Njombe – Makete, pamoja na Njombe Lupembe.

Katika swali lake la pili, kuhusu *time frame*, maana fedha tumezipanga kwenye Bajeti kwa hiyo ile *phase* ya kwanza ya kilomita 50, mkandarasi atakapoleta zile *details* za usanifu basi tutaanza kipande hicho cha barabara kuweza kuanza kujenga. (Makofii)

MHE. APHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa fursa kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuelekeza nguvu kwenye barabara ya Itoni – Manda. Lakini nilitaka kuiuliza Serikali kwamba sijui kama wanazo taarifa kwamba ile barabara ya Itoni Manda ambayo ni kilomita 140.

Kutoka Itoni kwenda Ludewa kilomita 140, tulitoka Njombe tukiwa na mwili wa marehemu Filikunjombé saa tatu usiku Njombe, tukaingia Ludewa kesho yake saa nne asubuhi na tukiwa tunashuka kwenye magari tunakuma magari yanaacha njia, sasa nilitaka kujua tu kama Serikali inajua kwamba hii barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiililia mara kwa mara ina kero za namna hii kwa wananchi wa Ludewa. Je Serikali ina taarifa hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, taarifa hiyo mnayo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hiyo tuna taarifa nayo kwamba ni mbaya na ndiyo maana Serikali imechukua hatua. Hatua ya kwanza kwamba tumetoa bilioni nane kwanza tuitengeneze barabara hii kwa kiwango cha Changarawe tunapanua kona zote zile.

Kwa hiyo, adha hii ambayo umeipata Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Deo Filikunjomba, nategemea haitatokea, lakini kwa sababu tutaijenga kwa kiwango cha lami basi tutakuwa tumetatua hili kwa kudumu. (Makofii)

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza ningependa kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayofanya katika jimbo langu la Kalenga. Lakini ningependa tu kufahamu ni kwa kiwango gani au ni kwa uharaka wa namna gani Serikali inaliangalia tatizo

Nakala ya Mtando (Online Document)

la barabara inayoanza Ifunda kuelekea Kiponzelo barabara hii itaisha lini na itaanza lini katika kiwango cha lami? Ahsanteni sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Swali nzuri sana kama alikuwepo miaka yote.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikupongeze kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na pili kwamba unatambua barabara hizi ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi. Suala ya barabara hii ya Ifunda Kiponzelo ni barabara ya mkoa tutaiangalia katika mipango ya Serikali ya baadaye kuona tuweze kuangalia kujengwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Na. 129

Athari za Mabadiliko ya Kisiasa ya Nchini Misri

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (K.n.y. MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU) aliuliza:-

Mabadiliko makubwa ya Kisiasa yametokea nchini Misri hivi karibuni:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani mabadiliko hayo yataathiri Tanzania katika makubaliano ya matumizi ya rasilimali za Maji ya Mto Nile?

(b) Je, ni sekta zipo za kibiashara zitakazoathirika na hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi ya Misri imekubwa na mabadiliko makubwa ya uongozi tangu kuvuka kwa vuguvugu la kisiasa katika nchi za kiarabu mwaka 2011.

Aidha, leo tarehe 26 na kesho tarehe 27 Mei, 2014 wananchi wa nchi hiyo wapo katika zoezi la kupiga kura kumchagua Rais wa Nchi hiyo. Mabadiliko ya uongozi nchini Misri hayatarajiwi kuathiri Tanzania katika makubaliano ya matumizi ya rasilimali ya maji ya Mto Nile.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kubadilika kwa uongozi, Misri imeendelea kuwa na msimamo ule ule unaotetea Mkataba wa Kikoloni wa mwaka 1929 unaoipa Nchi hiyo haki ya kipekee ya kutumia maji ya Mto Nile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba, Nchi za Bonde la Mto Nile ambazo ni Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda, Ethiopia, Burundi, Congo DRC, Misri na Sudan zilijadili namna bora ya matumizi ya Mto Nile katika hali ya usawa. Majadiliano hayo yalihitimishwa kwa kutiwa saini mkataba ujulikanao kama *Comprehensive Framework Agreement on the Nile Basin* wa mwaka 2010. Nchi zote za Bonde la Mto Nile isipokuwa Misri na Sudan zilitia saini Mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania, Mchakato wa kuridhia mkataba huo bado haujakamilika. Nchi yetu kwa kuzingati amazingira ya nchi ya Misri ambayo yanajumla ya watu milioni 78 wanategemea chanzo kimoja tu, yaani maji ya Mto Nile nchi ambayo ni jangwa na kwa sehumu kubwa haipati mvua na nchi ambayo inategemea kilimo cha umwagiliaji maji tu, tunadhani ni vyema tukajiuliza tena iwapo ni sahihi kuwa na mkataba unaoziruhusu nchi zote tisa za Bonde la Mto Nile tunasisitiza kutumia maji ya mto huo kwa usawa. Tunadhani pia kuwa nchi kama Misri ambayo ina mto mmoja tu na ndiyo chanzo cha uhai wao itakuwa na haki ya upendeleo wa kutumia maji mengi kuliko sisi wa nchi zingine ambao tuna vyanzo vingine vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mkataba huo uanze kufanya kazi nchi sita zinahitajika kuridhia. Ni matarijo yetu kwamba nchi zote zilizosaini mkataba huo zitakutana tena ikiwemo pia Misri baada ya kutengemaa ili kuangalia uwezekano wa kutoa upendeleo rasmi na wa kipekee kwa Misri badala ya kupitisha Sheria ya usawa kwa matumizi ya Maji kwa nchi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya Uongozi Nchini Misri hayaathiri Tanzania katika makubaliano ya matumizi ya rasimali za maji ya Mto Nile.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa mabadiliko ya Uongozi Nchini Misri hayaataathiri Tanzania katika msimamo wake kuhusu matumizi ya maji ya Mto Nile ni dhahiri kwamba mabadiliko hayo pia hayatkuwa na athari katika sekta yoyote nchini mwetu.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Tanzania ilitia saini Mkataba wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

Nile Basin Comprehensive Framework Agreement ya mwaka 2010 na kwa kuwa bado haujaletwa Bungeni kuridhiwa. Ni lini utaletwa Bungeni kuridhiwa?

Pili, ni sababu zipi zilizopelekea Misri na Sudan kutotia saini?

NAIBU SPIKA: Ni sababu zipi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Lini Mkataba huo utaletwa Bungeni kuridhiwa? Tumesema kwamba hatua kwanza hazijakamilika, lakini pia kwa kuzingatia uhalisi na ukweli kwamba Misri wao Mto Nile ni Uhuru wao, tumeona kipengele ambacho kinasema kwamba nchi zote ziwe na fursa sawa ya kutumia Mto Nile kinahitaji kuzingatiwa upya.

Kwa hiyo, Tanzania tunatarajia kuandaa Mkutano Mkubwa wa kuzikutanisha nchi zote ambazo ni chanzo cha mto Nile, nchi tisa au kumi kuweza kuzingatia tena Juu ya Mkataba huo.

(b) Kwa nini Misri na Sudan hawakutia saini Mkataba huo ni kwa sababu Mkataba wa Kikoloni wa mwaka 1929 ambao uliingiwa na Uingereza kwa niaba ya Kenya, Uganda na Tanganyika kwa wakati ule na upande mwingine kwa Misri ulikuwa unapendelea sana Misri. Hata hivyo, baadaye mwaka 1959 Misri waliingia Mkataba mwingine na Sudan ambao unawapendelea wao wenywewe.

Kwa hiyo, ni dhahiri mabadiliko yoyote yataathiri zile fursa za kipekee ambazo wanazo chini ya mikataba hiyo na kwa hiyo, ndiyo maana hawakutaka kuingia tena katika Mkataba ambao umejadiliwa hivi karibuni.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mchungaji Peter S. Msingwa na Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya atakuwa wa Mwisho!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani kwenye Maliasili tulizungumza jinsi ambavyo Wizara ya Mambo ya Nchi za nje hayajafanya ushirikiano mzuri pamoja na Maliasili kuweka Mabalozi wawakilishi ambao wanaitangaza nchi yetu katika sekta hii kupanua.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Pamoja na kwamba Waziri amesema kwamba Tanzania hajjathirika kutokana na mabadiliko hayo. Hata hivyo, bado Misri ni moja ya nchi shindani wa utalii katika Bara la Afrika.

Je, wizara hii ina mipango gani na mikakati gani kuhakikisha inatumia advantage hiyo kuitangaza Tanzania ili tuweze kunufaika na utalii kuzidi nchi ambazo zinatushinda kama Kenya, Afrika Kusini pamoja na Egypt.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge swali la nyongeza ni lazima lihusiane na suala la msingi. Suala hili halihusiani kabisa na suala la msingi. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Kama majibu yake unayo unaweza ukajibu tu! Mheshimiwa Waziri Mwenyewe wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. (Makofii)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Majibu mazuri sana ya Naibu Waziri wangu, katika suala la faida kwa upande wa Utalii, Wizara iliusika kikamirifu katika kuhakikisha kwamba Egypt Air inafanya shughuli zake pamoja na matatizo yote kati ya Cairo na Dar es Salaam na sasa tuna ndege mbili za Egypt Air na kwa sababu kuna wakazi milioni 78 wanaopenda sana Utalii katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kwa mujibu wa taarifa tuliyopewa na Egypt Air waliletwa Watalii 13,000 katika kipindi cha mwaka 2012/2013. Kwa hiyo, sekta ya usafiri ambayo inahusika sana na kuleta utalii nyumbani bado haijaathirika pamoja na matatizo yanayojitokeza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe nakushukuru sana. Swali la mwisho kwa leo Mheshimiwa Sanya!

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Je, huu mkataba wa mwaka 1929, ulitoa haki gani kwa nchi ya Misri na nchi zote za Bonde la Mto Nile na kwa nini Sheria hii haibadilishwi?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu kama ifuatavyo:-

Moja ni kwamba, Mkataba wa mwaka 1929 pamoja na mambo mengine una mambo makubwa manne. Kwanza ulitoa asilimia 55 za matumizi ya Mto Nile kwa Misri, pili ulitoa asilimia 15 kwa maji yote ya Nile kwa Sudan, tatu ulitoa veto power yaani nguvu kwa Egypt kuweza kuyasimamia maji yale na kutokurusu mtu mwingine yoyote kuyatumia, iwe kwa kunywa, kwa umwagiliaji na kwa ujenzi wa mabwawa, nne asilimia 30 maana ukijumlisha 55 na 15 ni

Nakala ya Mtando (Online Document)

sabini, asilimi 30 zilitengwa kwa ajili ya kitu kinaitwa evaporation. Kwa maneno mengine hakuna nchi mbali ya Egypt na Sudan kati ya zile nchi zinazozunguka Bonde la Nile zilizoruhusiwa kuyatumiwa maji yale.

Kilichotokea mwaka 2009/2010 kukawa na hicho kitu kinaitwa Entebbe Agreement. Kwenye makubaliano ya Entebbe sasa ndiyo hizi nchi tisa (9) zikakubali kutiliana mkataba wa kusema kwamba, maji ya Mto Nile yatumiwe sawa na nchi zote tisa za Bonde la yale maji.

Sasa kwa maana gani? Kwa maana ya kwamba ukitaka kujenga mabwawa jenga, ukitaka kufanya *irrigation* umwagiliaji fanya hivyo, ukitaka kuyanywa fanya hivyo. Ndiyo maana Tanzania tukasema lazima tuwe sensitive na matatizo ya Egypt kwa sababu kuna mto mmoja tu katika nchi ile, hawapati mvua ya kutosha, hakuna maji chini yake, kwao Nile ni Uhai.

Kwa hiyo, tukiamua nchi zote tisa (9) kujenga Dam za umeme, nchi zote tisa zikiamua kumwagilia maji ya ule Mto, Nchi zote zikiamua kutumia maji inavyotaka, tutauwa watu wa Egypt. Ndiyo maana Serikali ya Tanzania tutaitisha kikao kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, ili nchi zote tisa zikutane tu-review na tutakutana Foreign Affairs Ministers na Waziri wa Maji ili pamoja na matumizi ya kunywa maji yetu, tuwe kidogo sensitive kwa wenzetu ambaao Uhai ni Mto Nile. (Makof)

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, matangazo kwanza halafu mengine yatafuata.

Naomba nitambue wageni waliopo katika Ukumbi wetu asubuhi hii ambaao ni wanafunzi 91 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wanafunzi kutoka UDOM pale mlipo simameni, hongereni sana na karibuni sana katika ukumbi wa Bunge, mjifunze namna ambavyo Bunge linaendeshwa na sisi Wabunge tunajivunia sana kuwepo kwa Chuo hiki Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. (Makof)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Uchukuzi, Mheshimiwa Charles Tizeba, samahani wasukuma wote kila mtu Charles hao. Mheshimiwa Charles Tizeba ambaao ni Wenyewe viti wa Vijiji 100 kutoka Jimbo la Buchosa Sengerema. Wenyeviti wa Vijiji pale mlipo simameni! Karibuni sana Dodoma, karibuni sana watani wangu, hii ndiyo Dodoma na hapa ndiyo Bungeni. Huwa nawaasa wenzeni mkija hapa magari ni mengi muwe mnaangalia amnapokatiza barabara ninyi wasukuma. Karibuni sana.(Makof)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Tuna wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Usafirishaji Dar es salaam msimame pale mlipo wanafunzi kutoka Chuo cha Usafirishaji. Karibuni sana sana.

Viongozi watano wa CCM kutoka Jimbo la Buchosa wakiongozwana Ndugu George Sumwile pamoja na Katibu wa CCM Wilaya Ndugu Muhamed Muhamed. Karibuni sana viongozi wote, niwahakikishieni Mbunge wenu Mheshimiwa Charles Tizeba anafanya kazi nzuri sana Bungeni na leo mtamwona Wizara yake ikiwasilisha Makadirio na Matumizi ya fedha mwaka ujao. Tunaomba mumpe ushirikiano wa kila aina kule Buchosa. Ahsante sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge hapa naomba tusikilizane, mnisikilize vizuri. Tuna wageni maalum kabisa maana kundi hili halijwahi kupatikana katika Bunge letu. Naomba niwatambulish kwa upekee wao, maana hawa ni maalum. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na ni wafuatao:-

Madreva wa Treni Wanawake wa nane (8), wako kwenye kona pale. (Makofi/Vigelegele)

Kwa hiyo, kama kuna Watanzania walikuwa hawajui, wajue sasa kwamba kuna madreva wa treni wanawake, miongoni mwao 8 wamewakilisha hapa. (Vigelegele)

MBUNGE FULANI: Waonyeshwe waonyeshwe!

NAIBU SPIKA: Camera peleka vizuri kule kwa madreva wetu wa treni.

Mheshimiwa Waziri ametuletea Marubani wa Ndege wanawake wanane (8). (Makofi/Vigelegele)

MBUNGE FULANI: Huyo mwenye Camera ana vivu huyo. (Makofi/Vigelegele)

NAIBU SPIKA: Pamoja nao wapo Waongoza Ndege pia wanawake, naomba mwendelee kusimama Wahandisi Wanawake wa Ndege, wa Mitambo, wa Mawasiliano na wa Ujenzi Wanawake. Hao ni Wahandisi Wanawake. (Makofi/Vigelegele)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Haya ninyi naomba sasa mkae, naomba nitambulisse kundi jingine maalum kabisa hili. Hawa ni Madereva Wanawake wa Mabasi wanaopiga Dar es Salaam Tunduma. Route yao hawa ni Dar es salaam kwenda Tunduma na kurudi. Akina mama hao. Ahsante sana naomba mkae. (Makofi/Vigelegele)

Lakini kana kwamba haitoshi, naomba niwatambulisse Madereva wa Malori Makubwa wanawake, wanaosafiri kati ya Dar es salaam na Lubumbashi. (Makofi/Vigelegele)

Jamani wanawake wanaweza hawawezi?

WABUNGE: Wanaweza!!

NAIBU SPIKA: Wakiwezeshwa au siyo?

MBUNGE FULANI: Wanaweza, wanaweza bila kuwezeshwa! (Vicheko)

NAIBU SPIKA: Wanawake wanawezajamani. Wanawake wanaweza kabisa na akina mama hawa nichukue fursa hii kuwapongezeni sana, kwa kuingia katika taaluma za kipekee, mnaweza kuihakikishia nchi na Dunia kwamba kweli wanawake wanaweza. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Wanaweza!

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wanasema safari ijayo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe tuletee madereva wa boda boda, wa Meli na maeneo mengine.

Pia Bajaj na aina nyingine za usafiri. Karibuni sana Bungeni ahsanteni sana. (Makofi)

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Matangazo ya kazi kabla, Mheshimiwa Abdul Karim Shah Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Ardhi, Maliasili na Mazingira anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira Saa saba na robo Msekwa (C).

Mheshimiwa Idd Azzan Zungu, Mwenyekiti wetu wa Bunge Sports Club anawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee na mazoezi kwenye uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma kama kawaida kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa siku ya Jumapili tarehe 1 Juni, 2014 kati yetu Bunge Sports Club na NMB kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

michezo ya mpira ya miguu pamoja na Netball. Anawasitizia kwamba usafiri wa mabasi utawapitia katika maeneo yenu kama kawaida.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Capt. John Komba, ngoja kidogo niwapate wote, Mheshimiwa Nchambi, tajeni majina yenu mlion mbali, Mheshimiwa Kangi Lugola, ni watatu tu!

MHE. SULEMANI M. N. SULEMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7). Wakati wa maswali na majibu yalipokuwa yakiendelea hapa Bungeni, Mheshimiwa Ana-MaryStella John Malaki, dada yangu mwenye majina matatu mazuri kabisa yaliyoyabeba akina mama wengine, ni mashuhuri, alilieleza Bunge hapa na Watanzania milioni arobaini na tano wakiwa wanasikia kuwa katika aidha Wilaya yake au Mkoa wake Zahanati zimejengwa hovyo hovyo.

Kwa kuwa yeye pengine katika Wilaya ama Jimbo analotoka ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani ambaye pia anayo mamlaka kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za aidha kutoa hoja ya ujenzi wa zahanati ovyo ovyo ambazo kwa tafsiri rahisi zinatekelezwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu Watanzania wameiamini Serikali inayotekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa kwa tafsiri ya ujenzi wa zahanati ambazo zimejengwa hovyo hovyo, pengine ilipotakiwa kuwa chumba cha akina mama kumewekwa washroom ama vyovyote vile. Kwa mujibu wa sharia, taratibu na kanuni za nchi yetu, sina imani zahanati zinazoendelea kujengwa katika nchi yetu kwenye vijiji na mitaa yetu zitakuwa zimejengwa hovyo hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ilikuwa, kwa tafsiri rahisi kabisa na maana nzuri, nimuombe dada yangu aliombe radhi Bunge kwa niaba ya Watanzania wote kwa sababu Serikali yetu haiwezi kuruhusu ujenzi wa zahanati hovyo hovyo kama anavyofikiri yeye. Kama hatafanya hivyo, ni wajibu wake kuthibitisha zimejengwa wapi zahanati hizo hovyo hovyo na kama hawezi kuthibitisha, ni wajibu na ni dhahiri shahiri, kwa sababu Waarabu wanasesma muhadatu maghrum ismi kunaakilu (msimulaji akiwa hana akili, wasikivu tuwe na akili) na kama hawezi kuthibitisha ni dhahiri shahiri, hahudhuri vikao na hatembelei eneo ambalo amelitaja ili kuona kuwa kuna ujenzi wa hovyo hovyo unaoendelea. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja na kama hatathibitisha basi niombe mwongozo wako either utoe majibu kwa sasa ama baadaye, atudhihirishie haya aliyojasema ili kuwadanganya na kuwalaghai Watanzania. (Makofij)

Nakala ya Mtando (Online Document)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
walikuwa wakiongea)

NAIBU SPIKA: Naomba utulivu jamani, Mheshimiwa Mbunge anapokuwa anaongea, tusikilizane, ndiyo demokrasia yenyewe, tupeane nafasi kidogo. Mheshimiwa Captain Komba.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, natumia Kanuni ya 68(7). Weekend hii wakati tuko hapa ndani Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu alisema kwamba kuna baadhi ya Wabunge ambao wanakopa kwenye mashirika ya jamii au wanachukua fedha kwenye mashirika ya jamii. Jana amekaa na waandishi wa habari na leo zimetoka habari kwamba katika Wabunge hao na mimi ni mmojawapo! Katika Wabunge hao wanaofilisi mashirika ya umma na mimi ni mmojawapo! (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikumbuki hata ofisi ya LAPF iko wapi, wala Meneja wake, wala mfanyakazi wake na sijachukua fedha yoyote LAPF. Nachokumbuka tu ni kwamba kuna Nyasa Development Fund ambao ni wadau wa LAPF waliomba misaada kununua boti na LAPF wakatoa shilingi milioni moja na laki tano kuwasaidia kama ustawi wa jamii wao kule wanakotoka, siyo Captain Komba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo Bwana Tundu Lissu amekuja hapa anadanganya watu, kwamba mimi nimehusika na kutoa fedha LAPF. Sijui huu ni wendawazimu ama ni namna gani? Hizi ni siasa za maji taka kabisakabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, kama kweli anahakika na alithibitishie Bunge hili ama sivyo aniombe radhi. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Kangi Lugola.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7). Nimepata taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wangu wa LAAC ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi kwamba waliitaka Serikali iwasilishe hapa Bungeni haraka iwezekanavyo Muswada wa VAT ili Bunge hili liweze kupitia na kufuta misamaha yote isiyokuwa na tija katika nchi yetu. Kwa kuwa bajeti yetu imekuwa tegemezi kwa miaka mingi, bajeti ambayo inategemea bia, soda, pamoja na Pay As You Earn kwa wafanyakazi; na kwa kuwa ripoti ya CAG mwaka 2013/2014, imeonyesha kuwepo kwa misamaha ya kodi shilingi trilioni 1.5; na kwa kuwa bajeti yetu pia ya mwaka jana ilikuwa na deficit ya shilingi trilioni 1.5, hii inaonyesha dhahiri

Nakala ya Mtando (Online Document)

kwamba kama misamaha ile isingekuwa imetolewa tusingekuwa na bajeti deficit katika bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ambazo zimetangulia hapa, Wabunge wote ni mashahidi, kila Waziri alikuwa analia kwamba hatekelezi miradi kwa sababu hapati fedha kutoka Wizara ya Fedha na Wabunge hapa tulikuwa tunailazimisha Serikali iongeze fedha kwenye Wizara mbalimbali ambazo zimeleta taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako, kwa kuwa Wabunge hawa ndiyo waliomchagua Spika na kwa kuwa Spika anaonyesha dhahiri kuibeba Serikali; kwa kuwa anaonyesha dhahri kuitetea Serikali ilhali wananchi wa Tanzania wanashindwa kupata maendeleo kwa kukosa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, ni lini Muswada huu utaletwa Kusomwa Mara ya Kwanza kwa sababu shughuli za Bunge zinaelekea mwisho ili Wabunge tupate fursa ya kutosha, tuweze kufuta misamaha yote ya kodi ambayo inafilisi nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge wa Mwibara, nawaomba Wabunge wenzangu, haya mambo ya Wabunge kutishwatishwa kwamba tukikataa bajeti ya Serikali Bunge linavunjwa, mimi niko tayari Bunge livunjwe, nirudi Mwibara nikalime pamoja nakuvua dagaa lakini safari hii lazima Muswada huu uletwe. Nitakuwa Mbunge wa kwanza, kama Muswada huu hautaletwa kabla ya Bunge hili kuisha, nitaleta hoja ya kumfukuza na kumuondoa Spika kwenye Kiti hicho kwa sababu ya kuibeba Serikali. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, ni lini Muswada huu muhimu wa VAT utaletwa hapa Bungeni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mawili, la kwanza ni hili alilosema Mheshimiwa Lugola, ni kweli amepata taarifa kwa huyo Mwenyekiti ambaye nafikiri ni Mheshimiwa Rajab. Amekutaja hapa kwamba wewe ndiye uliyemwambia kwamba Muswada wa VAT unakuja. Kwa hiyo, ni kweli, kwa utaratibu wa Kamati ya Uongozi, mimi kwa niaba ya Serikali huwa ndiyo nataja shughuli zinazotarajiwa kufanywa ndani ya Bunge hili. Niliomba nafasi kwenye Bunge hili siyo kwa kutaka yeye lakini kwenye Bunge hili kwamba Serikali inataka kuleta Muswada wa VAT. Kwa hiyo, sisi Serikali ndiyo tuliosema wala siyo Spika na wala hana sababu ya kumsingizia Spika hapa kuibeba Serikali kwa sababu hii ni kazi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya Serikali. Anayeleta shughuli za Serikali humu ndani ni Serikali yenyewe, siyo Spika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niliyetoa taarifa ni mimi kwa niaba ya Serikali. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Lugola kwamba Muswada huo utakuja pindi Kamati ya Uongozi ikitupa nafasi, siyo Spika, Kamati ya Uongozi ambayo ina Wenyeviti hapa mliowachagua ndiyo wanaotupa nafasi. Muswada huo tunakusudia Kuusoma Mara ya Kwanza hapa na tungependa upite katika hatua zote katika Bunge hili. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa ya kweli lakini maneno uliyotumia siyo ya kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, maelezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu ya watu kuomba si jambo la ajabu. Mimi niliomba kwa barua na nadhani ndiyo barua ambazo wamekupa. Kwenye mashirika haya na taasisi za umma na wengine, wana-Corporate Social Responsibility, bajeti ambayo mtu unaweza kuomba hata milioni 10, 20, lakini inategemea watakachokupa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ku-declare interest, mimi nimeshaomba zaidi ya mara tatu LAPF lakini kwa mara zote wamenipa shilingi milioni tatu na walininunulia taa za solar baada ya kugundua shule yangu moja ya Idodi iliungua na watoto wakafariki kwa sababu walikuwa wanatumia vibatari. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka kusema kwamba hili jambo si kubwa kiasi hicho, kwa sababu fedha hizi zipo na ni za maendeleo hata Serikali huwa tunaomba. Mfano ni kwamba CRDB katika maafa ya Morogoro juzi tumeomba na mimi kama Waziri nayeshughulikia maafa na wametupa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kushughulikia maafa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ukiniuliza kwamba uliomba, nitasema ndiyo, niliomba ngapi, ulipata, nimepata shilingi milioni tatu, wamepelea wapi, wamenunua vifaa kwa ajili ya shule. Ni jambo la kawaida kwa sababu makampuni na mashirika haya yanazo fedha za shughuli za maendeleo. (Makofi)

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba mwongozo kwako na siyo kwa Mheshimiwa Lukuvi. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Naomba twende kwa kufuata utaratibu kidogo ili twende vizuri. Kwa swali la Mheshimiwa Kangi Lugola, tumepeata taarifa za Serikali hapa

Nakala ya Mtando (Online Document)

za uhakika kwamba jambo hili linakuja, itakuwa ni jukumu la Kamati ya Uongozi kuangalia nafasi na fursa ili tuweze kumshauri Mheshimiwa Spika na ukweli ni kwamba Mheshimiwa Spika hahusiki katika kuzuia Muswada huo usiweze kuja. Kwa hiyo, hilo tunalifunga hapo.

Kwa masuala mawili, la Mheshimiwa Nchambi na Mheshimiwa Komba, bahati nzuri yanawahusu Wabunge na wenyewe wapo. Nitawapa dakika mbilimblji, kwa kifupi sana. Mheshimiwa Tundu Lissu haukuwepo, sijui kama umeelewa tuhuma dhidi yako lakini aanze Mheshimiwa Anna Mallac kwanza, kifupi sana tafadhalii, kuhusiana na maoni ya Mheshimiwa Nchambi na kutokuhudhuria kwako vikao vya Halmashauri.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kumjibu Mbunge mwenzangu kwamba awe makini katika kuyasoma maswali na kuyaelewa na bado nahitaji asinifunge mdomo katika kuongea mambo ambayo ni ya hatari katika jamii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe kwa macho yangu niliitwa na wananchi nikashuhudia wototo wanarushiana *drips* za maji na ile mirija yake na syringes ambazo wameokota. Sasa kwa hali hiyo, wananchi walisema Mheshimiwa Mbunge haya ni mambo mnayotakiwa kuyasimamia. Kwa hiyo, nimelileta Bungeni ili kuieleza Serikali ifanye jitihada kuhakikisha mashine za kuteketeza taka zinaletwa kama hizo zinazotokana na matibabu ya wagongwa. Naomba awe makini na maswali. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Suala lake lilikuwa ni kwamba umesema zahanati zilizojengwa ni mbovu.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu halikuwa hilo.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongelea mashine za kuteketeza taka na siyo ujenzi wa Zahanati, naomba aelewe hivyo. (Makofii)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nchambi, naomba ukae chini, basi suala hilo hamkuelewana. Naomba tulimalizie hapo kwa sababu hamkuelewana.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, yeye ndiye hakuelewa.

NAIBU SPIKA: Kwa sababu hamkuelewana suala hilo nalimalizia hapo. Mheshimiwa Tundu Lissu, dakika mbili.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza malalamiko ya Mheshimiwa John Komba na nimesikiliza maelezo ya Mheshimiwa Lukuvi na naomba nijibu kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba moja, inaelekea kwamba LAPF kwenye hilo fungu lake la huduma za jamii, ni kwa ajili ya Wabunge wa CCM peke yao.

MBUNGE FULANI: Siyo kweli.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Kwa sababu Wabunge ambao wamepewa fedha za LAPF ambao nyaraka zao zipo, ni hao wanaopiga kelele, siyo kweli, kina Pindi Chana, kina Mwigulu Nchemba na wenzao, Wabunge wa CCM peke yao ndiyo wanaochukua fedha za LAPF na nyaraka zipo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, Wabunge tuna jukumu la kusimamia Serikali na taasisi zake, kama tunachukua fedha za taasisi za Serikali...

MBUNGE FULANI: Tutawasimamiaje?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Tunaingia moja kwa moja kwenye mgongano wa maslahi. Tutawasimamiaje hao wanaotupa fedha ambazo zinapelekwa kwa watu wa chama kimoja tu.

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge walikuwa wakiongea*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Siyo kweli, umechukua fedha, unalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba nimalizie na hili ni baya zaidi, fedha za wafanyakazi zilizowekwa kwenye LAPF zinatumika kununua jezi na mipira kwa ajili ya Majimbo, Jimbo la Mheshimiwa John Magufuli. Fedha za wafanyakazi zinatumika kununua jezi! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, fedha za wafanyakazi zimetumika kununua komputa na printer kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambayo inatengewa fedha na Bunge hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nilisema, hili suala ni kubwa sana linahitaji Kamati Teule ya Bunge kuchunguza uchafu huu. (Makofii)

WABUNGE FULANI: Aaaah!

Nakala ya Mtando (Online Document)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, hajajibu la kwangu, la Komba je?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa LAPF Mheshimiwa Kabaka!

MBUNGE FULANI: Aaah, Hawa Ghasia.

NAIBU SPIKA: Badala yake Mheshimiwa Hawa Ghasia!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Aanze na mimi nitamalizia.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, aliyoyazungumza Mheshimiwa Lissu na alivyojibu Mheshimiwa Lukuvi, kwa kweli ni sahihi. Unajua huwezi ukapewa kitu kama hujaomba na Wabunge wanaokwenda kuomba misaada si tu katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii lakini na kwenye maeneo mengine yoyote kwa ajili ya maendeleo ya Majimbo yao inaruhusiwa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Hifadhi ya Jamii wanasaidia masuala ya elimu, ya afya na masuala mengine ya kiuchumi katika Majimbo na kwa watu wengine ambao wanakwenda kuomba, kwa ajili ya Social Corporate Responsibility. Kwa hiyo, kama hujaenda kuomba, usilazimishe kwamba hii Mifuko inasaidia watu wa aina moja, kwa maana ya Wabunge wa CCM maana ndiyo wanaokwenda kuomba kwa ajili wananchi wao. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, siyo vizuri kusema kwa sababu haya ni masuala binafsi, lakini kuna waliokopa fedha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ukiwepo Mfuko wa NSSF ambao uko chini ya Wizara yangu.

WABUNGE FULANI: Wataje!

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Nimesema siyo vizuri...

WABUNGE FULANI: Wataje!

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mfuko huu...

MBUNGE FULANI: Mbewe!

Nakala ya Mtando (Online Document)

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mfuko huu una arrest warrant ya kumchukua Mheshimiwa ambaye amekopa kwa muda mrefu hajarudisha.

WABUNGE FULANI: Mtaje!

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Kwa hiyo, hiyo ndiyo fedha ambayo si halali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Mbewe, Mbewe!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Ghasia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nadhani baadhi niliyotaka kuyasema Mheshimiwa Kabaka ameyasema. Nililotaka kuliongezea ni kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu amesema ana ushahidi na kwamba hayo ni mambo makubwa, kitaratibu ndani ya Bunge unapokuwa una ushahidi unaweka mezani. Tunaomba Mheshimiwa Tundu Lissu hayo anayoyasema ambayo ana ushahidi nayo, kama kweli ni sahihi, aweke hapo na mimi nasema Mheshimiwa Kabaka kashindwa kusema, anayedaiwa ni Mheshimiwa Mbewe, akalipe deni. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, nawaomba utulivu, nawaomba utulivu, naomba nimalizie jambo hili kwa sababu ya suala la muda.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge walikuwa wakiongea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, order, order, order, nawaombeni tusikilizane. Mimi ambacho napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, ni kuwa na utulivu, huu ubingwa ambao tunataka kuingia sasa hivi, kurusharusha maneno bila kukaa chini na kutulia, ni kuleta matatizo tu katika Bunge.

MBUNGE FULANI: Kweli!

NAIBU SPIKA: Lugha iliyotumika na Mheshimiwa Tundu Lissu akizungumza hapa, amesema Wabunge wanachukua fedha za LAPF yaani anatoa picha

Nakala ya Mtando (Online Document)

kwa wananchi kwamba Mbunge anachukua anaweka mfukoni mwake anatumia yeye na familia yake, ndiyo picha inayotoka, kitu ambaco siyo kweli. Sasa ni vizuri tunapopeleka habari kwa wananchi, sisi kama Wabunge, tupeleke ujumbe amba ni kweli, kwa sababu tukienda na hili la Wabunge waliochukua fedha wao na familia zao, majina yatacaa hapa, itakuwa ni aibu. Sasa unapoanzisha jambo, uwe umelichunguza kidogo kuona salama vinginevyo linarudi kwako tena! (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, naomba tukubaliana kwa sababu muda hauko upande wetu, sasa Katibu, kinachofuata.

KAULI ZA MAWAZIRI

Mashine za Matibabu ya Mionzi za Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI)

NAIBU SPIKA: Naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii endelea.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi, kwa kutoa kauli ya Serikali. Hii inafuatia mwongozo amba aliouomba Mheshimiwa Ester Bulaya, Viti Maalum kuhusu mashine za matibabu ya mionzi pale Taasisi ya Ocean Road.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ilianzishwa kwa Sheria Namba 2 ya mwaka 1996. Hii ni taasisi kubwa na pekee yenye majengo na mashine za kisasa za kutoa tiba ya wagonjwa ya saratani hapa nchini. Aidha, taasisi hii inatoa huduma bora za saratani katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ukiacha Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendelea kuwa na ongezeko la wagonjwa wa saratani hapa nchini, Serikali inaendelea na ujenzi wa kituo kingine cha tiba ya saratani katika hospitali ya rufaa ya Bugando. Jengo kwa ajili ya tiba limekamilika na mashine za kutoa tiba ya mionzi zinategemewa kufika nchini mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa wapya wa saratani wapatao 4,712. Hili ni ongezeko la wagonjwa 976 ukilinganisha na kipindi cha Julai - Machi 2012/2013. Wagonjwa wapatao 3,295 walitibiwa kama wagonjwa wa nje na wagonjwa 1,417

Nakala ya Mtando (Online Document)

walilazwa. Hadi Machi 2014, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa wa marudio 16,543 wa saratani katika kliniki. Vilevile jumla ya wanawake 4,985 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na matiti. Kati ya hao wanawake 197 waligundulika na dalili za awali za saratani ya shingo ya kizazi na 61 walikuwa na dalili za kuwa na saratani ya matiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine zinazotoa tiba ya mionzi ya nje katika Taasisi ya Ocean Road zipo mbili na ndizo zinazotumika kwa karibu asilimia 95 ya wagonjwa wa saratani ambao wanahitaji mionzi. Mashine ya tatu ni ndogo na inatumika kwa wagonjwa wachache hasa wenye saratani ya ngozi. Mashine moja ilinunuliwa na Serikali kupitia Wakala wa Nguvu za Atomic na ya pili iliitolewa kama msaada na kampuni ya *Best Theratronics* ya Canada katika mkakati wa kudhibiti saratani kitaifa. Mashine nyingine mbili za tiba ya mionzi ya ndani yaani *intracavitary* ambazo hutumika kwa akina mama wenye saratani ya shingo ya kizazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida mashine hizi zinatakiwa kufanyiwa matengenezo kinga (*preventive maintenance*) kila baada ya miezi mitatu. Aidha, mafundi wa kutengeneza mashine hizi wanatoka nje ya nchi. Hivyo, kuharibika kwa mashine hizo husababisha wagonjwa kukosa huduma kwa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine zinazohitaji matengenezo ni *Equinox 80* namba 2002 ambayo chanzo chake cha mionzi bado ni kizima lakini imeharibika na *Equinox 100* namba 2004 ambayo inahitaji chanzo kipyta cha mionzi yaani cobalt source. Mtengenezaji pekee wa mashine hizi ni kampuni ya *Theratronics* ya nchini Canada. Kampuni hiyo ndiyo iliopewa zabuni ya kufanya matengenezo hayo. Aidha, kampuni hiyo itatakiwa kuharibu vyanzo vyote vya mionzi vitakavyotokana na utengenezaji wa mashine hizo za mionzi na ubadilishaji wa vyanzo vipya vya mionzi, ufungaji wa vipuri vipya katika mashine hizo na kubeba masalia yote ya vipuri kutoka katika mashine zote mbili na kurudisha nchini Canada ili kudhibiti mionzi isiletu madhara kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hiyo ya Canada imeshapewa taarifa ya kuleta vifaa na kuja kufanya marekebisho ya mashine hizo. Gharama zote zinafikia jumla ya Sh.740,000,000, na tayari dola za Kimarekani 221,240, ambayo ni sawa na shilingi za Kitanzania 365,046,000 ikiwa ni asilimia 50 zimeshalipwa na Serikali Ijumaa ya tarehe 16 Mei 2014, hii ni kulingana na makubaliano. Mafundi na vifaa vinategemewa kufika nchini kwa dharura muda wowote kuanzia sasa. Matengenezo ya mashine hizo yatachukua muda wa siku nne, hivyo mashine hizo zitaanza kufanya kazi mara tu matengenezo yatakapokamilika. Aidha,

Nakala ya Mtando (Online Document)

Serikali inafanya matengenezo ya mashine za mionzi ya ndani kwa wanawake. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuona mashine hizo zinaanza kufanya kazi mapema iwezekanavyo ili wananchi waendelee kupata huduma hizo za mionzi. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya taasisi ya Ocean Road kwa ajili ya matengenezo-kinga ya mashine hizo kama inavyotakiwa. Vilevile, Serikali itajiri *Biomedical Engineers* katika hospitali zetu za rufaa ikiwemo Ocean Roan Cancer Institute ili waweze kushirikiana na kupata elimu kwa wataalam hawa kutoka Canada katika kufanya matengenezo ya mashine hizo na baadaye waweze kujenga uwezo wa kutengeneza matengenezo-kinga wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Uchukuzi

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia masuala ya Uchukuzi, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara Hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015
Kama ilivyosomwa Bungeni**

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusiana na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Bunge ya Kamati Miundombinu kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013 kuhusu taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, pamoja na maoni ya Kamati hukusu

Nakala ya Mtando (Online Document)

makadirio na matumizi ya mapato ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Uchukuzi kwa ushirikiano na mawasiliano mazuri yaliyofanywa na Wizara mbele ya Kamati yangu kuhusu utekelezaji wa maoni ha ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014, pamoja na makadirio ya bajeti na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji na ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kujadili bajeti ya Wizara ya Uchukuzi mwaka 2013/2014. Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na kuchambua utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi hicho. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali. Napenda kulitaarifa Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imefanya kazi ushauri na maagizo yaliyotolewa na Kamati isipokuwa katika maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, mambo mengine sitayasoma, yako kwenye kitabu changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2013, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Sh.420,521,220,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo ni Sh.252,680,000,000 ni fedha za ndani na Sh.167,441,220,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni na miradi kwa taasisi za Wizara. Katika kipindi cha 2013/2014, taasisi zilizo chini ya Wizara zilikuwa zinadaiwa jumla ya Sh.142,666,759,512/=, kutokana na hati za madai na huduma katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Viwanja vya ndege Sh.103,701,385,679/=; Shirika la Reli 12,790,000,000/= pamoja na RAHCO 25,411,373,833/=, pamoja na ndege za Serikali Sh.764,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Uchukuzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kama ilivyooneshwa kwenye jedwali kwa miaka minne mfululizo. Hata hivyo, pamoja na bajeti hii kuongezeka kila mwaka bado kiwango kinachotengwa ni kidogo na hakipatikani kwa wakati, hivyo kushindwa kukidhi mahitaji makubwa tuliyo nayo hasa ya reli, bandari na ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu ilisafiri kwenda Malaysia. Moja ya jambo kubwa tulilojifunza ni kuwa wenzetu wanatumia PPP kwa takribani

Nakala ya Mtandao (Online Document)

asilimia 90 kwa miradi yote ya miundombinu. Maana yake ni kuwa wanatekeleza miradi yao kwa haraka, kwa viwango vya hali ya juu, hasa miradi ya bandari, reli, barabara na viwanja vya ndege. Ni vyema Serikali iijipange, iamue kuipa sekta binafsi nafasi hii kuleta mabadiliko ya haraka na yenye ufanisi kama walivyofanya Malaysia na chi nyingine zilizoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali ipunguze utegemezi wa fedha za wahisani kwani mara nyingine zimekuwa hazitolewi kwa wakati uliopangwa na hivyo kukwamisha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya Sh. 434,627,329,000. Kiasi hiki bado ni kidogo ukilinganisha na mahitaji muhimu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati. Dhana ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ni dhana ambayo haiwezi kuepukika ikiwa kama Taifa linahitaji maendeleo ya haraka na yenye ufanisi wa hali ya juu. Nchi mbalimbali duniani zimefanikiwa kutokana na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi mikubwa ya ujenzi wa mtandao wa reli. Mifano ya nchi hizo ni pamoja na Malaysia, Brazil, Jumuiya ya Ulaya na Peru. Kwa nchi za Afrika zilizoimarisha reli kwa kutumia ushirikishwaji wa sekta binafsi ni Cameroon na Ivory Cost, ambazo zinaelezwa katika miaka ya 1990 – 1999 miradi yao ya reli ilikuwa imekwama. Baada ya kuanza kushirikisha sekta binafsi usafiri wa reli umeimarika na kustawi haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutegemea usafiri wa barabara kusafirisha mizigo mikubwa hasa ukizingatia ukubwa wa nchi yetu, pamoja na kutegemewa na nchi zinazotuzunguka katika sekta za uchukuzi kunachangia barabara zetu kuharibika kwa haraka na kuigharimu Serikali fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara. Aidha, usafiri wa malori umekuwa ukichukua muda mrefu kutokana na hali ya barabara zetu pamoja na vizuizi mbalimbali vinavyokuwa vimewekwa barabarani, hususani mizani, pamoja na vizuizi vya ukaguzi wa Jeshi la Polisi ambavyo navyo vinatutoa katika ushindani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Isitoshe, matuta makubwa na madogo yajulikanayo kama rasta yamekuwa visababishi vya ajali vya malori ya mizigo na hivyo kufanya biashara kuitopia barabara zetu kutovutia nchi jirani. Vilevile ghamama za uchukuzi wa mizigo pamoja na bidhaa mbalimbali zimekuwa juu hasa kwa Mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha reli na kuboresha usafiri wa reli utaiwezesha nchi yetu kusafirisha abiria na mizigo mingi kwa muda mfupi, pia kutachochea na kufungua maendeleo ya nchi kikanda katika sekta ya kilimo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

na biashara. Hizi ndizo baadhi ya sababu za msingi zinazosababisha Kamati ya Miundombinu kuishauri Serikali mara kwa mara kuhusu kuchukua hatua mahsusizi za kukarabati na kuimarisha mtandao wa usafiri wa reli nchini na kutafuta fedha nje ya bajeti ya kawaida. Japokuwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa reli ni miradi inayotumia fedha nyingi, lakini ikiimarishwa kwa muda mrefu haihitaji matengenezo ya mara kwa mara kama barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mpango wa kujenga mitandao ya usafiri wa reli nchini, ambapo kati ya mipango hiyo ni kuifanya reli ya kat iwe *standard gauge*, mradi wa reli kati ya Tabora-Kigoma, Isaka hadi Mwanza, kujenga reli ya Mtwara – Mbambabay, Mchuchuma hadi Liganga, pamoja na ukarabati wa reli kutoka Manyoni hadi Singida, Kaliua mpaka Mpanda, Mpanda hadi Kalema na kujenga reli ya kuunganisha bandari ya Mwambani Jijini Tanga na Bandari ya Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uboreshaji wa huduma za usafiri wa reli nchini, Kampuni ya Reli Tanzania ilisaini mkataba wa kununua mabehewa 274 mnamo Machi 2013, ambapo malipo ya awali yalifanyika Februari 2014. Hata hivyo, ikiwa Kampuni ya Reli Tanzania haitapatiwa Sh.9,800,000,000, ambazo ziko katika bajeti ya 2013/2014, mabehewa hayo 274 hayataanza kuwasili nchini mwezi Septemba 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inashirikiana na nchi za Malaysia kukarabati vichwa vinane vya treni. Kamati inaipongeza Serikali kwani hadi kufika mwezi Aprili, 2014, vichwa vitatu vimekamilika na vinafanya kazi. Aidha, vichwa vitano vilivysosalia vinatarajiwa kukamilika mnao mwezi Septemba, 2014. Kamati inashauri, ili kuendeleza utaalamu wa ndani pamoja na kukuza pato la Taifa, ni vyema sasa Serikali ikazipa kipaumbele, kuziwezesha karakana zetu za ndani kama vile Karakana ya treni Morogoro ambayo ina wataalam wanaoweza kutengeneza na kukarabati treni kama ambavyo inafanyika Malaysia. Pia, kuimarisha Chuo cha Reli cha Tabora ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la kujirudiarudia mara kwa mara kuharibika miundombinu katika stesheni ya Kilosa hadi Gulwe Morogoro. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali sasa ipange mikakati madhubuti namna ya kuzuia uelekeo wa maji, yanapotoka milimani kwa kufukua mabwawa ya Kidete na Munisagala. Itambulike kuwa reli ni usafiri wa wanyonge, tunapoitelekeza ujumbe tunaoutoa kwa wanyonge ni kwamba hatujali, jambo ambalo sio nia ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tazara. Pamoja na mafanikio na mipango mizuri ya kuimarisha reli, bado TAZARA imeendelea kukabiliwa na changamoto za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kiuendeshaji, ambao kwa kiasi kikubwa zimesababishwa na Sheria iliyoanzisha TAZARA, Sheria Na.4 ya mwaka 1975. Kamati imefarijika kusikia mchakato wa kurekebisha Sheria hii umeanza. Kamati inashauri kasi ya mchakato huo iongezwe ili kupunguza kero mbalimbali katika uendeshaji wa reli hii. Umefika wakati sasa Serikali itoe suluhisho la mgomo wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa treni ya kusafirisha abiria Dar es Salaam. Vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kiasi kikubwa kwa kutafuta kampuni tanzu mahsus za usafiri wa treni ya abiria ambayo itatoa fursa kwa sekta binafsi katika kutoa huduma za reli Dar es Salaam na miji mingine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Kamati inaipongeza Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kuanza kutekeleza miradi ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN) bandarini ambayo kwa kiasi kikubwa imeweza kupunguza changamoto zilizokuwa zinaikabili bandari ya Dar es Salaam. Kati ya mafanikio hayo ni kupunguza muda wa meli kukaa bandarini kwa ajili ya kupakua na kupakia mizigo kutoka siku saba hadi siku 4.8; ongezezo la tani la shehena zilizohudumiwa kutoka milioni 12 mwaka 2012 hadi milioni 13.7 mwaka 2013; kupakua magari kutoka magari 400 Desemba 2012 hadi kufikia magari 671 Desemba 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha huduma zinatolewa kwa haraka bandarini, Kamati inashauri kuharakisha kukamilika kwa utekelezaji wa mradi wa malipo kwa njia ya mtandao (*electronic payment system*), kuwaunganisha pamoja watoa huduma kwa njia za mtandao, sambamba na kuhakikisha bandari pamoja na Mamlaka ya Mapato (TRA) zinafanya kazi masaa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kumeendelea kuwa na malalamiko ya wasafirishaji wa mizigo kwa kutumia magari makubwa kwa kutokuwa na maegesho bandarini na kwenye hifadhi za nchi kavu (*ICDs*). Kamati inasisitiza Mamlaka ya Bandari, kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, ziishauri Serikali kujenga haraka maegesho ya malori yanayoingia na kutoka bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka minane sasa tangu mchakato wa ujenzi wa gati 13 na 14 uanze, ambapo Kamati imekuwa na ushauri kuhusu umuhimu na faida ya upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa kitovu (*hub*) cha biashara ya usafirishaji katika Ukanda wa Afrika ya Mashariki. Hata hivyo, pamoja na miaka hiyo yote kupita, bado hakuna matumaini ya kuipanua Bandari ya Dar es Salaam hasa katika ujenzi wa gati 13 na 14.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati, ilielezwa kwamba Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari imeamua kuachana na mkopo wa Exim Bank ya China na makampuni ya kichina ya *China Communications Construction Company (CCC)* na *China Harbour Engineering Company (CHEC)*. Hii ni kwa sababu ya kukosekana kwa utashi wa kisisiasa (*political will*) kwa upande wa Serikali ya China katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara ya Uchukuzi imeamua kuipa sekta binafsi kutekeleza mradi wa ujenzi wa gati 13 na 14. Hata hivyo, Benki ya Dunia kwa kupitia *International Bank for Reconstruction and Development (IBRD)*, kwa kushirikiana na *DFID* na *TMEA* wameonesha nia ya kutoa mkopo wenyewe masharti ya bei nafuu wa asilimia 35 kwa ajili ya uendelezaji wa gati 13 na 14 na uboreshwaji wa gati 1 – 7 pamoja na kuongeza kina cha lango la Bandari ya Dar es Salaam. Baada ya uamuhi huu wa msingi kufanyika, ni matarajio ya Kamati kwamba sasa mradi huu utakwenda haraka na kwa uwazi na bila urasimu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Boya la mafuta. Katika taarifa ya Kamati ya mwaka 2013/2014, Kamati yangu ilipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi wa Boya jipya la Mafuta tangu mwezi Novemba 2012, ambapo kuwepo kwa boy a hilo kungeongezea ufanisi wa kuhudumia meli kubwa za tani 80,000 hadi 100,000 ambazo zina uwezo wa kushusha shehena ya mafuta kwa kiasi cha tani 3000 kwa saa. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, Kamati iliitaka Serikali kutoa maelezo kuhusu taarifa ya kusitishwa *flow meter* iliyokuwa imewekwa kwa ajili ya kupima kiasi halisi cha mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa malori. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia usharuri uliotolewa na Kamati kuhakikisha inapunguza ama kumaliza kabisa tatizo la msongamano wa magari ya mizigo katika mpaka wa Tanzania na Zambia mjini Tunduma. Kwa sasa huduma zinatolewa kwa saa ishirini na nne. Hii imepunguza kwa kiwango kikubwa hali ya msongamano wa malori ya mizigo katika mpaka huo. Hata hivyo, ifikapo June, 2014 msongamano unatarajiwa kupungua zaidi kwani jengo linalojengwa kwa upande wa Zambi la One Stop Boarder Post linatarajiwa kukamilika na hivyo kupelekea kufunguliwa gate la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika biashara ya usafirishaji wa mizigo kwenda nje ya nchi (*transit goods*) bado tunakabiliwa na changamoto kubwa ya urasimu, taratibu zilizopo hapa nchini hazina mvuto pia si rafiki wa mazingira ya biashara hasa ukizingatia ushindani wa kibashara ulipo katika Afrika ya Mashariki. Kati ya changamoto hizo ni pamoja na kuwa na vituo vingi vya mizani ambavyo vinapoteza muda mwingi njiani. Upimaji katika vituo hivi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuchukua muda mrefu hasa ukizingatia kuwa kunakuwepo na foleni kubwa ya malori, magari ya mafuta na mabasi ya abiria. Vilevile vituo vingine njiani vinavyosimamiwa na mamlaka nyingine kama vile Mamlaka ya Mapato (TRA) na Askari wa Polisi Barabarani. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwani imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto ya migogoro mingi ya ardhi baina ya wananchi wanaishi kandokando ya viwanja vya ndege. Kamati inaishauri Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, pamoja na Mamlaka nyingine zinazohusika na Ardhi, kuhakikisha inaweka mipaka katika maeneo ya viwanja vyote vya ndege na kuvipa Hati Miliki. Vilevile, kwa maeneo ambayo yametwaliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kama vile Omukajunguti-Bukoba, malipo ya fidia kwa wananchi yafanyike haraka. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa (*Terminal III*). Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Kambarage Nyerere kilianzishwa mwaka 1956 kikiwa na jengo moja tu la abiria na barabara moja ya kurukia ndege yenye urefu wa mita 2,400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu, mwezi Februari, 2014, ilijulishwa kuwa mradi huu kwa awamu ya kwanza unatarajiwa kugharimu Euro milioni 133 sawa na Sh.293,000,000,000/=. Awamu ya pili, itagharimu Euro milioni 235 ni sawasawa na Sh.518,000,000,000/=. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka HSBC ya Uingereza kwa dhamana ya Serikali ya Uholanzi na CRDB ya Tanzania. Aidha, ili kufanikisha mradi huu, Serikali kupitia Kamati ya Madeni ya Taifa, tarehe 5 Julai, 2012 ilitoa kibali cha kutekeleza mradi huu kwa njia ya mkopo. Hata hivyo, jambo la kushangaza ni kwamba hadi Kamati inakutana mwezi Mei, 2014, Hazina walikuwa hawajasaini mkataba wa makubaliano ya mkopo wa mradi huo. Inashangaza kuona, Kamati ya Miundombinu imeshauri, Kamati ya Bajeti imeshauri, Mheshimiwa Rais wakati anaweka jiwe la msingi katika kiwanja hiki aliagiza jambo hili lishughulikiwe. Kamati inaiuliza Wizara ya Fedha aseme nani ili mtekeleze wajibu wenu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwa hatua ya kuchukua mkopo katika Benki ya Biashara na kuanza hatua za awali za ujenzi huo. Pamoja na jitihada hizi, Kamati inasikitishwa kuona kuwa, mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga Sh.89,000,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika kiwanja

Nakala ya Mtando (Online Document)

cha Julius Kambarage Nyerere, fedha Sh.80,000,000,000/= ni fedha za nje na Sh.9,000,000,000 ni fedha za ndani kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi katika eneo la Kipunguni. Hadi kufikia mwezi Mei, 2014, fedha hizi ziliwa bado hazijatolewa. Kamati inashauri kama kweli Serikali inayo nia ya dharti ya kutaka kuanza kujenga jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere, itoe fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2013/2014. Aidha, ni vema Serikali ikawa inatoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kwani kucheleweshwa kwa fedha hizo kunapunguza kasi ya maendeleo ambayo wananchi wanategemea kuyapata kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka mmoja na nusu sasa tangu Kiwanja cha Ndege cha Songwe kilipoanzishwa mnamo mwezi Desemba, 2012. Uwanja huu umerahisisha na kuongeza wigo wa safari za anga kwa wananchi wa Nyanda za Juu Kusini. Vilevile, uwanja huu unatoa fursa kwa wakazi wa Mkoa wa Mbeya na Mikoa ya jirani kwani unawezesha kukua kwa uchumi. Kamati inashauri Serikali iendelee kukamilisha maeneo ya ujenzi yaliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Upanuzi kiwanja hiki ulianza mwaka 2012/2013. Kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi, mradi huu ultakiwa ukamilike ndani ya miaka mitatu kwa gharama ya Sh.105,000,000,000/=. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ilitenga Sh.8,000,000,000/= tu, mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga Sh.8,000,000,000/= ambapo hadi Aprili, 2014, kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 1.6 tu. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, kimetengewa shilingi bilioni 12 tu. Kamati inajiliza, je, mradi wa thamani wa shilingi bilioni 105, utaisha ndani ya miaka mitatu katika utaratibu huu? Kamati inaitaka Serikali kutoa tamko rasmi kuhusu nia thabiti ya utekelezaji na muda wa kukamilisha mradi huu wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ugunduzi wa gesi na ujenzi wa viwanda kama vile ujenzi kiwanda cha Simenti cha Dangote, katika Mkoa wa Mtwara ni ahahiri ya kuwa umuhimu wa mahitaji ya usafiri wa anga yataongezeka. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Kamati imeshauri Serikali kukamilisha mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha ndege cha Mtwara. Vilevile Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu kuhusu mkakati mahsus wa kujenga na kuimarisha kiwanja hiki. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi na kuhakikisha matokeo yanaonekana kwa haraka, ni vema Serikali iweke vipaumbele katika miradi michache na kuikamilisha kwa wakati kuliko kuwa na miradi mingi kwa wakati mmoja jambo linalosababisha miradi hiyo kutokamilika kwa wakati. Mwandishi mmoja wa vitabu anayeitwa Steven Convey aliyahi kusema, naomba ninukuu: “*The key is not to prioritize what is on your schedule*

Nakala ya Mtando (Online Document)

but to schedule your priority, mwisho wa kunukuu. Kwa tafsiri isiyo rasmi la msingi siyo kuweka vipaumbele katika ratiba yako bali ni kuratibu vipaumbele vyako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Kampuni hii imepitia matatizo mengi sana. Kwa sasa Kampuni hii ina ndege moja tu (Das 8 Q300) na ndege nyingine ya kukodi (CRJ 200). Pia Kampuni ya ATCL inadaiwa takriban shilingi bilioni 133. Makampuni mbalimbali duniani yameonesha nia ya kuwekeza katika Kampuni ya ATCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamatii inauliza maswali yafuaayo. Je, Serikali inatambua umuhimu wa Kampuni hii? Je, bado tunaihitaji Kampuni hii? Kama bado tunaihitaji Kampuni hii kwa nini Serikali haitoi mtaji wa kutosha? Kamati inaishauri Serikali iamue kuwekeza mtaji wa kutosha ili kuweza kulipa madeni ya ATCL na hatimaye iifufue upya kamupni hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). Kamati inaishauri SUMATRA kwa kushirikiana na vyombo vingine kama vile Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi, Wizara ya Ujenzi, kukaa pamoja na kujadiliana namna nzuri ambayo itaweza kupunguza matukio ya ajali nchini kwani yanaisababishia Serikali hasara kwa kupoteza nguvu kazi ya Taifa. Pia kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa mabasi haya yaendayo vijijini kwani mengi ni mabovu, jambo linalohatarisha maisha ya wananchi wetu waishio katika maeneo hayo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, SUMATRA, kwa kushirikiana na wadau wengine wa usalama barabarani iendelee kuratibu taratibu ambazo zitasaidia usafiri wa abiria kwa kutumia pilipiki kuwa usafiri wa uhakika na wenye usalama kwa wananchi. Vilevile Kamati inaishauri SUMATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kufanya udhibiti wa vyombo vidogo vya usafiri wa majini kama vile majahazi kwani imebainika kuwa baadhi ya vyombo hivi vimeduwa vikishiriki katika biashara haramu hasa dawa za kulevyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha ununuzi wa rada hiyo pamoja na kuandaa miundombinu yake ambayo inatarajiwa kuanza rasmi 2014. Hata hivyo, elimu na tahadhari ziendelee kutolewa kwa wananchi wanaojenga karibu na eneo linalotarajiwa kuwekwa rada ili kuepusha migogoro pindi mtambo huo utakapoanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka ya Hali ya Hewa ilitengewa shilingi bilioni 3.6, mwaka 2013/2014 ilitengewa shilingi bilioni 4.0, mwaka 2015 shilingi blioni 5.6. Kamati wanaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Mamlaka hii mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, pamoja na kuongezea Mamlaka hii fedha, mwenendo wa utoaji wa bajeti kwa Mamlaka hii siyo wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

kuridhisha kwani hadi kufika Aprili, 2014 kati ya shilingi bilioni 4 zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu ni Sh.695,000,000,000/= zilizokuwa zimetolewa sawa na asilimia 17.4 ya fedha zote zilizokuwa zinatarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ya Uchukuzi inaombwa kuidhinishiwa Sh.527,937,790,000/=. Kati ya fedha hizo Sh. 93,306,391,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kati yake Sh.33,027,291,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara na Sh.60,279,100,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha Wizara ya Uchukuzi imetengewa Sh.434,627,399,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh.273,140,000,000/= ni fedha za ndani na Sh.161,487,000,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina makadirio ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, kifungu kwa kifungu na sasa naliomba Bunge lako Tukufu, kuyajadili na kuyapitisha maombi ya Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha taarifa ya Kamati yangu. Aidha, nawashukuru pia Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Harrison George, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Katibu Mkuu, Dkt. Shaaban R. Mwinjaka, Naibu Katibu Mkuu, Mama Monica L. Mwamunyange pamoja na wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizoko chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwangao kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa wa kupitia na kuchambua Mpango wa Maendeleo wa Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashillilah, kwa kuiwezesha Kamati na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Vilevile Katibu wa Kamati hii, Bibi Hosiana John na Bibi Fransisca Haule kwa kuihudumia Kamati yangu. Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge wa Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014; Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara Hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015
Kama Ilivyowasilishwa Mezani

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, naomba nichukuwe fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Uchukuzi kwa ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara mbele ya Kamati yangu, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI ULIOTOLEWA WAKATI WA KUJADILI BAJETI YA WIZARA UCHUKUZI KWA MWAKA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, na kuchambua utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imefanya kazi ushauri na maagizo yaliyotolewa na Kamati isipokuwa katika maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa kutokana na ukosefu wa fedha.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

3.1 Fedha za Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha 2013/2014 bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ni **shilingi bilioni 108,884,774,000**. Kati ya fedha hizo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

shilingi bilioni 32,305,674,000 ni kwaajili ya Mishahara ya Watumishi. **Shilingi bilioni 76,579,100,000** ni kwa ajilili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi Aprili 2014, kiasi kilichotolewa ni **shilingi bilioni 56,736,998,612.** **22** sawa na **asilimia 52.12** ya bajeti yote ya Matumizi ya kawaida.

3.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 420,521,220,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 252,680,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 167,841,220,000** ni fedha za nje.

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 kiasi kilichotolewa na Hazina kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ni **shilingi bilioni 201, 213,050,000** sawa na **asilimia 47.85** ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizotolewa **shilingi bilioni 180,132,570,000** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 71.29**. Aidha, **shilingi 21,080,480,000** ni fedha za nje zilizotolewa sawa na **asilimia 12.56**.

3.3 Madeni ya Miradi kwa Taasisi za Wizara

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikuwa zinadaiwa jumla ya ya **shilingi bilioni 142,666,759,512** kutokana na hati za madai na huduma katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Taasisi hizo ni (**TAA- bilioni 103,701,385,679**), (**TRL-bilioni 12,790,000,000**), (**RAHCO- bilioni 25,411,373,833**) na (**TGFA- milioni 764,000,000**).

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

4.1 Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi

Mheshimiwa Spika, bajeti ya miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Uchukuzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Lifuatalo ni jedwali linaloonesha bajeti ya fedha za Maendeleo zilizotengwa kwa miaka minne mifululizo;

MWAKA	BAJETI YA MAENDELEO ILIYOTENGWA
2011/2012	Bil. 167.978
2012/2013	Bil. 252.758
2013/2014	Bil. 390.521
2014/2015	Bil. 434.627

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo pamoja na bajeti hii kuongezeka kila mwaka, bado kiwango kinachotengwa ni kidogo na hakipatikani kwa wakati hivyo kushindwa kukidhi mahitaji makubwa tuliyonayo hasa ya reli, bandari na ndege.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilisafiri kwenda Malaysia, moja ya jambo kubwa tulilojifunza ni kuwa wenzetu wanatumia (*Public Private Partnership-PPP*) kwa takribani asilimia tisini (90%) kwa miradi yote ya miundombinu. Maana yake ni kuwa wanatekeleza miradi yao kwa haraka na kwa viwango vya hali ya juu hasa miradi ya bandari, reli, barabara na viwanja vya ndege. Ni vyema Serikali ijipange na iamue kuipa sekta binafsi nafasi ili kuleta mabadiliko ya haraka na yenyе ufanisi kama walivyofanya Malaysia na nchi nyingine zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kupitia kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati imebaini pamoja na Serikali kuainisha miundombinu ya Uchukuzi kuwa ni kati ya maeneo ya kipaumbele katika mwaka 2014/2015 kuwa utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo imeshindwa kukamilika kutokana na kutotolewa kwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kama ilivyotarajiwa, ambapo hadi mwezi Aprili 2014 kati ya **shilingi bilioni 420,521,220,000/=** zilizoidhinishwa na Bunge ni **shilingi bilioni 201,213,050,000/=** tu ya fedha zote zilizotolewa sawa na asilimia **47.85**.

Kamati ilijulishwa kuwa kati ya **shilingi bilioni 252,680,000,000** za fedha za ndani zilizokuwa zimetengwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu ni **shilingi bilioni 180,132,570,000** tu zilizotolewa sawa na **asilimia 71.28**. Aidha, mtiririko wa fedha za nje unaonesha kati ya **shilingi bilioni 167,841,220,000** zilizoidhinishwa ni **shilingi bilioni 21,080,480,000/=** sawa na **asilimia 11.70** ya fedha zote za nje zilizoidhinishwa. Muelekeo huu unaonyesha kuwa uwezekano wa kupata fedha zote kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha ni mdogo. Kamati inashauri Serikali ipunguze utegemezi wa fedha za wahisani kwani mara nyingi zimekuwa hazitolewi kwa wakati uliopangwa na hivyo kukwamisha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika makadirio ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya **shilingi bilioni 434,627,399,000/=**. Kiasi hiki bado ni kidogo ukilinganisha na mahitaji na umuhimu wa Wizara hii.

4.2 Reli ya Kati

Mheshimiwa Spika, dhana ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ni dhana ambayo haiwezi kuepukika ikiwa kama taifa linahitaji maendeleo ya haraka na yenyе ufanisi wa hali ya juu. Nchi mbali mbali duniani zimefanikiwa kutokana na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi mikubwa ya ujenzi wa mtandao wa reli. Mifano ya

Nakala ya Mtando (Online Document)

nchi hizi ni pamoja na Malaysia, Brazil, Jumuiya ya Ulaya na Peru. Kwa nchi za Afrika zilizoimarisha reli kwa kutumia ushirikishwaji wa sekta binafsi ni pamoja na Cameroon na Ivory Coast ambazo zinaelezwa katika miaka ya 1990-1999 miradi ya reli zao ilikuwa imekwama. Baada ya kuanza kushirikisha sekta binafsi usafiri wa reli uliimarika na kustawi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kutegemea usafiri wa barabara kusafirisha mizigo mikubwa hasa ukizingatia ukubwa wa nchi yetu pamoja na kutegemewa na nchi zinazotuzunguka katika sekta ya uchukuzi, kunachangia barabara zetu kuharibika kwa haraka na kuigharimu Serikali fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara. Aidha, usafiri wa malori umekuwa ukichukuwa muda mrefu kutokana na hali ya barabara zetu pamoja na vizuizi mbalimbali vinavyokuwa vimewekwa barabarani hususani mizani pamoja na vizuizi vyta ukaguzi wa jeshi la polisi ambavyo kwa pamoja vinatutoa katika ushindani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Isitoshe matuta makubwa na madogo yajulikanayo kama rasta, yamekuwa visababishi vyta ajali ya malori ya mizigo na hivyo kufanya biashara kupitia barabara zetu kutovitia nchi jirani. Vilevile ghamra za uchukuzi wa mizigo pamoja na bidhaa mbalimbali zinakuwa juu hasa kwa mikoa ambayo ipo pembezoni.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha na kuboresha usafiri wa reli nchini kutawezesha kusafirisha abiria na mizigo mingi kwa muda mfupi, pia kutachochea na kufungua maendeleo ya nchi kikanda hasa katika sekta ya kilimo na biashara. Hizi ndizo baadhi ya sababu za msingi zinazosababisha Kamati ya Miundombinu kuishauri Serikali mara kwa mara kuhusu kuchukuwa hatua mahsus za kukarabati na kuimarisha mtando wa usafiri wa reli nchini hata kwa kutafuta fedha nje ya utaratibu wa kawaida wa bajeti. Japokuwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa reli ni miradi inayotumia fedha nyingi, lakini reli ikiimashwa hudumu kwa muda mrefu (*long lasting*) na haihitaji matengenezo ya mara kwa mara kama ikilinganishwa na barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mipango ya kujenga mitando ya usafiri wa reli nchini ambapo kati ya mipango hiyo ni kuifanya reli ya kati iwe ya (Standard Gauge), mradi wa reli kati ya Tabora, Kigoma, Isaka hadi Mwanza, kujenga reli ya Mtwara, Mbambabay, Mchuchuma hadi Liganga, pamoja na ukarabati wa reli kutoka Manyoni Singida na Kaliuwa Mpanda, Mpanda hadi Kalema na kujenga reli ya kuunganisha bandari ya Mwambani jijini Tanga na Bandari ya Musoma mkoani Mara.

Mheshimiwa Spika, katika uboreshaji wa huduma za usafiri wa reli nchini Kampuni ya Reli Tanzania ilisaini mkataba wa kununua mabehewa 274 mnamo mwezi Machi 2013, ambapo malipo ya awali yamefanyika Februari 2014. Hata hivyo, ikiwa Kampuni ya Reli Tanzania itapatiwa ndani ya mwaka huu wa fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

shilingi bilioni 9.8 ambazo zipo katika bajeti ya 2013/2014, mabehewa hayo 274 yataanza kuwasili nchini mwezi Septemba 2014.

Kamati inashauri Serikali ikamilishe kutoa fedha za mradi huu ambazo ni **shilingi bilioni 9.8** kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ili mabehewa hayo yaanze kuwasili nchini na kuboresha huduma za usafiri wa reli nchini. Kwa Serikali kushindwakutoa fedha hizo kutafanya behewa hata moja lisiletwe na hivyo kukwamisha huduma za treni mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashirikiana na nchi ya Malasyia kukarabati vichwa vinane (8) vya treni. Kamati inaipongeza Serikali kwani hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 vichwa vitatu (3) vimekamilika na vinafanya kazi, aidha vichwa vilivyosalia vitano (5) vinatarajiwa kukamilika mnamo mwezi Septemba 2014. Kamati inashauri ili kuendeleza utaalam wa ndani pamoja na kukuza pato la Taifa, ni vema sasa Serikali ikazipa kipaumbele na kuziwezesha karakana zetu za ndani kama vile karakana ya treni Morogoro ambayo ina wataalam wanaoweza kutengezeza ama kukarabati treni kama ambavyo inafanyika Malaysia. Pia, kuimarisha Chuo cha Reli Tabora ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo la kujirudia rudia la kuharibika kwa miundombinu ya reli katika stesheni ya Kilosa- Gulwe Morogoro. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali sasa ipange mkakati madhubuti wa namna ya kuzuia uelekeo wa maji yanayotoka milimani kwa kufukuwa mabwawa ya Kidite na Munisagala. Itambulike kuwa reli ni usafiri wa wanyonge, tunapoitelekeza ujumbe tunaotoa kwa wanyonge ni kwamba hatujali, jambo ambalo sio nia ya Serikali yetu.

4.3 Uendeshaji wa Reli ya TAZARA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kwamba TAZARA imeandaa Mpango wa maendeleo wa miaka mitano yaani (2013/2014 – 2017/2018) ulioanisha maeneo ya miradi ya uwekezaji yenyelengo la kuijengea uwezo na kuimarisha utendaji ambapo miradi hiyo itaigharimu **shilingi bilioni 307.2**. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itatoa fedha hizo kwa wakati ili kufanikisha mpango huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio na mipango mizuri ya kuimarisha reli hii, bado TAZARA imeendelea kukabiliwa na changamoto za kiuendeshaji ambazo kwa kiasi kikubwa zinasababishwa na sheria iliyoanzisha TAZARA Na. 4 mwaka 1975. Kamati imefarrijika kusikia mchakato wa kurekebisha Sheria hii umeanza. Kamati inashauri kasi ya mchakato huu iongezwe ili kupunguza kero mbalimbali katika uendeshaji wa reli hii. Imefika wakati sasa Serikali itoe suluhisho la mgomo ya wafanyakazi.

4.4 Mradi wa Treni ya Kusafirisha Abiria Jijini Dar es Salaam (City Train)

Mheshimiwa Spika, msongamano katika jiji la Dar es Salaam umeendelea kuwa changamoto kubwa kutokana na ongezeko la watu, magari pamoja na hali halisi ya miundombinu ya barabara ambayo mpaka sasa haikidhi mahitaji ya usafiri Dar es Salaam. Serikali kwa kupitia Wizara ya Uchukuzi katika kuhakikisha inapunguza kero ya msongamano wa usafiri Dar es Salaam mnamo mwezi Oktoba, 2012 ilianzisha usafiri wa treni. Treni hii ya abiria imekuwa ikisafiri kutoka Dar es Salaam Stesheni, kwenda Ubungo Maziwa kupitia Buguruni na Tabata. Aidha, treni ya TAZARA inayosafiri kutoka Pugu, Mwakanga hadi Kurasini.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayoukabili mradi huu ni gharama za uendeshaji ambazo zipo juu zaidi ya mapato yatokananyo na tozo la nauli. Gharama hizi zinahusisha mafuta ya dizeli, mafuta mazito kwa ajili ya injini, mishahara na gharama za Bima (Premium) kwa abiria. Aidha, changamoto nyingine kubwa ambayo ni Kampuni ya Reli Tanzania kutumia injini zilizokuwa za treni za safari ndefu ambazo zinatumia mafuta mengi sana. Kamati inasisitiza ushauri wake kuwa, ili mradi uweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuondokana na hasara, Serikali iharakishe kununua angalau treni mbili za kisasa na maalum kwa safari fupi ambazo gharama yake ni takribani **shilingi billioni 8** kila moja.

Vilevile, Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi katika kutafuta Kampuni tanzu mahsus kwa usafiri wa treni ya abiria ambayo itatoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma ya usafiri wa treni katika jiji la Dar es Salaam na miji mingine nchini.

4.5 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kuanza kutekeleza miradi ya Matokeo Makubwa Sasa (*Big Result Now-BRN*) bandarini ambayo kwa kiasi imeweza kupunguza changamoto zilizokuwa zikiikabili bandari ya Dar es Salaam. Kati ya mafanikio hayo ni pamoja na;:-

- i. Kupunguza muda wa meli kukaa bandarini kwa ajili ya kupakuwa na kupakia mizigo kutoka siku saba (7) desemba 2012 hadi siku 4.8 desemba 2013;
- ii. Ongezeko la tani za shehena zilizohudumiwa kutoka tani milioni 12.0 mwaka 2012 hadi tani milioni 13.7 mwaka 2013;
- iii. Kupakuwa magari kutoka magari 400 desemba 2012 hadi kufikia magari 671 desemba 2013.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Hata hivyo, muda wa makasha kukaa bandarini uliongezeka kutoka siku tisa (9) desemba 2012 hadi siku 9.3 mwezi desemba 2013. Ongezeko la muda wa makasha kukaa bandarini lilitokana na mgomo wa wamiliki wa malori uliotokea mwaka 2013. Inakadiriwa kuwa hasara iliyosababisa na mgomo huu ni shilingi bilioni 20 - 30. Ili kuepusha hasara kubwa kama hii, Kamati inashauri kuwepo kwa ushirikiano mkubwa na wakaribu kati ya Serikali na wadau wa usafirishaji. Vile vile, katika kuhakikisha huduma zinatolewa kwa haraka bandarini, Kamati inashauri kuharakishwa kukamilika kwa utekelezaji wa mradi wa malipo kwa njia ya mtando (Electronic Payment System), kuwaunganisha pamoja watoa huduma kwa njia ya mtando (Electronic Single Window System) sambamba na kuhakikisha bandari pamoja na Mamlaka ya Mapato-TRA zinafanya kazi masaa ishirini na nne.

Mheshimiwa Spika, bado kumeendelea kuwa na malalamiko ya wasafirishaji wa mizigo kwa kutumia magari makubwa kwa kutokuwa na maegesho bandarini na kwenye hifadhi za nchi kavu (ICDS). Kamati inasisitiza Mamlaka ya Bandari kwa kushirikiana na Halmashauri za jiji ziishauri Serikali kujenga haraka maegesho ya malori yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inaitaka Serikali kutoa maelezo kuhusiana na maendeleo ya bandari za Mwambani –Tanga, Mtwara, Kigoma na Itungi-Mbeya. Aidha, Wakala wa Meli nchini uliahidi kujenga meli mpya tatu kwenye ziwa Tanganyika, Victoria na Nyasa. Kamati inauliza mpango huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, ni miaka minane sasa tangu mchakato wa ujenzi wa gati namba 13 na 14 uanze ambapo Kamati imekuwa ikishauri kuhusu umuhimu na faida za upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam na kufanya bandari ya Dar es Salaam kuwa kitovu (*Hub*) cha biashara ya usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Hata hivyo, pamoja na miaka hiyo yote kupita bado hakuna matumaini ya kuipanua bandari ya Dar es Salaam hasa katika ujenzi wa gati namba 13 na 14. Katika taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati, ilielezwa kwamba Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari imeamua kuachana na mkopo wa Exim Bank ya China na makampuni ya Ki-china ya China Communications Construction Company Ltd (CCCC) na China Harbour Engineering Company Ltd (CHEC). Hii ni kwasababu ya kukosekana kwa utashi wa kisiasa (*political will*) kwa upande wa Serikali ya China katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara ya Uchukuzi imeamua kuipa sekta binafsi kutekeleza mradi wa ujenzi wa gati namba 13 na 14. Hata hivyo Benki ya Dunia kwa kupitia International Bank for Reconstruction and Development

Nakala ya Mtando (Online Document)

(IBRD) kwa kushirikiana na DFID na TMEA wameonesha nia ya kutoa mkopo wenye masharti ya bei nafuu wa asilimia 65 na msaada wa asilimia 35 kwa ajili ya uendelezaji wa gati namba 13 na 14 na uboreshwaji wa gati namba 1 - 7 pamoja na kuongeza kina cha lango la Bandari ya Dar

Baada ya uamuzi huu wa msingi kufanyika, ni matarajio ya Kamati kwamba, sasa mradi huu utakwenda haraka, kwa uwazi na bila urasimu wowote.

4.6 Boya la Mafuta (Single Point Mooring)

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya kamati ya mwaka 2013/2014, Kamati yangu iliipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi wa boyo jipya la mafuta tangu mwezi Novemba, 2012 ambapo kuwepo kwa boyo hili kungeongeza ufanisi wa kuhudumia meli kubwa za tani 80,000 hadi 100,000 ambazo zinauwezo wa kushusha shehena ya mafuta kiasi cha tani 3000 kwa saa. Hata hivyo pamoja na pongezi hizo, Kamati iliitaka Serikali kutoa maelezo kuhusu taarifa za kusitishwa "flow meter" iliyokuwa imewekwa kwa ajili ya kupima kiasi halisi cha mafuta.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa kwamba "flow meters" zilizofungwa katika kituo cha kupakulia mafuta cha Kurasini (KOJ) zimesitishwa kutumika na Wakala wa Vipimo mnamo mwezi Februari, 2011 kutokana na kulalamikiwa kwa kutokuwa na vipimo sahihi. Aidha, kwa kuzingatia Mkataba wa Kimataifa wa ulinzi na usalama wa Meli na bandari (ISPS Code), mamlaka ya bandari inafikiria kuondoa miundombinu ya (KOJ) katika magati ili kuweza kuendana na matakwa ya Kimataifa wa Usalama wa Meli na Bandari. Hivyo, kwa hali ilivyo sasa Mamlaka inalazimika kukarabati boyo lake la zamani kwa ajili kuhamishia huduma.

Kamati inajjiuliza je wataalam bandari waliohusika katika ujenzi wa boyo hili walikuwa na utaalam wa kutosha kuweza kuona athari za ambazo zingetokana na ujenzi wa boyo hili katikati ya magati ya Bandari? Kamati inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu undani wa suala hili.

4.7 Usafiri wa Malori

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati wa kuhakikisha inapunguza ama kumaliza kabisa tatizo la msongamano wa magari ya mizigo katika mpaka wa Tanzania na Zambia mjini Tunduma. Kwa sasa huduma zinatolewa kwa saa ishirini na nne. Hii imepunguza kwa kiwango kikubwa hali ya msongamano wa malori ya mizigo katika mpaka huu. Hata hivyo, ifikapo mwezi juni, 2014 msongamano unatarajiwa kupungua

Nakala ya Mtando (Online Document)

zaidi kwani jengo linalojengwa kwa upande wa Zambia la (One Stop Boarder Post) linatarajiwa kuwa litakamilika na hivyo kupelekea kufunguliwa kwa geti la pili.

Mheshimiwa Spika, katika biashara ya usafirishaji wa mizigo kwenda nje ya nchi (*transit goods*) bado tunakabiliwa na changamoto kubwa ya urasimu. Taratibu zilizopo hapa nchini hazina mvuto na pia si rafiki kwa mazingira ya biashara hasa ukizingatia ushindani wa kibashara uliopo katika Jumuia ya Afrika Mashariki. Kati ya changamoto hizo ni pamoja na kuwa na vituo vingi vya mizani ambavyo vinapoteza muda mwingi njiani. Upimaji katika vituo hivi huchukuwa muda mrefu hasa ukizingatia kuwa kunakuwepo na foleni kubwa ya malori, magari ya mafuta na mabasi ya abiria. Vilevile, vituo vingine njiani vinavyosimamiwa na mamlaka nyingine kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na askari wa usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea kuchukuwa muda mrefu katika kufanya maamuzi ya kupunguza urasimu barabarani unaosababishwa na kuwa na vizuizi vingi, nchi jirani kama vile Kenya wanakazana kuhakikisha wanaweka mazingira yenye mvuto na urahisi kwa wafanyabiasha jambo ambalo kwa hakika litasababisha wafanyabiashara wengi hasa wa magari makubwa ya mizigo kuamua kupidisha mizigo yao bandari ya Mombasa-Kenya na Beira- Msumbiji. Vilevile Kamati inaiomba Serikali iangalie upya sheria yake ya “Transit Goods” hasa mafuta kutoka siku 30 hadi 60.

4.8 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwani imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege nchini. Pia na kwa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ukarabati wa viwanja vya ndege vya Tabora, Kigoma na kukamilisha kiwanja cha ndege cha Mafia. Ni matarajio ya Kamati kwamba ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Bukoba, ujenzi wa viwanja vya Songwe na Mwanza navyo vitakamilishwa kwa wakati ili kuendelea kurahisisha usafiri wa anga kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto na migogoro mingi ya ardhi baina ya wananchi wanaishi kando kando ya Viwanja vya Ndege. Kamati inaishauri Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi pamoja na Mamlaka zingine zinazohusika na Ardhi kuhakikisha inaweka mipaka katika maeneo ya viwanja vyote vya ndege na kuvipa Hati Miliki. Vilevile kwa maeneo ambayo yanetwaliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kama vile Omukajunguti-Bukoba, malipo ya fidia kwa wananchi yafanyike haraka.

4.8.1 Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere; Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III)

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere kilianzishwa mwaka 1956 kikiwa na jengo moja tu la abiria na barabara moja ya kurukia ndege yenye urefu wa mita 2400. Hata hivyo kutokana na ongezeko la ndege na abiria, mwaka 1984, Serikali ilikamilisha jengo la pili la abiria likiwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni moja na nusu kwa mwaka. Jengo la tatu la abiria litakapokamiliika, Kiwanja hiki kitawezza kuhudumia abiria takribani milioni sita kwa mwaka kutoka abiria milioni mbili na laki tano wa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu mwezi Februari, 2014, ilijulishwa kuwa mradi huu kwa awamu ya kwanza unatarajiwa kugharimu Euro 133 milioni sawa na shilingi Bilioni 293 na awamu ya pili itagharimu Euro 235 milioni sawa na shilingi Bilioni 518. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka HSBC ya Uingereza kwa dhamana ya Serikali ya Uhlanzi na CRDB ya Tanzania. Aidha, ili kufanikisha mradi huu, Serikali kupitia Kamati ya Madeni ya Taifa tarehe 05 Julai 2012 ilitoa kibali cha kutekeleza mradi huu kwa njia ya mkopo. Hata hivyo, jambo la kushangaza ni kwamba, hadi Kamati inakutana na Wizara mwezi Mei, 2014, **HAZINA walikuwa hawajasaini mkataba wa makubaliano ya mkopo wa mradi huo. Inashangaza kuona kuwa Kamati ya Miundombinu imeshauri, Kamati ya Bajeti imeshauri na pia Mheshimiwa Rais wakati anaweka jiwe la msingi katika Kiwanja hiki aliagiza lishughulikiwe. Kamati inaiuliza Wizara ya Fedha, aseme nani ili mtekeleze wajibu wenu?**

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa hatua ya kuchukuwa mkopo katika benki za biashara na kuanza hatua za awali za ujenzi. Pamoja na jitihada hizi, Kamati inasikitishwa kuona kuwa katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga **shilingi bilioni 89** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika kiwanja cha Julius Nyerere. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 80** ni fedha za nje na **bilioni 9** ni fedha za ndani kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wa eneo la Kipunguni. Hadi kufikia mwezi Mei, 2014 fedha hizi ziliikuwa bado hazijatolewa. Kamati inashauri kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuanza kujenga jengo la tatu la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, itoe fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2013/2014. Aidha, ni vyema Serikali ikawa inatoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kwani kucheleweshwa kwa fedha hizo kunapunguza kasi ya maendeleo ambayo wananchi wanategemea kuyapata kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ni mwaka mmoja na nusu sasa tangu kiwanja cha Ndege cha Songwe kilipoanzishwa mnamo mwezi Desemba, 2012. Uwanja huu umerahisisha na kuongeza wigo wa safari za anga kwa wananchi wa Nyanda za Juu Kusini. Vilevile uwanja huu unatoa fursa kwa wakazi wa Mkoa wa Mbeya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

na Mikoa ya jirani kwani unawezesha kukuwa kwa uchumi. Kamati inashauri Serikali iendelee kukamilisha maeneo ya ujenzi yaliyobaki.

4.8.2 Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ulianza katika mwaka wa fedha 2012/2013. Kwa mujibu wa Mkataba wa Wajenzi mradi huu ilitakiwa ukamilike ndani ya muda wa miaka mitatu (miezi 36) kwa gharama ya **shilingi bilioni 105**. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ilitenga na kutoa **shilingi bilioni nane 8** tu, mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilitenga **shilingi bilioni nane 8** ambapo hadi Aprili, 2014 kiasi kilichotolewa ni **shilingi bilioni 1.6** tu. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kimetengewa **shilingi bilioni 12 tu**. Kamati inajuliza, Je mradi wa thamani ya **shilingi bilioni 105** utaisha ndani ya miaka mitatu katika utaratibu huu? Kamati inaitaka Serikali kutoa tamko rasmi kuhusu nia thabiti ya utekelezaji na muda wa kukamilisha mradi huu wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya ugunduzi gesi na ujenzi wa viwanda kama vile kiwanda cha Simenti Dangote katika Mkoa wa Mtwara, ni dhahiri ya kuwa umuhimu na mahitaji ya usafiri wa anga yataongezeka. Ni kwa kuzingatia umuhimu huo Kamati inashauri Serikali kukamilisha mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha ndege cha Mtwara. Vilevile Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu kuhusu mkakati mahsus wa kujenga na kuimarisha Kiwanja hiki.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi na kuhakikisha matokeo yanaonekana kwa haraka ni vema Serikali iweke vipaumbele katika miradi michache na kuikamilisha kwa wakati kuliko kuwa na miradi mingi kwa wakati mmoja jambo linalosababisha miradi hiyo kutokamilika kwa wakati. Mwandishi mmoja wa vitabu anayeitwa Steven Convey aliyahi kusema, **Nanukuu “The key is not to prioritize what is on your schedule but to schedule your priority” mwisho wa kunukuu** kwa tafsiri isiyo rasmi alisema “La msingi si kuweka vipaumbele katika ratiba yako bali ni kuratibu vipaumbele hivyo”.

4.10 Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii imepitia matatizo mengi sana. Kwa sasa Kampuni ina ndege moja tu (Das 8 Q300) na ndege nyingine moja ya kukodi (CRJ 200). Pia, Kampuni ya ATCL inadaiwa takribani **shilingi bilioni 133**. Makampuni mbalimbali duniani yameonesha nia ya kuwekeza ndani ya Kampuni ya ATCL, baadhi ya makampuni hayo ni Shirika la Ndege la Uturuki, Kampuni ya IVIC International ya China, Kampuni ya Emirates, Aghakan Development Foundation, Gaits ya Marekani na Kampuni ya Al Hayat ya Oman. Hata hivyo, kutokana na madeni inayodaiwa ATCL wawekezaji hao wamekuwa wakisita. **Mheshimiwa Spika, Kamati inauliza, je Serikali inatambua**

umuhimu wa Kampuni hii? Je bado tunaihitaji Kampuni hii? kama bado tunaihitaji Kampuni hii kwanini Serikali haitoi mtaji wa kutosha? Kamati inashauri Serikali iamue kuwekeza mtaji wa kutosha ili iweze kulipa madeni yote ya ATCL hatimae kuifufua upya Kampuni hii.

4.11 Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ina majukumu ya kusimamia vyombo vya usafiri wa nchi kavu na majini ambao unahusisha reli, barabara na bandari. Mamlaka hii pia inatoa leseni za usafirishaji kwa magari ya abiria yanayozingatia masharti ya usalama. Pamoja na kuwa na chombo hiki muhimu bado kumekuwa na ajali nyingi ambazo zinasababishwa na uzembe na kutokuwa uwezo kwa wanaoendesha vyombo vya usafiri.

Kamati inashauri SUMATRA, kwa kushirikiana na vyombo vingine kama vile Wizara ya Mambo ya Ndani- Jeshi la Polisi, Wizara ya Ujenzi kukaa pamoja na kujadiliana namna nzuri ambayo itaweza kupunguza matukio ya ajali nchini kwani yanaisababishia Serikali hasara kwa kupoteza nguvu kazi ya taifa. Pia kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mabasi hasa yaendayo vijijini kwani mengi yao ni mabovu jambo ambalo linahatarisha maisha ya wananchi waishio katika maeneo hayo.

Aidha, SUMATRA kwa kushirikiana na wadau wengine wa usalama barabarani iendelee kuratibu taratibu ambazo zitasaidia usafiri wa abiria kwa kutumia pipipiki kuwa usafiri wa uhakika na wenyewe usalama kwa wananchi.

Vilevile, Kamati inashauri SUMATRA kwa kushirikiana na jeshi la polisi kufanya udhibiti katika vyombo vidogo vya usafiri wa majini kama majahazi kwani imebainika kuwa baadhi ya vyombo hivi vimeduwa vikishiriki katika biashara haramu hasa madawa ya kulevya.

4. 12 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Mheshimiwa Spika, Majukukumu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa ni kuanzisha, kusimamia na kuendesha mtando wa vituo vya hali ya hewa nchini, kutoa utabiri wa hali ya hewa na tahadhari kuhusiana na hali mbaya ya hewa, kubadilishana taarifa za hali ya hewa na kutafiti kisayansi mabadiliko ya hali ya hewa na kubadilishana taarifa za hali ya hewa katika mtando wa dunia (GTS) kulingana na mabadiliko ya Kimataifa. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014, Mamlaka ya hali ya hewa nchini ilipanga kukamilisha ununuvi wa Rada, vifaa vya hali ya hewa na matayarisho ya ujenzi wa jengo la utabiri wa hali ya hewa (*Central Forecasting Office*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha ununuvi wa rada hiyo pamoja na kuandaa miundombinu yake ambapo inatarajiwa kuanza kazi rasmi mwezi Julai, 2014. Hata hivyo elimu na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tahadhari ziendelee kutolewa kwa wananchi wanaojenga karibu na eneo linalotarajiwa kuwekwa rada ili kuепusha migogoro pindi mtambo utakapoanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2012/2013 Mamlaka ya Hali ya Hewa ilitengewa shilingi bilioni 3.6, mwaka 2013/2014 **shilingi bilioni 4.0** na mwaka 2014/2015 **shilingi bilioni 5.6**. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za mamlaka hii mwaka hadi mwaka. Hali hii inadhihirisha kuwa Serikali imeanza kuona umuhimu wa Mamlaka hii hasa ukizingatia mabadiliko ya tabia nchi yanayojitokeza mara kwa mara na kuhitaji uchunguzi, utafiti na hata kutoa tahadhari kwa jamii. Hata hivyo, pamoja na kuongezea Mamlaka ya Hali ya Hewa fedha, mwenendo wa utoaji wa bajeti kwa Mamlaka hii sio wa kuridhisha kwani hadi kufikia mwezi April,2014, kati ya **shilingi bilioni 4** zilizokua zimeidhinishwa na Bunge ni **shilingi milioni 695** tu zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 17.4** ya fedha zote zilizokua zinatarajiwa. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha kwa wakati kwani pamoja na vipaumbele vingine, Mamlaka hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kilimo, usafiri wa anga na wa majini, pamoja na shughuli za kila siku za maisha ya watu.

5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 527,933,790,000/=**. Kati ya fedha hizo:-

(a) **Shilingi bilioni 93,306,391,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati yake **shilingi bilioni 33,027,291,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara na **shilingi bilioni 60,279,100,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

(b) Aidha, Wizara ya Uchukuzi imetengewa shilingi **bilioni 434,627,399,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 273,140,000,000/=** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 161,487,000,000/=** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kifungu kwa kifungu, na sasa inaliomba Bunge lako tukufu kuyajadili na kuyapitisha maombi ya Fedha kwa Wizara hii, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Aidha, nawashukuru pia Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, Mb; Naibu Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mb; Katibu Mkuu Dkt. Shaaban

Nakala ya Mtando (Online Document)

R. Mwinjaka, Naibu Katibu Mkuu Monica L. Mwamunyange, pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mhesimiwa Spika, naomba pia niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa kwa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha taarifa hii.

Mhesimiwa Spika, kwa heshima kubwa napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu kwa majina: -

1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya, MbM/ Mwenyekiti
3. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb Mjumbe
4. Mhe. Hussein Mussa Mzee, Mb Mjumbe
5. Mhe. Zarina Shamte Madabida, Mb "
6. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb "
7. Mhe. Rebecca Michael Ngodo, Mb "
8. Mhe. Aliko Nikusuma Kibona, Mb "
9. Mhe. Eng. Ramo M. Makani, Mb "
10. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb "
11. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb "
12. Mhe. Mussa Haji Kombo, Mb "
13. Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura, Mb "
14. Mhe. Abdul Rajab Mteketa, Mb "
15. Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga, Mb "
16. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb "
17. Mhe. Said Amour Arfi, Mb "
18. Mhe. Horoub Mohamed Shamis, Mb "
19. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb "

Mhesimiwa Spika, mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashillilah, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Vilevile Katibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John na Ndugu Francisca Haule kwa kuihudumia Kamati. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhesimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha na ninaunga mkono Hoja.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Peter Joseph Serukamba, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU

24 Mei 2014

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, kwa kupitia maoni ya Kamati, kuhusiana na Wizara ya Uchukuzi na Bajeti ambayo imewasilishwa hapa na Mheshimiwa Waziri Mwakyembe. Sasa naomba nimuite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye eneo hili. Naona anakuja hapa Waziri Kivuli mpya kabisa, Mheshimiwa Machali. (Makofij)

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyosomwa Bungeni

MHE. MOSES J. MACHALI - MSEMAMI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Uchukuzi, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kusimama mahali hapa siku hii ya leo kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati viongozi wangu wa vyama CHADEMA, NCCR Mageuzi na CUF, kwa kuona umuhimu wa kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani ya pamoja Bungeni. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa shukrani za pekee kwa Kiongozi wetu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe kwa kunitfea kuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Uchukuzi. Ni imani yangu ushirikiano huu utakuwa wa kudumu na wale wote wenye hila na chuki za ushirikiano huu, watashindwa na kulegea na kutuachia nafasi ya kufanya kazi kulikombua Taifa na majanga yaliyolikumba Taifa letu kwa miaka 50 iliyopita. Kwa hiyo, nawashauri CCM wajiandae kisaikolojia kukubaliana na mabadiliko pindi tutakaposhika hatamu za kuongoza taifa hili mapema mwaka 2015. (Makofij)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Kasulu Mjini, Mkoani Kigoma ambao wanashirikiana nami bega kwa bega katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Kibunge ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa malengo mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa Wizara, Idara na Taasisi zake. Kwanza kabisa ni utekelezaji wa Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now - BRN Transport*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uchukuzi ilikusudia kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), kwenye maeneo ya bandari, reli ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2013 hatua iliyokuwa imetikiwa ilikuwa kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa kipindi cha mwaka 2013/2014, utendaji wa bandari kwa viashiria vya BRN, imeelezwa kwamba muda wa meli kukaa bandarini umepungua kutoka siku 7 za mwaka 2012 hadi siku 4.8 kwa mwaka wa fedha 2013 ilhali lengo ilikuwa ni siku 4.5. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba inawezekana kupunguza muda wa meli kukaa bandarini zikisubiri kupakuliwa shehena za mizigo hadi kwa kiwango cha chini kabisa cha siku mbili kama siku moja. Katika mazingira ya namna hiyo ni wazi Serikali ilikuwa ikifanya uzembe siku za nyuma kwa hiyo kuwasababishia wafanyabiashara kupata hasara kutokana na mizigo yao kuchelewa kupakuliwa katika bandari zetu na hasa bandari ya Dar es Salaam. Juhudi zinahitajika kuhakikisha ufanisi unakuwepo siku zote katika bandari zetu na hivyo kuiwezesha nchi yetu kujipatia fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeeleza kwamba tani 13.7 milioni za shehena za mizigo zilizohudumiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba kiasi hicho ni kidogo ikilinganishwa na eneo la bandari yetu na pia kiasi hicho kinapungua kwa sababu nchi kama Rwanda na Uganda zinatukimbia kutokana na ukiritimba uliokithiri katika bandari yetu. Kama huduma zingekuwa zinatolewa kama inavyotakiwa ni wazi bandari yetu ingeweza kupakua mzigoto mkubwa kuliko huo unaotajwa na kupigiwa chapuo na Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado ina mtazamo kwamba bandari zetu hazijaweza kutumika vizuri kutokana na tatizo la uzembe na urasimu katika kushugulikia mizigo ya wafanyabiashara wanaopitisha mizigo yao kwenye bandari zetu. Inasikitisha sana kuona Serikali ikitumia fedha nyingi kwenda katika maeneo mbalimblai duniani kujifunza juu ya mafanikio ya wenzetu kuhusu sekta ya bandari halafu hakuna hatua za

Nakala ya Mtando (Online Document)

haraka zinazochukuliwa ili kuhakikisha sekta ya bandari inafanya vizuri katika kuimarisha mapato ya nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nyakati tofauti utasikia kwamba Waziri na Watendaji fulani fulani pamoja na Wabunge wamefanya ziara za mafunzo huko Singapore, Hong Kong, Uholanzi na kwingineko duniani lakini ujuzi na maarifa yaliyopatikana huko hayaonekani kuzaa matunda jambo linalotia shaka kama Mawaziri na Watendaji wanaofanya ziara mbalimbali wana nia njema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufisadi katika ujenzi wa gati ndani ya Ziwa Tanganyika. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Bandari Tanzania mnamo tarehe 20 Novemba, 2009, iliingia makubaliano na Kampuni ya MODSPAN ENTERISES Ltd, kusanifu na kujenga gati katika Ziwa Tanganyika kwenye maeneo ya Lagosa, Kyala, Karema, Kirando kwa gharama ya shilingi bilioni 4.870 ikijumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani. CAG anasema kwamba, naomba kunukuu.

“Kumbumbu zilizokaguliwa ni kwamba mkataba huu ulikuwa ni wa miezi 18, ulioratibiwa na kutakiwa kukoma mwezi Julai, 2011. Mapitio ya utekelezaji wa mkataba huu, yaligundua kwamba, mkandarasi ambaye ni MODSPAN ENTERISES Ltd hakusimamia mradi vizuri kitu ambacho kimesababisha mkandarasi kutumia muda mrefu na matokeo yake kuongezeka kwa gharama za manunuzi bila ya sababu. Pamoja na mapungufu yote hayo, Menejimenti ilitoa nyongeza ya kazi kwa mkandarasi kwa kiasi cha shilingi milioni 647.865, hivyo kusababisha gharama za mradi huu kuongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 5.518 kutoka gharama za awali za shilingi bilioni 4.870. Hadi kufikia kipindi nilichokuwa ninakamilisha Ukaguzi huu, jumla ya shilingi bilioni 3.127, sawa na asilimia 56.6 ya jumla ya gharama za mradi zilishalipwa kwa mkandarasi ambapo sehemu ya kazi iliyokuwa imekamilika ilikuwa asilimia 34 tu”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari Tanzania na Malipo yasiyo na Tija kwa Mamlaka yenyewe. Mamlaka ya Bandari Tanzania inatajwa kuwa mwezi Novemba, 2008, iliingia mkataba na Kampuni ya OCEANA ADVANCED INDUSTRIES Ltd wa kukarabati eneo la meli kutia nanga katika Iango Namba 1 - 11, na kituo cha kupakulia mafuta cha Kurasini katika bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa CAG, makubaliano ya gharama za mkataba huu, zilikuwa shilingi bilioni 4.634 bila Kodi ya Ongezeko la Thamani ambapo ukarabati huu ulikuwa ukamilike kufikia tarehe 11 Mei, 2009. Mapitio yaliyofanyika katika mkataba huo, ilibainika kuwa mradi haukamilika kwa muda

Nakala ya Mtando (Online Document)

ulipangwa na hivyo kulazimu nyongeza ya miezi nne hadi Agosti, 2009. Yote hayo yalitokana na Menejimenti ya bandari kushindwa kumkabidhi mkandarasi eneo husika la kazi kama walivyokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushindwa kutekelezwa kwa mkataba huo, kulisababisha kuibuka kwa kazi za ziada zilizogharimu kiasi cha dola za Kimarekani 753,807.60. Baadaye mnamo tarehe 15 Mei, 2010, Mamlaka ya Bandari Tanzania iliamua kusitisha mkataba wake na Oceana Advance Ltd, kwa kisingizio kwamba kulikuwa na msongamano wa meli katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo isingeweza kuendelea na kupelekea kuilazimu Mamlaka kumliipa mkandarasi kiasi cha shilingi bilioni 1.657 zikiwa ni gharama za fidia kwa vitendea kazi vyake kukaa muda mrefu bila kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mpaka tarehe 1 Julai, 2010, ni kiasi cha shilingi 641.844 kilichokuwa kimelipwa na kiasi cha shilingi milioni 955.388 kililipwa Aprili, 2011 miezi tisa baadaye baada ya majadiliano ya muda mrefu kumalizia malipo hayo. Hata hivyo, kutokana na malipo haya kutolipwa kwa wakati CAG anaeleza kwamba ilisababisha mkandarasi kutoza riba ya shilingi milioni 584.634 na hivyo hali hiyo ilisababisha Mamlaka ya Bandari kulipa kiasi cha shilingi bilioni 2.242 bila kunufaika kwa namna yoyote. Hii ni hasara kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu linawajibika kujuliza na kutafakari kwa kina juu ya ujisadi huu uliojitekeza ndani ya Mamlaka ya Bandari Tanzania. Ujisadi wa kutumia fedha nyingi kwa miradi muhimu halafu miradi haikamiliki lakini fedha zimelipwa na hivyo kulisababishia Taifa hasara kubwa na kuendelea kuwabebesha walipakodi wa Tanzania mzigo mkubwa wa kugharamia miradi ambayo haikutekelezwa kutokana na uzembe wa watu wachache Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wale wote waliosababisha hasara ya mabilioni haya ya shilingi kupotea. Kama hakuna hatua zozote zilizochukuliwa, ni kwa nini Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania haijawajibishwa kutokana na madudu haya. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uchukuzi na ujisadi wa matumizi mabaya ya madaraka. Taarifa ya CAG ya mwaka 2012/2013 imebainisha na kudhihirisha kwamba kuna matumizi mabaya ya madaraka ndani ya Wizara ya Uchukuzi unaosababisha matumizi mabaya ya fedha za umma. Hali hiyo inajitokeza ukurasa wa 100 -101 wa taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma ambapo Wizara ya Uchukuzi imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kwa Mamlaka ya Bandari ikiagiza kufanya matumizi kwa ajili hiyo kinyume na taratibu za utawala bora.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka unaoishia Juni 2013, CAG alibaini kuwa kiasi cha shilingi milioni 44.320 zililipwa na Mamlaka kwa niaba ya Wizara hiyo. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 18.156 kililipwa kwa ajili ya kugharamia safari za Naibu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Wizara ya Uchukuzi kwenda Ghana kwa safari ya kikazi. Mamlaka ya Bandari TPA ilipata mwaliko wa watu wanne kuhudhuria maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Afrika yaliyofanyika Accra Ghana kuanzia tarehe 16 – 23 Juni 2013. Mamlaka ilimteua Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu kuiwakilisha Bandari na Wizara ikamteua Naibu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu ili kuiwakilisha Wizara katika maadhimisho hayo. Gharama za washiriki wote wawili ziligharamiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya CAG inaendelea kubainisha kwamba jumla ya shilingi milioni 15 zililipwa kwa Wizara ya Uchukuzi tarehe 25 Machi, 2013 kwa ajili ya Baraza la Wafanyakazi liliyofanyika tarehe 25 Aprili, 2013. Maagizo ya kulipa yalitolewa kupitia barua yenye kumbukumbu namba ambayo inatajwa hapa ya tarehe 25 Machi, 2013. Kwa maoni ya CAG malipo kama haya ya Baraza la Wafanyakazi wa Wizara yanatakiwa yalipwe kwa kutumia fedha za Wizara na siyo fedha za Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tarehe 16 Aprili, 2013, Wizara iliandika barua nyininge yenye kumbukumbu namba inayotajwa hapa ikiagiza Mamlaka ya Bandari kulipa posho kwa ajili ya Afisa atakayehudhuria kikao cha Kamati ya Ufundji juu ya fedha na uhamasishaji wa rasilimali kilichoendeshwa na ISCOS (Intergovernmental Standing Committee on Shipping).

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, bali pia mnamo tarehe 14 Machi, 2013, Wizara ya Uchukuzi iliandika barua yenye kumbukumbu namba inayotajwa iliyoomba Mamlaka ya Bandari ilipe gharama ya kiasi cha shilingi milioni 11.164 katika hoteli ya New Africa kwa ajili ya Naibu Waziri wa Uchukuzi. Malipo haya yalilipwa na Bandari tarehe 28 Machi, 2013. Hata hivyo, taarifa haijaaeleza fedha hizo zililipwa kwa ajili ya shughuli gani zilizokuwa zikitekelezwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi na shughuli hizo hazieleweki zilikuwa na maslahi gani mapana kwa umma wa Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, CAG anaeleza kwamba kitendo cha Wizara mama kuingilia masuala ya kifedha kwa Mashirika ya Umma na Taasisi nyininge za umma kinaathiri uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi kwenye masuala ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Meli ya MV Liemba ndani ya Ziwa Tanganyika, Mkoani Kigoma. Hali ya meli ya Mv Liemba ya Kigoma inayofanya safari zake katika Ziwa Tanganyika kwa mujibu wa maelezo ya watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa Mkoa ni kwamba hali ya meli hiyo ni mbaya

Nakala ya Mtando (Online Document)

kiasi kwamba inahatarisha maisha ya watumiaji wanaotumia meli hiyo. Meli hiyo mara kadhaa imekuwa inazima injini yake ikiwa safarini ndani ya Ziwa Tanganyika na hivyo kulazimika mafundi kuingia chumba cha injini kuifanya marekebisho ikiwa majini. Hii ni hali ya hatari sana kwa maisha ya watu wetu wanaotumia usafiri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna taarifa kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa inafikiria kusimamisha meli hiyo isifanye safari ili kuepusha vifo kama ilivyokuwa kwa MV Bukoba. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Uchukuzi alikwishatoa ahadi kuwa meli hiyo itakarabatiwa au kununua nyingine lakini hadi leo hakuna kilichofanyika au hata kiungwana kuwaambia wadau wa meli hiyo nini kinachoendelea. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu na wananchi wanaotegemea usafiri wa meli hiyo ni lini meli nyingine itapatikana au ni lini meli hiyo itakarabatiwa ili kuepusha madhara ya vifo mionganoni mwa wasafiri na mizigo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhujumu uchumi katika kampuni ya Marine Service Company Limited. Licha ya upungufu mwingi wa kiuongozi na kiutendaji katika Kampuni ya Marine Service Company Limited, kumekuwa na uhujumu uchumi katika kampuni hiyo kwa kughushi tiketi za meli jambo ambalo linaikosessa Serikali mapato. Hapa ninazo tiketi feki za kampuni hiyo na nitaomba Waziri wa uchukuzi azitolee maelezo wakati akifanya majumuisho kama ni mpango wa Serikali kulea tabia. Serikali imekuwa ikipoteza mapato kwa sababu ya kulea ujisadi wa wachache na kuanza kusema ooh, Sungura mdogo, Sungura mdogo! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze ni kwa nini inalea madudu haya na kuanza kulialia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Bodaboda nchini Tanzania. Katika kipindi cha mwaka wa 2013/2014 na hata katika mijadala ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 katika vikao mbalimbali vya mukutano huu wa 15 wa Bunge, Wabunge wa Majimbo mbalimbali wameeleza malalamiko juu ya madhira wanayofanyiwa vijana walioajiriwa kwa kuendesha pikipiki maarufu kama Bodaboda. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tarehe 23 Mei, 2014, gazeti la Tanzania Daima limechapisha habari yenye kichwa cha habari 'Giza nene faini za Bodaboda' ambayo imeeleza madai ya kuwepo kwa makusanyo na matumizi yasiyoeleweka ya faini zinazokusanywa kwa Bodaboda zinazodaiwa kuingia katika Jiji la Dar es Salaam kinyume na agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uchukuzi ndiyo yenyewe dhamana ya kusimamia sekta ya usafirishaji, hivyo Waziri wa Uchukuzi anapaswa katika majumuisho kutoa majibu ya maswali ambayo Wabunge mbalimbali wamehoji na kutoa maelezo juu ya masuala yaliyoibuliwa kuhusu malalamiko ya unyanyasaji unaofanywa kwa vijana wa Bodaboda na madai ya ujisadi unaoendelea juu ya faini zinazokusanya kutoka kwa vijana hao wanaofanya biashara ya kutoa huduma kwa wananchi na pia watumiaji wengine wa kawaida wa usafiri wa pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya reli nchini. Miradi ya miundombinu ya reli chini ya RAHCO. Kwa mujibu wa Wizara ya Uchukuzi ni kwamba RAHCO inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 32 kwa ajili ya matengenezo ya Reli ya Kati na miradi mingine ya reli iliyo chini ya Wizara hiyo inayopaswa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 kama ifuatavyo: Utandikaji wa reli nzito kutoka Kitaraka hadi Malongwe, ujenzi wa madaraja, ujenzi wa kituo cha kuhifadhi makasha cha Mwanza, ukarabati wa tuta la Reli ya Kati ya Kaliua - Mpanda katika eneo la mto Ugara na ukarabati wa daraja lake. Kazi ya usanifu wa kina wa Reli ya Kati Tanga hadi Arusha na upembuzi yakinifu wa Reli ya Arusha Musoma, kazi ya usanifu wa Reli ya Kati Isaka - Mwanza inaendelea pamoja na kazi ya kuboresha njia ya reli kwa ajili ya usafiri wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa deni hilo ni wazi Serikali haijali usafari wa reli nchini na dhamira siyo ile ya kuhakikisha usafiri wa reli ukiimariika kama ilivyokusudiwa, kwani ni ajabu sana Serikali makini kuchelewesha malipo ya kiasi hicho cha fedha. Ni wazi hata utengenezaji wake huenda umekuwa wa kusuasua. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ijipime na kujitafakari upya na kisha kuueleza umma wa Watanzania iwapo ina nia ya kuimarisha usafiri wa reli nchini. Shilingi bilioni 32 ya uimarishaji wa reli ni fedha kidogo sana kwa Serikali iliyo makini. Haiingii akilini kusikia wala kuona kwamba Serikali imekosa kiasi hicho cha fedha kwa wakati iwapo kweli inathamini usafiri huo ulio rahisi katika usafirishaji wa shehena za mizigo na abiria. Haya ni maajabu ya dunia na hakuna namna ya kuweza kumshawishi mtu ye yeyote mzima na makini katika kupanga vipaumbele vya miradi ya maendeleo. Haiingii akilini na kamwe hakuna mtu mwenye akili timamu anayeweza kushawishiwa kiurahisi kuhusu suala hilo na inaweza kuwa haki kwa mtu ye yeyote makini kuendelea kuamini kwamba Serikali hii ya CCM kuitia Wizara ya Uchukuzi iliyowekwa mfukoni na wafanyabiashara wa usafirishaji wanaotumia malori kusafirisha mizigo ili waendelee kufanya biashara ya kujipatia fedha huku Serikali ikikosa mapato ambayo yanepatikana kuitia usafirishaji kwa njia ya reli ilihali Watanzania wengi hasa wa Mikoa ya Tabora, Kigoma, Mwanza, Shinyanga na kwingineko wakiumia sana kutokana na usafiri wa reli kuwa wa kusuasua.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na miradi ya uboreshaji wa reli nchini inayoratibiwa na Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilikusudia kuimarisha huduma za reli nchini chini ya TRL kwa kufanya shughuli zifuatazo: Kufanya matengenezo na ukarabati wa mabehewa na vichwa vya treni ambapo mikataba kwa ajili ya matengenezao na ukarabati wa vichwa na mabehewa ya treni ilisainiwa kati ya mwezi Aprili na Juni 2013. Malipo ya awali ili kuwawezesha wazalishaji kuanza kazi yalihitaji kiasi cha shilingi bilioni 124.5. Kwa mujibu wa taarifa za utekelezaji wa mipango ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni kwamba hadi sasa ni kiasi cha shilingi bilioni 67.69 zilizopelekwa na hivyo kuendelea kudaiwa kwa mujibu wa mikataba kiasi cha shilingi bilioni 75.435. Tayari kichwa kimoja cha treni kutoka Karakana ya Morogoro kimeshakamilika na vichwa vingine viwili vinatarajiwa kukamilika hivi karibuni. Jumla ya vichwa nane vilipangwa kutengenezwa upya katika Karakana ya Morogoro mwaka 2013/2014. Huu ni mwendelezo uleule wa Serikali kutojali usafiri wa njia ya reli na hivyo kuwasababishia wananchi usumbufu mkubwa sana katika kusafirisha shehena za mizigo na abiria kwa ujumla wake hususani wale wa Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Tabora, Singida na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka na kuishauri Serikali kuacha uzembe katika kutekeleza mipango iliyojiwekea kwa sababu hata kiasi cha shilingi bilioni 143.124 kilichotengwa kwa ajili ya usafiri wa reli nchini bado ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na mahitaji ya sekta hiyo ya usafirishaji lakini bado Serikali imeendelea na tabia ya kutokutoa fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya TRL. Huo ni mzaha na mwendelezo uleule wa kutenga bajeti za kiini macho pasipo kutekeleza mipango iliyoidhinishwa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mvutano wa TRL na RAHCO. Zipo taarifa za kuwepo kwa mvutano kati ya RAHCO na TRL wa kiutendaji. Mvutano huo unatajwa kusababisha ajali mbalimbali za treni zinazojitokeza hivi sasa. Kwa mfano, inaelezwa kwamba treni ya mizigo yenye namba B451 yenye injini namba 8906 iliyokuwa ikitokea Mkoani Morogoro kwenda Dodoma na kisha kuendelea na safari nyingine ilipata ajali na kuzama mtoni katika eneo la Gulwe Station mnamo tarehe 28 Machi, 2014, saa nane usiku na hivyo kusababishia TRL hasara ya injini na mabehewa matano. Sababu inayotajwa ya kusababisha ajali hiyo ni Serikali ya CCM kupitia Wizara ya Uchukuzi inayoongozwa na Dkt. Harrison George Mwakyembe kutokuwalipa Wakaguzi wa njia posho ya saa za ziada kazini. Aidha, taarifa zilizopo ni kwamba hakuna hatua zilizochukuliwa hadi sasa kutokana na tukio hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, ni kwa nini Serikali inawapuuza watumishi wa TRL na RAHCO kwa kutokuwalipa posho za stahiki zao mbalimbali kama vile mishahara na malimbikizo yao wanayostahili kulipwa? Ni lini haki za wafanyakazi hao zitalipwa kwa wakati ili kuliepusha taifa na hasara hii ya vichwa na mabehewa ya treni

Nakala ya Mtando (Online Document)

kupinduka na hivyo kusababisha fedha za walipa kodi kuendelea kutumika pasipo tija kwa Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, madereva hao wa garimoshi wanaeleza kwamba Waziri wa Uchukuzi Dkt. Harrison George Mwakyembe alielezwa matatizo haya lakini hajayatatua kama alivyowaahidi kati ya tarehe 8 na 9 Februari, 2013 alipokutana nao. Wafanyakazi hao wanaskitishwa na kitendo hicho cha Waziri wa Uchukuzi kuwaahidi uwongo na sasa amekuwa kimya kiasi cha kuwatia mashaka. Aidha, wanaeleza kwamba imefikia mahali wanadai wamechoshwa na ahadi za uwongo na kamwe isitarajiwe kuona tija katika kuliendesha Shirika la Reli nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge inataika Serikali ieleze ni lini itaacha tabia hii mbaya na chafu ya kuwahadaa watumishi hawa wanaofanya kazi ngumu hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo haya yanawakuta hata watumishi wengine wa Shirika la Reli nchini wanaoeleza kwamba Serikali imewadhulumu malimbikizo ya mishahara yao ya miezi sita yaani Julai hadi Desemba 2013. Serikali iliongeza mishahara yao mwaka 2013/2014 lakini watumishi hao wa TRL walikaa muda mrefu pasipo kubadilishiwa mishahara yao hadi ilipofika mwezi Aprili, 2014 ambapo walilipwa na arreas za kuanzia mwezi Januari hadi Mei 2014 tu na kuambiwa kwamba zile za mwezi Julai hadi Desemba mwaka 2013 hazipo na kwamba wawe wapole.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi jambo hili linawezekanaje? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza malipo ya malimbikizo haya ya mishahara ya watumishi wa TRL yatalipwa lini? Kutokuwalipa itakuwa ni wizi wa mchana kweupe na kwa kweli itampasa Waziri wa Uchukuzi kuwajibika kwa mambo haya kama siyo Serikali nzima ya CCM kuwajibika. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya Askari wanaofanya kazi Shirika la Reli nchini. Sekta ya Reli nchini ina Askari Polisi ambao wana jukumu la kuhakikisha usalama wa abiria, mizigo na mali za Shirika la Reli zikiwa katika hali ya usalama. Taarifa zilizopo zinaeleza kwamba Askari hao wananyanyasika sana kwa kutolipwa stahiki zao mbalimbali hususani posho za safari, posho za maji na umeme. Hali hiyo ni kikwazo na chukizo kwa Askari hao wanaofanya kazi katika mazingira magumu sana, ni wazi inawavunja moyo wa kuifanya kazi hiyo na wakati mwingine hali hiyo inaweza kuapelekea wahujumu mali za shirika hilo kama vile kuuza mafuta, vipuri vya mitambo mbalimbali na kadhalika kutokana na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Askari hawa wanaeleza kwamba tangu shirika hilo liondolewe mikononi mwa Wahindi waliokuwa wamebinafsishiwa mwaka 2012, Askari hawajalipwa posho za safari ambazo ni

Nakala ya Mtando (Online Document)

kati ya shilingi 20,000/= na 45,000/= kwa safari walizokuwa zamu. Posho za umeme na maji nazo ni tatizo kubwa kwa Askari wote wanaofanya kazi katika shirika hilo hasa wale wa Mikoa ya Kigoma, Tabora, Dodoma, Morogoro, Mwanza, Tanga na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tabia mbaya kwa Wizara kutoona umuhimu wa maisha ya Askari hawa na wafanyakazi wengine kutokwalipa stahiki zao lakini posho zao mabwana mkubwa wa Wizara hii wanajitengea na kujilipa huku wenzao wakibaki kulalamika na kupiga miyayo kibao. Huu ni usaliti mkubwa kwa Askari na watumishi wote wa Shirika la Reli wanaoidai Serikali posho mbalimbali, ni wazi matokeo yake ni hujuma dhidi ya shirika letu na hatuwezi kuendelea kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha inawalipa Askari hao na watumishi wote ili kulikoa Shirika hili ambalo liko taabani hivi sasa. Aidha, viongozi wote wa Wizara watambue kwamba ni aibu kwa sekta ya reli kushindwa kujilipa mishahara na posho mbalimbali wanazostahili watumishi kwa sababu iwapo lingeboreshwa kila kitu kingelipwa kwa kutumia mapato yanayotokana na usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, umilikishwaji haramu eneo la reli Mjini Arusha. Ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni. Katika hali ya kushangaza Serikali imediriki kumpatia mfanyabiashara mmoja Mjini Arusha eneo moja linalohusisha eneo la reli na hivyo kuwashangaza watu. Tunajiuliza na inawezekanaje kumpatia mtu eneo la reli kiasi kwamba treni haitaweza kupita? Waziri Mwakyembe na Naibu wake walishaelezwa juu ya suala hili na kwa hiyo kilichobaki ni kutupatia majibu kuhusu ni nini hatma ya reli ile na eneo lote kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ufisadi na uwongo kuhusu umiliki wa hisa katika Shirika la Usafiri Dar es Salaam, UDA. Itakumbukwa kwamba tarehe 15 Mei, 2014 katika kipindi cha maswali na majibu, Serikali kupitia Waziri wa Fedha ilijibui kwamba hisa za Serikali ndani ya shirika la UDA hazijauzwa. Mmiliki wa Shirika la UDA ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Msajili wa Hazina. Mgawanyo wa hisa halali ni kama ulivyosajiliwa kwa Msajili wa Makampuni kwa maana ya Halmashauri ya Jiji 51% na Serikali kupitia Msajili wa Hazina 49%. Hata hivyo, mara baada ya Serikali kutoa majibu hayo Bungeni Simon Group Ltd kupitia Mwenyekiti wake Mtendaji Robert Kisena ilifanya mkutano na Waandishi wa Habari na kueleza kwamba mgawanyo halali wa hisa za UDA ni Simon Group Ltd 76.79% na Msajili wa Hazina kwa maana ya Serikali 23.26%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba kuna mazingira ya kumuonea Bwana Simon Group. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuna nini nyuma ya pazia kiasi haitaki kuhakikisha mgogoro uliopo unakwisha kwa kurejea maagizo ya Kamati ya Bunge ya TAMISEMI iliyofanya kazi kubwa na kupata suluhisho la mgogoro huo. Inashangaza kuona na kusikia kampuni ya Simon Group Ltd ikilaumiwa wakati yenyewe iliuziwa hisa na Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia kimsingi ni kwamba Wizara ya Uchukuzi katika mwaka wa fedha 2014/2015 imetenga posho nyingi. Kwa mfano, kuna vifungu vya posho tu ambavyo ukijaribu kuangalia vina jumla ya shilingi bilioni 1,119,861,550. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano, katika Program 10 – Utawala, Subvote 1001 - Administration and HR Management, Kasma 221400. Katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara ilitenga kiasi cha shilingi 13,959,000/= kwa ajili ya Hospitality, Supplies and Services, ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Uchukuzi chini ya Dkt. Harrison George Mwakyembe, wamejiongezea fedha kiasi cha shilingi 91,641,000/=; na hivyo kuwa jumla ya shilingi 105,600,000/=, ambapo ongezeko hilo ni sawa na 86.7% au 87 %.

Kasma 410500 - Acquisition of Household and Institutional Equipment, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara ilitenga shilingi 18, 000, 000/=, ilihali mwaka 2014/2015 Wizara imetoka shilingi milioni 18 na kutenga shilingi 50, 000, 000/. Ongezeko la zaidi ya shilingi 32,000,000/=, sawa na ongezeko la 64 %.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, taarifa yangu ninaomba iingie kwenye Hansard kama ilivyo, kwa sababu nimeweza kufanya uchambuzi, Waheshimiwa Wabunge watapitia na wataweza kujadili baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu hivyo tu vina jumla ya kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni moja. Katika hali hiyo, nchi hii haiwezi kamwe ikaendelea haraka kwa sababu fedha nyingi zinaishia kwenye utafunaji, yaani kulipana posho na kadhalika. Hali hiyo ipo pia katika Wizara nyingine kwa kiasi cha kutisha.

Tabia hiyo ni mbaya na haiukubaliki hata kidogo. Tujiulize iwapo kila Wizara imetenga kiasi hicho cha shilingi bilioni moja na ushehe, ni wazi zaidi ya shilingi bilioni 50 zitatumika kwa mambo ambayo hayaleti tija kwa Taifa huku walipa kodi wa Taifa hili ambao ni maskini wakifa vijijini kwa kukosa dawa; Walimu na Watumishi wengine wakilipwa mishahara kiduchu, Watoto wakikosa vitabu na madawati shulenii, lakini Mawaziri na Watendaji Wizarani wakitanua kama vile wako peponi. Aidha, bajeti maendeleo ya shilingi bilioni 549.664 zinazoombwa kwa ajili ya Miradi ya Mendeleo ni wazi bado ni ndogo sana ikilinganishwa na hali halisi ya Miradi inayopaswa kutekelezwa na Wizara hii hususan...

Nakala ya Mtando (Online Document)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MOSES J. MACHALI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaomba taarifa yangu iingie kwenye rekodi za Bunge kama ilivyowasilishwa. (Makofii)

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Uchukuzi kama ilivyowasilishwa Mezani

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, MHE. MOSES JOSEPH MACHALI (MB) KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
YA FEDHA ZA WIZARA YA UCHUKUZI KWA MWAKA
WA FEDHA 2014/2015**

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la 2013 naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mpango na makadirioya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Uchukuzi, napenda kutumia fursa hii kumshukuru mwenyezi mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kusimama mahali hapa siku ya leo kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati viongozi wangu wa vyama vya CHADEMA, NCCR-MAGEUZI na CUF kwa kuona umuhimu wa kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani ya pamoja Bungeni. Aidha natoa shukrani za pekee kwa Kiongozi wetu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni **Mhe.Freeman Aikaeli Mbowe(Mb)** kwa kunitfea kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Uchukuzi. Ni imani yangu ushirikiano huu utakuwa wa kudumu na wale wote wenye hila na chuki dhidi ya ushirikiano huu watashindwa na kulegea na kutuachia nafasi ya kufanya kazi kulikomboa taifa na majanga yaliyolikumba kwa miaka 50 iliyopita. Kwa hiyo nawashauri CCM wajiandae

Nakala ya Mtando (Online Document)

kisaikolojia kukubaliana na mabadiliko pindi tutakaposhika hatamu za kuongoza taifa hili mapema 2015.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashkuru wapiga kura wangu - wananchi wote wa jimbo la Kasulu Mjini Mkoani Kigoma ambao wanashirikiana na mimi bega kwa bega katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Kibunge ndani na nje ya Jimbo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi ni moja ya wizara nyeti katika kuleta mageuzi ya kiuchumi nchini. Miongoni mwa majukumu yanayoshughulikiwa na Wizara ni pamoja na: Uandaaji na usimamizi wa sera za usafiri na usafirishaji, Usafirishaji kwa njia za reli na bandari; Usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga na viwanja vya ndege (Vikubwa na vidogo); Utoaji wa leseni za usafirishaji; Usalama katika usafirishaji na hali ya hewa; Kuongeza tija katika utendaji kazi pamoja na kuendeleza raslimali watu na kusimamia Idara na taasisi zilizo chini ya wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya uchukuzi katika kutimiza majukumu yake ilijiwekea malengo mbalimbali kwa mwaka wafedha 2013/2014 kwa Idara na Taasisi zake, miongoni mwa malengo hayo ni pamoja na kutekeleza programu za utawala bora na uzuiaji wa Rushwa; Kusimamia utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa mteja; Kushirikiana na wadau mbalimbali kuweka mazingira mazuri ya kuhamasisha na kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika sekta za uchukuzi; Kuendelea kushirikiana na taasisi za kimataifa ili kuiwezesha Tanzania kutimiza viwango vya Kimataifa katika utoaji wa Huduma za uchukuzi na hali ya hewa; Kujenga uwezo wa Watumishi pamoja na kuboresha vyuo vya mafunzo ya kisekta; Kuendelea kufanya mapitio sheria na Mikataba ya uchukuzi ili kutoa huduma za uchukuzi katika viwango vya kimataifa; pamoja na Kuendelea kutekeleza awamu ya pili ya programu ya Uwekezaji katika sekta ya Uchukuzi (Transport Sector Investment Programme-**TPSIP II**).

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO MBALIMBALI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 KWA WIZARA, IDARA NA TAASISI ZAKE

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TEKELEZA KWA MATOKEO MAKUBWA SASA (Big Results Now-BRN Transport)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya uchukuzi ilikusudia kutekeleza Mpango wa Matokeo makubwa sasa yaani BRN kwenye maeneo ya bandari na reli ambapo hadi kufikia mwezi Desemba 2013, hatua iliyokuwa imefikiwa ilikuwa kama ifuatavyo:-

SEKTA YA BANDARI:

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa kipindi cha mwaka 2013/2014, utendaji wa Bandari kwa viashiria vya BRN imeelezwa kwamba Muda wa Meli kukaa Bandarini umepungua kutoka siku 7 za mwaka 2012 hadi siku 4.8 kwa mwaka 2013 ilihali lengo ilikuwa ni siku 5. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaaamini kwamba bado inawezekana kupunguza muda wa Meli kukaa Bandarini zikisubiri kupakuliwa kwa shehena za mizigo hadi kwa kiwango cha chini kabisa cha siku 2 kama siyo siku moja. Katika mazingira ya namna hiyo ni wazi serikali ilikuwa ikifanya uzembe siku za nyuma na hivyo kuwasababishia wafanyabiashara kupata hasara kutokana na mizigo yao kuchelewa kupakuliwa katika Bandari zetu na hasa bandari ya Dar es salaam. Aidha, bado kuna hali ya uzembe katika eneo la Makasha, kwa kuwa kwa mujibu wa Wizara ni kwamba lengo kwa mwaka 2013 ilikuwa ni siku 7 lakini Makasha bado yalikaa Bandarini kwa muda wa siku 9.3, muda ambaa ni nyuma kabisa ya lengo la mwaka 2012 ambalo ilikuwa ni siku 9. Katika hali hiyo ni wazi kuna uzembe katika eneo hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa na kususua kwa hali hiyo, na inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba muda au siku za kupakua makasha zinapungua hadi kiwango cha walau siku 2 hadi 3. Vifaa vya kisasa vitafutwe kwa ajili ya kurahisisha kazi Bandarini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeeleza kwamba Tani milioni 13.7 za shehena ya mizigo zilihuhudumiwa kwa kipindi cha mwaka 2013/2014. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kiasi hicho ni kidogo ikilinganishwa na eneo la Bandari yetu. Na pia kiasi hicho kinapungua kwa sababu nchi kama Rwanda na Uganda zinatukimbia kutokana na Ukiritimba uliokithiri katika bandari yetu. Kama huduma zingekuwa zinatolewa kama inavyotakiwa, ni wazi Bandari yetu ingeweza kupakua mizigo mkubwa kuliko huo unaotajwa na kupigiwa chapuo na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado ina mtazamo kwamba zetu hazijaweza kutumika vizuri kutokana na tatizo la uzembe na urasimu katika kushughulikia mizigo ya wafanyabiashara wanaopitisha mizigo yao kwenye bandari zetu. Inasikitisha sana kuona serikali ikitumia fedha nyingi kwenda katika maeneo mbalimbali duniani kujifunza juu ya mafanikio ya wenzetu kuhusu sekta ya bandari halafu hakuna hatua za haraka zinazochukuliwa ili kuhakikisha sekta ya bandari inafanya vizuri katika kuimarisha mapato ya nchi yetu. Kwa nyakati tofauti utasikia kwamba Waziri na watendaji fulanifulani pamoja na wabunge wamefanya ziara za mafunzo huko Singapore, Hongkong, Uhlanzi na kwingeneko duniani lakini ujuzi na marifa yaliyopatikana huko hayaonekani kuzaa matunda jambo linalotia shaka kama mawaziri, na watendaji wanaofanya ziara mbalimbali wama nia njema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, ni kwa nini hatuoni sekta ya bandari ikikua vizuri kama ilivyo katika nchi nyingine licha ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mafunzo na uzoefu tuanopata kutoka nchi nyinge?. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuacha mara moja tabia ya kutokutumia ujuzi na maarifa yanavyokuwa yamepatikana katika zile ziara zinazoitwa za mafunzo nje ya nchi ili kuiepusha nchi yetu kutumia fedha hovyo wakati bado nchi inakabiliwa na matatizo lukuki. Aidha Bunge lako tukufu linashauriwa kuitaka serikali iache kwenda nje ya nchi kufanya mafunzo tena juu ya maendeleo ya bandari na badala yake iwatake wale wote waliowahi kufanya ziara za mafunzo kukusanyika kwa pamoja na kutoa mrejesho juu ya yale waliyofunza kuhusu maendeleo ya sekta ya bandari na hatimaye tuweze kujitathmini ni kwa kiasi gani tuna watu wenyewe weledi wa kutosha kuhusu maendeleo ya bandari.

Mheshimiwa Spika, Binadamu aliyeelimika niyule anayetumia ujuzi na maarifa aliyyoyapata mahala popote pale na kwa ajili ya maendeleo ya jamii au nchi yake. Tujiulize, tangu watendaji wa Wizara ya uchukuzi wamefanya ziara za mafunzo bado hawajajua nini wafanye kwa ajili ya kuboresha sekta ya Bandari kiasi kila mwaka wanaendelea kutenga bajeti za mafunzo? Hilo halikubaliki nani wazi tabia hiyo ikiendelea kuachwa, Bunge hili litapaswa kulaumiwa na kulaaniwa na mtu ye yeyote mwenye akili timamu. Ni wakati sasa kwa Bunge lako tukufu kuitaka Wizara ya Uchukuzi itakiwe kutathminiwa juu ya mafunzo waliyokwishafanya ili kujua tatizo ni nini kiasi kwamba hali iendelee kuwa ya kusuasua.

UFISADI KATIKA UJENZI WA GATI KATIKA NDANI YA ZIWA TANGANYIKA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Bandari Tanzania, mnamo tarehe 20 November, 2009, iliingia makubaliano na Kampuni ya MODSPAN ENTERPRISES Ltd kusanifu na kujenga Gati katika Ziwa Tanganyika kwenye maeneo ya Logosa, Kyala, Karema na Kirando kwa gharama ya shilingi **billioni 4.870** ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani. CAG anasema kwamba, naomba kunukuu: "Kumbukumbu zilizokaguliwa ni kwamba Mkataba huu ulikuwa wa miezi kumi na nane (18) ulioratibiwa na kutakiwa kukoma mwezi Julai, 2011. Mapitio ya utekelezaji wa mkataba huu yaligundua kwamba mkandarasi ambaye ni MODSPAN ENTERPRISES LTD hakusimamia mradi vizuri kitu ambacho kimesababisha mkandarasi kutumia muda mrefu na matokeo yake kuongezeka kwa gharamaza manunuvi bila sababu. Pamoja na mapungufu yote hayo menejimenti ilitoa nyongeza ya kazi kwa mkandarasi kwa kiasi cha shilingi milioni 647.865 hivyo kusababisha gharama za mradi huu kuongezeka hadi kufikia shilingi 5.518 bilioni kutoka gharama za awali za shilingi **billioni 4.870**. Hadi kufikia kipindi nilichokuwa nakamilisha ukaguzi huu jumla ya shilingi bilioni 3.127 sawa na asilimia 56.6 ya jumla ya gharama za mradi zilishalipwa kwa mkandarasi ambapo sehemu ya kazi iliyokamilika ilikuwa asilimia 34 tu".

**MAMLAKA YA BANDARI TANZANIA NA MALIPO YASIYO NA TIJA KWA MAMLAKA
YENYEWE**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya bandari Tanzania inatajwa kuwa mwezi Novemba 2008 iliingia mkataba na kampuni ya OCEANA ADVANCED INDUSTRIES LTD wa kukarabati eneo la meli kutia nanga katika lango Na. 1- 11 na kituo cha kupakulia mafuta cha Kurasini katika Bandari ya Dar es Salaam. Kwa mujibu wa CAG Makubaliano ya gharama za mkataba huu zilikuwa **sh. Bilioni 4.634** bila kodi ya ongezeko la thamani ambapo ukarabati huu ultakiwa ukamilike kufikia tarehe 11 Mei, 2009. Mapitio yaliyofanyika katika mkataba huo ilibainika kuwa mradi haukukamilika kwa muda uliopangwa na hivyo kulazimu nyongeza ya miezi minne (4) hadi Agosti, 2009. Yote hayo yalitokana na menejimenti ya bandari kushindwa kumkabidhi mkandarasi eneo husika la kazi (GATI 7) kama walivyokubaliana. Kushindwa kutekelezwa kwa mkataba huo kulisababisha kuibuka kwa kazi za ziada zilizogharimu kiasi cha dola za kimarekani **753,807.60**. Baadaye mnamo tarehe 15 Mei, 2010, mamlaka ya Bandari Tanzania iliamua kusitisha mkataba wake na **Oceana Advanced Ltd** kwa kisingizio kwamba kulikuwa na msongamano wa meli katika bandari ya Dar es Slaam na hivyo kazi isingeweza kuendelea na kupelekea kuilazimu Mamlaka kumlipa mkandarasi kiasi cha shilingi **bilioni 1.657** zikiwa gharama za fidia kwa vitendea kazi vyake kukaa muda mrefu bila kufanya kazi. Hata hivyo mpaka kufikia tarehe 1 Julai 2010 ni kiasi cha shilingi **milioni 641.844** kilichokuwa kimelipwa na kiasi cha shilingi **milioni 955.338** kililipwa Aprili, 2011 miezi tisa baadaye, bada ya majadiliano ya muda mrefu ya kumalizia malipo ya mwisho. Hata hivyo kutokana na malipo hayo kutolipwa kwa wakati, CAG anaeleza kwamba ilisababisha mkandarasi kutoza riba ya shilingi milioni 584.634 na hivyo hali hiyo ilisababisha Mamlaka ya Bandari Tanzania kulipa kiasi cha Shilingi **bilioni 2.242** bila kunufaika kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, bunge lako tukufu lina wajibika kujiuliza na kutafakari kwa kina juu ya ufisadi huu uliojitokeza ndani ya Mamlaka ya Bandari Tanzania; ufisadi wa kutumia fedha nydingi kwa miradi muhimu halafu miradi haikamiliki lakini fedha zimelipwa na hivyo kulisababishia taifa hasara kubwa, na kuendelea kuwabebesha walipa kodi wa Tanzania mzigo mkubwa wa kugharamia miradi ambayo haikutekelezwa kutokana na uzembe wa watu wachache serikalini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni hatua gani zimechkuliwa dhidi ya wale wote waliosababisha hasara ya mabilioni haya ya shilingi kupotea. Na kama hakuna hatua zozote zilizochukuliwa ni kwa nini Bodi ya Wakurugenzi wa mamlaka ya Bandari Tanzania haijawajibishwa kutokana na madudu haya?

WIZARA YA UCHUKUZI NA UFISADI WA MATUMIZI MABAYA YA MADARAKA

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya CAG ya mwaka 2012/2013 imebainisha na kudhihirisha kwamba kuna matumizi mabaya ya madaraka ndani ya Wizara ya Uchukuzi unaosababisha matumizi mabaya ya fedha za umma. Hali hiyo inajitokeza Ukurasa wa 100 – 101 wa taarifa ya CAG Kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma ambapo Wizara ya Uchukuzi imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kwa Mamlaka ya Bandari ikiagiza kufanya matumizi kwa ajili ya Wizara hiyo kinyume na taratibu za utawala bora. Katika mwaka unoishia tarehe 30 Juni, 2013, CAG alibaini kuwa kiasi cha shilingi **milioni 44.320** zililipwa na Mamlaka kwa niaba ya Wizara hiyo. Aidha kiasi cha shilingi **milioni 18.156** kililipwa kwa ajili ya kugharimia safari ya Naibu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Wizara ya Uchukuzi ya kwenda Ghana kwa safari ya kikazi. Mamlaka ya Bandari (TPA) ilipata mwaliko wa watu wanne (4) kuhudhuria maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Afrika yaliyofanyika huko Acra Ghana kuanzia tarehe 16 hadi 23 Juni, 2013. Mamlaka ilimteua Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu kuiwakilisha Bandari na Wizara ikamteua Naibu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu ili kuiwakilisha Wizara katika maadhimisho hayo. Gharama za washiriki wote wawili ziligharamiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya CAG inaendelea kubainisha kwamba jumla ya shilingi milioni 15 zililipwa kwa Wizara ya Uchukuzi tarehe 25 Machi, 2013 kwa ajili ya Baraza la Wafanyakazi lilofanyika tarehe 25 Aprili, 2013. Maagizo ya kulipa yalitolewa kupitia barua yenyne Kumb.JA 230/553/01 ya tarehe 25 Machi, 2013. Kwa maoni ya CAG, malipo kama haya ya Baraza la Wafanyakazi wa Wizara yanatakiwa yalipwe kwa kutumia fedha za Wizara.Vilevile, tarehe 16 Aprili, 2013, wizara iliandika barua nyingine yenyne kumbukumbu Na. CB.94/436/01/69 ikiagiza Mamlaka ya Bandari kulipa posho kwa ajili ya afisa atakayehudhuria kikao cha kamati ya ufundi juu ya Fedha na Uhamasishaji wa Rasilimali kilichoendeshwa na ISCOS (*Intergovernmental Standing Committee on Shipping*).

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu bali pia mnamo tarehe 14 Machi, 2013, Wizara ya Uchukuzi iliandika barua yenyne kumb. Na. CB 230/364/01/A iliyoomba Mamlaka ya Bandari ilipe gharama ya kiasi cha shilingi milioni 11.164 katika Hoteli ya New Africa kwa ajili ya Naibu Waziri wa Uchukuzi. Malipo haya yalilipwa na bandari tarehe 28 Machi, 2013.Hata hivyo taarifa haijaaeleza fedha hizo zililipwa kwa ajili ya shughuli gani zilizokuwa zikitekelezwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi na shughuli hizo hazieleweki zilikuwa na maslahi gani mapana kwa umma wa Watanzania. CAG anaeleza kwamba kitendo cha wizara mama kuingilia masuala ya kifedha ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kunaathiri uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi kwenye masuala ya fedha.

UHAMISHAJI WATUMISHI KINYUME CHA TARATIBU KIASI CHA KUTIA MASHAKA MIONGONI MWA DATU

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa spika, ni aibu kwa Wizara inayoongozwa na Waziri msomi tena siyo msomi wa taaluma ya nyingine bali msomi wa taaluma ya sheria kukutwa na tatizo la kuhamisha watumishi kinyume cha sheria. Imetokea Watumishi kuhamishiwa Mamlaka ya Bandari Tanzania Kutoka Wakala wa Barabara Tanzania na Wizara ya Ujenzi bila Idhini ya Bodi ya Wakurugenzi jambo linalotia mashaka kwamba huenda kuna nia ovu na au ya kifisadi iliyokusudiwa kiasi cha kuifanya wizara kuvunja sheria za utumishi nchini. Kwa mujibu wa CAG ni kwamba sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 kifungu cha 31 na sheria ya mashirika ya umma kifungu cha 8(2) kinatamka kuwa watumishi wote wa mashirika amba ni wakala wa serikali katika utendajiwataongozwa kwa kuzingatia sheria zilizoanzisha taasisi husika. Katika taasisi hizo madaraka ya kuajiri wafanyakazi yamekasimiwa kwa Bodi za Wakurugenzi za mashirika na taasisi husika.

Maajabu ni kwamba CAG alibaini kuwa nafasi mbalimbali za kazi katika Mamlaka ya Bandari zilijazwa na Wizara ya Uchukuzi bila kupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi. Kwa mfano, wizara ilimuhamisha Mkadiriaji Majengo (Quantity Surveyor) kutoka Wizara ya uchukuzi kuwa mkuu wa kitengo cha usimamizi wa manunuvi katika Bandari ya Dar es Salaam. Afisa huyu hana sifa zinazotakiwa jambo ambalo ni kinyume na kifungu cha 34 (4) cha Sheria ya Manunuvi ya umma ya mwaka 2004 ambayo inahitaji mkuu wa kitengo cha manunuvi awe na taaluma ya ugavi na uzoefu wa shughuli za manunuvi. Wizara pia ilihamisha watumishi wengine wakiwamo wahandisi, maafisa ugavi, dereva na katibu mukhtasi.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa kanuni za utawala bora, wajibu wa kuajiri wafanyakazi katika mashirika ya umma ni wa Bodi ya Wakurugenzi. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka serikali kueleza ni kwa nini Wizara imekiuka matakwa ya kisheria kama imevyobainishwa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali? Je, kulikuwa na sababu gani za kufanya hivyo kama siyo mwendelezo wa kuandaa mianya ya kufanya ujisadi kwa maslahi ya watu wachache kupitia watu hao wanaotajwa kukosa sifa za kufanya kazi wasizostahili?

HALI YA MELI YA MV-LIEMBA NDANI YA ZIWA TANGANYIKA MKOANI KIGOMA

Mheshimiwa Spika, hali ya meli ya MV-Liemba ya Kigoma inayofanya safari zake katika Ziwa Tanganyika, kwa mujibu wa maelezo ya watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa Mkoa ni kwamba, hali ya meli hiyo ni mbaya kiasi kwamba ina hatarisha maisha ya watumiaji wanaotumia meli hiyo. Meli hiyo mara kadhaa imekuwa inazima injini yake ikiwa safarini ndani ya ziwa Tanganyika na hivyo kulazimika mafundi kuingia chumba cha injini kuifanya marekebisho ikiwa majini. Hii ni hali ya hatari sana kwa maisha ya watu wetu wanaotumia usafiri huo.

Mheshimiwa Spika, aidha kuna taarifa kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kigoma inafikiria kuisimamisha meli hiyo isifanye safari ili kuepusha vifo kama ilivyokuwa kwa Mv-Bukoba. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Uchukuzi alikwishatoa ahadi kuwa Meli hiyo itakarabaitiwa au kununua nyingine lakini hadi leo hakuna kilichofanyika au hata kiuungwana kuwaambia wadau wa meli hiyo nini kinacho endelea. Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu na wananchi wanaotegemea usafiri wa meli hiyo ni lini Meli nyingine itapatikana au ni lini meli hiyo itakarabatiwa ili kuepusha madahara ya vifo mionganoni mwa wasafiri na mizigo yao?

UHUJUMU UCHUMI KATIKA KAMPUNI YA MARINE SERVICES COMPANY LIMITED.

Mheshimiwa Spika, licha ya mapungufu mengi ya kiuongozi na kiutendaji katika Kampuni ya **Marine Services Company Limited**, kumekuwa na uhujumu uchumi katika Kampuni hiyo wa kughushi tiketi za meli jambo ambalo linaikosesho Serikali mapato. Hapa ninazo tiketi feki za Kampuni hiyo, na nitaomba Waziri wa Uchukuzi azitolee maelezo wakati akifanya majumuisho kama ni mpango wa Serikali kulea tabia hii. Serikali imekuwa ikipoteza mapato kwa sababu ya kulea ufisadi wa watu wachache na kuanza kusema oooh! Sungura mdogo sungura mdogo. Kambi rasmi ya upizani Bungeni inaitaka serikali ieleze ni kwa nini inalea madudu haya na kuanza kulia lia?

SUMATRA-KITUO KIKUU CHA MABASI-UBT

Mheshimiwa Spika; Wizara ya Uchukuzi ina wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali katika Sekta ya Usafirishaji. Aidha, katika kutekeleza wajibu huo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), Wizara ya Uchukuzi ina majukumu mahususi ambayo ni muhimu majibu yatolewe Bungeni juu ya utekelezaji wake katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika; majukumu hayo ni pamoja na: Kukuza ushindani na ufanisi katika soko la usafirishaji wa nchi kavu na majini; Kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma; Kuendeleza na kuhakikisha kuwa huduma za usafirishaji zinakidhi mahitaji ya watumiaji ikiwa ni pamoja na wenye kipato cha chini na wasiojiweza na kuboresha na kusimamia viwango vya usalama katika sekta zinazosimamiwa na kudhibitiwa na Mamlaka.

Mheshimiwa Spika; Kwa kuzingatia wajibu na majukumu hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu kutoka Waziri wa Uchukuzi kuhusu

Nakala ya Mtando (Online Document)

ilivyoshirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Halmashauri juu ya uboreshaji wa vituo vya kitaifa na kimataifa kwa ajili ya usafirishaji wa mabasi.

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia Waziri Kivuli wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilihoji kuhusu ufisadi na udhaifu uliopo katika Kituo kinachoitwa cha “Kimataifa” cha Ubungo. Hata hivyo, katika majumuisho mawaziri wenye dhamana katika Wizara tajwa hawakutoa majibu ya maana na mpaka sasa hatua hazijachukuliwa.

Mheshimiwa Spika; hivyo, kupitia mjadala wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka majibu kutoka kwa Waziri wa Uchukuzi ama Waziri Mkuu kuhusu masuala na maswali yafuatayo: Kituo Kikuu cha Mabasi Ubungo (UBT) kilifunguliwa rasmi tarehe 6 Desemba 1999 pamoja na mambo mengine uanzishwaji wa kituo hiki ulikuwa na dhumuni la kutoa huduma kwa wasafiri pamoja na watumiaji wengine kikiitwa kuwa ni cha Kimataifa. Kwa sasa kituo hicho ni aibu na adha ya kitaifa kwa kuwa hali ya uchafu ikiwemo utiririkaji wa maji machafu ndani ya Kituo cha Mabasi ambayo yanatuama na hadi kubadilika rangi na kuwa ya kijani ambapo ni hatarishi kwa abiria na watu wanaofanya shughuli zao ndani ya kituo. Pia, kuna vyoo vichache ukilinganisha na idadi ya abiria na watumiaji wengine wa Kituo. Hali hiyo inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko. Je, kwa hali hiyo Serikali bado itathubuti kulieleza Bunge kwamba Kituo hicho kina viwango vya Kimataifa?

Mheshimiwa Spika; Katika hatua ya sasa baada ya sehemu kubwa ya Kituo kubomolewa, huduma mbovu zilizopo na udhaifu mkubwa wa miundombinu bado fedha zinaendelea kutozwa milangoni katika mazingira yenyе mianya ya ufisadi; mapato hayo hayatumiki kuboresha vya kutosha huduma katika kituo. Waziri wa Uchukuzi ni muhimu katika majumuisho akaeleza iwapo yeye na SUMATRA wametembelea katika kituo hicho na kuridhika na hali ambayo ni adha kwa wasafiri na watumiaji wengine wa Kituo tajwa. Je, Serikali ipo tayari kutoa kauli bungeni ya kusitisha kutoza kiingilio katika Kituo hicho chenye huduma mbovu na badala yake mapato yaliyokusanywa mpaka hivi sasa yaongezewe na ya vyanzo vingine ili Kituo mbadala kijengwe au wala Kituo kilichopo kiboreshwe kwa haraka wananchi waweze kupata huduma zinazostahili?

Mheshimiwa Spika; aidha, Katika Kituo hiki kuna malalamiko pia ya mawakala wa mabasi juu ya utaratibu uliowekwa ya ‘Pasi za kupitia Getini’ (Gate Passes) unaodaiwa kupitishwa kinyemela kwa kuhusisha wamiliki wachache wa makampuni ya mabasi na hivyo kuibua usumbufu kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

makampuni pengine pamoja na kupunguza ajira za waliokuwa wakifanya kazi na makampuni hayo. Pia, utaratibu huu umekuwa kichaka cha ufisadi na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu wenye kuhusisha baadhi ya askari polisi, mgambo na watumishi wasio waaminifu katika mahakama ya Jiji. Je, Waziri wa Uchukuzi na SUMATRA na mawaziri wengine wenye dhamana wako tayari kufika katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo (UBT) kukutana na mawakala hao kusikiliza malalamiko yao na kuupatia ufumbuzi mgogoro unaoendelea?

Mheshimiwa Spika; Serikali iliulizwa Bungeni juu ya ufisadi na udhaifu katika Kituo hiki kuitia maswali ya kawaida kwenye mkutano wa Nne wa Bunge Kikao cha Ishirini na Sita Tare 15 Julai 2011 na majibu yaliyotolewa ni pamoja na ahadi ya kuwa "Mpango wa Serikali ni kukijenga upya kituo cha Mabasi kama ilivyoainishwa katika mpango wa biashara wa mwaka 2007". Ni kwanini ahadi hiyo haijatekelezwa mpaka hivi sasa hata baada ya Kituo kubomolewa, eneo lililochukuliwa na Mradi wa Mabasi ya Haraka (BRT) unaoratibiwa na wakala (DART) kujulikana na lini kituo hicho kitajengwa kama Serikali ilivyoahidi bungeni?

Mheshimiwa Spika; kwa upande mwingine Serikali kwa nyakati mwaka 2012 viongozi wa Serikali walinukuliwa wakitoa ahadi nyingine tofauti kwamba Kituo hicho kingehamishiwa katika eneo la Mbezi Luis kuanzia Januari 2013 kuitisha ujenzi unaoendelea wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka (DART) hata hivyo zaidi ya mwaka umepita bila ahadi hizo kutekelezwa. Hata hivyo, ahadi hiyo nayo mpaka sasa haijatekelezwa na haielekei kukumilika karibuni. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu ni lini hasa kituo hicho kipyta kitakamilika na ni kwanini katika kipindi hiki cha mpito isiboreshe huduma katika Kituo kilichopo cha Mabasi ya Mikoani cha Ubungo kuondoa adha na aibu iliyopo?

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze pia hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Ujenzi wa Kituo kingine ambacho iliahidi kingejengwa Bunju. Kwa upande mwingine, kwa ajili ya kuboresha huduma za mabasi ya kutoka Kusini mwa nchi, Serikali ieleze hatua iliyofikiwa katika kutekeleza ahadi ya muda mrefu ya kujenga Kituo eneo la Mbagala. Kwa sasa abiria kutoka Mikoa ya Kusini wanaotumia maeneo madogo na yasiyo vituo muafaka kama Tandika Sudan wanapata adha kubwa. Aidha, kwa kuwa na Vituo katika Nchi kuu mbalimbali za kuingia Jijini, Serikali itakuwa imechangia pia katika kupunguza msongamano uliopo hivi sasa.

BODA BODA:

Mheshimiwa Spika; Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 na hata katika mijadala ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 katika vikao mbalimbali vyta Mkutano huu wa Kumi Tano wa Bunge,

Nakala ya Mtando (Online Document)

wabunge wa majimbo mbalimbali wameeleza malalamiko huu ya madhila wanayofanyiwa vijana waliojiri kwa kuendesha pikipiki maarufu kama "Bodaboda". Aidha, Tarehe 23 Mei 2014 Gazeti la Tanzania Daima limechapisha habari yenye kichwa cha habari "Giza nene faini za bodaboda" ambayo imeeleza madai ya kuwepo kwa makusanyo na matumizi yasiyoeleweka ya faini zinazokusanywa kwa "Bodaboda" zinazodaiwa kuingia katikati ya Jiji la Dar Es Salaam kinyume na agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam.

Mheshimiwa Spika; Wizara ya Uchukuzi ndiyo yenye dhamana ya kusimamia Sekta ya Usafirishaji hivyo, Waziri wa Uchukuzi anapaswa katika majumuisho kutoa majibu ya maswali ambayo wabunge mbalimbali wamehoji na kutoa maelezo juu ya masuala yaliyoibuliwa kuhusu malalamiko ya unyanyasajji unaofanywa kwa vijana wa bodaboda na madai ya ujisadi unaoendelea juu ya faini zinazokusanywa kutoka kwa vijana hao wanaofanya biashara ya kutoa huduma kwa wananchi na pia watumiaji wengine wa kawaida wa usafiri wa pikipiki.

Mheshimiwa Spika; Wizara ya Uchukuzi ina wajibu wa moja kwa moja wa kufanya hivyo kwa kutoa taarifa bungeni namna ilivyosimamia Sheria inayohusika ambayo ni The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act; sheria namba 9 ya mwaka 2001. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Uchukuzi kueleza ni kipi katika Sheria hicho kinachoruhusu unyanyasajji kwa bodaboda pamoja na ujisadi katika faini zinazokusanywa kutoka kwa waendesha pikipiki Jijini Dar Es Salaam na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika; Wizara ya Uchukuzi inapaswa kuzingatia kwamba sheria hiyo kifungu cha 5 kimetamka kwamba wajibu wa Mamlaka ya Udhhibit wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ni pamoja na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma na kuhamasisha upatikanaji wa huduma ikiwemo kwa wateja wa kipato cha chini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali inayoongozwa na CCM ieleze iwapo unyanyasajji unaofanywa kwa waendesha bodaboda na ujisadi katika faini ndio utekelezaji wa masharti ya kifungu hicho cha Sheria?

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge inaitaka Wizara ya Uchukuzi kutoa maelezo juu ya sababu halisi za Serikali kupitia Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam Said Mecky Sadiq kutoa agizo la usafiri pikipiki/bajaj kuishia Buguruni, Ubungo, Tazara na Chuo cha Uhasibu na hivyo kuibua mgogoro unaoendelea mpaka hivi sasa na kutoa mwanya pia wa ujisadi katika faini zinazokusanywa. Aidha, Serikali haijazuia tu bodaboda za kibiashara bali pia hata watumiaji mbalimbali wa pikipiki wenye ofisi zao katikati ya Jiji ambao sasa wanapaswa kuingia mjini kwa vibali maalum vinavyolipiwa kwa mwaka kwa gharama kubwa kuliko hata za kuegesha magari ya mjini. Maelezo hayo ni muhimu kwa kuzingatia kwamba usafiri wa pikipiki/bodaboda na bajaj sio tu

Nakala ya Mtando (Online Document)

umetoa fursa ya ajira kwa vijana bali pia unasaidia wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika: Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba vifungu vya 6, 38 na 39 vya Sheria ya SUMATRA vimetoa fursa ya mamlaka zinazohusika kuweza kutunga Kanuni mbalimbali. Aidha, katika kutekeleza matakwa ya Sheria hiyo no. 9 ya mwaka 2001 mwaka 2010 kulitungwa Kanuni za Transport Licensing (Motor Cycles and Tricycles) ambazo zilichapwa katika gazeti la Serikali namba 144 la tarehe 2 Aprili 2010.

Kanuni hizo zilizosainiwa na aliyekuwa Waziri wa Miundombinu Wizara ambayo ilikuwa na dhamana ya uchukuzi hazikutoa maagizo ya kukataza bajaj/bodaboda kama ambavyo Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam anavyotoa kauli. Aidha, Serikali inatumia nguvu kubwa kusimamia kamata kamata ya pipipiki/bodaboda na bajaj kwa madai ya kwamba anasimamia Sheria wakati suala hilo likiwa halijatajwa kwenye Sheria lakini wakati huo huo akishindwa kusimamia sheria nyingine nyingi kwenye sekta ya usafirishaji katika masuala ambayo yapo chini ya mamlaka yake.

Hali hii inaleta hisia mionganini watumiaji, waendeshaji na wamiliki wa pipipiki/bodaboda na bajaj kwamba pengine zipo sababu nyingine za ziada ambazo Waziri wa Uchukuzi anapaswa kuzieleza wazi bungeni kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika: Kambi Rasmi ya Upinzani imepitia Kanuni hizo katika vipengele cha 13 na 14 ambavyo vimetoa mamlaka kwa Halmashauri za Serikali za Mitaa kuweza kutenga maeneo ya vituo vya pipipiki/bodaboda na bajaj na pia mipaka ya maeneo ambayo vyombo hivyo vya usafiri vinaweza kutoa huduma.

Kambi Rasmi ya Upinzani imewasiliana na baadhi ya wabunge wa Dar Es Salaam na wameeleza kwamba katika kipindi cha tangu kutungwa kwa Kanuni hizo, hakuna vikao vya mabaraza ya madiwani (Full Council) ya Halmashauri za Jiji la Dar Es Salaam na Manispaa zake za Kinondoni, Ilala na Temeke viliviyokaa na kutunga Kanuni zenye kuruhusu unyanyasaji kwa bodaboda na ufisadi wa faini zinazotozwa kwa waendesha pipipiki.

Mheshimiwa Spika: hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Wizara ya Uchukuzi kuwasilisha bungeni ushahidi wa nyaraka zote za kisheria za vikao vyote vya Wizara za Serikali, SUMATRA na Halmashauri zote za Jiji viliviyotunga Kanuni kwamba ni marufuku kwa pipipiki/bodaboda na bajaj kuvuka zaidi ya Ubungo, Buguruni, Tazara na Chuo cha Uhasibu (Temeke) kwa madai ya kwamba maeneo ya zaidi ya mipaka hiyo ni katikati ya Jiji (Central Business District- CBD). Aidha, ni hatua gani Wizara zote zenye dhamana

Nakala ya Mtando (Online Document)

zimechukua juu ya malalamiko ya unyanyasaji wa bodaboda na madai ya ufisadi yaliyotolewa, na kutoa majibu bungeni juu ya maswali yafuatayo:-

Ni kwa nini faini zinatozwa na Halmashauri ya Jiji kwa stakabadhi za zamani za mwaka 2012 na faini hizo zinaingia katika Mfuko gani na je, SUMATRA imeridhia viwango hivyo na utaratibu huo?

Je, Mahakama ya Jiji ya Hakimu Mkazi Sokoine Drive imepewa na nani stakabadhi hizo na ni kwanini yawepo madai ya kwamba watuhumiwa na wahukumiwa hulipishwa viwango vya juu vya faini tofauti na viwango vinavyoandikwa katika risiti?

Je, ni wakina nani kwa majina wanaodaiwa kufanya unyanyasaji na ufisadi huo kwa bodaboda na kwa waendesa pikipiki na wamechukuliwa hatua gani mpaka hivi sasa na Mamlaka zinazohusika?

SEKTA YA RELI

MIRADI YA MIUNDOMBINU YA RELI CHINI YA RAHCO

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Wizara ya uchukuzi ni kwamba RAHCO inadaiwa zaidi ya shilingi Bilioni 32 kwa ajili ya matengenezo ya reli ya kati na miradi mingine ya reli iliyochini ya wizara hiyo inayopaswa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo: utandikaji wa reli nzito kutoka Kitaraka hadi Malongwe; Ujenzi wa madaraja; Ujenzi wa kituo cha kuhifadhi makasha cha Mwanza; Ukarabati wa tuta la reli ya kati ya Kaliua – Mpanda katika eneo la mto Ugalla na ukarabati daraja lake; Kazi ya usanifu wa kina wa reli kati ya Tanga – Arusha na upembuzi yakinifu wa reli ya Arusha – Musoma; Kazi ya usanifu wa kina wa reli ya kati Isaka – Mwanza inaendelea; pamoja na Kazi ya kuboresha njia ya reli kwa ajili ya usafiri Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa deni hilo, ni wazi serikali haijali usafiri wa reli nchini na dhamira siyo ile ya kuhakikisha usafiri wa reli ukiimari kama ilivyokusudiwa. Kwani ni ajabu sana kwa serikali makini kuchelewesha malipo ya kiasi hicho cha fedha, ni wazi hata utengenezaji wake huenda umekuwa wa kusuasua. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka serikali ijipime na kujitafakari upya na kisha kuueleza umma wa Watanzania iwapo ina nia ya kuimarisha usafiri wa reli nchini. Bilioni 32 kwa ajili ya uimarishaji wa reli ni fedha kidogo sana kwa serikali iliyomakini; haiingii akilini kusikia wala kuona kwamba serikali imekosa kiasi hicho cha fedha kwa wakati iwapo kweli inathamini usafiri huo ulio rahisi katika kusafirisha shehena ya mizigo na abiria. Haya ni maajabu ya dunia, na hakuna namna ya kuweza kumshawishi mtu ye yote mzima na

Nakala ya Mtando (Online Document)

makini katika kupanga vipaombele vya miradi ya maendeleo. Haindingii akilini na kamwe hakuna mtu mwenye akili timamu anayeweza kushawishiwa kiurahisi kuhusu suala hilo. Na inaweza kuwa haki kwa mtu ye yeyote makini kuendelea kuamini kwamba Serikali hii ya CCM kuitia Wizara ya Uchukuzi imewekwa mfukoni na wafanyabiashara wa usafirishaji wanaotumia malori kusafirisha mizigo ili waendelee kufanya biashara na kujipatia faida huku serikali ikikosa mapato ambayo yanepatikana kuitia usafirishaji kwa njia ya reli ilihali watanzania wengihasa wa mikoa ya **Kigoma, Tabora na Mwanza** wakiumia sana kutokana na usafiri wa reli kuwa wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, mbali na miradi ya uboreshaji wa reli nchini inayoratibiwa na wizara ya uchukuzi, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 serikali ilikusudia kuimarisha huduma za reli nchini chini ya TRL kwa kufanya shughuli zifuatazo: Kufanya matengenezo na ukarabati wa Mabehewana vichwa vya treni ambapo Mikataba kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa vichwa na mabehewa ya treni ilisainiwa kati ya mwezi Aprili na Juni 2013. Malipo ya awali ili kuwawezesha wazalishaji kuanza kazi yalihitaji kiasi cha **shilingi bilioni 124.5**. Kwa mujibu wa tarifa ya Utekelezaji wa mipango ya wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni kwamba hadi sasa ni kiasi cha **shilingi bilioni 67.69** zilizopokelewa na hivyo kuendelea kudaiwa kwa mujibu wa mikataba kiasi cha shilingi **bilioni 75.435**. Tayari kichwa kimoja cha treni kutoka karakana ya Morogoro kimeshakamilika na vichwa vingine viwili (2) vinatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Jumla ya vichwa 8 vilipangwa kutengenezwa upya katika karakana ya Morogoro mwaka 2013/2014. Huu ni mwendelezo uleule wa serikali kutojali usafiri wa njia ya reli na hivyo kuwasababishia wananchi usumbufu mkubwa sana katika kusafirisha shehena za mizigo na abiria kwa ujumla wake hususani wale wa mikoa ya Kigoma, Mwanza, Tabora, na Singida. Kambi rasmi ya Upinzania Bungeni inaitaka na kuishauri serikali kuacha uzembe katika kutekeleza mipango iliyojiwekea kwa sababu hata kiasi cha shilingi Bilioni 143.124 kilichotengwa kwa ajili ya usafiri wa reli nchini bado ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na mahitaji ya sekta hiyo ya usafirishaji lakini pia bado serikali imeendelea na tabia ya kutokutoa fedha zote zilizoidhinishwakwa ajili ya TRL. Huo ni mzaha na mwendelezo ule ule wa kutenga bajeti za kiini macho pasipo kutekeleza mipango iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, hali ndani ya kampuni au shirika la Reli siyo shwari kutokana na Miradi mbalimbali iliyopangwa kutekelezwa katika katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014 kutopata fedha hadi sasa kama ifuatavyo:-

- i. Ununuzi wa vichwa vipyta 13 shilingi bilioni 34.21;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- ii. Ukarabati wa mabehewa 125 Shilingi bilioni 1.108;
- iii. Ununuzi wa mabehewa 274 shilingi bilioni 22.38 ambayo nusu imebaki kwa ajili ya kufungua LC;
- iv. Ununuzi wa mabehewa ya abiria 22 shilingi bilioni 13.591;
- v. Ununuzi wa Toroli mpya 30 shilingi bilioni 2.84;
- vi. Ujenzi wa magenge shilingi bilioni 1.51;
- vii. Ukarabati wa njia ya mawasiliano shilingi bilioni 2.166;
- viii. Ukarabati wa karakana na majengo 8 ya stesheni shiling bilioni 1.335;
- ix. Matengenezo ya kawaida ya vichwa na mabehewa shilingi bilioni 2.264;
- x. Ukarabati mdogo wa njia ya reli shilingi bilioni 4; na
- xi. Malipo ya madeni kwa watoa huduma shilingi bilioni 5.5.

Mheshimiwa Spika, ni wazi hakuna “seriousness” serikalini katika kuhakikisha reli yetu inarejea **ku-perform** kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kabla ya mwaka 2000. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka serikali ilieleze Bunge lako tukufu ipo wapi dhati au dhamira ya serikali katika kuhakikisha reli yetu inafanya kazi ipasavyo wakati hata fedha kiduchu iliyotengwa haitolewi kwa wakati na hakuna uhakika iwapo fedha hiyo itatolewa au la? Ni kwa namna gani reli yetu itaweza kufanya kazi kwa kuwa na mwenendo uleule wa siku zote wa kutenga fedha kupitia bajeti halafu fedha hazitolewi ili kuhakikisha malengo yanafikiwa? Viini macho hivi vya serikali ya CCM dhidi ya Watanzania wanaohitaji usafiri wa reli nchini vitaendelea hadi lini? Nashawishika kutojizua kuwaoomba watanzania kuamini kwamba CCM na serikali wanayoiongoza wameshindwa kazi na wakubali kufanya mabadiliko kwa kutokukichagua chama hicho katika chaguzi zijazo kwa sababu ahadi za uwongo zimekuwa nyingi mno.

MVUTANO WA TRL NA RAHCO

Mheshimiwa Spika, zipo tarifa za kuwepo kwa mvutano kati ya RAHCO na TRL kiutendaji. Mvutano huo unatajwa kusababisha ajali mbalimbali za Treni zinazojitokeza hivi. Kwa mfano inawelevwa kwamba Treni ya mizigo Namba

Nakala ya Mtandao (Online Document)

B451 yenyé Injini Namba 8906 ILIYOKUWA IKITOKEA Mkoani Morogoro kwenda Dodoma na kisha kuendelea na safari nyingine ilipata ajali na kuzama Mtoni katika eneo la GULWE STATION mnamo tarehe 28/03/2014 saa 8 Usiku na hivyo kusababishia TRL hasara ya Injini na Mabehewa matano. Sababu inayotajwa kusababisha ajali hiyo ni serikali ya CCM kupitia Wizara ya uchukuzi inayoongozwa na Waziri Dr. Harison George Mwakyembe kutokuwalipa Wakaguzi wa njia posho ya saa za ziada kazini. Aidha tarifa zilizopo ni kwamba hakuna hatua zilizochukuliwa hadi sasa. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inahoji, ni kwa nini serikali inawapuuza watumishi wa TRL na RAHCO kwa kutowalipa posho na stahiki zao mbalimbali kama vile mishahara na malimbikizo yao wanayostahili kulipwa? Ni lini haki za wafanyakazi hawa zitalipwa kwa wakati ili kuliepusha taifa na hasara hii ya vichwa na mabehewa ya treni kupinduka na hivyo kusababisha fedha za walipakodi kuendelea kutumika pasipo kuleta tija kwa taifa?

Mheshimiwa Spika, hata madereva wa Gari Moshi na wengine wanalamika sana kunyanyaswa kwa kutolipwa stahiki zao mbalimbali. Mfano hawalipwi posho nzuri wawapo safarini kiasi wanazidiwa na Madereva wa Malori ya mizigo wnaotajwa kulipwa Sh laki 3 kwa safari ya kutoka DSM hadi Mwanza au Dsm hadi Kigoma kwenda na kurudi (Madereva wa Malori) dereva wa Gari moshi akibakia kulipwa sh 36,480/= anapoendesha gari moshi kutoka DSM hadi Mwanza Km 1216, na Dsm hadi Kigoma analipwa sh 37,620/= kwa umbali km 1254. Hata hivyo madereva hao wanaeleza kwamba wanapofika mwisho wa safari yao hawalipwi posho nyingine yoyote ile bali wanapelekwa kulala na kula mahala ambapo panatajwa kuwa na mazingira mabaya mno kiasi cha kuwakatisha tamaa na kuwasikitisha sana. Wanaeleza kwamba Wizara haiwathamini na inawanyonya mno, kwa sababu hata maji yanakosekana kwa ajili yao pale wanapofikishiwa kwa ajili ya makazi mfano Dodoma wanaishi mahala pabaya sana. Wanaeleza kwamba hata chakula wanachopewa ni kibaya na kisichoendana na hadhi zao lakini kisichoendana na kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Madereva hao wa gari moshi wanaeleza kwamba, Waziri wa Uchukuzi Dr. Harrison George Mwakyembe alishaelezwa matatizo haya lakini hajayatatua kama alivyowaahidi mwaka jana tarehe 8 na 9 February, 2013 alipokutana nao. Wafanyakazi hawa wanositishwa na kitendo hicho cha waziri wa uchukuzi kuwaahidi uwongona sasa amekuwa kimya kiasi cha kuwatia mashaka. Aidha wanaeleza kwamba imefikia mahala wanadai wamechoshwa na ahadi za uwongo na kamwe isitarajiwe kuona tija katika kuliendesha shirika la reli nchini. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ieleze ni lini itaacha tabia hii mbaya na chafu ya kuwahadaa watumishi hawa wanaofanya kazi ngumu?

Mheshimiwa Spika, Matatizo hayo yanawakuta pia hata watumishi engine wa shrikika la Reli nchini wanaeleza kwamba Serikali imewadhulumu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

malimbikizo ya mishahara yao ya miezi sita (6) yaani mwezi JULY hadi DESEMBER 2013. Serikali iliongeza mishahara yao mwaka jana 2013/2014 lakini watumishi hao wa TRL walikaa muda mrefu pasipo kubadilishiwa mishahara yao hadi ilipofika mwezi April 2014 ambapo waliliwa na Arreas za kuanzia mwezi January hadi May, 2014 tu na kuambiwa kwamba zile za mwezi July hadi Desember 2013 hazipo na kwamba wawe wapole. Mheshimiwa spika, hivi jambo hilo linawezekanaje? Kambi rasmi ya upinzania Bungeni inaitaka Serikali kueleza malipo ya malimbikizo haya ya mishahara ya watumisishi wa TRL yatalipwa lini? Kutokuwalipa itakuwa ni wizi wa mchana kweupe na kwa kweli itampasa Waziri wa Uchukuzi kuwajibika kwa mambo haya kam siyo serikali nzima kuwajibika.

MALALAMIKO YA ASKARI WANAOFANYA KAZI SHIRIKA LA RELI NCHINI

Mheshimiwa Spika, sekta ya Reli nchini ina askari polisi ambao wana jukumu la kuhakikisha usalama wa Abiria, Mizigo na Mali za shirika la reli zikiwa katika hali ya usalama. Taarifa zilizopo; zinaeleza kwamba askari hao wananyanyasika sana kwa kutolipwa stahiki zao mbalimbali hususani Posho za Safari; posho za Maji na Umeme. Hali hiyo ni kikwazo na chukizo kwa askari hao wanaofanya kazi katika mazingira magumu sana. Ni wazi inawavunjwa moyo wa kuifanya kazi hiyo na wakati mwengine hali hiyo inaweza kuapelekea wahujumu mali za shirika hilo kama vile kuza mafuta, vipuri vya mitambo mbalimbali nk kutokana na ugumu wa maisha. Kwa mfano, askari hao wanaeleza kwamba tangu shirika hilo liondolewe mikononi mwa Wahindi waliokuwa wamebinafsishiwa mwaka 2012; askari hawajalipwa Posho za Safari ambazo ni kati ya SH. 20,000/= na 45,000/= kwa siku walizokuwa zamu safarini. Posho za umeme na maji nazo ni tatizo kubwa kwa askari wote wanaofanya kazi katika shirika hilo hasa wale wa mikoa ya Kigoma, Tabora, Dodoma, Morogoro, Mwanza na Tanga.

Mheshimiwa Spika, ni tabia mbaya kwa Wizara kutoona umuhimu wa maisha ya askari hawa na wafanyakazi wengine kutokuwalipa stahiki zao wafanyakazi hawa lakini posho zao mabwana mkubwa wa wizara hii wanajitengea na kujilipa huku wenzao wakibaki kulalamika na kupigwa miayo kibao. Huu ni usaliti mkubwa kwa Askari na watumishi wote wa Shirika Reli wanaoidai serikali posho mablaimbali. Ni wazi matokeo yake ni hujuma dhidi ya shirika letu na hatuwezi kuendelea. Kambi rasmi inaitaka serikali kuhakikisha inawalipa Askari hao na watumishi wote ili kuliokoa shirika hilo ambalo liko taabani hivi sasa. Aidha Viongozi wote wa Wizara hii watambue kwamba ni aibu kwa Sekta ya reli kushindwa kujilipa mishahara na posho mbalimbali wanazostahili watumishi kwa sababu iwapo lingeboreshwa kila kitu kingelipwa kwa kutumia mapato yanayotokana na usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli.

UMILIKISHWAJI HARAMU ENEO LA RELI ARUSHA MJINI

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ukistaajabu ya Musa utayaona ya filauni. Katika hali ya kushangaza serikali imediriki kumpatia mfanyakiasahara mmoja wa mjini Arusha eneo moja linalohusisha eneo la Reli na hivyo kuwashangaza watu. Tunajiulizainawezekanaje kumpatia mtu eneo la reli kiasi kwamba Treni haitaweza kupita?

Waziri Mwakyembe na Naibu wake walishaelezwa juu ya suala hili na kwa hiyo kilichobaki ni kutupatia majibu kuhusu ni nini hatma ya reli ile na eneo lote kwa ujumla? Kama ni halali kufanya kile kilichofanywa watuleze; na iwapo siyo halali watuleze kwa kuwa ni ajabu kuendelea kubinatsisha maeneo nyeti kwa watu wenye fedha nyingi tu huku Machinga wa nchi hii wakikumbana na fukuza fukuza mijini lakini watu wenye fedha zao wanaendelea kuhodhi maeneo ambayo ni very Potential. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inahitaji kujuua suala hilo limefikia wapi na je, wale wote waliohusika katika kugawa eneo la reli wamechukuliwa hatua gani?

USAFIRI WA RELI NCHINI JAPAN NA CHINA

Mheshimiwa Spika, nchi ya Japan inatajwa kuwekeza sana kwenye usafiri wa reli kiasi cha kuiwezesha nchi hiyo kusifika na kutambuliwa duniani pamoja na kukabiliwa na changamoto ya kupungua kwa ongezeko la watu nchini humo. Watu zaidi ya 25,000 wameajiliwa katika viwanda vya utengenezaji reli nchini japan, achilia mbali wale waliopata ajira katika usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli nchini humo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo maajabu zaidi yanapatikana nchini china ambako serikali imekuwa ikienda kujifunza juu ya mambo mbalimbali ikiwemo kujifunza namna China walivyopiga hatua kwenye usafiri wa reli lakini utekelezaji wa kile wanacho jifunza hawakifanyii kazi vile inavyopaswa kufanywa. Kwa mujibu wa Michael Renner na Gary Gardner katika tarifa yao ya **Global Competitiveness in the Rail and Transit Industry ya Septembe 2010** inaelezwa kwamba maendeleo makubwa yanayohusiana na usafiri wa reli pamoja na mambo mengine yalitokana na Uongozi wa China kufanya maamuzi magumu na makini katika kuboresha sekta ya usafiri wa Reli ambapo inatarajiwa kwamba ifikapo mwaka 2020 watakuwa wametandaza reli nchini humo kiasi cha umbali wa **MILE 93,000** huku **MILE 16,000** zitakuwa ni HIGH SPEED LINES.

Mheshimiwa Spika, aidha tarifa hiyo inaeleza kwamba China itakuwa ni mtumiaji wa Reli kwa zaidi ya nusu ya watumiaji wengine duniani kwa miaka michache ijayo. Vilevile ASILIMIA 70 – 90 ya Reli huzalishwa nchini humo baada ya China kukubaliana na makampuni ya kigeni yenye Teknolojia mbalimbali za kutengeneza Reli na Mabehewa kwa kutumia viwanda vyao vya ndani ambapo makampuni makubwa mawili ya Kichina yaani CSR ambayo **ni China**

Nakala ya Mtandao (Online Document)

South Locomotive and Rolling Stock na CNR yaani **China Northern Locomotive and Rolling Stock**; kwa pamoja makampuni hayo yametoa ajira zaidi ya watu 200,000 nchini humo. Ajira hizo ni nje ya zile zinazopatikana kupitia makampuni mbalimbali yanayotoa ajira kupitia huduma ya usafirishaji inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, Dr. Harison Mwakyembe(mb) ambaye ndiye msimamizi au rubani na msemaji mkuu wa Wizara ya uchukuzi anawajibika kuufanya ubongo wake kuwa Flexible kwanza, kisha akahakikishe kwa kutumia makeke yake analishawishi baraza la Mawaziri kuachana na tabia ya kupenda kurundikiwa fedha nyingi katika wizara zao kwa mambo ambayo taifa linaweza kuacha kuyatengea fedha kwa muda flani pasipo kuacha madhara katika jamii, na hakika inawezekana kabisa; na hivyo mkazo iwe ni kutenga fedha nyingi kwa ajili ya Kuimarisha sekta ya uchukuzi katika eneo usafiri wa reli na bandari ili kuliwezesha taifa letu kupakua shehena kubwa ya mzigo utakaopitishwa hapa nchini katika bandari zetu na hatimaye kusafirishwa kwa njia ya reli ambayo ni haraka na nafuu kwa gharama. Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inasikitishwa sana na mwenendo wa Serikali hii ya inayoongozwa na CCM inayofanya kwa makusudi vitendo vinavyolifanya taifa letu kuendelea kuwa masikini kwa sababu ya mipango mibovu.

Mheshimiwa Spika, Ubovu wa mipango hiyo upo katika maeneo yafuatayo; Moja serikali imeendekeza kutenga fedha nyingi kwa ajili ya vitu kama viburudisho maofisini huku usafiri wa reli na Bandari ukisua sua kila mwaka ambaao ungeiwezesha nchi yetu kujipatia fedha nyingi baada ya kuboreshwa kwa njia hizo pamoja na vyombo vyake. Ni aibu nchi masikini inayotamani kuendelea, kutenga fedha nyingi kwa vitu visivyokuwa na matokeo mazuri kwa maendeleo na ustawi wa uchumi wetu, kwa mfano Wizara ya Uchukuzi imetenga fedha zifuatazo katika bajeti yake kwa ajili ya vitu ambavyo kwa mtu mwenye kiu ya maendeleo hawezi kuvifanya.

USHAURI WA JUMLA KWA SERIKALI

Mheshimiwa Spika, Serikali hii inayoongozwa na CCM inapaswa kuachana na tabia ya kujifanya kiziwi na kipofu wakati ina watu wenye masikio na macho lakini wasiotaka kuyatumia kama ilivyokusudiwa na mwenyezi mungu. Kwa miaka mingi imekuwa ikishauriwa na Wabunge na wananchi mbalimbali kwa kutakiwa kuachana na tabia ya kuwa na vipaombele vingi kuliko uwezo wake wa kifedha na hatimaye nchi yetu kuendelea kuwa masikini. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka serikali kuzijali sekta zinazoweza kuisaidia nchi yetu kuingiza fedha nyingi kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu; Baadhi ya Wizara hizo ni pamoja na Wizara ya Uchukuzi inayoshugurikia maendeleo ya Usafiri wa Reli; Usafiri wa majini; na Usafiri wa Anga. Ni ukweli usiopingika kwa mtu yejote mwenye akili timamu kwamba Usafiri kwa Reli na ule wa Majini ndizo ni njia rahisi za kusafirisha mizigo kwa gharama kidogo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ikilinganishwa na njia nyingine. Hivyo basi serikali hii ya CCM inapaswa uamuzi wa kutenga fedha za kutosha kwenye bajeti ili kuhakikisha Reli na bandari vimeimarisha ili kuiwezesha nchi yetu kujipatia fedha nyingi kupitia usafirishaji wa shehena za mizigo na abiria.

Mheshimiwa Spika, Mazingira yaliyopo ni wazi na ni vigumu kuinasua serikali ya CCM katika kile kinachadaiwa kwamba baadhi ya watendaji na viongozi mbalimbali wenyewe mamlaka ya kuandaa mipango na kufanya maamuzi wamenunuliwa na wafanyabisahara wenyewe makampuni ya usafirishaji kwa njia ya Malori yanayotumia barabara zilizopo nchini. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni haiwezi kushawishiwa na serikali inayoongozwa na CCM kwamba dhamira ya kuboresha sekta ya uchukuzi hususani Reli na Bandari ipo, kwa sababu ahadi zake za kuboresha sekta hizo zimekwa katika makaratasi pasipo kufanyiwa utekelezaji. Mazingira yaliyopo ni wazi rushwa imewafanya kutokujali maslahi mapana ya wananchi wa nchi yetu. Tani milioni 13 zinazotajwa kupakuliwa katika bandari ya Dar es Salaam bado ni kiduchu kwa eneo inapopatikana bandari hiyo ikiwa ni pamoja na bandari nyingine zinazopatikana katika maziwa yetu. Nchi yetu leo hii imepoteza fursa ya kupokea na kusafirisha mizigo ya nchi ya Uganda na muda siyo mrefu itapoteza kupokea na kusafirisha mizigo ya nchi kama za Zambia na DRC iwapo Reli na Bandari zetu hazikuimashwa.

Mheshimiwa Spika, Siyo vibaya kujifunza na kuiga kutoka katika nchi nyingine Duniani kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo suala la kufanya maamuzi yanayohusu vipaombele vya kushughurikia kwa maslahi mapana ya nchi husika. Kwa mfano Nchi kama China; Ujeruman; Spain; Japan; Canada; Uingereza; Marekani; Ufaransa nk zimejithadi sana kuwekeza katika kuimashwa usafirishaji na usafiri kwa njia ya reli. Sababu zinazoelezwa kuhusu ni kwa nini wamewekeza sana katika usafiri wa reli ni kwamba ni Usafiri wa gharama nafuu katika kusafirisha mizigo lakini pia wa haraka kwa kuwa hauna bughudha kama ilivyo kwa njia ya barabara. Kwa Mujibu wa Michael Renner na Gary Gardner katika tarifa yao ya **Global Competitiveness in the Rail and Transit Industry ya September 2010**, wanaeleza kwamba Ujerumani wamewekeza sana kwenye sekta ya usafiri wa reli kiasi cha kuwa mara mbili ya uwekezaji uliofanywa na marekani na hivyo kutengeneza ajira 580,000. Nchi ya Spain imeendelea pia kuwekeza katika usafiri wa reli kwa kiasi kikubwa, kwa mfano Mpango mkakati wa nchi hiyo wa mwaka 2004 kuhusu Miundombinu ya usafirishaji wa reli (Plan for Infrastructures and Transport – PEIT) na Mpango mkakati wa Miundombinu wa Aprili 2010 ilitenga 70% ya Dola za Kimarekani kiasi cha **24 bilioni** sawa na shilingi za kitanzania **Trillioni 38.4** ambayo ni mara mbili ya bajeti nzima ya Serikali ya Tanzania inayoongozwa na CCM. Uwekezaji huo umeiwezesha Spain kutoa ajira za moja kwa moja kwa watu wasiopungua 116,000 mwaka 2008 kupitia makampuni mbalimbali yanayotoa huduma za kuwezesha usafiri wa reli nchini humo.

UFISADI NA UONGO KUHUSU UMILIKI WA HISA KATIKA SHIRIKA LA USAFIRI DAR ES SALAAM (UDA)

Mheshimiwa Spika:

Itakumbukwa kwamba tarehe 15/05/2014 katika kipindi cha maswali ya kawaida katika kutoa majibu, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilijibu kwamba: "Hisa za Serikali ndani ya Shirika la UDA hazijauzwa. Mmiliki wa Shirika la UDA ni Halmashauri ya Jiji na Serikali kupitia Msajili wa Hazina. Mgawanyo wa Hisa halali ni kama ulivyo sajiliwa kwenye msajili wa Makampuni kwa maana ya Halmashauri ya Jiji 51% na Serikali kupitia Msajili wa Hazina 49%".

Hata hivyo, mara baada ya Serikali kutoa majibu hayo Bungeni Simano Group Limited kupitia Mwenyekiti wake Mtendaji Robert Kisena ilifanya Mkutano na waandishi wa habari na kueleza kwamba, mgawanyo halali wa hisa za UDA ni Simon Group Limited asilimia 76.79 na Msajili wa Hazina (Serikali) asilimia 23.26.

Mheshimiwa Spika; Kwa maelezo haya naomba kauli ya serikali kuhusu maswali yafuatayo;

1. Je, ni nani muongo kati ya Serikali na Simon Group Limited? Je, aliye muongo kati yao, ndani na nje ya Bunge anachukuliwa hatua gani?
2. Iwapo majibu ya Serikali ni ya kweli, kwa nini mpaka sasa Kampuni ya Simon Group inaendelea kumiliki Shirika la UDA kama mwana hisa mkuu wakati ambapo Serikali imesema kuwa ilishazuia mauzo ya hisa za Shirika hilo.
3. Serikali imechukua hatua gani mpaka sasa dhidi ya wamiliki wa Kampuni ya Simon Group, Watumishi wa Halmashauri ya Jiji, Msajili wa Hazina, Bodi ya Wakurugenzi ya UDA, juu ya kukiuka Sheria ambapo Serikali imeeleza bungeni?
4. Je serikali ipo tayari kuweka wazi wakati wa majumuisho ya Wizara ya Uchukuzi taarifa ya uchunguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Fedha za Serikali (CAG) ili kujadiliwa na Bunge kwa ajili ya kuweka jambo hili wazi na Bunge kupendekeza hatua stahiki za kuchukua.

Mheshimiwa Spika; Itakumbukwa pia kwamba wakati wa majumuisho yake hapa Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 baada ya kuhojiwa na Waziri Kivuli wa Ofisi ya Rais, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utawala Bora Mhe. George Huruma Mkuchika hakugusia kwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

undani wala kutoa majibu ya kuridhisha kuhusu sakala la UDA hata baada ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutoa maelezo ya kina kuhusu sakata zima.

Mheshimiwa Spika: Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya Waziri wa Uchukuzi na Waziri Mkuu juu ya ufisadi katika Shirika la Usafiri Dar Es Salaam (UDA) na uongo ulioelezwa ndani na nje ya Bunge juu ya umiliki wa hisa katika kampuni hiyo ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa manufaa ya nchi na wananchi.

PROGRAMME 10 UTAWALA

Subvote 1001: Administration and HR management

- **Kasma 221400:** Katika mwaka fedha wa 2013/2014 Wizara ilitenga kiasi cha shilingi 13,959,000 kwa ajili ya Hospitality Supplies and Services ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Wizara ya Uchukuzi chini ya Dr. Harrison George Mwakyembe wamejiongeza fedha kiasi cha Sh. 91,641,000/= na hivyo kuwa jumla ya Sh. 105,600,000/= ambapo ongezeko hilo ni sawa na 86.7% au 87 %.
- **Kasma 410500:** Acquisition of Household and Institutional Equipment: Kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Wizara ilitenga sh 18,000,000/= ilihali mwaka 2014/2015 Wizara imejitengea Sh. 50,000,000/=, Ongezeko ni sh 32,000,000/= sawa na ongezeko la 64 %.
- **Kasma 221200:** Communication & Information: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 20,400,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha Wizara imetenga Sh 40,600,000/=, Ongezeko ni sh 20,200,000/=, sawa na Ongezeko la 49.753 % au 50%.
- **Kasma 220100:** Office and General Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 16,187,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 183,620,000/=, Ongezeko ni sh 167,433,000/=, sawa na Ongezeko la 91 %.
- **Kasma 210500:** Personal Allowances In-kind: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 67,430,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 86,400,000/=, Ongezeko ni sh 18,970,000/=, sawa na Ongezeko la 21.956 % au 22 %.
- **Kasma 210000:** Travel in Country: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 85,638,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 347,220,000/=, Ongezeko ni sh 261,220,000/=, sawa na Ongezeko la 75.336 %.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- **Kasma 410600:** Acquisition of Office and General Equipment: Travel in Country: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 0/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 26,500,000/=, Ongezeko ni sh 26,500,000/=, sawa na Ongezeko la 100 %.
- **Kasma 411000:** Rehabilitation and Other Civil Works: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 600,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 18,000,000/=, Ongezeko ni sh 17,400,000/=, sawa na Ongezeko la 96.666 % au 97 %.

Subvote: 1002: Finance and Accounts

- **Kasma 210400:** Personal Allowances-(Discretionary)- Optional: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 7,050,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 18,000,000/=, Ongezeko ni sh 10,950,000/=, sawa na Ongezeko la 60.833 % au 61 %.
- **Kasma 210500:** Persona allowances in Kind: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 5,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 32,320,000/=, Ongezeko ni sh 32,315,000/=, sawa na Ongezeko la 99.984 % au 100 %.
- **Kasma 220100:** Office and General Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 9,422,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 17,330,000/=, Ongezeko ni sh 7,908,000/=, sawa na Ongezeko la 45.631% au 46 %.
- **Kasma 220300:** Fuel, Oils, Lubricants: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh. 11,650,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 22,400,000/=, Ongezeko ni sh 10,150,000/=, sawa na Ongezeko la 47.991% au 48 %.
- **Kasma 221000:** Travel in Country: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh.15,158,000 /= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh27,800,000 /=, Ongezeko ni sh 12,642,000/=, sawa na Ongezeko la 45.474%.
- **Kasma 221100:** Travel Out of Country: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh.1,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 8,550,000 /=, Ongezeko ni sh 8,549,000/=, sawa na Ongezeko la 99.988% au 100 %.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- **Kasma221400:** Hospitality Suplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh.20,500,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 27,100,000/=, Ongezeko ni sh 6,600,000/=, sawa na Ongezeko la 24.354 %.
- **Kasma 410600:** Acquisition of Office and General Equipment: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 11,000,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 25,000,000/=, Ongezeko ni sh 14,000,000/=, sawa na Ongezeko la 56 %.

Subvote 1003: 1003 Policy and Planning

- **Kasma 220300:** Fuels,Oils, Lubricants: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 13,660,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 50,860,000/=, Ongezeko ni sh 37,200,000/=, sawa na Ongezeko la 73.141 %.
- **Kasma 221400:** Hospitality Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 15,450,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 27,850,000/=, Ongezeko ni sh 12,400,000/=, sawa na Ongezeko la 44.524 %.

Subvote 1005: Government Communication Unit

- **Kasma 210400:** Personal Allowances-(Discretionary)-Optional: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 0/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 5,000,000/=, Ongezeko ni sh 5,000,000/=, sawa na Ongezeko la 100 %.
- **Kasma 220100:** Office and General Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 6,017,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 11,192,000/=, Ongezeko ni sh 5,175,000/=, sawa na Ongezeko la 46.238 %.
- **Kasma 220300:** Fuel, Oils, Lubricants: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 188,500/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 11,450,000/=, Ongezeko ni sh 11,261,500/=, sawa na Ongezeko la 98.353 %.
- **Kasma 220700:** Rental Expenses: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh1,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh7,000,000 /=, Ongezeko ni sh 6,999,000/=, sawa na Ongezeko la 99.985 %.
- **Kasma 221400:** Hospitality Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 29,000,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

2014/2015 Wizara imetenga Sh 37,000,000/=, Ongezeko ni sh 8,000,000/=, sawa na Ongezeko la 21.621 %.

- **Kasma 410600:** Acquisition of Office and General Equipment: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 2,000,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 23,780,000/=, Ongezeko ni sh 21,780,000/=, sawa na Ongezeko la 91.589 %.

Subvote 1005: Procurement Management Unit

- **Kasma 210500:** Personal Allowances- In- kind:Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 4,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 18,500,000/=, Ongezeko ni sh 18,496,000/=, sawa na Ongezeko la 99.978%.
- **Kasma 221400:** Hospitality Spplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 9,900,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 12,500,000/=, Ongezeko ni sh 2,600,000/=, sawa na Ongezeko la 20. 8 % au 21.

Subvote 1006: Internal Audit Unit

- **Kasma 210500:** Personal Allowances In Kind: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 11,822,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 29,820,000/=, Ongezeko ni sh 17,998,000/=, sawa na Ongezeko la 60.355 %.
- **Kasma 220300:** Fuel,Oils, Lubricants: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 6,401,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 10,127,500/=, Ongezeko ni sh 3,726,500/=, sawa na Ongezeko la 36.795 % au 37 %.
- **Kasma 220700:** Rental Expenses: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 2,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 4,000,000/=, Ongezeko ni sh 3,998,000/=, sawa na Ongezeko la 99.95 % au 100%.
- **Kasma 221000: Travel in Country:** Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 14,368,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 72,650,000/=, Ongezeko ni sh 58,282,000/=, sawa na Ongezeko la 80.222%.
- **Kasma 221400:** Hospitality Spplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 7,702,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

2014/2015 Wizara imetenga Sh 18,000,000/=, Ongezeko ni sh 10,298,000/=, sawa na Ongezeko la 57.211%.

- **Kasma 229900:** Other Operating Expenses: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 1,002,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 16,000,000/=, Ongezeko ni sh 14,998,000/=, sawa na Ongezeko la 93.737 % au 94 %.

Subvote 1007: Legal Services Unit

- **Kasma 210400:** Personnel Allowances-(Discretionary)-Optional: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 0/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 6,600,000/=, Ongezeko ni sh 6,600,000/=, sawa na Ongezeko la 100 %.
- **Kasma 220100:** Office and General Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 4,400,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 9,257,000/=, Ongezeko ni sh 4,857,000/=, sawa na Ongezeko la 52.468 %.

Subvote 1008 Information and Communication Technology Unit

- **Kasma 220100:** Office and General Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 17,570,800/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 32,756,000/=, Ongezeko ni sh 15,185,200/=, sawa na Ongezeko la 46.358 %.
- **Kasma 221400:** Hospitality Supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 7,900,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 15,200,000/=, Ongezeko ni sh 7,300,000/=, sawa na Ongezeko la 48.026 %.
- **Kasma 229900:** Other Operating expenses: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 0/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 13,601,250/=, Ongezeko ni sh 13,601,000/=, sawa na Ongezeko la 100 %.
- **Kasma 230700:** Routine maintenance and Repair of Office Equipment and Appliances: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 11,800,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sh 26,600,000/=, Ongezeko ni sh 14,800,000/=, sawa naOngezeko la 55.6639 %.

- **Kasma 410600:** Acquisition of Office and General equipment: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 8,299,950/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 10,000,000=, Ongezeko ni sh 1,700,050/=, sawa na Ongezeko la 17 %.

PROGRAMME 50 BUILDING CONSTRUCTION AND MAINTANANCE

Subvote 5002: Transport Safety and Environmental Division

- **Kasma 210500:** Personal Allowances in kind: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 56,460,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 87,460,000/=, Ongezeko ni sh 31,000,000/=, sawa na Ongezeko la 35.444 %.
- **Kasma 220100:** Office general supplies and Services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 14,424,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 22,711,000/=, Ongezeko ni sh 8,287,000/=, sawa na Ongezeko la 36.488 %.
- **Kasma 220300:** Fuel, Oils, Lubricants: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 10,325,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 29,970,000/=, Ongezeko ni sh 19,645,000/=, sawa na Ongezeko la 65.548 %.
- **Kasma 221400:** Hospitality Supplies and services: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 3,505,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 9,200,000/=, Ongezeko ni sh 5,695,000/=, sawa na Ongezeko la 61.902% au 62 %.
- **Kasma 229900:** Other operating expenses: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 600,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 6,000,000/=, Ongezeko ni sh 5,400,000/=, sawa na Ongezeko la 90 %.
- **Kasma 410600:** Acquisition of Office and General Epuipment: Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Sh 6,800,000/= zilitengwa ilihali kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 Wizara imetenga Sh 19,900,000/=, Ongezeko ni sh 13,100,000/=, sawa na Ongezeko la 65.829 %.

Mheshimiwa Spika, vifungu hivyo tu, vina jumla ya Shilingi **bilioni 1,119,861,550/=;** katika hali hiyo nchi hii haiwezi kamwe ikaendelea haraka kwa sababu fedha nyingi zinaishia kwenye utafunaji yaani kulipana posho nk. Hali

Nakala ya Mtando (Online Document)

hiyo ipo pia katika wizara nyingine kwa kiasi cha kutisha. Tabia hiyo ni mbaya na haiukubaliki hata kidogo. Tujiulize iwapo kila wizara imetenga kiasi hicho cha shilingi bilioni 1 na ushehe, ni wazi zaidi ya shilingi Bilioni 50 zinatumika kwa mambo ambayo hayaleti tija kwa taifa huku walipa kodi wa taifa hili ambao ni masikini wakifa vijiji kwa kukosa madawa; Walimu na watumishi wengine wakilipwa mishahara kiduchu, Watoto wakikosa vitabu na madawati shulenii lakini Mawaziri na Watendaji Wizarani wakitanua kama vile wako peponi. Aidha bajeti maendeleo ya shilingi bilioni 549.664 kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya mendeleo ni wazi vado ni kidogo sana ikilinganishwa na hali halisi ya miradi inayopaswa kutekelezwa na Wizara hii hususani ile ya sekta reli na Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Spika, Mbaya zaidi ni kwamba wakati Wizara hii inahitaji walau Sh. Trilioni 1.763 ambapo katika fedha hizo Sekta ya Reli pekee inahitaji shilingi Bilioni 773.355 lakini katika mwaka wa fedha 2014/2015 bado imetengeewa Shilingi Bilioni 126.9 tu na hivyo kukabiliwa na upungufu wa Shilingi Bilioni 646.455. Hata hivyo miradi yote ya maendeleo kwa Wizara hii imetengewa kiasi cha Sh Bilioni 549.664 ambapo Shilingi Bilioni 289.664 Zinatarajiwa kutoka kwa Wajomba yaani Wahisani ambao wanaitwa Washirka wa maendeleo kwa lugha nyingine. Bajeti nzima ya maendeleo haiwezi hata kukidhi mahitaji ya sekta ya Reli pekee ili iweze kuimarika lakini ni maajabu ya serikali ya CCM kujisifu kwamba inafanya vizuri katika maendeleo ya nchi yetu; Waheshimiwa Wabunge huu ni utani. Inatupasa tujiulize maswali yafuatayo: Je, Vipi wajomba au wahisani wakigoma kutupatia fedha hizo?

Je, kuna tatizo gani kwa serikali hii ya CCM ikiachache kujitengea fedha za kulipana posho kibao kama vile zile za vitafunwa, Soda nk na mkazo ukawa ni kutenga fedha nyingi kwa maendeleo? Watanzania tuache ujingga wa na sasa tuamue kuwekeza fedha zetu kwenye maeneo yanayoweza kuzalisha fedha ili fedha zitakazo patikana tuziwekeze kwenye sekta za huduma kama vile ELIMU; Afya; Maji; na nyine zote muhimu. Ni rai yetu kambi rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba tuamue mwaka huu kuhamisha fedha za wizara fulani fulani ili tuziwekeze kwenye maeneo yafuatayo yanayoweza kuifanya nchi yetu kupata fedha: Tuwekeze kwenye Sekta za Bandari na Reli; viwanda na Biashara; Sekta ya Utalii na Usafiri wa Anga; Sekta za Nishati na Madini. Tukifanya hivyo, muda siyo mrefu tutaiwezesha nchi yetu kujipatia fedha zitakazotusaidia kutatua matatizo mbalimbali yanayotukabili nchini. Hali ya sasa imekaa kisiasa zaidi na haina tija kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Ukweli ni kwamba bado haiingii akilini kuona Watumishi wa Wizara na baadhi ya wakuu wa idara na tasisi za Wizara wakilipwa walau vizuri huku watumishi wa kada za kati na chini wakilipwa mishahara kidogo lakini pia watumishi hawa wanaolipwa mishahara kidogo wakiwa hawana malipo ya hizo posho wanazolipwa au kutengewa wale

Nakala ya Mtando (Online Document)

wanaolipwa mishahara mikubwa kwa ajili ya kujinunuliwa Juisi, Vitafunwa maofisini nk. Hii ni kuwahadaa na kuwakejeli wale watumishi wanaolipwa mishahara kidogo bila hiso posho hususani walimu; Watumishi wa Afya; Kilimo nk kwa kada za chini. Kwa Mfano mtumishi kama Mwalimu wa Sekondari mwenye Degree unamkuta analipwa mshahara wa sh laki 5 kwa mwezi halafu hana usafiri wala hana posho ya chakula; malazi nk bali anaishi kwa kutegemea mshahara wake huo wa sh laki 5 tu kila mwezi kwa ajili ya matumizi yake yote kama vile chakula; Nauli ya usafiri kwenda kazini; Chai yake kazini; Ada ya watoto nk.

Mheshimiwa Spika, hali iko hivyo kwa watumishi wengi lakini Bunge lako tukufulinakubali kupidisha bajeti za wizara zilizosheheni utitiri wa posho kibao kwa ajili ya watumishi wenyе mishahara ambayo kwa kiasi fulani inaridhisha hali ambayo ni tofauti ikilinganishwa na ile ya watumishi kama walimu wenyе viwango vya elimu sawasawa na wale wengine wanaolundikiwa utitiri wa posho na mishahara yenyе unaifuu. Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inalishauri Bunge lako tukufu kutokukubali kupidisha bajeti ya Wizara hii hadi Waziri akubali kuondoa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya posho mbalimbali ambazo wanaweza kwa kujigharamia kwa kutumia mishahara wanayolipwa ili kuonesha mfano kwa nchi yetu na hatimaye fedha hiso zipelekwe kwenye Miradi ya maendeleo hususani Elimu; Reli; Bandari; Sekta ya Viwanda; Nishati na Madini; Utalii; na Kilimo . Hiso ni sekta ambazo nchi ikiamua kuacha upuuzi wa kuwekeza fedha nyngi kwenye matumizi ya kawaida kama kulipana posho za ajabuajabu tena kwa kuanzisha vitengo na vikao visivyokuwa na tija; hakika taifa letu litatoka hapa tulipo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Chonde chonde tuache siasa za kutaka tuonekane kuna mambo yamefanyika katika majimbo au Mikoa fulani katika enzi za utawala wabunge ilihali jambo liliolofanywa ni dogo sana na halina manufaa mapana kiuchumi kwa nchi bali kwa umaarufu wa kisasa kwa mtu fulani, haitusaidii.Kwa mfano kila mmoja ajiulize hivi kuna faida gani kutumia bajeti ya Ujenzi wa Barabara kwa kutawanya bajeti ya sh bilioni 500 kwa ajili ya Km 100,000 nchi nzima? Ni wazi km hiso zipo mikoa yote na kwa hiyo Bilioni 500 zikigawanywa kwa km laki 1 ni wazi kila barabara itapata mgao wa sh milioni 5 tu. Je sh Milioni 5 kwa barabara yenyе Km 300 au Km 50 au km 100 zitafanya nini kwa ajili ya ujenzi wa lami ilihali km 1 inakadidiriwa kugaharimu sh bilioni 1? **Nothing.**

Nadhani tubadili tabia tukubali kuacha ubinasi kwamba na mimi mwaka huu nipewe barabara bali tuamue kama taifa kujenga barabara za Lami kikanda na kwa miradi mingine iwe hivyo hivyo ambapo hata kama ni bajeti kidogo lakini mwisho wa siku *Impact assessment* ikifanyika kwa fedha hiso kidogo zitaonesha matokeo mazuri tofauti na sasa Reli au barabara inahitaji sh bilioni 500 lakini tunakuwa wajinga kupindukia hadi tunashindwa kuamua ziende

Nakala ya Mtando (Online Document)

labda barabara za mikoa au ukanda fulani wa kusini mwa nchi yetu au ukanda wa kati au ukanda wa mashariki au ziende zikajenge reli huku miradi mingine ikisubili bajeti zijazo. Mheshimiwa Spika tutoke huko tujenge nchi yetu, siasa hizi hazitatusaidia.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasilitiza kwamba tuweke mkazo katika kuinua sekta zote zinazozalisha mali na huduma muhimu kama vile Usafiri wa Anga; Barabara; Maji; Elimu; Afya. Kuwekeza fedha nyingi kwenye maeneo ya matumizi ya kawaida kama ilivyo hivi sasakunaligharimu taifa letu na kamwe hiyo reli na sekta za bandari, elimu, Sekta ya utalii na nyinginezo hazitaimarishwa kwa kuendekeza utaratibu wa sasa. Utamaduni huo ni mbaya, haufai mahala popote pale na umepitwa na wakati. Wanasiasa wenzangu tujenge nchi yetu, tuamue sasa kwamba tuanze na kuhamisha mafungu ya fedha za matumizi yasiyo ya lazima na kuzipeleka kwenye reli na bandari mwaka huu na tuanze na hizo za uchukuzi zenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Moses Joseph Machali (Mb)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI NA
WAZIRI KIVULI WA UCHUKUZI**
24 MEI 2014

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Machali, kwa kuitia Hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Uchukuzi. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya uchangiaji kuanza, wakati Mheshimiwa Tundu Lissu anaongea hapa ndani, aliwagusa baadhi ya Waheshimiwa humu ndani akiwemo Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Kwa kweli huwa ni *natural justice* kwamba, Mbunge akiguswa na yupo, ni vyema akapewa dakika mbili au moja ya kuweza na yeye ku-clarify kidogo. Kwa sababu kuitia uguswaji huo, jina la mtu linaweza likawa limechafuka sana.

Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ninakupa na wewe dakika mbili za kugusia jambo hilo kwa namna ulivyoguswa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kabla sijaongelea hoja aliyoisema Mheshimiwa Lissu, nikuombe Mwongozo wako na ultendee haki Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni kwa ajili ya muda sitasoma, lakini nadhani ni ya 68(7), ambayo inamzuia

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mbunge kuongelea jambo ambalo ana masilahi nalo ya binafsi, kwa namna ambayo linampa yeye masilahi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Lissu ni Wakili na anamtetea Mfanyakazi aliyefukuzwa na Shirika hili ambalo analishambulia kwa matumizi mabaya ya madaraka. Amefuja fedha na yeye ndiye anamtetea. Leo hii anapokuja kuongea *against* Shirika hilo, kwa mujibu wa Kanuni, Mheshimiwa Naibu Spika utaongoza, nadhani anakiuka Kanuni hii ambayo inamtaka kwanza aweke wazi masilahi aliyonayo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mimi namshangaa sana Mheshimiwa Lissu; kwanza, anamtetea mtu aliyefuja fedha kwenye Shirika lile lile, lakini yeye anawashambulia Viongozi waliofafuta fedha kwa ajili ya madawati, maji na solar. Mimi kwa kweli huwa nashangaa sana! Sasa hii anayoisemea na anasema Wabunge wengi walipata fedha kwa ajili ya maendeleo ya Majimbo yao ni wa CCM. Mimi sioni kama ni jambo baya, hii inaonesha tu ni kiasi gani Wabunge wa CCM wanashughulikia matatizo ya Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunavyoongea, baada ya Katibu Mkuu wa CCM kupitia Jimboni kwake na kukuta kuna kijiji kimoja tu kwake kimepata umeme, nadhamiria kuandika Mradi mwingine kuomba solar zipelekwe kwenye jimbo lake. Ninategemea nitaomba kwenye *corporate social responsibilities* za mashirika haya haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba ulitolee Mwongozo suala la Tundu Lissu, kushambulia Shirika ambalo limemsimamisha kazi mtu aliyetumia vibaya madaraka na yeye akiwa Wakili anaanza kuwashambulia watu waliochukua hatua dhidi ya mtu huyo. Anatetea watu walioharibu kwenye Shirika hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tumkumbushe tu kwamba, ni kazi ya Mbunge kuyakumbusha Mashirika ambayo yana *corporate social responsibility*, kusaidia katika mambo ya maendeleo katika Majimbo. Nakushukuru. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU): Mheshimiwa Naibu Spika, samahani kabla hujasimama. Pia kuna jambo limeguswa hapa kwamba, katika Kambi yao kuna mtu amechota mabilioni. Yeye anafuatilia shilingi milioni mbili, lakini kwenye Kambi yao kuna mtu amechota zaidi ya shilingi bilioni moja. Basi Kiti chako nacho kwa sababu hiyo ni fedha ya umma, kiseme ni hatua gani zinachukuliwa? Waziri anayehusika anasema kuna mtu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ana warrant ya kukamatwa kwa ajili ya kuchukua fedha for personal benefit, siyo kama hizi ambazo zimeenda kuhudumia Watanzania. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwigulu Nchomba, kwa hayo uliyoyazungumza, nitayapitia wakati mwingine, sasa hivi tuokoe muda. Tunaendelea na uchangiaji, kama nilivyosema wakati ule, ni vizuri kuwa makini, ukinyoosha kidole hiki kimoja basi kuna vidole vingine vinakunyoooshea na wewe; ni vizuri kuwa makini katika mambo haya.

Mimi Shule ya Msingi nilisoma Singida, Wilaya mpya ya Ikungi, ninaposikia ni kijiji kimoja tu kina umeme ninaogopa kabisa, lakini 2015 ndiyo hiyo inakaribia.

MJUMBE FULANI: Ni CCM hiyo.

NAIBU SPIKA: Utasema CCM lakini mwakani hawatasema CCM, ni Mbunge uliyepo madarakani; hakuna cha CCM wala NCCR, wala CUF. Mbunge aliyepo madarakani kama hakuna umeme kwenye Jimbo lako utajibu Mbunge wewe. (Kicheko)

MBUNGE FULANI: Uongo!

NAIBU SPIKA: Kwa mgombea mpya anaweza akawa na kisingizio, kwa Mbunge uliyeko madarakani andika umeumia. Mbunge mwenyewe ndiye utakayejibu kila hoja ya Jimbo lako. Hivi visingizio ni saa hizi, wakati huo hautapata muda wa kusema hayo.

Katika uchangiaji, mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mmh, piga sana. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kusema kidogo tu katika hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Timu yake, kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika eneo hili muhimu; hongereni sana, kazeni buti twende mbele. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nitakuwa na maeneo kama mawili, matatu tu, nikianza na Bandari yetu ya Dar es Salaam, ambayo ni kitovu cha kukuza biashara, huduma na uchumi wa nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ipo, ni mizuri, lakini tuanze na yale ya haraka ambayo tunayaweza na hatuhitaji msaada wa mtu yeyote. La kwanza, ni hili la kuongeza ufanisi katika Bandari yetu.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejitalidi kwa maeneo ya muda wa meli kukaa bandarini, lakini tunaweza tukafanya zaidi ya hapo na inawezekana. Haiwezekani wenzetu wa hapa nchi jirani, Bandari ya Mombasa, wao ni chini ya siku moja, ya kwetu bado ni siku nne na nusu, tuseme siku tano. Tunaweza kabisa kuongeza ufanisi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni meli kukaa nje zikisubiri kuingia bandarini, bado msongamano ni mrefu sana, tukileta ufanisi bandarini hata msongamano wa meli utapungua kutoka kiwango cha sasa cha wastani wa siku saba mpaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la msingi sana ambalo ni għarama kubwa za wharfage ambazo tunalipa katika Bandari ya Dar es Salaam ukilinganisha na Bandari ya Mombasa. Hili ni la msingi sana, wakati nilipobahatika kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mheshimiwa Spika ya kutafuta vyanzo vipyā vya mapato, eneo hili tumeliona na Serikali isiposikiliza, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Ni vyema tukalichukua mapema sana, wharfage fees viwango vyake viko juu sana kulinganisha na Bandari ya Mombasa. Kuna visingizio vingi sana kwamba, kwa nini eti haziwezi kushuka, zinaweza kushuka. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Gati na 13 na 14; jaani, jamani nchi gani hii, miaka 13 tunaongelea wimbo huo huo, mtindo huo huo, tatizo ni nini hasa? Kwenye Ukurasa wa 58 na 59 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wamesema maneno matamu kuhusiana na Gati na 13 na 14. Tahadhari yangu, Benki ya Dunia sote tunaifahamu, tusifikirie kwamba, tumepata mwarobaini. Mtakuja kukumbuka maneno yangu ya leo, watakuja na stori lakini ninawaambieni Gati na 13, 14 haitajengwa mwaka ujao wa fedha na wala mtondogoo. Kama tunataka meli kubwa zije katika Bandari ya Dar es Salaam, wao wataangalia makasha ambayo yanaingia kwa mwaka, hata tukipandisha wao watasema haiwezekani labda mpaka mwaka 2025. (Makofij)

Kumbukeni mchango wangu wa leo kwa njia ambayo mmependekeza, lakini Bandari ya Dar es Salaam kama bandari zote Duniani, ukienda kwa utaratibu wa kushirikisha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, utaona wapo wawekezaji. Tusiende na njia hizi za watu ambao tunawafahamu kama Benki ya Dunia; ninwapenda sana, nimefanya nao kazi lakini siyo katika utaratibu huo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ndiyo huo, Airport ya Mwanza. Mimi nilipobahatika kuwa kwenye Wizara hii ikiwa inaitwa Miundombinu, nilikataa ile michoro ya awali ambayo ilikuwa imepitwa na wakati. Nikasema tuhu ishe kwa sababu unaiona traffick ya Mwanza inavyopanda haraka, kipindi kile ilikuwa 200,000 kwa mwaka, sasa hivi ni zaidi ya 650,000 na tunaona inavyopanda. Sasa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuna urasimu ndani ya Wizara ya Fedha ambao ni lazima, mimi ningelipenda, leo nitaondoa shilingi nisipoelezwa kwa nini kuna danadana katika ujenzi wa Kiwanja cha Mwanza. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia fedha ambazo zimetolewa tangu Mkandarasi aingie pale mwaka 2012/2013. Naungana na Kamati ya Kisekta kwa hayo waliyoyasema kwenye taarifa yao. Kuna vitu fulani tufike kama Wabunge na kama Watanzania tuseme, haya tunayakataa. Fedha za Mwanza lazima zitoke. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeona niyaseme hayo, lakini kwenye reli naiomba Serikali, naelewa hatuwezi kujenga Miradi hii bila kufanya usanifu, upembuzi yakinifu, usanifu wa awali na baadaye usanifu wa kina; lakini haiwezekani kwa kipindi cha miaka mitano tunafanya usanifu, usanifu, usanifu, tufike mwisho. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa timu iliyopo pale Wizarani inayaweza haya, tujipange kwa yale ambayo tunaweza tukayatafutia fedha: Dar es Salaam – Tabora – Isaka kwenda Kigali – Keza – Msangati. Tabora – Kigoma, Kaliua – Mpanda na hata hii mpya mnayofikiria ya Uvinza – Msongati, lakini baadaye Isaka – Mwanza, tumalize stori hizi. Vilevile Reli ya Tanga – Arusha – Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiyaafanya haya ndiyo utaona jinsi unavyosema Mwenyezi Mungu alipendelea Tanzania kijiografia kuweza kutumia nchi jirani hasa Ukanda wa Maziwa Makuu. Tukienda na maneno maneno, we have now to walk the talk, tuone vitendo vinakuwa vingi kuliko maneno. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru kwa hayo. Narudia, Gati na 13 na 14 na ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam, ni muhimu. Tunaweza kuyafanya yale ambayo hayahitaji fedha. Mwanza Airport, lazima fedha itoke na Reli ya Kati na mitandao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa ushauri wako. Mheshimiwa Abdulkarim Shah, atafuatiwa na Mheshimiwa Rita Mlaki!

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya pili kuweza kuchangia katika Wizara hii nyeti, inayosimamia masilahi ya uhai wa Wananchi na Taifa letu kwa ujumla, kama moja ya mishipa ya damu. (Makof)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kwa dhati kwa niaba ya Wananchi wa Mafia, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jinsi alivyoweza kupigania na kuhakikisha Uwanja wa Mafia na Gati la Mafia vinajengwa na vinakamilika. Naomba nimshukuru kwa niaba ya Wananchi wa Mafia, kwa heshima za kipekee. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, heshima hizo pia naomba nizipeleke kwa Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe, Naibu wake Dkt. Chizeba na Katibu Mkuu Dkt. Mwinjaka. Nakumbuka siku ile ambayo Mheshimiwa Rais, alipokuwa anafungua Uwanja ule alitamka na kusema, Wizara hii ina watu wenye taaluma kubwa, kila mtu Daktari. Alimtaja Dkt. Mwakyembe, akamtaja Dkt. Chizeba na akamtaja Dkt. Mwinjaka, kwamba, ni watu ambao kama alivyowasifia Mheshimiwa Chenge, naamini yale wanayoyapanga wakiyataka yatakamilika. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Gati limefunguliwa, lakini nimefurahi zaidi, ninaomba niwe wakala wa Mheshimiwa Waziri wa kuwaambia Watu wa Mafia kwamba, lile Gati, maana yake tulikuwa tunapigiwa kelele halitumiki, lilikuwa halitumiki kwa sababu lilikuwa halijakamilika. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake pamoja na Mamlaka ya Bandari, kwa kuweza kututengea shilingi milioni 400 kwa ajili ya kutengeneza baji la pale chini ili vyombo vidogo viweze kufika na boti ndogo ndogo ziweze kufika pale na Wananchi wao kama abiria na mizigo yao waweze kupanda juu au kuteremshwa kwa hali ya usalama. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Wizara nzima na ninaomba apokee shukrani hizo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimshukuru zaidi Mheshimiwa Waziri, kilio chetu Watu wa Mafia ambao wengi tunatumia bahari, baada ya kuona kwamba tutatengeneza Mafia, lakini akakumbuka na Nyamisati. Japokuwa kwenye kitabu hapa ameandika Nyamisati Mkuranga; Nyamisati ipo Rufiji. Nasema kwamba, tendo la kutuwekea shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukarabati au kuijenga vizuri zaidi Bandari ya Nyamisati, kwetu sisi ni faraja kubwa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fursa hii nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Marombwa, maana na yeyé pia alikuwa ananisaidia hata kupiga kelele wakati wa ziara za Viongozi wanapokuwa Rufiji, basi na yeye alikuwa akilizungumzia sana na mimi nilikuwa napata taarifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Marombwa, *Inshallah* na wewe Mwenyezi Mungu atakubariki, kutohana na sisi ndugu zako Watu wa Mafia.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Amina.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ABDULKARIM E. SHAH: Jambo la pili, tumejengewa Kiwanja cha Ndege cha Mafia, bahati mbaya, naomba uangalie picha, picha unayoiona ile ni uzio, ndiyo mwisho wa Uwanja wa Ndege. Eneo la mkono wa kushoto unaona kama barabara ya udongo, ile ni barabara ya tatu. Ilikuwepo ya kwanza pakabomokea, ikaja ya pili ikabomokea na ile pale ya mwisho ya tatu, kilikuwa kimebakia kinjia kwa ajili ya kupita kwa miguu na sasa hapapitiki tena.

Sasa ninaomba sana, umeniambia umetenga hela kwa ajili ya kulifika lile shimo; ninachokuomba na ninaomba nitoe ushauri na mimi japokuwa siyo injinia, ninaomba niseme kwamba, wakati wa kuandaa miundombinu ya kutiririsha maji kutoka uwanja wa ndege, sasa hivi utaratibu wekeni mabomba kama nilivyokuwa nimewaambia wale wataalamu japokuwa sijui walidharau au pengine pesa ilikuwa haikutsha; kwamba, mabomba yale yafike mpaka baharini. Maji yakifika baharini kama lile bomba lililokuwa pale mbele ya lkulu, hali ya Kisiwa chetu itakuwa salama.

Kwa hali ilivyo sasa hivi, dalili zote za kugawanyika Kisiwa chetu zinaonekana kutokana na maporomoko ya maji yaliyosababishwa na mitaro miwili iliyokuwa inapokea maji kutoka Kiwanja cha Ndege na mvua kuwa nydingi na hatimaye kuwa vile. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, aangalie lile karavati ilikuwa limeshakatika na sasa linaingia ndani ya Uwanja wa Ndege. Kwa hiyo, hili ninaomba aliangalie. Nimeongea na watu wa MCC wamesema watacaa na ninyi muweze kuona, lakini ninaamini katika ukaazi huo pesa itapatikana.

La mwisho, nimshukuru zaidi Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kuhusu ujenzi wa jengo jipya. Umetenga shilingi bilioni moja nukta sifuri tano ya ujenzi wa jengo jipya la abiria pamoja na mambo mengine yanayohusu kukamilika kwa uwanja huo. Ninaomba sana angalieni tuweze kumalizia na taa za ndege za kuwezesha ndege kutua wakati wote; hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Sasa tunapokwenda tena na mpaka tukimaliza uchaguzi, wakati mwingine jambo dogo tu, yale mema yote yaliyofanywa yanaweza yasiwe na maana tena kwa baadhi ya watu ambao vichwa vyao wewe mwenyewe unavijua na wengine tunawasikia kila siku. Kwa hiyo, ninaomba sana, nimesimama hapa leo kwa ajili ya kuwashukuruni kwa niaba ya Wananchi wa Mafia.

La mwisho kabisa ni ushauri, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri, kutokana na hali jinsi ilivyo pale sasa hivi, huwa tunapata shida kubwa sana ya kukatisha kwenda hospitali, kwa sababu Hospitali ya Wilaya iko upande wa pili wa uwanja na karibu 75% ya Mji wa Mafia uko upande huu wa pili ambao umekatika. Kukatiza uwanja ni marufuku hata mimi sikubaliani, lakini ninakuomba sasa hivi mtusaidie tuweze kutumia angalau mita kumi kutoka

Nakala ya Mtando (Online Document)

kwenye uazio ule, itengenezwe njia ndogo ya dharura ili watu waweze kupita angalau ambulance tu iweze kufika kwa haraka au bajaji katika kusaidia watu kama ni wazazi au wagonjwa kwa ujumla pale mtakuwa mmetusaidia sana wakati huo tukisubiri kufukiwa kwa hili korongo.

Uwanja wetu ni mita 1,600, wakati tunaangalia huku basi ninaleta tena ombi ili ATR 72 iweze kutua kwa uhakika. Zile mita 400 tumalizieni kabisa nafasi ipo, kwa hiyo, tumaomba mwongeze mita 400 mpunguze mita 100 upande wa huku ili magari na watu waweze kupita hasa katika shughuli hizi wakati mtu anapokuwa mgonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nikushukuru sana, niwashukuru Mawaziri, Viongozi wote, TAAs, Kaka yangu Suleiman, Bandari na wengine wote, Mwenyezi Mungu awabariki. Ahsante sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Abdulkarim Shah. Mheshimiwa Rita Mlaki, atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia!

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa kuchangia hoja ya Waziri. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, kwa kazi nzuri sana anayoifanya na wote tunaiona. Pale ambapo ninaona mambo hayaendi sawasawa, nina uhakika ni Serikali kwa ujumla wake imeshindwa kumpatia fedha. (Makofii)

Nitaongelea Shirika la Ndege tu na siyo kitu kingine. Ni jambo la kusikitisha sana, kuona hali halisi ya ATCL. Hali ya hilo Shirika ni mbaya sana na kuna umuhimu mkubwa sana wa nchi kuwa na usafiri wa ndege; hiyo inasaidia kukuza uchumi, kuleta maendeleo na pia kuondoa kero za mara kwa mara. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hiyo ni *National Flag Carrier*, ambayo ni prestigious kwa nchi kuwa na ndege zetu wenyewe. Tunasikitishwa sana kuona tunashindwa na nchi kama Rwanda, Malawi na Uganda, ambao wana economy ndogo kuliko sisi. Tumeambiwa kwamba, ATCL inadaiwa shilingi bilioni mia moja na thelathini na tatu; hilo siyo deni kubwa kabisa kwa Serikali; Serikali itafute pesa. Nami ninaweza kusema, kama mnaona inakuwa ngumu, kuna mapendekezo yalikuja ya Kamati ya Chenge One, ambayo ameyataja hata yeye mwenyewe Mheshimiwa Chenge, ambaye tunaye hapa. Serikali itafute fedha tuweze kununua ndege au tutafute mbia vilevile; lakini kwanza tulipe hili deni la ATCL bilioni mia moja thelathini na tatu, kama tuko serious tunaweza tukailipa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mawazo kwamba, tutafute wataalamu kama Kenya Airways ilivyofufuliwa. Alikuwepo Mwenyekiti,

Nakala ya Mtando (Online Document)

ninadhani alikuwa anaitwa Titus Naikuni, aliisaidia sana Kenya Airways mpaka sasa inashindana na Mashirika ya Kitaifa kama Emirates, KLM na mengine. (Makofij)

Tusiogope kwa sababu Duniani Mashirika mengi ya ndege yanaendeshwa na Wataalamu, hili ni Shirika ambalo liko very sensitive. Ninakumbuka kuna tajiri mmoja anaitwa Richard Brownson, alisema, *if you want to be bankrupt, start an airline*. Akimaanisha kwamba, tafuta Wataalamu wa kutosha. Kwa hiyo, mimi ninaomba tujitahidi sana na nina uhakika Tanzania wapo, tumeona mfano wa watu wenye akili sana kama DG wa National Housing, Nehemia Mchechu au DG wa NSSF, Ramadhani Dau, wamefanya mambo makubwa. Hebu tujaribu kutafuta watu wenye uwezo ili waweze kuendesha Mashirika kama haya. (Makofij)

Tukubaliane kabisa na kwa mara ya kwanza leo ninaogopa kwamba nitatoa shilingi mpaka nione huu mkakati Serikali ilionao kuweza kulisadia Shirika la ATCL. Ninakumbukla Serikali walisema kuwa, wangenunua ndege mbili mwaka uliopita, nina uhakika Mheshimiwa Waziri Serikali ilikubana japo wewe pia ni Serikali. Ningombwa sana na mkasema mna mazungumzo na Watu wa China ili kutazama tutaweza kufanya namna gani. Pia huyu Prime Minister wa China alipoongelea katika Mkutano wa AU na Heads wa AU, aliahidi kusaidia Aviation Sector ya Afrika. Wenzetu Kenya waliposikia tayari wamekwishasaini MoU na Kampuni ya Hainan Airline; sisi vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona sasa Wachina wengi wanakuja na Watali wengi wanatoka China. Nchi yetu sasa hivi kwa sababu ya amani tunafaidika sana kwa ajili ya hayo. Bado nitarudia kwamba, hili suala la kuwa na ndege siyo suala la starehe; hapana, lina umuhimu mkubwa sana wa kuweza kusaidia nchi yetu na pia kuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza sana jinsi ambavyo wameweza kukarabati viwanja vya ndege ambavyo vitasaidia, lakini tunakarabati kwa ndege za wenzetu. Tujitahidi kukarabati tununue ndege tuweze kutumia hivi viwanja. Nimeona hapa katika page 83 ya Hotuba ya Waziri, anaongelea kulisaidia Shirika la ATCL kuijendesha kibiashara. Ninashindwa kuelewa hapa ni kwa vipi kwa sababu sioni kabisa jinsi ambavyo litajiendesha ikiwa bado kuna deni na hapohapo tunaambiwa kuwa tusubiri, hatuwezi kupata mbia kwa sababu ya deni hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile bado nina muda, ninaomba sana specifically, Waziri atakapokuwa anajibu jioni, aongelee sana kuhusiana na Kampuni ya Wachina ambayo mmekwishaanza mazungumzo na ikiwezekana

Nakala ya Mtandao (Online Document)

watusaidie, watukopeshe ndege. Kama wao wanasema wanaweza kutukopesha, sisi tunakopesheka na hilo ningeomba sana kulisikia.

Vilevile tuna mpango gani na hii kauli ya *Prime Minister* ambaye ameongelea kwamba, wanaweza wakasaidia *Aviation Industry* na tumeona wenzetu China wana mapenzi na sisi na tunaweza kusaidia sana sekta hii ikiwa kama tutachukulia umuhimu wake?

Baada ya kusema hayo, bado ninaomba tutumie Kamati yetu ya Bajeti, tutumie Ripoti ya *Chenge One*, ambayo imeeleza mikakati hii na tujaribu kutafuta fedha za kuweza katika hii *Airline*; ni aibu na tunasikitishwa sana na popote pale tutakapokuwa *Airport* kukiwa na cancellation ya ndege za watu, tunashutumiwa sana kama Viongozi kwamba, kwa nini mpaka leo nchi kama hii kubwa bado hatuna ndege ztu wenyewe!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, nikitegemea majibu ya jioni kama nitajibiwa, ama sivyo nitatoa shilingi. Ninashukuru sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rita Mlaki. Mheshimiwa James Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Amour!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Bandari ya Dar es Salaam. Kwenye Bandari kuna vigezo vikuu viwili, Bandari iaminike na ufanisi wake. Sasa Bandari yetu ya Dar es Salaam ni kweli imeanza kujitahidi, lakini kwa kiasi kikubwa bado mshindani wetu ni Bandari ya Mombasa kwenye Ukanda huu. Ukipanua Bandari au ukipanua Bandari, ni lazima uunagnishe na reli na Reli yetu ya Kati bado mkakati wake huoni ukienda kwa kasi kama wenzetu wanavyokwenda kwa kasi Mombasa na Lamu kule Kenya. (Makofii)

Tusipowekeza kwa makusudi kabisa tunaweza kuona hapa kwamba, tunategemea fedha za Serikali, Gati Namba 13 na 14, zaidi ya miaka mitano sasa tunazungumza lugha hiyo hiyo, ingebidi tutafute wawekezaji tuwe na Miradi ya PPP kwa pamoja na tuingie kwenye *Build, Operate and Transfer*; na hii inafanyika Duniani kote. Tukitegemea Serikali ibaki na kazi yake ya huduma za Mahakama, Haki za Binadamu, kuhudumia huduma muhimu, lakini Miradi mikubwa kama ya Bandari, ya Reli, PPP ifanye kazi yake. Wawekezaji hawa wakiwekeza, ukipanua Bandari ya Dar es Salaam vizuri, kile kina sasa hivi kipo kwenye mita kumi, kikienda mpaka mita kumi na nne, ukafungua hili lango, ukafungua na lango la Reli ya Kati, tutakuwa tumefungua Uchumi wa Taifa letu la Tanzania.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Geographically, location yetu tuko vizuri, lakini ningeshukuru sana Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha, atueleze kwa wakati huu Bandari ya Dar es Salaam tunapata kiasi gani cha mapato ukilinganisha na Bandari iliyoko karibu ya Mombasa na wengine ili tujione tuko kwenye eneo la namna gani? (Makofii)

Swali lingine ni je, Bandari ya Dar es Salaam katika Bandari zilizoko Afrika tuko namba ngapi kwa masuala ya efficiency na liability?

Tukiweza kuunganisha pia na kutengeneza bandari kavu Kisarawe, Mradi wa Kisarawe wa Bandari Kavu umefikia wapi ili mizigo ikitolewa bandarini moja kwa moja Bandari Kavu ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam?

Msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa wakati huu limekuwa ni janga, muda wa kufanya kazi unapotea barabaran, uchafuzi wa mazingira, mafuta yanayounguzwa katika msongamano wa magari katika Jiji la Dar es salaam; hali hii ni mbaya sana. Ukiunganisha Bandari vizuri na Reli hata hizi barabara zinazobomoka kila siku kwa kipitisha malori makubwa, tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwekeza zaidi kwenye barabara, tukiacha reli na bandari, hali inazidi kuwa mbaya. Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Ujenzi kwa pamoja, mkakati wa kuwa na parking facilities kwa ajili ya ku-park magari, sasa hivi yapo mambo kiholelaholela tu, niwe mkweli, ninampongeza sana Mzee Sabodo, ambaye ameweza kutengeneza parking facility ya kuweza ku-park magari mia sita. Tarehe 18 ya mwezi huu, Waziri Mwandosya aliifungua ile parking facility. Sasa tuna mikakati gani ya kutafuta wawekezaji wengine na wao waweze kujenga parking facility za namna hiyo ili kuweza kufanya Jiji liwe kwenye order iliyo nzuri. (Makofii)

Msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ni janga, kwa mwaka unatugharimu zaidi ya trilioni moja point five, huku hatuna fedha, huku tunajiongezea umaskini sisi wenyewe. Kufanya maamuzi na kupanga ni kuchagua, tufanye maamuzi magumu tuweze kuondokana na hii kelele ya kila siku panda shuka, panda shuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni namna gani kwa pamoja kwenye viwanja vyetu vya ndege; Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam sasa hivi Terminal III sawa inaenda kwa kasi kubwa. Viwanja vya Ndege kwa mfano Mwanza, life span, muda wa kuupanua ule Uwanja ni miezi thelathini na sita, mwaka huu ni mwaka wa mwisho, miezi ishirini na minne imeshapita. Mwaka juzi walipewa bilioni nane, mwaka jana walipewa bilioni nane, lakini fedha zilizokwishatoka mpaka Aprili mwaka huu ni bilioni moja nukta sita tu na fedha zinazohitajika ni

Nakala ya Mtando (Online Document)

bilioni mia moja na tano. *Life span* yake inakwisha mwaka huu; kwa nini tusitafute wawekezaji wakawekeza tukawa na ubia nao kwa ajili ya kuujenga uwanja huu?

Uwanja wa Mwanza ni muhimu sana kwa Uchumi wa Taifa la Tanzania kama vivilyo viwanja vingine. Viwanja vinavyotakiwa kupewa kipaumbele, fanya maamuzi, weka kipaumbele Kiwanja cha Dar es Salaam, Kiwanja cha Mwanza, Kiwanja cha Kilimanjaro, Kiwanja cha Songwe, ukimaliza hiyo kwa pamoja ndiyo unaenda hatua ya pili. Ukigawa kidogo kidogo ni kwamba, tunajiongezea umaskini tu. Tunasema sungura mdogo lakini ni umaskini tu, hapa kidogo na hapa kidogo, unamridhisha huyu, unamridhisha Yule, fanya maamuzi magumu yasiwe ya kisasa. Mheshimiwa Mwakyembe, ninaamini mkiamua kufanya maamuzi hayo mtaweza. (Makofij)

Suala la usafiri katika bahari na hasa Jiji la Dar es Salaam, kwa kutumia maji kuanzia Bagamoyo huko njoo mpaka katikati ya Jiji la Dar es Salaam, tumekuwa tukiimba, ahadi zinatolewa; utaratibu huu umefikia wapi? Tunaweza kutumia Jeshi letu la Wananchi wakatutengenezea gati pale Kunduchi, wakatengeneza gati Msasani, wakatengeneza gati kule Mbweni na usafiri wa boti ukafanyika katika Jiji la Dar es Salaam, tukaondoa kwa kiasi kikubwa msongamano ambao unalitesa sana Jiji la Dar es Salaam. Tusipowekeza na tukawa makini, Jiji la Dar es Salaam hakuna movement yoyote inayofanyika na hili ni janga la Kitaifa. Ninaiomba Serekali ifikirie kwa mapana, kwa nia njema kabisa, la sivyo tunajiongezea umaskini wa kutisha wa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. (Makofij)

Nimalize kwa kuomba na kumshauri Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Timu yake, kazi wanayoifanya ni nzuri, lakini matokeo yake tusipowekeza kwa kiasi kikubwa na kuwa na kitengo cha kufikiri, yaani *think tank* ya kuwa na mawazo mapana, Dunia ya leo inavyoenda kwa kasi; Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda, wiki tatu zilizopita alishiriki kule Kenya kwenye Uzinduzi wa Bandari kupakua mizigo kwa njia ya kieletronikia. TEHAMA inavyofanya kazi katika kuondoa mizigo katika Bandari ya Mombasa. Wametoka kutoka siku saba, zikawa tano, sasa wamefika tatu na Airport ya Jomo Kenyatta siku moja. Sasa tunaenda kwa wenzetu na tuko kwenye Region hii hii, tunaona wenzetu wanaenda kwa kasi hiyo; je, sisi twende kwa kasi gani?

Je, sisi ambao tuko giant katika Ukanda huu tufanye nini? Uwezo tunao, tufanye maamuzi, tusiogope, akili tunazo, tukubali kwa pamoja mengine tuweke pemberi, tuwekeze heavily kwenye Bandari, Reli na kwenye Sekta ya Anga tutaweza. (Makofij)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa muda ulionipatia. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia. Mheshimiwa Amina Amour, atafuatiwa na Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa!

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kumpongeza Waziri na Watendaji wake, kwa kuwawezesha akina mama kuwa Marubani, Wahandisi, Madereva na kadhalika. Hili ni jambo zuri sana, lakini ninamwomba ni vyema akatueleza mpango endelevu ili tuje mpango kamili wa kuwawezesha wanawake kwa kipindi kijacho cha miaka mitano na miaka kumi, isiwe kwa mwaka huu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepitisha Sheria ya PPP, lakini katika bajeti yetu huwa tunategemea mapato ya ndani, mikopo na misaada. Hatushirikiani na PPP, hakuna nchi yoyote ambayo inaweza kuendelea bila ya kuwa na ushirikishwaji wa sekta binafsi; kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aone umuhimu wa suala hili na alitilie mkazo.

Nina maswali mawili ninataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri; katika Wizara yake ni Miradi mingapi ambayo ameipeleka PPP iliyokuwa tayari na kufanyiwa *feasibility study?* Miradi mingapi ambayo anaitangaza ili wenyewe uwezo kama sisi tuingie PPP?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea nakuja kunako maendeleo ya viwanja vya ndege. Viwanja vya ndege, vina uwezo wa kujitegemea vyenyewe endapo Wizara ya Fedha itawapa asilimia mia ya mapato wanayokusanya. Kwa namna hiyo, wataweza kuendelea kuleta maendeleo katika viwanja vyao vya ndege na mapato mengine yatakuja kwenye bajeti. Bila kufanya hivyo tutaanza kusuasua na vizuri Wizara ya Fedha ikiwapa iwaambie mapato mnayochukua ni kwa ajili ya maendeleo, siyo tena msururu uwe mrefu, leo, kesho, sijui ipite wapi halafu wanapewa 20% au 80%.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Fedha awape mapato yote asilimia mia moja ili waweze kuendesha viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo tu, ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Amina Amour, kwa kutunza muda. Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nataka nizungumze mambo mawili tu. Jambo la kwanza,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

napenda niishauri Serikali na Wizara hii kwa ujumla; matatizo makubwa tunayoyapata katika uchukuzi na misongamano mingi Dar es Salaam ni kwa sababu tumeshindwa kutofautisha kutengenisha Dar es Salaam na Dodoma. Ni kwa nini Serikali hatujaifanya Dar es Salaam ibaki kuwa business city na tukahamisha shughuli zote za Kiserikali zikawa Dodoma? (Makofii)

Tukifanya hivyo, Uwanja wa Ndege wa Dodoma utapanuliwa utakuwa mkubwa na shughuli nyingi za Kiserikali zikifanyika hapa, wageni watakuja, utakuwa Uwanja wa Kimataifa watatua hapa. Mambo ya *lobbying, deals* nyingi zitafanyika hapa za Kiserikali tukaicha Dar es Salaam kule inashughulika na mambo ya kibiashara.

Huu ni ushauri, nautoa bure kabisa, hamhitaji kulipia fees, ni kitu ambacho kinawezekana kabisa. Mji huu ukiwa wa Kiserikali na Mikoa mingine ya jirani itanufaika sana na shughuli za Kiserikali zikiwa hapa. Mmesema muda mrefu Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba, mtahamia Dodoma, mmekuwa hamhami, haya yote yanababisha matatizo. Shughuli zote Mawaziri mngekuwa hapa, kila kitu kingefanyika hapa, tuiache Da es Salaam ikiwa na shughuli za kibiashara ili Mikoa ya Iringa, Singida na Mikoa jirani, iweze kunufaika na kuifanya Dodoma uwe Mji wa Kiserikali.

Kwa kusema hivyo, nina maana kwamba, lazima Serikali na Wizara hii muwe *strategic*. Tukiweka Uwanja wa Ndege hapa Dodoma, utarahisisha utendaji kazi wa watu wote wanaokuja Dodoma, kwa sababu upo katikati kama mawazo ya Nyerere alivyokuwa anafikiri.

La pili, nilitaka nizungumze tena kwa sababu hizi Wizara zote zinaingiliana na Wizara zingine. Kiwanja chetu cha Ndege mwaka jana Mheshimiwa Makyembe na mimi niseme kabisa na niwaombe Wabunge wa Iringa hapa tuungane mkono kuitoa shilingi leo. Mheshimiwa Profesa Msolla, Mheshimiwa Lukuvi na Wabunge wengine akina Mheshimiwa Chiku Abwao na Mheshimiwa Ritta Kabati, wote tusaidiane kutoa shilingi. Kiwanja hiki mwaka jana mlituahidi kwamba, mtaleta pesa na mtakitengeneza. Leo kwenye kitabu hiki sioni matengenezo ya Uwanja wa Ndege wa Nduli. Ndugu zangu, Kiwanja cha Ndege cha Nduli nacho kipo katika maeneo mazuri. Nimesema Wizara hizi mnategemeana wote, hatuwezi kupata pesa kama hatuta-boost utalii. Hivi sasa Wizara ya Maliasili imetangaza wazi kwamba, inataka ku-boost utalii Kusini mwa Tanzania.

Mta-boost vipi wakati Kiwanja hiki ambacho kingeleta watalii wengi pale Iringa Mjini na maeneo mengine wangenufaika nacho hamjakiwekea pesa? Ningombaa Mheshimiwa Mwakyembe, kama mlivyoahidi mwaka jana ni kwanini sasa hivi hamjaweka? Vilevile mna utaratibu gani na ni lini kiwanja kitafanya kazi ili tuongeze utalii? Kwa sababu tutakuwa tunasema tu kwamba,

Nakala ya Mtando (Online Document)

tunataka kukuza utalii upande wa Kusini wakati utekelezaji wake haupo. (Makofii)

Kiwanja hiki kikipanuliwa zikatua ndege za abiria, tuna mbuga ya wanyama kubwa ambayo nimesema ni kubwa kuliko zote hapa nchini. Kwa nini tunapata kigugumizi; kwa nini hamna ushirikiano na Wizara ya Maliasili mkaona uwezekano wa kupandisha watalii pale? Kama nilivyosema, matokeo tutakayoyapata kupata pesa, zitasaidia kuleta maendeleo katika maeneo mengine ambayo hii ina-link pamoja na kukifanya Kiwanja cha Ndege cha Dodoma kiwe kikubwa. Hakuna sababu ya kuhangai. Misongamano mingi tumeiweka Dar es Salaam ni kwa sababu ya watu wana *personal interest*, watu hawataki kuhamisha hapa!

Kwa hiyo, ninaomba katika maelezo yenu mniambie, kwa sababu mwaka jana tuliondoka hapa kifua mbele na Mheshimiwa Mwakyembe ni shahidi, toka nimeingia Bungeni hapa mwaka wa kwanza, nimezungumzia Kiwanja cha Nduli. Mwaka wa pili Kiwanja cha Nduli na sasa hivi mwaka wa tatu na wa nne Kiwanja cha Nduli, sioni kama mnanisikiliza. Naomba leo mniipe majibu nikawaambie nini Wananchi wa Manispaa ya Iringa kuhusu Kiwanja hiki?

Viwanda vilivyokuwepo Iringa vyote Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliviuua. Sasa kwa sababu viwanda hivi vingi viliuliwa Iringa Mjini hatuna viwanda. Mkao wa Iringa tunatoa mbaa nyngi na Mungu ametujalia hiyo mbuga ya wanyama ili tuongeze vipato. Tunategemea Kiwanja hiki kikitengenezwa madereva taksi watapata pesa na wauza mchicha na mbogamboga, wale wakulima wadogo wadogo watafaidika na si Iringa Mjini tu, tutagusa Majimbo matatu; Jimbo la Iringa Mjini, Isimani na Kalenga.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, leo ninawaomba, nirudie tena; Mheshimiwa Profesa Msolla, Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Kigola, tusaidiane kutoa shilingi, kiwanja chetu muda mrefu hakitengenezwi kwa ajili ya uchumi wa Iringa Mjini. Bila kumsahau Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Chiku Abwao, wote tusaidiane kuhakikisha Kiwanja hiki kinapata pesa msimu huu. Ninawashukuru Wabunge waliotangulia kama Marehemu Galinoma na Wabunge wengine, kwa kweli walisaidia, hii barabara inayokuja Iringa inayoendelea kujengwa itaongeza utalii.

Nisisitize kwamba, ili tuondokane na tatizo la msongamano Dar es Salaam, tunasema bandari inachelewa kufanya kazi, tunazungumzia misongamano mingi; kama Serikali haitahamia Dodoma, mtakuwa mnadanganya. Tutaendelea kupoteza pesa nyngi na tutaendelea kuwahadaa Wananchi pesa nyngi zitapotea. Kwa hiyo, Serikali iamue kwa makusudi kabisa, Dar es Salaam ibaki kama business city halafu shughuli zote za Kiserikali zihamie huku.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini hili utaliunga mkono kwa sababu na wewe utanufaika nalo kama Uwanja wa Ndege hapa utapanuliwa pamoja na Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Msigwa. Kama kuna siku umeongea Mzee kwa kweli leo umegusa penyewe kabisa.

Mheshimiwa Kikwembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Paulina Gekul!

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda niwapongeze Wizara hii, kwa namna ambavyo wanajipanga katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Moja kwa moja siyo kwamba nawapongeza tu pongezi hizi ziishie hapa wasiendelee kukarabati reli zetu za kutoka Tabora – Kaliua – Mpanda; hapana, waendelee na mipango hiyo, ili waweze kuleta ufanisi katika reli hiyo, kwa sababu Mjerumani alikuwa anaelewa umuhimu wa ile reli ndiyo maana ikawepo. Kwa hiyo, naomba na Serikali pia ijue umuhimu wake ili kuweza kuwasaidia Wananchi wa eneo lile na kuwarahisishia usafiri wa ujumla kutoka Mpanda mpaka Tabora, kwani nilikwishaongelea umuhimu wa hiyo reli.

Lingine, niliomba mabehewa ya daraja la kwanza na la pili, ambayo mpaka sasa hayajafika, niliomba mwaka jana na mkaahidi kutuapatia hamjaleta. Niliomba ukarabati wa Stesheni ya Mpanda kuhusiana na huduma za kijamii na afya, halijafanikiwa hilo. Nawaomba sasa hivyo vichwa vipyta mtakavyovileta na mabehewa, basi yafike Mpanda, Kaliua, Tabora na Urambo yafike ili Wananchi wa maeneo hayo waweze kunufaika na Mkoa mpya. Lengo la kuanzisha Mkoa mpya ule lilikuwa ni kusogezza huduma karibu kwa Wananchi na ili waweze kuwa na maisha bora ambayo ni Sera ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, niwaombe kabisa msituangushe Wananchi wa Katavi na sisi tunataka kunufaika na matunda ya uhuru.

Nawapongeza kwa kuendelea kutengeneza Daraja la Ugala. Sasa bado eneo korofi la Katumba, Kaboronge na Kambuzi. Ninawaomba eneo la Kambuzi tupate stesheni pale, ni mbali kutoka Kaboronge mpaka Katumba, Kambuzi ipo katikati, kwa hiyo, tunaomba muwapatie stesheni. Palikuwa pana *halt* pale na magenge, sasa naona katika mpango kazi wenu mtakarabati na magenge; ni jambo jema kwani magenge yatawasaidieni kulinda zile reli kwa sababu watakuwa wanapita mara kwa mara na kuzuia wizi unaotokea wa vyuma chakavu.

Ninawasifu kwa kuanzisha reli ya kutoka Mpanda mpaka Kalema. Sasa sawa, tunaenda mpaka Kalema, lakini Mkandarasi wa Kalema aliyekuwa anajenga lile gati, Mheshimiwa Dkt. Tizeba shahidi ulikwenda pale, ukawaambia Wananchi lile gati litamalizika, lakini mpaka leo hatujui hatima ya Gati la Kalema. Kwa hiyo, tunaomba tupate majibu, kwa sababu tutapeleka reli pale, mnaanza upembuzi yakinifu. Upembuzi yakinifu kama alivyosema Mheshimiwa Chenge, hatutaki uchukue zaidi ya mwaka, miaka miwili. Naelewa kabisa mnaweza mkafanya ndani ya miezi mitatu mpaka sita na mambo yakaendelea. Gati la Kalema tunataka tujue mwisho wake lini?

Mmeleta Mkandarasi, mmempa Miradi mingi, amepewa hela kiasi hajafanya kazi mmemfukuza! Kwa nini msimpeleke mahakamani na zile kodi za Wananchi?

Ninaomba niongelee suala la Meli ya MV Liemba. Katika Mipango inaonesha kwamba, ile Meli kutokana na ukubwa wake na uzee wake, itaegeshwa kwa ajili ya maonesho, kwa ajili ya vivutio vya utalii. Nini mbadala wa usafiri sasa hii meli mwisho wa mwaka mtakapoitoa kwa Wananchi wa Kalema, Sibwesa, Kabwe na Ikola wanapovuka kwenda ngambo ya pili? Tunataka kujua ama wanapokwenda Kigoma siyo lazima kwenda Burundi, hatima yao ni nini katika njia mbadala ya usafiri? Mtaiweka kwenye utalii sawa hatukatai, lakini tunataka mbadala wa meli.

Lingine, naomba niungane na Mheshimiwa Rita Mlaki, aliyemaliza kuongea, tuna viwanja vingi, hata Katavi tuna kiwanja cha ndege, lakini hatuna ndege! ATCL ichukue juhudhi za makusudi kuhakikisha ndege zinakuwepo. Sasa ule uwanja sasa hivi ndugu zangu wameu-nick name wanauita Uwanja wa Ndege za Viongozi. Maana yake ni kwamba, mpaka Viongozi waje ndiyo ndege itatua. Ina maana Viongozi wakiondoka hakuna, ule uwanja utabaki kama ulivyo. Kujenga uwanja ni jambo jema, lakini lazima tuwe na vyombo vya usafiri. Kwa hiyo, naomba sana mliwezeshe Shirika hili la ATCL angalau liweze kupata ndege kwa ajili ya kusaidia usafiri. Kama alivyosema Mheshimiwa Rita Mlaki, kupanda ndege siyo ufahari ni katika kuharakisha tu shughuli kutokana na muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la magenge naomba litiliwe mwazo; mkarabati yale magenge ili yaweze kuwasaidia wafanyakazi watakaokuwa katika yale maeneo kulinda miundombinu yenu. Mnawekeza hela ya kutosha lakini kama hamtakuwa na ulinzi wa kutosha hiyo ni kazi bure. Kwa sababu vinaibiwa vile vyuma, ni kweli mataruma, reli, wanang'oa. Yale magenge yalikuwa yanasaki sana. Aliyeyatengeneza yale magenge na aliyeweke ile reli hakuwa mjinga, kwa hiyo, tusije na mambo mapya.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Suala lingine ni ukarabati wa stesheni; kwa mfano, majengo ya Tabora pale, Jengo la Tanga, Kaliua, Stesheni ya Urambo na Singida huko, Dodoma, Morogoro. Kwa kweli mnajitahidi sana kufanya kazi, lakini na ukarabati uende sambamba na majengo. Majengo yale yamejengwa na Mkoloni hayana hata ufa, lakini leo yanageuka kuwa nyumba za Popo. Majengo mazuri kabisa, mnataka mbomoe muweke ya vioo, ya vioo yatacaa siku ngapi wakati kuna matetemeko ya ardhi huko? Kwa hiyo, tunaomba mkarabati ili tuone tunaendaje. Zile nyumba ni nzuri, tunaomba muweke msukumo katika hili suala la kukarabati Ofisi za Makao Makuu ya Stesheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa hili la upembuzi yakinifu kutoka Mpanda - Kalema ni jambo jema, mnatuwekea reli; nawashukuru sana katika hilo. Tunaomba upembuzi yakinifu sasa usichukue muda mrefu, kwa sababu tunapoongea hivi tunawapa matumaini Wananchi, wanaelewa sasa tunafunguka, sasa tunakombolewa. Tusiwape matumaini kwa kusikia masikioni, tuwape matumaini kwa kutoa mawazo yetu tuyaweke kwenye vitendo. Tufanye kazi kwa vitendo. Tumechoka kuongea, sasa tufanye kazi kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwakyembe, nimekuomba ukapande zile treni kule ukaniatalia mpaka leo. Nakuomba uende tena ukajiridhishe na mabehewa yako yalivyo. Niliwahi kusema yana panya wakubwa kama sungura ukanichecka humu ndani. Nilisema yana mende na kunguni ukanihangaa! Nakuomba uende ukajiridhishe na timu yako ama tuma timu ikajiridhishe kwenye haya mabehewa. (Makofi)

Tumeona juzi juzi yule Mwandishi wa ITV aliyeopata tuzo, aliyeongelea masuala ya reli, kama mliangalia zile programu ni mashahidi. Alioneshha halii halisi ya usafiri wa reli ni mbaya kweli na hiyo alioneshha kutoka Kigoma kwenda Tabora, sasa angeonesha nchi nzima sijui ingekuwaje ni matatizo matupu. Reli ni mkombozi wa Mwananchi wa kipato cha chini pamoja na mimi. Hebu tengenezeni reli vizuri hapa uone kama mimi nitapanda hilo shangingi, usafiri wa gari kwanza ni gharama. Nitasarisha mizigo yangu kwa treni kutoka hapa mpaka Katavi. Hebu tengenezeni reli jamani. Sawa, sambamba na barabara na nini, lakini reli ina umuhimu wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe. Mheshimiwa Paulina Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe!

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika Wizara hii ya Uchukuzi, ambayo ina mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara hii inakumbana na changamoto nyingi mno. Naishauri tu hii Wizara chini ya Mheshimiwa Mwakyembe, Waziri, ni vizuri ukaweka vipaumbele vyako walau vichache tu, ukavitekeleza kwa mwaka mmoja vikaonekana. Kwa Mwaka huu wa Fedha ukahangaika na masuala ya ndege na viwanja vyake, basi jambo likaonekana. Mwakani ukashughulikia bandari, jambo likaonekana. Kuliko kila mwaka tunazungumzia Gati Namba 14 na 13 hakuna kinachotekelezwa. Mimi ninavyoona, mnapeleka vitu vingi kwa wakati mmoja halafu mnazidiwa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishauri mwaka jana nikiwa Msemaji wa Wizara hii, nikazungumzia jinsi gani ambavyo mnapunjwa fedha zenu za Miradi ya Maendeleo na Wizara ya Fedha na nikatumia lugha kali kidogo kwa Mheshimiwa Mwakyembe. Naomba nisirudie lugha hiyo tena, niseme hivi; kupewa bilioni nne kupanga kwenye Miradi ya Maendeleo halafu ukapewa milioni 600 so far mpaka april ni fedha chache sana, ndiyo maana unaona kila mahali kilio hakiishi.

Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri ni vizuri sasa mkakaa na Wizara ya Fedha; kujua kwa nini Wizara zingine wanapelekewa fedha lakini wewe ambaye una Miradi mikubwa sana haupelekewi fedha na Miradi ambayo ingesaidia Watanzania kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye nitatoa shilingi endapo sitapatiwa ufanuzi juu ya ndege hizi zinanunuliwa kwa fedha zipo. ATCL, kwanza, wanadaiwa bilioni 133, lakini hata kuwatengea fedha wametengewa chache sana na wasipolipa haya madeni wakati huo huo kuna watu wameonesha nia ya kuwekeza; Emirates wameonesha nia, China na Kampuni yao ya IVC wameonesha nia, lakini sasa wamesita, kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati, kuwekeza katika Shirika letu hili la ATCL kwa sababu deni la bilioni 133 halijalipwa.

Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie hili deni linalipwa lini ili hawa wadau wanaotaka kuwekeza basi wawekeze? Hii ni aibu, nimewahi kusema tunapanda ndege za wenzetu Watanzania, tunatia aibu, tena tunakaa first class huko lakini ndege zetu hazipo.

Napata wasiwasi kidogo, ameandika hapa atanunua ndege mbili mwaka huu wa fedha, ukienda kwenye Kitabu cha Maendeleo, fedha hizo hazionekani! Mimi nitangaze mapema, utuambie hizi fedha unatoa wapi za kununua ndege na kila moja ina gharimu kiasi gani kwa sababu huku

Nakala ya Mtando (Online Document)

hujaonesha? Hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo mnatuhadaa Wabunge, mabook makubwa kumbe ni stori lakini hakuna kilichotengwa.

Mheshimiwa Waziri, baadaye uniambie hizi ndege mbili unanunua kwa fedha zipo na zipo kwenye kitabu gani? Mimi binafsi sijazona naona tu kama unatuhadaa.

Sambamba na hilo, Mheshimiwa Waziri unakumbuka, mwaka jana lilizungumzwa suala la Kiwanja chetu ambacho kipo Babati. Miaka yote unaweka kwenye Kitabu chako, lakini kutengeta fedha hutengei! Mwaka huu umekuja na stori, mwaka jana uliniambia hicho kiwanja kilichopo Manyara kinaitwa Ngungungu, hilo jina linakuchanganya. Ukafikiri kwamba, ni kile cha Manyara na fedha zetu ukapeleka huko Karatu. Naomba leo uniambie hilo jina limekuchanganya tena? Kwa sababu unaweka kwenye vitabu vyako, fedha huweki, unasingizia jina linakuchanganya, basi tukibatize tukiite Kiwanja cha Babati kama jina tu linakuchanganya.

Mheshimiwa Waziri, ni muda mrefu hiki kiwanja tukikileta kwako, RCC tumepitisha. Cha kushangaza, tuna Hifadhi ya Tarangire pale, watalii wote wanaotokea Arusha wanashindwa kuitia Manyara pale. Ule Mji uchumi unashindwa kukua kwa sababu hutaki kikitengea fedha hicho kiwanja, kila mwaka unasema upo kwenye upembuzi yakinifu, kitu ambacho hakiwezekani.

Naomba nipatiwe majibu kiwanja changu cha Babati umetenga kiasi gani, kila mwaka unaahidi hivyo. Vinginevyo, nitaona kitabu kikubwa ambacho kinatudanganya, lakini haujatenga chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutoza bajaji nililipeleka kwa Mheshimiwa Waziri na nimeonesha ushirikiano wa hali ya juu sana. Nilikuletea document kwamba, bajaji maeneo mengi na bodaboda na guta, tumezisamehe mwaka jana kwenye suala zima la TRA, lakini wenzangu wa Manyara wanatozwa shilingi laki moja. Nililipeleka suala hili kwa Mheshimiwa Waziri, nikamwonesha na document hiyo ya TRA, jinsi gani ambavyo wanachajiwa wakati Bunge lilisamehe wale ambaa mapato yao hayazidi milioni nne kwa mwaka wasichajiwe, tukashangilia hapa. Ninaamini alilichukua, amelifanya kazi, leo atalitolea tamko, maana amesema hata huko kwake Kyela hata zile tozo za Halmashauri, shilingi 500 kwenye stendi wakipita hawachajiwi. Kwa nini Manyara wakati Bunge tulishalisemea suala hili?

Ninaomba baadaye nipatiwe majibu ya kutosheleza na nisiponipatiwa hayo basi nitashika shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajali za barabarani, naomba mfanye ukaguzi. Madereva wa masafa marefu, let say Mwanza kwenda Dar es Salaam,

Nakala ya Mtando (Online Document)

mabasi mengi yana dereva mmoja, wanapiga mwezi mzima hawapumziki, wanachoka mwisho wa siku wanasababisha ajali. Mheshimiwa Waziri kwa nini siku moja usipande basi kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza uone dereva huyo huyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uzembe au barabara zetu kuwa mbovu wakati mwingine na yale matuta, lakini kwenye suala la uchukuzi madereva wengi, mabasi mengi yanaendeshwa na dereva mmoja, jambo ambalo linasababisha ajali. Naomba hili lifanyiwe utafiti halafu tupatiwe majibu, litasaidia sana kupunguza ajali za barabarani; vinginevyo, hali ni mbaya, ajali mnafahamu Watanzania wengi wanapoteza maisha. Kwenye hili la barabarani, naomba jitahidini muweze kuangalia nani afuutilie hili na SUMATRA ijitahidi pia ikague kwa nini haya yanajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la bima ambazo zinatolewa katika vyombo vya usafiri, maana unahuksika na uchukuzi; bima hizi wanatoa za private siyo za commercial. Chombo kile kikipata ajali utakuta hawalipwi, lakini pia hata wale abiria ambaao wamepata matatizo hawafidiwi vile inavyotakiwa. Naomba hili mlichukue, myakague hayo Makampuni ya Bima dhidi ya vyombo vyenu vya usafiri vya barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni bajaji na bodaboda, wanapewa bima ambazo siyo za commercial, lakini wanasafirisha. Siku chombo kikiharibika hawajui pa kwenda kwa sababu wao wamechukulia ni simple. Naomba mliangalie hili linaumiza abiria na vile vyombo. Kuna uzembe hapo, hayo Makampuni ya Bima hayako wazi sana na kwa kweli Watanzania hawajui haki zao pindi wanapopata ajali wakimbilie wapi. Kwa hiyo, hili halijafanyiwa kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala zima la bandari zetu. Ni kweli kuna bandari ambazo ni bubu, mnafahamu zinaingiza vitu vingi sana; madawa ya kulevyo, kuna njia nyingi sana za panya. Hivi ni kwa nini kila mwaka tunazungumza kuhusu hii Gati Namba 13 na Gati Namba 14? Kwa nini mnaongeza nguvu kubwa sana kule Bagamoyo mnaacha Magati ya Dar es Salaam wakati pale ndiyo chanzo kikubwa cha biashara? Ni nini ambacho kimeingilia kati kiasi kwamba Waziri unasema eti yule wa mwanzo aliyepewa kazi hiyo inaonekana ame-pledge hela ya juu sana, kwa hiyo, sasa mnahangaika kupata wale ambaao ni rahisi!

Kuna nini kimejificha Gati Namba 13 na Namba 14? Naomba nipatiwe sababu za kutosheleza ni hadi lini, Kamati imesema zaidi ya miaka minane tunazungumzia Magati haya. Bagamoyo imeanza juzi tu imeanza kufanya kazi upesi; je, kuna masilahi binafsi hapo?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya hayaelezeki na wala hatuwezi kuvumilia kila mwaka unatudanganya unatuambia unatengeneza, mara sijui mkopo umekuwa juu unamtafuta mtu mwingine wa bei rahisi, kumbe bandari zingine zinaendelea. Mimi naona kama vile kuna masilahi binafsi hapo. Sitaki nifike mbali, naomba utuambie mwenyewe na ninaamini wewe ni msikivu utatueleza kuna nini hapo? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nirudie yale ya kwangu ya Manyara, naomba yapatiwe ufumbuzi. Nisipopatiwa majibu, Mheshimiwa Mwakyembe, baadaye nitatoa shilingi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul. Nilimtaja Mheshimiwa Munde Tambwe na dakika zitakazobaki nitampa Mheshimiwa Juma Nkamia. Mheshimiwa Munde Tambwe!

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba niipongeze Menejimenti nzima ya Wizara. Naipongeza pia Kamati ya Kisekta. Nimpongeze binafsi Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, kwa juhudhi zake anazozifanya. Nampongeza sana, anajitahidi anafanya kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea nitoe pongezi zangu za dhati kwa mwanamke mwenzetu Mama Kijazi, nimeona kwenye Kitabu cha Bajeti ameomba rada mbili. Mama huyu kabla ya kupata rada hizi mbili, anafanya kazi vizuri, akikwambia mvua kwa kweli lazima utafute mwamvuli. Akikwambia hama mabondeni lazima uhame mabondeni. Nampongeza sana Mama Kijazi na ninaomba hizi rada mbili alizoziomba apewe ili aendelee kutuongoza na kutupa habari mapema tuweze kujandaa. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Munde na mimi nakuunga mkono, siku hizi halii ya hewa ni ya kweli aisee, zamani ilikuwa kizaazaa. (Kicheko)

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Waziri ukurasa wa 14 na ukurasa wa 15, nimeona amefanya kazi nzuri sana. Sisi watu wa Tabora, Kigoma na Mpanda ametutendea haki; kuna ununuvi wa mabehewa; vichwa 13 malipo tayari, mabehewa 22 malipo tayari, mabehewa 25 za kokoto malipo tayari, vichwa vitatu vinakarabatiwa na vitano viro njiani kukarabatiwa. Mabehewa 274 yameshalipiwa pesa zote, bado bilioni tisa tu. Kwa kweli sisi

Nakala ya Mtando (Online Document)

Watu wa Kanda ya Magharibi tunasema sasa ni saa ya ukombozi, haijawahi kutokea, mabehewa 274 ukiongeza haya yaliyokarabatiwa tunakarabia mabehewa 350. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulanza kulilia mabehewa siku nyingi, toka mimi nikiwa mdogo nilimsikia Mama yangu Marehemu Mosi Tambwe, aking'ang'ania mabehewa yanunuliwe mapya. Kwa mara ya kwanza, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, nampongeza Rais Jakaya Kikwete pamoja na Mheshimiwa Mwakyembe, kwa kutujali sana Watu wa Tabora, Kigoma, Mpanda, Mwanza na Shinyanga. Reli hii inatumika kubeba mizigo na inatusaidia kupunguza gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia katika kitabu cha bajeti, asilimia 88 ya pesa za maendeleo zimekwenda, bado asilimia 12. Asilimia 12 hii, naiomba Serikali hasa Wizara ya Fedha iwakelekee bajeti ikiwa ni bajeti ya mwaka jana na siyo ya mwaka huu ili waweze sasa kupata bilioni tisa wakalipie mabehewa 274, hatimaye tupate mabehewa 350. Ninaamini tatizo la usafiri wa treni itabakia kuwa ni ndoto. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwakyembe. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitaomba *commitment* ya Serikali kuhusu hili; suala hili ni suala nyeti, tunaomba *commitment* yako Mheshimiwa Mwakyembe wakati unaongea utuambie, umesema Disemba mabehewa haya yatakuwa tayari, lakini naomba *commitment* mabehewa yawe tayari kwa sababu tunapata adha kubwa sana kuhusu reli. Ulikuja Tabora ukatuahidi, lakini nimefurahi sana nilivyoona kazi imetendeka kama ulivyoahidi. Hongera sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea kuhusu ukarabati wa karakana. Mheshimiwa Waziri amefanya ukarabati wa Karakana ya Morogoro, lakini akumbuke Tabora tuna karakana, tunaomba wakati anakuja kufanya majumuisho yake, atuambie ana mpango gani sasa wa kukarabati Karakana ya Tabora. Amepeleka vichwa vyote vikatengenezwe Morogoro, tunaomba Tabora pia vipelekwe vichwa vikatengenezwe; tunao mafundi wazuri, tuna karakana nzuri ambayo mmeitelekeza hamjaikarabati. Mheshimiwa Mwakyembe, naomba uje na ufanuzi kuhusu Karakana ya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la reli ni la uchumi, tukiongelea reli tunaongelea uchumi. Tumeona nchi za India, South Africa, wamepiga hatua sana kuhusu uchumi. Masuala ya upembuzi yakinifu, mchakato unaendelea, kwa kweli tunaomba sasa yafikie mwisho, lakini tunamwamini sana Mheshimiwa Mwakyembe, ameanza kukarabati vipande vyta reli kwenye Reli ya Kati; kwa kweli ni jambo jema sana, tunashukuru na tunakuomba uendelee.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu kule kwetu vitu ni aghali sana, simenti tunanunua mpaka shilingi 20,000 kwa sababu ya usafiri wa magari makubwa. Usafiri wa magari makubwa ni gharama kubwa, tunashindwa kupata maendeleo, tunashindwa na sisi kuwa na nyumba nzuri. Viongozi wengi wamesoma Tabora, wakija kule wanashangaa jamani bado nyumba zenu ni za miti tu! Kwa kweli hali siyo nzuri, tunaomba reli iweze kutusaidia. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa kule wengi wana kipato cha chini, usafiri wa kumpandisha basi kumtoa Kigoma mpaka Dar es Salaam ni karibia 80,000, kwenda na kurudi ni shilingi 160,000; hivi watu hawa wa chini wataweza kusafiri? Tunaomba sana Serikali ituangalie sisi Watu wa Tabora, Kigoma na Mpanda, tukipata treni tutasafiri. Kwa sababu treni ina variety nyingi, kuna elfu tisa, kuna elfu ishirini, kuna thelathini mpaka arobaini na tano. Tunaomba mabehewa haya yaje na Serikali itupe commitment ya hizi shilingi bilioni tisa zilizobakia. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuvunja rekodi ya kutengeneza barabara ya lami kwa kilomita nyingi sana kuliko awamu yoyote iliyokuwepo. Tusipokuwa na reli, barabara hizi zitakufa muda siyo mrefu kwa kubeba mizigo mizito na historia hii itafutika haraka sana. Ninaamini Tutakapotengeneza reli, mizigo yote itapita kwenye reli, barabara hizi zitakuwepo kwa muda mrefu, zimetumia mabilioni ya shilingi ya walipa kodi, tuna haki ya kuzitunza. Historia ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete, itabakia kuwepo kwa hizi barabara nyingi za lami zilizotapakaa nchi nzima, ingawa Tabora bado hazijamalizika tunaomba mtumalizie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee suala zima la Wafanyakazi wa Railway. Mishahara ya Wafanyakazi wa Railway ni midogo sana, naomba Serikali iendelee kuwaongezea mara kwa mara kadiri inavyowezekana. Suala bayu zaidi ni madereva wa treni; cha kushangaza wanapotoka Dar es Salaam mpaka Kigoma au Dar es Salaam mpaka Mwanza kwa treni wanakuwa madereva wane na wote hao wanalipwa shilingi 18,000 wagawane. Mmoja wa Dodoma - Morogoro shilingi 3,000, Morogoro - Dodoma shilingi 3,900, Dodoma – Tabora shilingi 5,700, Tabora - Kigoma shilingi 6,010, Tabora - Mwanza shilingi 5,600, Tabora – Mwanza shilingi 4,900; haki inatendeka kweli?

WABUNGE FULANI: Hamna haki!

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Dereva anayeendesha gari la watu wane, analipwa *night allowance* shilingi 45,000, dereva wa treni anayeendesha watu zaidi ya maelfu analipwa shilingi 3,000! Anapakia mizigo mabehewa 20, tani 1,025 analipwa shilingi 3,000; akiiba simenti mtamwambia mwizi? Akiiba mafuta

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwenye mabehewa mtamwambia mwizi? Treni imekufa njiani siku tatu wana shilingi 3,000 mfukoni hajaacha kwa mke wake hata senti tano!

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Munde, ahsante sana tunakushukuru.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mhh, Mungu wangu wee!

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, lakini naomba wawalipe *night allowance* badala ya kuwalipa hizo shilingi 3,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, kwa kweli hilo itabidi aliangalie, maana yake kwa kweli looh hata dereva wa baiskeli ana nafuu kidogo.

Tunakushukuru Mheshimiwa Munde Tambwe.

Nilimtaja Mheshimiwa Juma Nkamia, atumie dakika chache zilizobaki.

MHE. JUMA S. NKAMIA – NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwa ufupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimpongeze sana Mwalimu wangu, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kwa kazi nzuri anayoifanya na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Tizeba, kwenye Wizara hii ya Uchukuzi. Ninapenda ku-declare *interest* pia mke wangu mimi ni Mfanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania, lakini siyo dereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mchango wangu kwenye eneo moja kubwa kwamba, kwa uchumi wa nchi yoyote Duniani, reli ni muhimu sana. Katika Mkoa wa Dodoma, kwa mfano, hii ndiyo center ya Tanzania. Leo Barabara ya Dodoma – Iringa, amesema Mheshimiwa Msigwa, inafunguka. Barabara ya Dodoma - Arusha inafunguka wakati wowote kuanzia sasa. Ninashauri kwamba, upo umuhimu mkubwa wa kuifanya Dodoma kuwa dry port kwa kuanzia kuimarisha reli kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma. Kwa sababu mtu wa Iringa hatafuata tena lita 13,000 za mafuta ya petrol ama diesel Dar es Salaam, atakuja hapa Dodoma. Mtu wa Manyara au mtu Arusha atakuja Dodoma badala ya kwenda Dar es Salaam. Vilevile mtu wa Mwanza hawezu kutoka kule akafuata Dar es Salaam ama Rwanda ama Burundi,

Nakala ya Mtando (Online Document)

watakuja hapa Dodoma; kwa hiyo, tutakuwa tume-create eneo zuri la investment kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama wenzetu Waingereza walivyofanya kwamba, huwezi kutoka Wales ukaja mpaka London, wametengeneza dry port nzuri pale Swansea. Kwa hiyo, mimi naamini hili linaweza kutusaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la Uwanja wa Ndege wa Dodoma, kwa kweli kiwanja kilichopo kipo katikati ya Mji na wakati mwengine ni very risk kwa maisha ya watu, kwa sababu watu wengi wamezunguka eneo hili la airport. Chochote kikitokea, Mungu pisha mbali, inaweza kuhatarisha maisha ya watu wengi sana wanaozunguka Mji wa Dodoma. Ninashauri kwamba, upo umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha kile Kiwanja cha Msalato kinakamilika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya lami inayokwenda Kondoa mpaka Arusha karibu inakamilika na inapita Msalato, itakuwa jambo rahisi tu kwa watu wanaoteremka kwenye uwanja wa ndege kufika Dodoma Mjini kwa urahisi zaidi napia tutakuwa tume-create employment pia katika eneo lile la kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusitiza kwamba, upo umuhimu wa Dkt. Mwakyembe na Naibu wake, kuangalia uwezekano wa namna gani Dodoma tunaweza ku-create kuwa dry port. Tutaokoa barabara nyingi sana hasa Barabara ya Arusha - Dar es Salaam na Iringa - Dar es Salaam. Vilevile hata msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam utapungua kwa kiwango kikubwa sana. Leo unapoingia Dar es Salaam ni kazi kubwa sana; magari ni mengi, malori ni mengi yanafuata mafuta, wakati mwengine unakuta lori linalochukua lita 10,000 linatoka Songea linakwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo, ninashauri kwamba, hili ni jambo ambalo linaweza likasaidia kuwa na dry port hapa Dodoma.

Dodoma ina eneo kubwa sana la ardhi, ambayo kama unakwenda Bahi ardhi iko kubwa, unaenda Kondoa na Chemba ardhi ni kubwa, kama unaenda Iringa ardhi ipo kubwa, unaenda Kongwa na Mpwapwa ardhi ni kubwa. Kwa hiyo, naamini tukifanya hivi tutakuwa tumeinua sana Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja.
(Makofij)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, muda haupo upande wetu, lakini wale ambao nina majina yenu kwenye orodha, niwahakikishie mtachangia jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Batenga, Mheshimiwa Chibulunje, Mheshimiwa Shabiby, Mheshimiwa Zarina Madabida na wengine mtapata nafasi ya kuchangia jioni kwa Wizara hii, endeleeni kijiandaa.

Waheshimiwa Wabunge, wakati ninawatambulisha wale Wataalam wetu akina mama asubuhi, kuna kundi dogo nililisahau la akina mama ambao ni Wataalam wa Uendeshaji wa kitu kinachoitwa TAG au Kiswahili kizuri wanaitwa tishali, ile meli ndogo inayovuta meli kubwa kule bandarini. Rubani wa tishali asimame; karibu sana mama. Jamani mnaona utalaam unazidi kuongezeka. Yupo pia Mhandisi wa tishali; karibu sana. Hii inazidi kudhihirisha wazi kwamba, katika uwanja wa Sayansi na Teknolojia na Ufundi wa aina mbalimbali, sasa akina mama wameanza kuchukua nafasi yao wanayostahili. (Makofij)

Naomba nisahihishe utambulisho wa asubuhi wa wale Wajumbe waliokuja kutoka Jimbo la Buchosa, kule Sengerema; niliwatambulisha kama ni Wenyeviti wa Vijiji hapana hawa ni Wenyeviti wa CCM wa Matawi na Kata za CCM kutoka Jimbo lote la Buchosa, wakiongozwa na Katibu wao wa CCM wa Wilaya, Ndugu Mohamed Mohamed. Naomba msimame tena Wenyeviti wangu. Eeh, hiyo ni CCM, ni shughuli kubwa hiyo, nataka kusema kwamba, Buchosa hakuingiliki. Ahsanteni sana na karibuni sana watani zangu, kaeni chini. (Makofij)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba niahirishe shughuli za Bunge kwa asubuhi hii hadi saa kumi jioni ya leo tutakapoendelea na shughuli zilizo mbele yetu.

(Saa 7.00 mchana Bunge *lilisitishwa* hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge *lilirudia*)

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Katibu. Majadiliano yanaendelea, kama nilivyosema asubuhi mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Suleiman Nchambi ajiandaye. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie katika sekta hii muhimu kwa maendeleo na kwa uchumi wa nchi yetu.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2009 uchumi wetu haukuwahi kupanda kwa kasi kama ilivyokuwa mwaka huu na tunaambiwa kwamba imefikia asilimia 7.5 kutokana na sekta mbili muhimu na sekta hiyo ni pamoja na sekta hii ya uchukuzi na sekta ya mawasiliano ambazo kwa pamoja wameweza kufikia asilimia 22.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli kwamba pamekuwa na changamoto nyingi sana, lakini wote tunakubaliana kwamba sekta hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Niseme tu kwamba Tanzania geographically tumepeata bahati kubwa sana ya kuwa na bahari na bandari na hivyo tukawa tumezungukwa na nchi kama tano hivi ambazo ni *land locked* au nchi ambazo hazina uhusiano wa karibu na bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo ni wazi kwamba kwa geographical position tuliyonayo na kama changamoto zisingekuwa nyingi kama zilivyo, ina maana sasa hivi uchumi wetu ungekuwa umepaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kuzungumzia suala zima la bandari. Bandari ya Dar es Salaam ni kweli na niwashukuru sana viongozi waliopo, Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, wamefanya kazi kubwa na tunaona kwa kweli mambo yanakwenda pamoja na kwamba kasi yao ni kubwa, lakini tunaona kwamba bajeti wanayopangiwa kila mwaka imekuwa ndogo ukilinganisha na Wizara ya Ujenzi. Lakini kwa hicho kidogo bado wanajitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu bado bandari yetu ingeweza kufanya kazi kwa kasi kubwa zaidi, pamoja na kwamba tunaona kwamba ule msongamano wa makonteina umepungua, lakini bado ukilinganisha na bandari ya Mombasa, bado tatizo ni kubwa. Kwa hiyo, naomba niwaambie kwamba bado wavute soksi, tunaweza vilevile na sisi tukapunguza mizigo pale bandarini kama wanavyofanya wenzetu majirani zetu wa Kenya. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme pia vilevile kuendana na hili kuna tatizo kubwa sana, tunakubaliana kwamba Dar es Salaam sasa hivi kuna msongamano mkubwa sana, na wengi wanaliangalia katika upande wa uchumi, lakini mimi naliangalia zaidi vile vile upande wa jamii. Nilizungumza wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu kuhusiana na msongamano huu ambao kwa kiasi kikubwa umevunja ndoa za watu, lakini vilevile watoto wanashindwa kuona wazazi wao. Ukweli ni kwamba watoto wanawaona wazazi wao labda weekend tu. Hili ni tatizo Kubwa sana na linawa-affect sana psychologically kwa sababu kwenye child development tunaambiwa kwamba wazazi ni muhimu sana wawe wanakaa na watoto. (Makofij)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa na ninaomba Serikali ilione. Lakini niseme tu kwamba moja ya mambo ambayo tungeweza kuyafanya yakapunguza msongamano Dar es Salaam ni pamoja na kuwa na boats. Kwa mfano, tukiwa na boat kutoka let us say Tegeta mpaka Dar es Salaam mijini itapunguza sana msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa mfano mimi nakaa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenda Salasala asubuhi saa 12.15 natumia dakika 15 tu nafika. Lakini kurudi unatumia saa tatu kufika Mwenge. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa sana na wote tunajua kwamba Dar es Salaam inachangia karibu asilimia 60 ya pato la Taifa. Kwa hiyo, nadhani Serikali ione ni kwa jinsi gani wanaweza kufanya msongamano huu ukapungua. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la reli: Reli ni suala la muhimu sana katika ukuzi wa uchumi. Lakini wote tumeshuhudia jinsi gani reli yetu hasa Reli ya Kati jinsi gani ambavyo sasa hivi abiria wamepungua, jinsi gani mabehewa yamepungua. Nashukuru kwamba wamenunua mabehewa, lakini bado ujenzi au ukarabati wa reli hii haujakkilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania ni wakulima, tunaona ni jinsi gani wakulima wanatozwa fedha nyingi na wafanyabiashara ambao wanaenda moja kwa moja mashambani. Kama reli ingekuwa tayari, inamaana kwamba wakulima hawa wasingelanguliwa bei zao za mazao. Kwa hiyo, ni rai yangu kwa Serikali kwamba watajitatihidi kuhakikisha kwamba reli hiyo inatengamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda nizungumzie hili suala la bajeti katika Wizara hii. Kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha sana. Kwa mfano ukiangalia mwaka huu bajeti yao ya maendeleo wamepata shilingi bilioni 273 tu za ndani, wakati wenzao wa Ujenzi wamepata bilioni 450 za ndani. Kwa hiyo unaona ni jinsi gani hawa jamaa watashindwa kabisa kufanya masuala yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, ni vema Serikali ikaipa kipaumbele Wizara hii kama ambavyo nimesema na jinsi ambavyo wengi wamesema kwamba kwa kweli ikipata bajeti ya kutosha, tunaamini kabisa uchumi wa nchi hii utakua kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni suala la anga. Wamezungumzia wengi suala la usafiri wa anga ni muhimu sana na kwamba siyo kwamba ni prestige, isipokuwa inafikisha mtu kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninajaribu kuangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwaka juzi 2012/2013 na ninaomba ni-quote. Alisema hivi;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

"Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013 ATCL itaendelea kutoa huduma kwa Kutumia ndege ya kukodi aina ya Boeing 737 500 na ndege yake aina ya Dash 8Q3 100 ambayo kwa sasa inafanyiwa matengenezo".

Aidha, kwa kutumia, anasema, aidha kwa kutumia fedha ambazo kampuni imelipwa shilingi bilioni 12.2 kutokana na Bima ya Ajali ya ndege iliyotokea mwezi Aprili, 2012 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.6 zitatumika kama malipo ya awali kwa ajili ya kununua ndege mbili mpya". Haya Mheshimiwa Mwakyembe ameyasema mwaka 2013. Sasa Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo ndege hazijanunuliwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kuuliza, na hii ni hotuba yake ambayo nimeweka kwenye Ipad. Sasa najaribu kuuliza hizi fedha ambazo alituaminisha kwamba wangeweka kwa ajili ya manunuzi ya awali ya ndege, leo Mheshimiwa Waziri huyu huyu kwenye kitabu chake ukurasa wa 84 anasema vile vile kwamba "ATCL inatarajia kununua ndege nyingine mbili zenyenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ta 50".

Sasa suala ni kwamba nataka kujua tu kutoka kwa Waziri aje atuambie, zile alizozungumza mwaka juzi bilioni 12 ziko wapi? Na leo hela ziko wapi? Kwa sababu anaposema anategemea kununua ndege mbili, nimejaribu ku-Google bei ya ndege ya abiria 50 ni dola za Kimarekani kati ya milioni 38 mpaka 45. (Makofii)

Sasa nataka kujua kwa sababu hapa anasema abiria 50, kwa hiyo, tunataka kujua kama kweli hizo fedha zipo, ziko wapi? Maana nimeangalia kwenye Kitabu cha Maendeleo fedha hakuna hata kidogo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ajue kwamba anaposema maneno hapa Bungeni yako-recorded na sisi wafuatiliaji tunafuatilia. (Makofii)

Kwa hiyo, naomba atakapokuja kufanya majumuisho atueleze, hizo fedha ziko wapi na tunafanyaje? Kwa hiyo, ajue kwamba tunaendelea kufuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Susan. Nakushukuru sana. Ahsante. Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Elizabeth Batenga. Mheshimiwa Nchambi!

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na nchi kwa kupata fursa ya kuchangia jambo muhimu sana la usafiri, bandari na mambo mengine ambayo kwa kweli ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusemea Mkoa wangu wa Shinyanga. Ni dhahiri Mkoa wa Shinyanga kati ya miaka ya 1995 kurudi nyuma ndiyo Mkoa uliokuwa una mapato mengi, unachangia mapato kwa wingi katika Taifa letu, ndiyo Mkoa wenye fursa nyngi, niliwahi kusema hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga kabla ya kugawanya Shinyanga na Simiyu, tulikuwa na wananchi takribani 4,200,000. Mkoa unaolima pamba zaidi ya asilimia 60 ya pamba ya nchi hii, Mkoa wenye mifugo mingi nchi hii, Mkoa wenye dhahabu nyngi nchi hii, Mkoa wenye tumbaku nchi nyngi nchi hii, Mkoa wenye rasilimali watu wengi wakaazi wa Shinyanga nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi ninasikitika sana, Shinyanga sisi *Airport* yetu imekuwa sasa kama uwanja wa kufugia kuku, hatuna fursa ya kiwanja cha ndege. Tumejitahidi kadri ya uwezo, tumeongea mapendekezo katika RCC zaidi ya mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nataka niseme tu, wewe ni mtani wetu na wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ni dhahiri kabisa ndiyo baba wa Taifa hili. Dhambi yetu sisi iko wapi? Naomba, Mheshimiwa Mwakyembe ni rafiki yangu. Ulikuja wakati ule na Mheshimiwa Mpendazoe Kishapu pale, unaifahamu Shinyanga vizuri, ukapiga piga maneno pale Kishapu, Kahama na sehemu nyngine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kukosa fursa ya uwanja wa ndege nitashika shilingi, laki, milioni, sitaiachia mpaka hapo Bunge hili litakaposema kwa kweli kwa ukarimu wa Wasukuma wa Shinyanga, wanahitaji *Airport* yao. Tumeteta sana na Mheshimiwa Masele swahiba wangu, ni lazima utakapokuwa una-windup, hapa hatuhitaji tu fedha zimetengwa, lini kazi inaanza, lini kazi inakamilika? *Oshila mhayogete nduhu shida.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ATC, hapa imefika mahala Bunge linajadili vazi la Taifa. Lakini, wakati mimi ni mdogo nilikuwa napanda *Boeing* moja imeandikwa *The Wings of Kilimanjaro*, ili kuwa inaitambulisha nchi yetu maeneo mbalimbali.

Leo nasikitika sana kama sisi hatuna ndege kubwa hata inayotoka nje ya nchi, sisi hatuna ndege zetu kama Taifa, mimi najaribu kusikitika Mheshimiwa Mwakyembe nakujua wewe ni mchapakazi sana, sana nakufahamu ni rafiki yangu. Naomba Mheshimiwa tuisubiri kununua tu ndege.

Sisi wengine tumefanya biashara za bus tumerithi, wazee wetu wamefanya kuanzia miaka ya 1959, professional mimi mwenyewe kazi ya abiria naijua inavyomtangaza mtu, lakini inavyolitangaza Taifa lake. Sisi hatuwezi kuwa tunapanda *FastJet* Mwanza ka-bag unaambiwa shilingi 10,000/= risiti hupewi. Umechelewa dakika moja unaambiwa nauli yako imekufa. Ni kwa sababu

Nakala ya Mtando (Online Document)

hatuna shirika letu la uzalendo. ATC lazima uifufue, lazima uwe na plan. Wazungu wanasema; "no one plans to fail but your plan will make you fail".

Sasa kama we are planning to fail you better tell us. If our plans make us go on failing, also you better tell us. Ni lazima ugangamale kweli kweli. Ni lazima usimame imara. We don't need to go on plans that will make us failing. We better make plans that will take out of failure. Lazima tujue hayo maneno.

Sasa tuwe tunatengeneza nini hapa, Mheshimiwa Mwakyembe nakuomba sana, Airport ya Shinyanga, Shirika la Ndege, siyo lazima tununue ndege mpya, tunaweza tuka-lease ndege kwa miaka miwili/mitatu na Serikali haiwezi ikafanya kila kitu. PPP, ita watu, ongea nao waweze kuhudumia shirika hili mpaka Serikali itakapopata mbawa zake.

Mheshiwa Naibu Spika, suala treni, leo barabara zinajengwa, zaidi ya kilomita 20,000 nchi hii, lakini kwa kweli kama hatutashughulika na treni, Serikali yetu baada ya miaka 15 itaingia kwenye maintenance ya barabara, bajeti kubwa itakuwa ni *repair* ya barabara. Lakini hata kwa mahitaji ya kawaida, treni inasafirisha vitu kwa bei nafuu. Mtanzania atapata unafuu kule Kigoma, shemeji zangu akina Peter Serukamba, wenzangu wa NCCR-MAGEUZI pale, akina Kafulilila, Mheshimiwa Zitto nyie ni shemeji zangu, isemeeni treni hii ili nikiwa nakuja na dada yenu Kigoma nakuja kwa treni raha mustarehe. (Makofii)

Kwa hiyo, shemeji nawaomba sana mniunge mkono kwenye suala la treni. Wakati Wachina wanatujengea reli ya TAZARA walituachia mabehewa 4,000. Vichwa vya treini zaidi 130. Leo tuna chini ya mabehewa 500. Vichwa chini ya vitano. Hiyo inatosha kuonesha tume-prove failure. Kama tume-prove failure kama Serikali, acha sekta binafsi zi-take cover. Tusing'ang'anie vitu. Tusing'ang'anie, kung'ang'ania wananchi wanakosa huduma.

Mheshimiwa Mwakyembe, suala la treni lipe kipaumbele. Najua umezindua treni mbalimbali. Lakini wanasema Waswahili, kunguru ni kunguru tu, hata ufuge miaka 100 hageuki kuwa njiwa. Uta-repair hizi treni mzee. Mimi nimefanya kazi ya abiria, uta-repair mpaka utakwenda upande, kama Serikali haiwezi kuleta treni mpya na mabehewa mapya, kama Serikali haiwezi kujenga reli pana, you better invite private sector uachane nalo hilo.

Jamani sisi ni mashahidi, Singapore barabara zinajengwa na Sector binafsi. Malaysia, China na maeneo mbalimbali, sisi tukikumbatia kila jambo Serikali ifanye, tutafeli tu. Kwa hiyo nakuomba sana wakati una-windup uje na mpango kamili ni namna gani sekta binafsi utazishirikisha ili tuondoke hapa tulipo.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshiwa Naibu Spika, bandari: Dubai walikuwa hawana mafuta, walikuwa hawana mchicha, hawana mahindi, hawana tumbaku wala ng'ombe wa Shinyanga. Lakini leo kwa kweli Dubai kwa bandari peke yake wamefanya maajabu.

Mimi nakuomba sana Mheshimiwa Mwakyembe, kama hutayachukua maneno yangu, nitayahifadhi bajeti ya mwakani nitakukumbusha na Waanzania wanaskia. Mimi ninakujua wewe ni mchapakazi, lakini hizi kasoro za kuendelea kuwakumbatia wataalam wachache, hizi Bodi Bodi hizi, kama unaona haikushauri vizuri tumekupa mamlaka vunja.

Kamati inakushauri mambo mengi, kuna mambo mengine *take risk* ili usaide Taifa hili. Bandari inaweza ikalisha nchi zaidi ya 12 hizi. Tusichimbe dhahabu, tusiuze ng'ombe wetu kwa kuhudumia bandari peke yake. *Invite private sector, watu wanao uwezo wa kujenga bandari.* Serikali isiweke hata shilingi moja, lakini ikapata kodi nyingi na ikawa na fursa nyingi.

Lingine, Madereva,: Mimi nimeendesha lori miaka 6. Nimekwenda Rwanda, Burundi, Congo na Zambia mwenyewe, gari la trela. Nimeendesha bus miaka mitano.

Mheshimiwa Mwakyembe, nitapenda sana kama utanikubalia hapa wakati unajibu, mimi na wewe na Katibu Mkuu Wizara yako nitoke na lori mpaka Rwanda au Zambia, uone ni bora dereva anayeendesha ndege au manowari ya kivita kuliko dereva anayeendesha lori ama gari kutoka Dar es Salaam hata kuja Dodoma. Hakuna vibao barabarani, sehemu ya bumps kibao kilishaibiwa. Sasa tutaendelea kuwa tunalaumu watu wetu. Hawa watu wanafanya kazi kubwa. Lakini hatuoni mazingira wanayofanyia kazi. Leo ameshuka pale Ubungo, anaangalia pancha, wanakuja watu Yono, kamata laki nne themanini. Tufanya kazi gani?

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. Obeja sana, obeja kulumba! (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunakushukuru sana. Sasa baada ya Mheshimiwa Elizabeth Batenga, atafuata Mheshimiwa Chibulunje ambaye simuoni, Mheshimiwa Shabiby ajiandaye.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipongeze juhudzi za Wizara katika kufanya matengenezo makubwa kwenye Reli ya Kati, lakini pia kushughulikia ili tuweze kupata mabehewa mengi na vichwa vya treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto kubwa ni bajeti ndogo. Hapa zinahitajika shilingi bilioni 9 ili ziweze kupelekwa huko walikotengeneza mabehewa hayo yaweze kuja kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha. Mimi sioni mtu ye yote wa Wizara ya Fedha, lakini Mheshimiwa aliyekaa kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba amwambie Waziri wa Fedha kwamba atakapowasilisha Bajeti yake ya Wizara yake, mimi nitatoa shilingi kama hatatueleza mpango mzima wa kutoa hizo bilioni 9 ambazo ziko katika bajeti hii. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati inayokwenda mpaka Mwanza, Kigoma, Kaliua mpaka Mpanda, ni ukombozi kwa wananchi wa huko, kwa sababu usafirishaji wa bidhaa kwa malori unawapa gharama kubwa ya bei za vitu. Kwa hiyo sisi tunaunga mkono sana juhudzi za Serikali na Wizara. Lakini changamoto hiyo niliyoisema basi naomba ishughulikiwe. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 80 wa hotuba ya Waziri ameeleza kwamba ana changamoto kubwa ya gharama kubwa ya kulipa fidia katika maeneo ambayo wamekusudia kuyatwaa kwa ajili ya viwanja vya ndege katika maeneo mbalimbali. Lakini mimi nisemee eneo la Omukajunguti katika Wilaya ya Misenyi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika ukurasa wa 82 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, ataendelea kupima maeneo hayo, ili aweze kupata hati kwa ajili ya maeneo hayo. Sasa najiuliza maeneo ya watu, hujawafidia na unasema kabisa huna fedha, sasa unayapimaje? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni kaka yangu, kwa hiyo mimi hata shilingi yake sina shida nayo. Lakini mimi namwomba atakapokuwa anahitimisha hoja yake basi asimame atueleze; awaeleze wananchi wa Misenyi Omukajunguti kama alivyowaeleza kwenye mkutano wa hadhara mbele ya Mheshimiwa Rais, kwamba wanashughulikia fedha ya kuwalipa na katika kipindi hiki tungetarajia kwamba wale watu wameshalipwa. Wameshamwandikia barua nydingi na Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba zinatifa barua 25. Sasa wale watu mnawajua ni shomile, wataandika zitatifa hata 30. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba awasaidie wale watu waache kulalamikalalamika. Siyo vizuri wanavijiji kulalamika, awasaidie, awape jibu la uhakika lenye kuwatuliza mioyo yao, maana katika maeneo yale hawafanyi kitu chochote. (Makof)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani amesema wanajiandaa kuitoa CCM madarakani. Lakini napenda nimwambie kwamba, CCM ni kisiki kisichong'oka. CCM ni Chama kikubwa, CCM ni chama dume, kiko imara, kwa hiyo, naomba matarajio yake ayaweke mwaka wa 5015 kama na yenye we itawezekana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi yangu ni mafupi. Nakushukuru, ninaunga mkono hoja. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Ahsante Sana Mheshimiwa Elizabeth Batenga. Na hasa kwa ujumbe wako mzito.

Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe na Mheshimiwa Hamad Rashid ajiandae.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Kwanza kabisa napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Mwakyembe pamoja na Naibu wake pamoja na wote katika Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ya Bunge hili Tukufu. Katika maoni yetu na aliyo soma Mwenyekiti tulizungumzia kuhusu habari ya Dry Port ambazo zipo katikati ya Mji wa Dar es Salaam.

Kwa hiyo, leo sitataka kuzungumza masuala mengi sana, lakini nataka kuzungumza tu nini ubaya wa Dry Port ambazo ziko mjini pale Dar es Salaam, hizi ICD?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi zimeleshakuwa ni tatizo, ni tatizo, ni tatizo kubwa sana katika Mji wa Dar-es-Salaam. Ukiangalia kutoka hii Mandela Road kwenda hadi hapa Ubungo ziko tatu. *Parking* za malori hawana, utakuta wote wanapaki kwenye ile barabara, kwa hiyo, ile barabara badala ya kuwa two way inakuwa one way. Ukiangalia misururu ya Dry Port zilizoko katika barabara ya Pugu, ukiangalia Chang'ombe, kwa hiyo, zimekuwa ni Dry Port, Dry Port Mji mzima. Kwa hiyo, mji mzima umekuwa na magari yanayofanya usafiri tu wa kutoa ma-container na mizigo kutoka Bandarini kuja kwenye Dry Port na kutoka Dry Port kwenda Mikoani na nchi zingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hizi Dry Ports zote ni za watu binafsi na zimekuwa na matatizo makubwa sana. Kwa mfano, mtu asipolipa kutoa mzigو wake kwa siku 7 anaanza kuchajiwa pale Dola 30 kila Container na hizo pesa zinakwenda kwa watu wenye Dry Port ambao ni watu binafsi; utakuta mtu huyo anacheleweshwa TRA, ukienda TRA unataka kulipia ule mzigو unaambiwa kwamba, system imegoma, unakaa wiki, wiki mbili, wiki tatu. Utakuta mtu ana

Nakala ya Mtandao (Online Document)

container 10, 15 anaweza akakaa hadi mwezi, atakuta analipa milioni 30, milioni 40, kwa ajili ya ule tu ucheleweshaji wenyewe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Mheshimiwa Waziri ana nia nzuri sana ya kuweka Extension ya Bandari kule Kisarawe, lakini hakuna utendaji kazi wa karibu kati ya Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Ujenzi. Hapa wote tumekuwa mashahidi, tumesikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Sasa kama patakuwa na Bandari Kisarawe, lakini hakuna barabara ya kutoka Mlandizi kwenda Kisarawe ambapo yale magari yatakwenda kule kuchukua ile mizigo kwa ajili ya kutoka hivi.

Kwa hiyo, ina maana hata ukiweka kule bandari pamoja na kuwa pana reli mbili, ya TAZARA na ya Kati, kitakachotokea ni kwamba, msururu wa magari utakuwa ni vilevile wa kutoka bandarini kwenda Kisarawe na kutoka Kisarawe kurudi tena mjini na kuja tena kufuata barabara ya Ubungo kwenda Mikoani. Kwa hiyo, itakuwa haina msaada wa aina yoyote. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu, ninaomba, kuna Reli ya Kati ambayo haitumiki sasa hivi, au kama inatumika labda kwa treni moja kwa miezi 6, hii ya kwenda Tanga, ambayo inapita pale Ruvu. Kwa nini sasa hivi tuisiachane na habari ya malori kuingia mjini na kuleta foleni? Kwa nini tusitumie ile reli? Tufanye extension iwe pale Vigwaza. Mizigo yote iwe inatoka kwa treni kutoka kule bandarini iwe inakuja mpaka huku Vigwaza, halafu malori yote yasiwe yanakwenda Dar es Salam, yawe yanaishia pale kama Dry Port na Dry Port ile iwe ya Serikali, badala ya kuruhusu malori yaingie mjini, yanaleta foleni, yanaleta mauaji mengie, ma-container yanaangukia vigari bila sababu ya aina yoyote. Kwa sababu, ukiangalia sasa hivi, kama Mandela Road, utakuta ni Dry Port, magari foleni, wenze magari madogo Dar es Salaam hawana raha. Ukienda mpaka Tegeta huko kote Dry Port, kwa hiyo, malori malori Dar-es-Salaam nzima. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri ulifikirie hili wakati wa kuigaiga kila kitu kwenye hii nchi umepitwa na wakati. Kila kitu tunataka tu-copy tu, kila kitu tunataka tu-copy tu, na sisi tuanzishe vyetu watu wa-copy kutoka kwetu. Siyo Mombasa wana Dry Port mahali Fulani, basi na sisi tunakuwanayo hivyo hivyo. Ukiangalia msongamano wa magari wa Dar es Salaam na Mombasa ni vitu viwili tofauti. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ndugu zangu hapa wamezungumza masuala mengi sana ya viwanja vya ndege, lakini sijasikia Mheshimiwa Waziri unataja kiwanja cha ndege cha Morogoro. Morogoro pale pana Airport na pana ndege kila siku inakwenda mara mbili Dar es Salaam na kurudi pale. Na siku nyingine huwa inatua kwa pua, inakosakosa kuua watu pale.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Ule uwanja una mashimo, uwanja hauna lami, uwanja mbaya. Lakini mimi nasikia tu Songwe, wapi, sijui wapi! Lakini Morogoro hata siku moja sijawahi kusikia kwamba, mnafikiria ile Airport ya Morogoro mtaitengeneza. Sasa sielewi hapa kuna nini au mpaka watu tushike shilingi ndiyo mkumbuke kwamba na sisi Morogoro pale tunataka Airport? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna kitu kingine, hii Reli ya Kati, kila siku Godegode, Mzaganza, sijui wapi. Kila siku mabilioni ya pesa yanapotea pale, yanaua watu kila siku. Hivi hakuna njia sahihi ya kuhamisha hii reli kupeleka sehemu ambayo ni muafaka? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, ukiangalia għarama zilizotumika kutengeneza reli kile kipande, ina maana hata mngeweza kutengeneza reli mpya kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma. Siku zote ni palepale Godegode, Godegode, Godegode sijui Mzaganza. Jamani sasa hii reli ya Godegode tuiite au tuite reli ya wapi? Fanyeni mbinu. Hawa ma-engineer kama wamechoka tafuteni ma-engineer wengine. Au ndiyo mahali ambapo sasa wanapatia mahali pakula pesa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijawahi kukaa humu Bungeni toka nazaliwa, Godegode, Godegode, Godegode! Tafuteni muafaka kwamba muache hiyo sehemu, tafuteni njia nyngine njia ya kati. Na kama walivyosema Waheshimiwa waliotangulia, bila reli, hizi barabara ni sawasawa na hakuna. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na accidents zitaendelea kuwepo kwa sababu, misururu ya magari ni mingi, barabara nyembamba, siyo kwamba, ni mbaya, isipokuwa magari ni mengi yamezizidi hizi barabara. Kwa hiyo, ni magari mazito yanapita, barabara zinakufa kila siku; mtalalamikia kwamba, zinatengenezwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutengeneze reli, bila reli hatuwezi kuwa na uchumi wa nchi hii, kila siku tutakuwa tuko kwenye barabara tu. Kwa sababu, kila lita moja ya mafuta zaidi ya shilingi 300, hata mtu anayetumia kibatari, mtu anayetumia generator, inaenda kwenye Mfuko wa Barabara. Sasa kama tungemaliza hizi barabara, ina maana hela hiso si zingehamia sehemu nyngine? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Naunga mkono hoja. (Makofi)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naomba nijielekeze moja kwa moja katika kuchangia kuhusiana na mgogoro kati ya Serikali, Mnejimenti ya Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro ya KADCO pamoja na wananchi wa Vijiji vya Sanya Station, Tindigani, Rundugai, Mtakuja, Chemka na Chekimaji katika Kata za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Masama Kusini na Kata ya Kia, Wilayani Hai ambako ndiko kwenye huu uwanja mkubwa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro nimelizungumza mara nyingi san na kwa kweli ni jambo ambalo limezungumzwa kwenye Bunge hili kwa zaidi ya miaka 10. Laiti Serikali ingekuwa iko serious katika kumaliza mgogoro wa KIA, ingeshalimaliza tatizo hili. Mheshimiwa Waziri Mwakyembe ni shahidi yangu kwamba, tumezungumza mara kadhaa kuhusiana na matatizo yaliyoko mahali pale, lakini kuna manyanyaso makubwa sana yanayofanyika kwa wananchi zaidi ya elfu 10 wanaouzunguka Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro wa KIA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anaelewa kwamba, tatizo la ardhi katika Mkoa wa Kilimanjaro ni tatizo kubwa sana. Na pale wananchi wanapoguswa katika masuala ya ardhi, ardhi ambayo kwao ni uhai, inakuwa ni tatizo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja huu wa Kilimanjaro umetengewa na Serikali eneo la kilometa za mraba 101. Katika mazingira ya hali ya uhaba wa ardhi katika Mkoa wa Kilimanjaro unatenga kilometa za mraba 101 kwa sababu ya uwanja mmoja wa ndege wa KIA, ni kitu ambacho ni *impossible*. Huo mgogoro umesababisha ugomvi mkubwa sana kati ya KADCO, Serikali na wananchi na hali hii inafanya mgogoro huu uendelee sasa kuwa hata kutishia amani kwa sababu wananchi wanachukua silaha kwenda kuanza kupinga Serikali kuchukua eneo lile. (Makofisi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja ambacho kiko bussy sana duniani, kiwanja cha Heathrow kule London, ambacho kina Terminal 1, Terminal 2, Terminal 3, Terminal 4, 5 na sasa wanajenga 6 na 7. Uwanja wa Heathrow London una eneo la jumla ya kilometa za mraba 12.14 na hii ndiyo bussiest Airport in the World. Airport ya Dubai, ambayo ni Airport iko bussy sana, nina hakika Wabunge wengi wamepita Dubai Airport, wanaelewa Dubai Airport ni kubwa na ni bussy kiasi gani. Dubai Airport ina eneo la kilometa za mraba 34, kilometa za mraba 34 tu. Uwanja wa Dar-es-Salaam una kilometa za mraba ambazo hazifiki 3, lakini uwanja wa KIA umetengewa eneo la kilometa za mraba 101, hii ni record ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunachoiomba Serikali na ninaomba sana Waziri leo, huu mgogoro mmeshausikia mara nyingi, tumeshashauriana mara nyingi. Kwa kweli, katika majibu yako ya msingi nitaomba sana utoe kipaumbele kutoa majibu ili wananchi wa Kata hizi za KIA na Kata ya Masama Rundugai kule Wilayani Hai wawewe kujua hatima yao ni nini. Kwa sababu, eneo hili la ardhi matokeo yake linakodishwa kwa wananchi, wanakodishiwa kwa 30,000/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanalipa pale, eneo ambalo kimsingi lilikuwa ni eneo la vijiji ambavyo nimevitaja mahali hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba tafadhali kauli ya Serikali itoke mahali hapa, ili tutafute namna ya kumaliza mgogoro huu ambao kwa kweli, hauna sababu ya kuwepo. Kilometra 101 za ardhi kwa uwanja wa ndege ni eneo kubwa na kubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kumekuwa kuna usiri mkubwa sana kuhusu mapato yanayopatikana katika Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Na tumeomba mara nyigi sana hebu tuelezeni wazi, kuweni wazi kuhusu huu mkataba wa KADCO. Hili Shirika la KADCO ni kina nani? Linaendeshaje Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro? Mapato pale yanapatikanaje? Yanakwenda wapi? Lakini Serikalini kumekuwa kuna usiri mkubwa na kuonekana kwamba, pengine kutoa taarifa za mapato ya KADCO, KADCO ni nani, ubia na KADCO ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, KADCO walikodishiwa uwanja huu, baadaye uwanja ukarudishwa Serikalini, lakini pamoja na kurudishwa Serikalini bado mpaka leo hakuna mambo yaliyoko wazi kwa wananchi. Sasa je, KADCO ni akina nani? Wanauendesha ule uwanja kwa mamlaka yapi? Mapato wanayopata yanakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika nizungumze jambo lingine kuhusu kwamba tunajadili bajeti za Serikali hapa, tunajadili Wizara mbalimbali, lakini hatuangalii vyanzo vya mapato ya ki-Wizara na mpaka leo katika Bunge lako Tukufu, Serikali haijaweza kuleta kitabu hiki Volume I, hiki ni cha mwaka jana, lakini tunajadili bajeti ya Serikali, mpaka sasa hivi huu ni mwezi mzima umepita Serikali haijaweza kuleta Kitabu Volume I cha bajeti. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ukiukwaji wa Kanuni. Tunajadilije mapato na matumizi ya Serikali kama vitabu vya mapato ya Serikali haviji Bungeni na hakuna maelezo yoyote yanayotolewa mpaka leo! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo tunaweza tukamhoji Mheshimiwa Mwakyembe mapato ya bandari kwa mfano, tunazungumza bandari, tunazungumza matumizi, lakini mapato vyanzo vyake viko wapi? Taarifa gani zinakuja katika Bunge kuhusu mapato ya kimaduhuli katika Wizara mbalimbali ambazo zinajadiliwa mahali hapa? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana ofisi yako ichukue nafasi ya msingi sana, iweze kutoa maelekezo kwa Serikali kuleta Kitabu Volume I, kitabu cha kwanza kile ambacho kinaonesha revenue ya Serikali. Ni haki kabisa kwa Wabunge kupata kitabu hicho, ili iiwasaidie katika kujenga hoja, kufananisha Wizara na Wizara, mapato ya Serikali yakoje, yanakwenda wapi,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ndiyo namna ya kujadili bajeti, huwezi kujadili bajeti ukajikita kwenye matumizi tu, msijikite vilevile katika mapato ambayo ni aidha ya kodi ama maduhuli, ambayo ni mapato nje ya utaratibu wa kikodi. Kwa hiyo, niombe sana Waziri atusaidie majibu kuhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, nizungumze jambo ambalo wamezungumza Wabunge wenzangu wote, umuhimu wa reli: Ninapozungumza umuhimu wa reli, tumekuwa tunazungumza sana Reli ya Kati ni muhimu sana na ni reli muhimu mno, lakini kuna Reli ya Tanga mpaka Kilimanjaro mpaka Arusha, ile reli vilevile imekufa na hakuna mtu anayeizungumza hata siku moja. Sasa hizi reli zetu kweli, kama tunataka kuzifufua, naomba tuszungumze Reli ya Kati peke yake, Reli ya Kati ni muhimu na inasaidia sana Watanzania walio wengi, lakini vilevile tujadili Reli ya Tanga; reli inayotoka Dar es Salaam, inakwenda mpaka Tanga, Korogwe, Kilimanjaro, Arusha mpaka Voi upande wa Kenya, ile reli ilikuwa inatuunganisha na Reli ya Kenya. Ile Reli imesahaulika, mataruma yanaabiwa, mali za Shirika la Reli zinaharibiwa na sioni kama Serikali kweli iko serious angalau basi kuilinda ile reli iweze kudumu. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iweze kutoa tamko kuhusiana na masuala ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho katika hatua ya sasa, nirudi tena katika suala la Uwanja wa Kimataifa wa KIA. Nilizungumza awali hapa kwamba, ule uwanja una mapato makubwa sana. Katika mwaka huu wa fedha, Mheshimiwa Waziri anatuambia katika hotuba yake, ukurasa wa 82 kwamba, mwezi wa Februari, Serikali imetia saini msaada wa bilioni 34.5 kwa ajili ya kuboresha Uwanja wa Kimataifa wa KIA. Na vilevile Serikali inaendelea kutafuta fedha nyingine bilioni 47.15 kwa sababu, ya kutekeleza awamu ya pili ya upanuzi wa uwanja wa KIA.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namuuliza Mheshimiwa Waziri may be atusaidie; hiyo ya awamu ya kwanza ilifanyika lini? Maana tangu KIA imejengwa miaka ya kwanza ya 70 uwanja ule haujawahi kufanyiwa upanuzi wowote wa maana. Sasa hiyo awamu ya pili ndiyo mnataka kuifanya je, awamu ya kwanza ilifanyika vipi na ilifanyika mwaka gani? Na katika kuifanya vilevile awamu hiyo watueleze hizi fedha zinaletwa na Serikali, je, yule anayeendesha uwanja yeye anashiriki vipi katika jambo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake mara ya kwanza tuliomba fedha kutoka benki ya dunia tukapanua run-way ya kia, lakini zile fedha zimelipwa na Serikali, hazikulipwa na wale wawekezaji. Sasa tunakopa tena fedha nyingine ambazo zinakwenda tena KIA ambazo ni fedha nyingi sana zaidi ya bilioni 50. Sasa tungeomba Mheshimiwa Waziri uweze kutoa majibu ya ziada kuhusu masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Freeman Mbewe. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Aden Rage.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru. Kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watu wao kwa kutuletea ajenda, kuanza kupata taaluma na kuweza kufanya kazi vizuri ya upilot, engineering na kadhalika. Nawashukuru sana tunaomba muendelee na juhudzi za kuwawezesha kina mama waweze kuwa marubani wazuri na mengineer wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba bajeti zote za maendeleo za Wizara zote hakuna ambayo imezidi asilimia 45, ya Waziri hapa amesoma ana asilimia 47. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba kwa kuendelea na utaratibu huu hatuwezi kabisa kabisa kubadilisha maendeleo ya nchi yetu kwa kutegemea bajeti ya Serikali.

Sasa wenzetu wanachokifanya kuna hili suala la PPP, Kenya wamepanga mpaka mwaka 2030, asilimia 80 ya development projects ziende kwenye PPP. Ivory Coast wao tayari wako asilimia 80 na 89 katika sekta hii kutoka distribution mpaka kuzalisha umeme. Nigeria wako mbali sana wanatumia almost 15 billion kwa mwaka katika PPP projects. Singapore mara hii wamepanga dola 978 billion mpaka 2030 katika miradi ya PPP. Kwa hiyo huwezi kubadilisha maendeleo ya nchi kwa kutegemea bajeti ya Serikali kwa miradi ya maendeleo

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati leo inataka trilioni nne ili uweze kuibadilisha, huwezi kutegemea bajeti hii ambayo pesa nyingi zinatumika kwa usafiri na mishahara karibu asilimia 60 halafu ukategemea kwamba ndiyo unaweza kuleta maendeleo katika nchi. Kwa hiyo lazima sasa Serikali ije baada ya kuitisha Sheria ya PPP kwa muda wa miaka tisa sasa, ije ituambie ni miradi ipi inakwenda kwenye PPP na inatangazwa kwenye magazeti, watu wanaomba ili ushindani upatikane, tuingie kwenye miradi ya PPP iwe wazi, siyo kama hivi inavyofanywa kwa siri siri. Hilo ningeliomba sana lifanyike ili tuondokane na tatizo hili tulilonalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la ATCL. ATCL imefufuliwa, lakini imefufuliwa kwa utaratibu ambao nafikiri una matatizo makubwa sana kwa sababu bado wanaendelea kutafuta videge vidogo vidogo. Hili ni shirika la Taifa, la nchi na limekuwepo muda mrefu.

Sasa mimi ningemuomba Waziri mkamilishe haya mahesabu, mkamilishe mahesabu ili muende kwa manufacturers wa ndege, mkakae mzungumze nao namna gani watakopesha shirika hili ndege kutohana na business plan proper itakayofanywa kuweza kulifufua shirika kikamilifu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, msirudie kosa la kuwa mna ndege moja mkawa na wafanyakazi 300, ndio tatizo lililotokea huko nyuma na mpaka leo kuna baadhi ya wafanyakazi walipunguzwa wale hawajalipwa haki zao, wako wengine wanalamika wamelipwa pungufu. Wako akina Mohamed Suyu na wengine wengi, wako wengi tu watakuja watawalalamikia, nafikiri na hilo mlimalize nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema kosa hilo msije mkarudia kwa hiyo mna kadege kamoja hicho mnakwenda mnaajiri watu mia tatu, mia nne hapana. Lazima muhakikishe kabisa kazi hizi ni *very technical* inahitaji watu wenyewe ujuzi, wenyewe uwezo, lakini vile vile efficiency lazima iwepo.

Airline industry ni *very expensive industry* haitaki mchezo hata kidogo, haitaki siasa ndani yake inataka maamuzi, uamue ufanye kazi. Wale *Ethiopian Airline* wame-manage kwa sababu wako wachache, Wakurugenzi watatu wanaamua biashara inaenda, hakuna siasa pale ukijaza siasa kwenye *Airline*, *airline industry* itakufa kesho asubuhi na haitafufuka hata kidogo. Kwa hiyo ningeomba hilo lifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu suala la kufufua *Airports*: Nawashukuru sana TAA wanafanya kazi nzuri. Lakini wametengenezewa *retention* hawa watu, *hundred percent retention* na ingekuwa *retention* hii inakamilika inapewa kikamilifu, viwanja vya ndege navyo vingekuwa katika hali tofauti sana. Mwaka jana walikuwa na *32 billion* wamepata, zimekwenda Serikali sijui kama zimekwenda Hazina au Wizarani, lakini wao wamerudishiwa *18.7 billion*, matokeo yake wameshindwa kufanya *development programs* zao kikamilifu. Sasa hili nafikiri lisahihishwe. Waziri utatueleza ama unazikata wewe pale Wizarani au zinakatwa Hazina, tuelezwe, maana ya a *hundred percent retention* maana yake warudishiwe fedha zao waendeleze miradi ambayo inakusudiwa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetaka vile vile Waziri atueleze hivi ni kwanini *FastJet* hawaruhusiwi kwenda Nairobi Kenya tunataka atueleze, kwa sababu wale wakifanya biashara ikiwa na ushindani ndio bei inakuwa kidogo nafuu. Tuelezwe ni suala la mikataba, ni kitu gani kwamba *FastJet* hawawezi kwenda Nairobi.

Lingine ambalo nilitaka vilevile atueleze Waziri, hawa wenzetu wa Rwanda na Burundi katika gharama zile za kutumia radar hatuwatozi chochote. Ni utaratibu gani unaotumika wa kutokuwatoza chochote. Nataka na hilo nalo uliweke clear.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kumwambia Waziri atusaidie; kuna hizi Government Aircrafts, kuna Gulfstream, kuna Fokker 28, Fokker 50 and so on and so forth. Hivi zinatumika kikamilifu? Kwa mfano Gulfstream kweli inaweza ikatumika kikamilifu, inatumika kikamilifu? Bado tunaona viongozi wanatumia mashirika ya kibiashara na ndege iko pale imekaa! Nina hakika kabisa kabisa *hours* ambazo ndege ile imeshachukua imeshakaa ni nyingi zaidi kuliko ambazo imeruka na gharama yake inazidi kuongezeka. Inawezekana pesa zote za gharama za kutengeneza ndege zikamalizika kwenye ndege moja ambayo haifanyi kazi sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kuelewa hii Gulfstream kweli inatumika kisawasawa wakati tunajua ina uwezo wa kutua hapa Dar es Salaam, Zanzibar, Kilimanjaro na pengine labda na Mtwara na Mwanza, *five airports, very expensive aircraft.*

Hebu tupate maelezo, kweli inatumika sawasawa, rasilimali zetu tunazitumia vizuri kwa ndege ile! Kama haitumiki, tuuze tutafute nyingine ambayo tunaweza kuitumia vizuri. Lakini sasa hivi nina hakika kabisa haitumiki vizuri na gharama yake ya kuitengeneza na kuisimamia pengine inakula hata ndege nyingine zote zilizoko pale na halafu haifanyi kazi sawasawa. Ninataka na hilo tupate maelezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la reli: Barabara zinatengenezwa kwa muda wa miaka miwili, mitatu zinakuwa mbovu kwa sababu tu usafiri wa reli ambao ndiyo unaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza mizigo wa mizigo ukasaidia. Sasa tumekuwa tunafanya matengenezo ya hii reli yetu kongwe.

Mimi nikuambie ukweli kabisa kama tunataka kufungua reli tujenge reli mpya, hii kongwe tutatengeneza kesho na keshokutwa, kila siku tutatengeneza. *You need a span of five years hujatengeneza kitu ndiyo tunaweza ku-survive katika uchumi, vinginevyo itakuwa kila siku pesa zinakwenda kwenye matengenezo haya.*

Sasa pengine tumechelewa, tumeshatoa maamuzi, mmeishafanya, lakini suala la kupata reli mpya katika maeneo ambayo hatujafanya, tusahau habari ya kufufua reli iliyopo, tujenge reli mpya kwa standard za sasa zilizoko, ambayo inaweza kuchukua mizigo, inaenda kwa speed kubwa zaidi ndipo tutaweza kufufua uchumi kwa haraka zaidi, vinginevyo tutashindwa kuingia kwenye ushindani hatimaye, gharama za uendeshaji zitakuwa kubwa, gharama za matengenezo zitakuwa kubwa na matokeo yake output yake itakuwa ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Hamad Mohamed, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Ismail Aden Rage atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu. Na mimi pia ningeungana na wenzangu kuunga mkono Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanywa na Madaktari wawili wote wakisaidiana na watumishi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha Bunge cha pili tu niliuliza Swali Na.6 kuhusiana na karakana ya Tabora. Naomba ni-quote paragraph moja tu; "karakana ya Tabora kazi yake ni kufanya matengenezo engine zinazohitaji utaalamu maalum, (*required specialty*)."
Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu nimeona kwenye taarifa hapa kuna habari njema, kuna vichwa vya treni karibuni 13 na mabehewa yasiyopungua 283 yatakuja.

Mwaka jana Dokta Mwakyembe alikuja Tabora na alifanya jambo moja ambalo hakuna hata Waziri mmoja amewahi kufanya hivyo, alipanda daladala ya baiskeli kutoka Tabora Hotel mpaka nyumbani kwangu kunifuata na nikampeleka kwenda kumuonesha matatizo ya reli pale Tabora na akawa muungwana akakubali, tukaenda nikamuonesha karakana ya Tabora. Karakana ile ya Tabora kwa sasa hivi ina upungufu mkubwa wa mafundi, ina watu 20 tu kati ya hao 10 tu ndiyo skilled workers wengine kumi ni watu ambao wanasaki.

Sasa kwa nini nasema umuhimu wa karakana ya Tabora? Mabehewa au vichwa vya treni vinavyopita pale Tabora, engine ikifika Tabora haiwezi kwenda mpaka ikae pale siyo chini ya saa mbili au tatu, kuna kitu wanafanya wale mafundi wanaita DTRS, yaani Daily Turn Round Locomotive Service na Causal repairs. Sasa ninapata wasiwasi tunanunua vichwa vipyta, hii karakana ambayo inawajibika, hivi vichwa vya treni vikitoka huko vinakotoka Tabora, Morogoro, vikifika pale kwa mujibu wa specification zake lazima hiyo service ifanyike hata kama imebeba abiria, ama imebeba mzigo, ichukue two hours to four hours. Bahati mbaya hivi sasa hakuna treni yoyote inayokwenda Tabora na hii tatizo ambalo niliwahi kutoa mapendekezo kwenye hotuba Waziri Mkuu niliyokuwa nachangia mwaka juzi pale Godegode. Wazee wa zamani ambao walikuwa wako Railways wanasma kulikuwa na Brigedia bridge, hawa wanaita wenyewe watu wanaoshughulika na madaraja. Wakati wa masika walikuwa wanawekwa pale, wanafanya diversion ya yale maji yanayotoka milimani badala ya kwenda yaka-cross over the railway line, walikuwa wanatengeneza mabwawa, very simple.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naanza na mimi kupata wasiwasi ukiangalia kwenye taarifa za mwaka jana zimetumika siyo chini za bilioni 16 kutengeneza hilo daraja. Kwa hiyo, mimi nafikiri iko haja hawa ma-engineer wa kizamani hebu tuchukue ushauri wao, yale maji badala ya kwenda yanavuka reli yawe diverted na kutengeneza bwawa lingine huko kuliko kungojea kila siku daraja linavunjika. Leo hii wananchi wa Tabora wanateseka, hakuna treni ya kwenda Kigoma, hakuna treni ya kwenda Mwanza, hakuna treni ya kwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo hatuwatendei haki hata kidogo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kuna chuo, napenda kumpongeza Waziri sasa kimefunguliwa tena, kilikuwa kimefungwa kwa muda mrefu, Tabora Railway Training School wako pale wanafunzi wanafundishwa udereva wa treni, ubwana gadi na TTE (*Train Ticket Examiner*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vilevile, siyo Mbunge kazi yako kulalamika, kuna mambo mengine mazuri yanafanywa na Wizara hii. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kututengenezea *Airport* yetu sasa kwa kiwango cha lami. Lakini nilikuwa naomba angalia kama kuna uwezekano ukatuwekea na taa ili ndege ziweze kutua usiku.

Nasema hivyo kwa sababu gani? Tabora ni sehemu ya katikati kwa wawindaji hawa *professional hunters* ambao wanakwenda Moyoosi, Katavi, Ugala, wanakwenda Maswa. Kwa hiyo na kituo kikubwa cha mafuta ya ndege, hata ndege zinazotoka Malawi ni Tabora. Kwa hiyo ukiweka na taa za usiku, kwa kweli utakuwa umetusaidia.

Ningependa vile vile kuwapongeza watu wa anga, ile *control tower* yetu pale ni safi sana, inafanya kazi nzuri, ina *control International flights* zote karibu zinazopita pale kutoka South Africa kwenda Europe. Kwa hiyo kwa kweli vijana wako Mheshimiwa Waziri, wanafanya kazi nzuri sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nilitaka kukumbusha tu kwamba bahati mbaya mimi nilipita kwenye reli ya kutoka Tabora kwenda mpaka Urambo, kuna majani mengi sana pale, kwa hiyo ma-engineer wanasema ni rahisi zile *wheels* kuteleza na zikatoa ajali. Kwa hiyo iko haja ya kuangalia wale watu wa magengeni wafanye kazi ya kuondoa majani na vilevile turudishe ile teknolojia ya kizamani ya kuweka michanga wakati wa kupanda kwenye reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, sina la ziada. Naunga mkono bajeti hii.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ismail Aden Rage. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Magolyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na mimi kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Kwanza kabisa sina budi kwa kweli na mimi nimpongeze kwa kiasi fulani Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyofanya kazi katika Wizara hii. Anafanya kazi katika hali ngumu kwa kweli kiasi cha kwamba Serikali inashindwa kumpatia fedha za kutosha kuweza kufanya yale ambayo ameyakusudia. Lakini nimpongeze zaidi rafiki yangu Dkt. Tizeba kwa namna anavyoshirikiana na Waziri wake kwa ukaribu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijielekeze katika hotuba ya Waziri ukurasa namba 61, ibara ya 89 aliyozungumzia kuhusu ununuzi wa *flow meters*. Katika bajeti ya mwaka huu Waziri amepanga kununua *flow meters* kwa shilingi bilioni 7.4.

Vilevile katika hotuba ya Kamati ukurasa wa 16, Kamati imetaka maelezo juu ya *flow meters* ambazo zilinunuliwa kabla. Katika taarifa ya Upinzani ilielezea vile vile suala zima la hizi *flow meters* na waka-quote maelezo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali au Wizara itueleze kwa sababu kabla Wizara ilinunua *flow meters* nane kwa shilingi bilioni 2.4 na *flow meters* hizi hazikutumika. Sasa leo katika hotuba ya Waziri anaendelea kusema kwamba wamepanga bilioni 7.4 kununua *flow meters* nyngine. Sasa tunataka Waziri atueleze ni kwa nini *flow meters* ambazo zilinunuliwa mapema hazikutumika na sasa hivi anataka kununua *flow meters* kwa ajili yakupimia mafuta?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa mafuta yanayoingia bandarini Dar es Salaam yanapimwa kwa kijiti, *flow meters* zote zilizonunuliwa zimebekwa pemberi, sasa hivi mafuta yanapimwa kwa kutumia kijiti. Sasa bado tunaendelea kusema kwamba tunapanga tena bilioni saba kununua hizi *flow meters* nyngine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie vilevile suala la ATCL. Tumesikia hapa ATCL sasa inafanya kazi na hiyo ndege moja ambayo wanayo na nyngine. Nataka kujua tu ni kwa nini mpaka sasa hivi ATCL haijaanza safari zake kwenda Pemba? Tunalo tatizo la usafiri Pemba, bado tunatumia videge vidogo vidogo. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri anieleze tu kuna tatizo gani? Kwa nini ATCL sasa hivi haiendi Pemba?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile ningeomba majibu kutoka kwa Waziri kuhusiana na kusitishwa kwa mkataba wa Mamlaka ya Bandari Tanzania na Kampuni ya Ocean Advance Industries Limited. Hili ni tatizo na inaonekana hapa kuna tatizo kubwa la kifisadi ambalo kwa kweli limesababishia hasara

Nakala ya Mtando (Online Document)

kubwa Serikali. Hasara hii ilitokana na ukarabati katika eneo la kutilia nanga la kituo cha kupakulia mafuta Kurasini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliingia mkataba na hii Ocean Advance Industries na kwa bahati mbaya mkandarasi huyu alibaki pale bila ya kupewa eneo la kazi. Kilichotokea mkandarasi huyu ilibidi aende Mahakamani adai fidia za kukaa pale kitu ambacho kilisababisha hasara kubwa kwa Serikali. Kwa hiyo ni vyema Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya upotevu huu wa shilingi bilioni 2.24 ambaao ulisababishwa na uzembe wa kutokupewa mkandarasi huyu eneo lile la kufanyika kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala ambalo mara nyingi napenda kulizungumzia hapa, suala la Bandari Kavu ya Katosho kule Kigoma. Nimelizungumza suala hili zaidi ya mara tatu, nne, tano na kila siku Serikali inasema tumetenga pesa kwa ajili ya bandari kavu ile. Lakini kinachotokea pale Katosho ni wananchi kudhulumiwa, kubughudhiwa kupigwa na kuonewa. Wala ujenzi wenyewe hauonekani wananchi wa Katosho wanapenda sana kuwa na bandari kavu. Lakini wanachotaka ni sheria ichukue mkondo wake. Sasa hivi tayari kuna vijana wengi ambaao wamefunguliwa kesi kutokana na mzozo ule wa Bandari Kavu ya Katosho.

Nakuomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri unalifahamu vizuri sana hili Mheshimiwa Dkt. Tizeba na mimi na wewe tumeshaliongelea sana hili suala. Hivi sasa hivi vijana wamewekwa ndani wamefunguliwa kesi mahakamani kwa suala hili la Katosho. Nakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri utakapokuja hebu tupatие maelezo kuhusiana na suala la bandari ya Katosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nilitaka nimuombe Waziri kutokana na kauli yake ambayo niliisikia juzi katika kipindi cha Jambo cha asubuhi cha TBC alipozungumzia suala la mgogoro wa TAZARA pamoja na wale wafanyakazi ambaao wamegoma pale TAZARA na kusema kwamba dawa anayo sasa hivi ya TAZARA na tayari ana vijana zaidi ya 2000 ambaao wanataka kazi. Kwa hiyo, anasubiri warudi mahakamani ili sasa yeye achukue hatua. Naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja, hili suala uliweke sawa ili tujue haswa nini unataka kukifanya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kabisa nilikuwa naiomba Wizara kwa sababu ina meli zile za SINOTA hebu iangalie namna gani ya kuipatia eneo la Dar es Salaam, Pemba, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara angalau kuwe na meli moja pale inayoweza ku-serve katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Nakala ya Mtando (Online Document)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed. Nilisema namuita Mheshimiwa Magolyo. Mheshimiwa Madabida utafuata.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuzungumzia bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutambua kazi kubwa anayofanya. Ni kweli tunasema usiposhukuru kwa dogo basi hata makubwa hutaweza kushukuru. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Ziwa ni muathirika mkubwa kiuchumi kutokana na tatizo la mawasiliano. Lakini jitihada ambazo zimeonyeshwa kupitia bajeti hii zinanipa matumaini. Taarifa kwamba kuna vichwa 13 vya treni vinatarajia kuwasili mwaka huu, mabehewa zaidi ya 200 yanatarajiwa kuwa yamefika ifikapo mwisho wa mwaka huu, ni habari njema sana kwa wananchi wote wanaotumia Reli ya Kati, napongeza sana juhudi hizo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba kusema tu mambo machache yafuatayo kuhusu wasiwasi wangu na uwepo wa bajeti hii:- Kwanza ni vizuri Mheshimiwa Waziri ajue hatua hii ya kutaja au kuweka fedha kwenye bajeti imekuja kwa kucheleta sana. Eneo hili ambalo uchumi wake umekuwa ukitegemea shughuli zaidi za usafirishaji kupitia reli limekuwa ndiyo mantiki uchumi kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita. Ukipita vimiji vidogo vidogo ambavyo miaka kumi iliyopita vilikuwa vinashamiri; Tinde, Didia, Ruhumbo, Isaka, Bukene, vyote sasa hivi viko deserted, ni vimiji ambavyo watu wamekwisha kusambaa, wamebaki watu wazima, vijana wengi wametoka maeneo hayo. Vitendo hivyo, au hali hiyo inamaanisha kwamba watu hao wameathirika sana kiuchumi.

Kipekee sana, nimuombe Mheshimiwa Waziri, katika kuzungumzia kuondoa msongamano Dar es Salaam na kuchochea uchumi Kanda ya Magharibi, eneo kuu ambalo liliwisha kupangwa siku nyingi kwa ajili ya kuweka bandari na linajulikana hivyo ni bandari ya nchi kavu ni bandari ya Isaka. Eneo hili limekuwa likitumika hivyo, sasa hivi ukifika eneo hili halitumiki kabisa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa kumsaidia tu Mheshimiwa Waziri nijaribu kumuonyesha umuhimu wa eneo hili na mji mzima wa Kahama. Kwa sasa mji wa Kahama unaitwa ni kama Dubai ya Tanzania. Mji huu ni shopping center kwa Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kigoma, Mkoa Geita, lakini pia nchi za Burundi, nchi ya Uganda na hata Kongo na Rwanda, wote hawa wanachukua mizigo yao myepesi na mizito kutokea mji wa Kahama. Na eneo ambalo ni nzuri sana kuweza kuwasogezza mizigo yao kwa reli ni bandari ya nchi kavu ya Isaka. Lakini pia kuna mizigo mwingine unaotoka eneo hilo kuja upande wa pili wa nchi yetu. Mji huu wa Isaka unahudumia migodi karibia minne mikubwa, mji

Nakala ya Mtando (Online Document)

huu unahudumia mgodi wa Buzwagi, mgodi wa Bulyanhulu, lakini pia na mgodi wa Geita. Hii migodi mitatu peke yake, mafuta yanayotumika mgodi wa Buzwagi peke yake ni zaidi ya lita milioni 2 kwa mwezi, mgodi wa Bulyanhulu mafuta yanayotumika pamoja na kwamba upo umeme, lakini ni mafuta zaidi ya lita milioni 1.5 kwa mwezi. Ukienda mgodi wa Geita na wenyе una zaidi ya lita milioni 10 kwa mwezi. Mafuta yote haya yanasafirishwa kwa malori.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitumia barabara kusafirisha mafuta kiasi hicho, kwa vyovyyote vile usitegemee barabara kama zitaweza kukaa muda mrefu. Njia pekee iliyoko ni ya kufufua bandari ya nchi kavu ya Isaka ili kuweza kupunguza msongomano wa mizigo kwenye bandari ya Dar es Salaam ili mizigo yote inayokwenda Kongo Mashariki kwa maana ya Goma, inayokwenda Rwanda, Burundi, Uganda, yote iweze kufanyiwa customs clearance kama ilivyokuwa zamani kwenye kituo cha Isaka ambayo ni ICD.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile hata mizigo unatoka kwenye migodi kama nilivyosema mgodi na wenyewe pamoja na kutumia mafuta lakini pia unasafirisha copper concentrate. Mgodi wa Bulyanhulu na mgodi wa Buzwagi unasafirisha coper concentrate zaidi ya malori 20 kwa siku, mgodi wa Buzwagi, zaidi ya malori kumi na mgodi wa Bulyanhulu zaidi ya malori 20 ambayo na yenyewe yanatumika sana katika kuharibu barabara. Niombe sana Mheshimiwa Waziri jambo hili pamoja na kazi iliyofanyika aweze kulitilia maanani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa anga na hasa nimpongeze sana Mheshimiwa Nchambi amelizingumzia sana hili, suala la uwanja wa ndege wa Shinyanga. Kutenga bilioni 12 kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Shinyanga ni habari njema, lakini hazitoshi na ninavyojuua hali ilivyo ya kifedha kwa Serikali itafika mwisho wa mwaka fedha zilizotoka labda ni bilioni moja, bilioni mbili. Nimuombe Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha atuhakikishie mgao wa kwanza fedha utakaotoka kwenye bajeti iwe shilingi ya kwanza itakayoipata kwenye Wizara yake iwe ni ya kupeleka kwenye uwanja wa ndege wa Shinyanga ili kweli inapofika mwezi wa sita mwakani uwanja ule sasa usiwe malisho ya mifugo wala mafugio ya kuku kama ambavyo baadhi ya wananchi wa Shinyanga wamezungumzia. (Makofi)

Pia, kuna viwanja vingine vidogo vidogo, Kahama kuna viwanja viwili, kuna uwanja wa ndege wa Mwendakulima, ambao kwa sasa hivi umewekewa fence na uko ndani ya eneo la Mgodi wa Buzwagi. Na kule kwangu Jimbo la Msalala kuna mgodi ambao kuna uwanja wa ndege ndani yake, ule uwanja wa Bulyanhulu. Viwanja hivi vilikuwa ni vya Serikali, sasa hivi vinatumika na mwekezaji peke yake.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Tulikuwa tunaomba sana yafanyike mazungumzo, viwanja hivi ni *public air strips*, viweze kutumika na umma. Kwa sasa hivi ukienda pale utasachiwa pale getini, mentality yao ni kwamba unakwenda kuchota mchanga wa dhahabu, japo tamaa ya kufanya hivyo inaweza ikawepo, lakini siyo nia ya kila mtu. (Makofii)

Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri viwanja vyetu uwanja wa Mwendakulima ni uwanja wa wananchi wa Kahama, uwanja wa Bulyanhulu ni uwanja wa wananchi wa Kahama. Viwanja hivi vitumike kwa *public* kama ambavyo ilikuwa zamani, watumiaji wa mgodi wawe ni watumiaji kama watumiaji wengine. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Mwanza, uwanja huu ni kitovu cha uchumi cha Nchi za Maziwa Makuu, uwanja huu hauhitajiki kwa ajili ya wananchi wa Mwanza peke yake, uwanja huu unahudumia hadi wananchi wa Sudani Kusini, wananchi wa Kenya Mashariki, Magharibi, wananchi wa Uganda. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Maige, nakushukuru sana.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, niombe hizi bilioni 16 zilizotoka hazitoshi ziongezwe na zitoke mapema. Nashukuru sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa nimuite Mheshimiwa Zarina Madabida na atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri Mary Nagu.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika mazingira magumu sana. Pia niwampongeze sana kwa kuwapa kipaumbele wanawake, kwa kweli ametoa nafasi nzuri sana yeye pamoja na watendaji wakuu kwa kuwapa nafasi wakinamama. Niwaombe wale wakinamama pamoja na mama Kijazi wa Hali ya Hewa, fanyeni kazi nzuri, kazeni buti, nginja nginja mpaka Ikulu, wanaume wametukubali kweli kweli. Nakushukuru Mheshimiwa Mwakyembe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Hapa tumeambiwa kuhusu masuala ya reli na kusema kweli ninawapongeza sana sana, lakini mabehewa yale zaidi ya 250 hayapatikani kama bilioni tisa hazikulipwa kabla ya mwezi Juni mwaka huu, mwezi Juni hii keshokutwa tarehe 30. Sasa mimi ninaomba commitment ya Serikali kwamba hizi pesa zitalipwa kabla ya tarehe 30 Juni, kwa sababu kinyume chake haya mabehewa hayawezi kuja na ninatarajia kutoa shilingi kwenye suala hilo. Kwa sababu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

tunajua kabisa kwamba reli ni uchumi, lakini pia reli itasaidia kupunguza uharibifu wa barabara, lakini vilevile itapunguza mzigo mkubwa kwa mwananchi kwa ajili ya kupunguza bei. Sisi sote hakuna asiyejua umuhimu wa reli, kwa hiyo tuisiwavute nyuma Wizara ya Uchukuzi kwa kutokulipia hizi bilioni tisa. Nataka *commitment* ya Serikali kwenye hilo, kinyume cha hapo mimi naomba nitoe shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakumbuka, na mimi ni mtoto wa reli, nimezaliwa kwenye reli, nimekulia kwenye reli kwa sababu baba yangu alikuwa anafanya kazi kwenye reli, kwa hiyo naijua vizuri reli. Mimi nakumbuka katika hii miaka ya hapa karibuni kulikuwa na watu ambao ni wawekezaji walinunua mabehewa na walikuwa wanayatumia wao wenyewe na kukodisha. Lakini tulipokwenda Malaysia wenzangu wamesema, tumekuta wenzetu wamejikita pia kwenye *Public Private Partnership*. (Makofii)

Sasa mimi ninataka kujua tu Wizara sisi tuna mpango gani? Kwanza haya mabehewa bado yapo? Huyu mtu bado anayo mabehewa? Lakini pia ni jinsi gani tutaweza kuvutia watu wengine. Kwa sababu haya mabehewa zaidi ya 250 yanayokuja ni kidogo sana, mabehewa yanayohitajika ni zaidi ya 3000 na vichwa zaidi ya 60. Kwa hiyo, mimi nilitaka kujua ni kwanini sasa basi tusiende kwenye *Public Private Partnership* kama wenzetu ili kusudi tuweze ku-speed up maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini reli ya Dar es Salaam, tumesoma hapa katika kitabu cha Waziri anasema kwamba watumiaji wa ile reli wameongezeka tokea 230,000 mwaka 2012 mpaka 1,300,000 kwa mwaka jana. Hili ni ongezeko kubwa sana na inamaanisha kwamba reli hii kama itafanyiwa mikakati itaweza sana kusaidia pia kupunguza msongamano. Hizo ni daladala nyingi sana sana Dar es Salaam. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeona mipango, lakini ili kusudi kuiboresha na hii reli iweze kuijendesha inahitaji siyo chini ya bilioni 8 ili kusudi iweze kupata treni angalau moja itakayokwenda kibiashara. Sasa nilikuwa napenda nijue kwa sababu kwenye kitabu cha maendeleo sioni, nimeona nimeoana kama bilioni 2.5. Kwanini tusiweke hizo fedha na mimi nakumbuka Mheshimiwa Magufuli hapa katika hotuba yake alisema mimi ningeomba Waheshimiwa Wabunge mkazane Wizara ya Uchukuzi iongezewe hela. Sasa Waheshimiwa Wabunge ni lazima waongeze hela ili kusudi waweze kufanya kazi, kinyume chake hawawezi kufanya kazi. (Maofii)

Mheshimiwa Naibu spika, TAZARA na Air Tanzania, mimi nasema Serikali inawapa TAZARA na Air Tanzania inawapa samaki badala ya kuwapa mshipi wakavue samaki. Pesa ambazo wana-*inject* kwenye TAZARA na Air Tanzania ni kidogo sana. Kwanini tusiweke hela za kweli ili kusudi TAZARA na Air Tanzania

Nakala ya Mtando (Online Document)

zikaweza kuijendesha. Kinyume chake tutakuwa tunawalipa mishahara kila siku bila kufanya kazi? Mimi naomba hili tupatiwe maelezo kidogo ni jinsi gani watawasaidia TAZARA na Air Tanzania ili kusudi waweze kufanya hiyo kazi wanayotakiwa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichukue fursa hii nimpongeze sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Mama Kijazi, kusema kweli huyu mwanamke anafanya kazi nzuri sana. Anafanya kazi nzuri sana, alituambia habari ya mafuriko muda mrefu kabla hata sisi kusema kweli wengine tulikaidi kidogo kutokuondoka kwenye mabonde, lakini anafanya kazi nzuri sana na hiyo ndiyo hulka ya wanawake kusema kweli wakipewa nafasi wanaweza, ndiyo maana nawaambia nginja nginja mpaka ikulu nafasi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ya kwangu ni hayo na ningeomba kupata maelezo hasa kwenye reli, kwenye masuala ya mabehewa.

Nimalizie kwa kusema nakipongeza sana Chama change cha Mapinduzi kwa kazi nzuri, kina watu mahili, kiko makini. Unajua ni rahisi tu kula ugali kwa picha ya samaki, halafu mwenzio mwingine anamla samaki. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Zarina Madabida. Sasa, Wabunge wengi mmechangia sana masuala ya PPP na tuna Waziri wa PPP, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, dakika saba.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua nafasi ya sekta binafsi katika maendeleo ya nchi yetu. Nawapongeza sana kwa kuleta hoja za kuharakisha utekelezaji wa sheria yetu ya PPP. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa mambo mengi, kwanza yeye ni moja ya Mawaziri waliokubali miradi mbalimbali kutekelezwa kwa njia ya PPP. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (Makofii)

Vilevile naungana na wenzangu kumshukuru sana kuonyesha uwezo wa wanawake kwa kuwaleta wanawake ambao wamechukua nafasi katika zile kazi ambazo watu wengi wanaamini ni za wanaume. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliona umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika miradi ya miundombinu na miradi mingine kwa kuleta sera ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ufupi PPP mwaka 2009, na ikapitisha sheria ya mwaka 2010 na tukapitisha kanuni za utekelezaji mwaka 2011. Serikali imetaka sana kuishirikisha sekta binafsi, lakini sheria tulioipitisha imeonyesha

Nakala ya Mtando (Online Document)

kwamba ina urasimu na sasa Serikali inaleta katika Bunge lako hili au lijalo mapendekezo ya kurekebisha sheria hii ili urasimu uondoke na PPP iende kwa haraka kuliko tulivyotegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, PPP itasaidia sana kwa sababu tumeona kwamba bajeti ya Serikali kwa mapato ambayo Serikali inayo haiwezi ikatekeleza miradi yote ya miundombinu ambayo tunataka iwepo kusudi maendeleo ya nchi yetu yaende kwa haraka sana. Kwa hivyo, nawashukuru sana kuona umuhimu huo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:- Kwanza, kuleta marekebisco ambayo yataondoa urasimu. Pili, kuwapeleka mafunzo wataalam wengi ambao watahusika na miradi ya PPP kusudi tusiwe na muda wa kupoteza tuweze kuishirikisha sekta binafsi ipasavyo. Lakini vile vile tumeona kuna umuhimu wa kuwa na mfuko wa PPP ambao utasaidia kwanza kutayarisha miradi itakayotangazwa na vilevile kuhamasisha sekta binafsi ambayo inaona ni mahali gani ambapo inaweza ikatekeleza na Serikali miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa sekta binafsi itakavyoshiriki katika kutengeneza miundombinu italeta hamasa kubwa. Kwa sababu miundombinu ni kama mishipa ya damu ndani ya mwili wa binadamu. Tunapokuwa na miundombinu ya barabara, miundombinu ya reli, miundombinu ya bandari kwa vyovypote vile gharama za kufanya biashara zitapungua, lakini vile vile miundombinu inachochoea miradi mingine ambayo ni ya manufaa na faida kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuhamasisha sekta binafsi na itambuliwe kwamba Wabunge wameikubali na wana nafasi pekee ya kuweza kuharakisha maendeleo ya nchi yetu na sisi Serikali tumekubali kuondoa urasimu na tumekubali kuunda Mfuko wa PPP ili hatimaye basi tuungane na sekta yetu binafsi, kuimarisha miundombinu yetu na miradi mingine ambayo itaharakisha maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno haya mafupi naamini na Waziri naye ataongeza kulieleza Bunge lako jinsi ambavyo yeye mwenyewe amechachalika kuitia PPP kuweza kutekeleza miradi ambayo kwa bajeti ya Serikali haitekelezeki. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba tutumie sekta yetu binafsi katika kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji.

MICHANGO KWA MAANDISHI

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu naWatendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika,kwakuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Tizeba amewajulisha wananchi wa Singida kuwa tarehe 25/05/2014,vichwa vipyta vya treni, mabehewa mapya na mengine yaliyokarabatiwa, sasa yamepatikana, wanaamini sasa usafiri wa treni kutoka Dodoma hadi Singida kupitia Manyoni utarudishwa. Reli ya Manyoni hadi Singida ni muhimu na ina msaada mkubwa kwa wananchi wa Singida. Naomba usafiri wa treni Manyoni – Singida urejeshwe.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Serikali inaadidi matengenezo ya uwanja wa ndege wa Singida, lakini hadi leo hii matengenezo hayo hayatafanyika, ni lini kiwanja cha Singida kitafanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alishaelekeza uwanja huu upanuliwe na kuboreshwa ili ndege za kibashara ziweze kutumia uwanja huu. Mheshimiwa Rais, alitahadharisha kuwa uwanja wa ndege wa Singida unaweza kutumika kwa minajili ya dharura, hasa ukizingatia usafiri wa ndege kutoka Mwanza - Shinyanga hadi Dar es Salaam, vinginevyo madhara yanaweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya TAZARA inasikitisha sana ni lini matatizo ya Tazara yatatatuliwa?

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni Sheria ya TAZARAambayo imepitwa na wakati. Inafaa ifanyiwe marekebisho hasa kifungu kinacholazimisha Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA lazima atoke Zambia, wengi walioteuliwa hawakuwa na uwezo, sheria lazima ibadilishwe ili mwenye uwezo ateuwiwe kuwa DG.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza Wizara ya Uchukuzi kwa kujenga Bandari ya Kipili pamoja na mpango wa kujenga bandari Kabwe. Lakini maoni yangu naomba Wizara ya Uchukuzi kuipa TPA yenewe kujenga hiyo Bandari ya Kabwe kuliko kutumia wakandarasi kwa kuwa wanachukua muda mrefu sana kujenga na kwa gharama kubwa sana na wengine hawana uwezo wakati TPA wana wahandisi waliobobeaa sana na watakamilisha kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, ombi, Bandari ya Kipili imekamilika, nimeomba Wizara ua Ujenzi na wameahidi kutengeneza barabara hiyo ya kilometra saba ili bandari ifanye kazi maana kwa sasa hakuna barabara. Nimezungumza na Katibu Mkuu Ujenzi Ndugu lyombe na kuniahidikujenga hiyo barabara.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sasa, naomba Wizara ya Uchukuzi kumkumbusha Katibu Mkoo Ujenzi suala hilo maana bandari ijengwe kwa mamilioni ya fedha itakuwa haina tija bila barabara, hivyo ushirikiano wenu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, usafiri umezorota sana Ziwa Tanganyika kutokana na Meli ya M.v Liemba kusimama mara kwa mara kwa ajili ya matengenezo. Tuliahidiwa meli tatu mpya katika Maziwa matatu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria, lakini mpaka sasa hakuna dalili ya hizo meli ambazo awali mlitueleza zinatengenezwa Korea Kusini. Juzi hotuba ya Waziri Mkoo inaeleza kuhusu ukarabati wa hizo meli kuukuu tu. Inaonyesha mpango wa meli mpya umeyeyuka kabisa. Naomba tupatiwe majibu sahihi.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA); Kuna wingu kubwa la kukosekana taarifa za uwazi na uhakika kuhusu uendeshaji wa uwanja huu wa ndege.

Mheshimiwa Spika, awali, uwanja huu ulibinafsishwa kwa kampuni ya *Kilimanjaro Airport Development Company (KADCO)* kwa miaka 25. Kwa mujibu wa taarifa za Serikali, mkataba huu ulivunjwa kisha Serikali kurejesha tena katika miliki yake ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuvunja mkataba huu, KADCO bado imeendelea kuendesha uwanja huu katika utaratibu ambao hauko wazi na kwa mazingira ya usiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali itoe taarifa za mazingira halisi yanayoukabili uwanja huu kwa kuweka wazi mambo yafuatayo:-

(1) KADCO ni nani?

(2) Nini nafasi ya KADCO katika uendeshaji wa uwanja huu?

(3) Nini mapato yatokanayo na uwanja huu kwa Serikali Kuu hata Halmashauri ya Hai ulipo uwanja huu?

(4) Nini vyanzo vya mapato katika uwanja huu?

(5) Mapato ya uwanja huu yanapelekwa wapi na kwa utaratibu gani? Mapato haya ni pamoja na yatokanayo na vyanzo vingine nje ya shughuli nyingine zilizo nje ya shughuli rasmi za uwanja wa Ndege (core business). Vyanzo hivi ni pamoja na upangishaji wa ofisi na maduka, maegesha ya magari, nyumba za KIA Estate, ukodishaji ardhi na kadhalika.

Nakala ya Mtando (Online Document)

- (6) Nini hatua ya vijiji vinavyozunguka uwanja huu ambao umechukua maeneo ya vijiji vya Sanya Station, Rundugai, Tindigani, Chemka na Kata za KIA na Masana Rundugai?
- (7) Nani mwenye hatimiliki ya ardhi inayozunguka uwanja huu (KIA Estate).
- (8) Ni utaratibu gani ulitumika kumpata mwendeshaji wa uwanja huu?

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nasema naunga mkono hoja hii.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri ya kusimamia shughuli za Wizara hii hasa katika kutengeneza reli, kufufua vichwa vya treni na ununuzi wa mabehewa mapya ya abiria na mizigo, pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Reli ya Dodoma – Singida, hotuba ya Mheshimiwa Waziri haikutoa mwelekeo wowote kuhusu kufufua usafiri wa abiria na mizigo kupitia reli hii. Wakati wa majumuisho tunapenda kusikia tamko la Serikali kuhusu hatima ya reli hii ambayo kwa takribani miaka mitatu sasa hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Singida: Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeeleza kuwa mradi wa kujenga kiwanja hiki upo katika hatua ya upembusi yakinifu. Hoja ya wana-Singida ni kwamba ujenzi wenyewe utaanza lini hasa?

Mheshimiwa Spika, usafiri wa njia ya maji Dar es salaam: Katika harakati za kupunguza msongamano Dar es salaam, pamoja na usafiri wa reli, lakini pia fursa ya usafiri wa maji bado haijatumika. Kwa kutumia sera ya PPP, inawezekana kabisa sekta binafsi ikiwekeza katika boti za kubeba abiria wanaoishi kando kando ya bahari kama Mbezi Beach, Kunduchi na Ununio nk.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauriwa kusimamia uanzishaji usafiriwa mjini kwa Jiji la Dar es salaam. Kwanini jambo linalowezekana lakini limecheleweshwa sana?

Mheshimiwa Spika, namalizia kusema naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mwakyembe na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii na kusimamia kazi kwa umakini na mafanikio makubwa. Vilevile nampongeza Katibu Mkuu na watendaji waliochini yake kwa ushirikiano wanaompa Waziri.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nachangia mambo yafatayo:-Nianze wa kuishukuru Serikali kwa kutenga Shilingi Bilioni 1.1 kwa ajili ya usanifu wa kina wa ujenzi wa Kiwanja Kipywa cha Ndege cha Msalato – Dodoma kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali itoe fedha hizo ili kazi ifanyike kwa wakati. Mtindo wa Serikali kutoa fedha zisizo kamiliika unachelewesha kazi. Kiwanja hiki ni muhimu kwa wakazi na wageni wanaosafiri kutoka na kuingia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inasimamia vitega uchumi ambavyo ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu ambavyo ni reli, viwanja vyta ndege, bandari, usafiri wa barabara n.k. Maeneo haya ni muhimu kupewa fedha kama zinavyoombwa.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo, pamoja na ufinyu wa bajeti, hivi Serikali haioni umuhimu kwa wazalishaji kupewa fedha zote ili wazalishe zaidi kama ufinyu wa bajeti unaendelea basi ni kwanini Serikali isikaribishe wawekezaji?

Mheshimiwa Spika, suala la mabasi kusafiri usiku lilipigwa marufuku na MheshimiwaJ. Malecela akiwa Waziri Mkuu na ajali zilipungua. Baada ya yeye kuondoka, agizo hili limepuuzwa.Naomba kujuahuo ndiyo utaratibu maana ajali zimeongezeka?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Pia nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara kwa utendaji mzuri.

Aidha, nampongeza Waziri kwa kuwaleta akina mama, umetimiza ombi langu kwa macho nimejionea, hongereni. Lakini bado wengi walioko bandarini, ombi langu la kutaka kuja bandarini kutoa elimu ya ujasiriamali bado liko palepale.

Mheshimiwa Spika, naomba Mkurugenzi wa bandari afungue milango sasa tukutane na wanawake wenzetu, kinyume na sasa tunakutana wakati wa Mei Mosi na Siku ya Wanawake Duniani.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bandari kumekuwa na mambo mengi, lakini achaneni nayo fanyeni kazi, kazi nzuri na ongezeko la mapato itakuwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

ndiyo mwisho wa majungu, uchumi utaongezeka na maslahi ya wafanyakazi yataboreka.

Mheshimiwa Spika, nipongeze mipango yote. Mlituahidi watu waDar es salaam, mmetimiza, malori yamepungua Kurasini na mengine n.k. Treni ya ubungo iendelee kuboreshwa na ile ya Pugu ianze sasa.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ni muhimu, naomba Wizara iongezwe fedha ina mambo mengi. Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, Serikali inataka kutwaa eneo la Vijibweni katika Jimbo la Kigamboni kwa ajili ya upanuzi wa bandari. Mimi kama Mbunge wa wananchi wa eneo hili tuna ufahamu mdogoo sana juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua kutoka kwa Waziri, mambo yafuatayo:-Nini TPA inataka kufanya pale Vijibweni? Je, mradi unahitaji eneo kiasi gani? Gharama ya mradi huu nishilingi ngapi? Je, fedha za kulipa fidia ziko tayari? Lini Serikali inataka kuanza mradi huu?

Mheshimiwa Spika, nimeandika barua mbili kwenda Wizarani bila majibu. Ili kupata ushirikiano wa kutosha toka kwa wananchi wa Vijibweni ni vyema barua zile zikapata majibu.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-Reli ya Mpanda: Naomba Wizara ihalakishe matengenezo yake yawe ya dhati hasa kati hya Kaliua na Ugalla. Mradi wastandard gauge ni muhimu na reli hii nayo iwemo.

Mheshimiwa Spika, unapoelekea Kigoma kutoka Kaliua, station ya kwanza ni Kombe. Hii ilifungwa miaka mingi iliopita sababu ilikuwa inatumika chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, Kombe sasa imekua na ukijumuisha na Vitongoji vyake kuna watu zaidi ya 5000 wenyе biashara kubwa kubwa kama mpunga, mahindi, tumbaku, ng'ombe na mbuzi. Isitosheabiria wapo wengi sana wenyе shida mbalimbali kama vile biashara, afya na zingine za mambo ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, kuwalazimisha hawa watu wakapandoe treni la abiria Kaliua au Usinge ni kuwapa adha kubwa sana maana Kaliua na Usinge zote ziko maili 20 toka Kombe na hasa ukizingatia kuwa treni inapita Kombe usiku,

Nakala ya Mtando (Online Document)

inapokwenda na kutoka Kigoma. Mheshimiwa Waziri, tafadhali rejesha station hii.

Mheshimiwa Spika, palepale Kombe tumeomba *check line* miaka mingi sana. Tafadhali sana Mheshimiwa Waziri tusaidie tupate *checkline* hii ili tuwezeshe watu wa Vitongoji vya Ikombaboba, Mwamapuli na Mwabusabiwaweze kufanya shughuli zao za kiuchumi na afya kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kaliua imeshakuwa ni Wilaya mpya, ni muhimu kiwanja chake cha ndege kikaongezwa urefu *runway* yake ili iweze kupokea ndege za Serikali zinazobeba viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimkiwa Waziri atakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuwa anaweka jiwe la msingi la kiwanja cha Julius Nyerere *Terminal 3* alikumbushia ahadi hii. Tafadhali tusaidie Mheshimiwa Waziri kukamilisha kiwanja hiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme: Namuomba Mheshimiwa Waziri hizi Stesheni za Kaliua, Kombe na Usinge ziwekewe taa za umeme ili kusaidia ulinzi.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuwa Stesheni ya Kaliua kuna umeme, lakini taa zake zimebekwa kwenye jengo la stesheni tu, sehemu kubwa ya yadi iko gizani. Hii inahatari kwa wasafiri na mizigo yao na hasa ukizingatia kuwa reli ya Mpanda inaanzia Kaliua.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru sana kwa ukarabati mlioufanya kwenye jengo la stesheni pale Kaliua. Lakini mmeacha jengo moja la Railway Polisi hali yake ni mbaya sana. Naomba jengo hili nalo mlkarabati lifanane na lile la stesheni.

Mheshimiwa Spika, mwisho stesheni ya Kaliua, ilikuwa inanywesha maji injini za treni. Kwa kuwa huduma hii inaelekea kuimarishwa tena, ni muhimu kisima cha reli kilichopo hapo kisafishwe na kitunzwe kama zamani. Kisima hiki kina maji mengi sana.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri, Mheshimiwa Tizeba kamuahidi Kikwembe kumpa stesheni ya Kambuzi. Mie nimeomba stesheni ya Kombe iliyofungwa miaka mingi ifunguliwe tena kwa kuwa watu wameongezeka sana, hakuligusia kabisa, kwanini au kwa kuwa mchango wangu ni kwa maandishi?

Mheshimiwa Spika, narudia kukushukuru na Kuunga mkono hoja.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, napongeza kazi nzuri za Wizara hii hasa inayofanywa na Viongozi waandamizi hasa Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono kwa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, usafiri wa majini: Ziwa Tanganyika kwa muda mfupi ujao litakosa usafiri wa meli kutokana na uzee wa meli ya Mv.Liemba. Tuliahidiwa na Mheshimiwa Rais kupata meli nyingine. Tafadhalii meli ipatikane, Serikali ina wajibu wa kuwapatia wananchi usafiri huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo lango la Nkasi Kusini, na Wilaya ya Nkasi kwa ujumla kuna Vijiji zaidi ya 33, vingi viko kandokando na karibu vyote havijaunganishwa na barabara ukiacha vile vya Kabwe na Kilorando, vinavyobaki hakuna barabara ya kutegemea.

Mheshimiwa Spika, vituo vya meli: Licha ya meli kuonekana kutokutegemewa sana katika siku za usoni, pamekuwa na mahitaji ya kutaka ianze kutua katika vituo vya Msamba ambapo ni eneo lina wavuvi wengi na hivyo kuwa na uwezekano wa mizigo mingi hata abiria pia.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Wampembe kujengwa bandari: Tuna kituo cha Kipili pekee katika Wilaya ya Nkasi ndicho kinaendelea kujengwa bandari. Lakini kituo cha Wapembe ni kikubwa sana na kile kinachotaka kujengwa Kabwe. Naomba Serikali ikubali maombi yangu ya kila siku kuwa Wampembe ni makao makuu ya Tarafa na kituo kikubwa kabisa, kwa nini tuiswajengee wananchi bandari kuboresha kituo na usalama kwani hali ya sasa inatishia sana maisha ya abiria na wananchi wa Wampembe. Nipe jibu leo, vinginevyo nashika mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Rukwa ni wazalishaji wa wakubwa wa nafaka aina ya mahindi. Mahindi yote yanayochukuliwa Mpanda kwenda maeneo ya Kaskazini yenye njaa yanatoka maeneo ya Nkasi, Sumbawanga na Kalambo.Jambo hili la kujenga reli hadi Sumbawanga lingeinua kilimo mkoani Rukwa, lakini pia kuiokoa Serikali kutokana na hasara inayopata sasa kila mwaka kukodi malori kutoa mahindi Sumbawanga kwenda Mpanda kwenye treni. Hii ni hasara na pia kuna uharibifu mkubwa wa barabara toka Sumbawanga kwenda Mpanda, hata kama itawekwa lami haitadumu. Okoa hasara ya Serikali, inua kilimo wakati uko kwenye maradaka wewe mchapakazi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, kutokana na vyombo vyua usafiri majini kutokuwa na usalama wa kutosha, SUMATRA ihakikishe inadhibiti na kukagua vyombo hivyo mara kwa mara, aidha meli zenyenye umri mkubwa zisiruhusiwe kufanya biashara ya kubeba abiria kwani ni risk kwa maisha ya abiria.

Mheshimiwa Spika, wanawake wanaofanya kazi katika Wizara hii, nawapongeza kwani jamii huzitizama kazi zao hizo, mfano, kuendesha malori, kuendesha treni kuwa ni kazi ngumu na hivyo kufanywa na wanaume.

Mheshimiwa Spika, napendekeza wapewe *special allowance* ili kuvutia wanawake wengi zaidi kufanya kazi ambazo wengi wanaamini ni za kiume.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa hivi sasa kuna ukosefu wa ramani mpya ndani yabahari kuu na maziwa yote kwa ajili ya kuonesha kina halisi cha maji, Serikali ione umuhimu wa kuwa na ramani mpya na hivyo kuweka mpango madhubuti pamoja na kutenga fedha za kutosha kukamilisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa zipo bandari nyingi sana na mialo isiyo rasmi ambayo ni hatari sana hasa kwa uingizaji wa dawa za kulevyta na wahamiaji haramu hapa nchini. Aidha usalama wa abiria hauratibwi jambo ambalo ni hatari sana kwa nchi yetu. Serikali iweke doria maalum (*special boat*) ili kubaini na kudhibiti bandari bubu.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa miundombinu ya kuongozea meli (*navigation aids*) hasa katika maziwa yetu ni jambo la kuturudisha nyuma sana. Itengwe fedha ya kutosha kushughulikia miundombinu hiyo kwa ajili ya usalama wa wananchi wanaotumia usafiri wa majini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vifaa vyua uokoaji katika usafiri wamajini havipatikani kwa urahisi kutokana na gharama yake kuwa kubwa, Serikali ipunguze kodi au iondolewe kabisa katika vifaa vyua uokoaji majini.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya wananchi kuifahamu SUMATRA zaidi, matangazo yenye muundo wa mtu kuelezea yaani (*special programme*) katika TV, Radio, yatumike zaidi badala ya tangazo la picha ili watu wengi waielewe SUMATRA na hivyo kuitumia zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. LOESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Uchukuzi kwa hotuba nzuri. Nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa utendaji mzuri.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mimi nitaongelea kiwanja cha ndege cha Mwanza. Kiwanja cha ndege cha Mwanza, kwa mujibu wa mkataba wa mradi ultakiwa ukamilike ndani ya muda wa miaka mitatu (miezi 36) kwa gharama ya shilingi bilioni 105. Mtiririko wa utoaji fedha tangu mwaka 2013/2014 hadi sasa siyo wa kuridhisha kabisa.

Naunga mkono hoja ya kamati ya kudumu ya Bunge katika hoja yake kwamba Serikali itoe tamko rasmi juu ya nia thabiti ya utekelezaji na muda wa kukamilisha mradi huu wa upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. Ni ukweli usiopingika kuwa taswira inaonyesha kuwa mradi huu unasuasua.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati: Katika nchi nyingi zilizoendelea kiuchumi usafiri wao wa uhakika ni treni, (usafiri wa reli). Mara nyingi hata usafiri mjini unaotumika mara nyingi ni usafiri wa reli. Katika nchi yetu tumejaliwa kuwa na rasilimali muhimu sana kama vile bahari ambapo tuna bandari, mizigo mingi sana inasafirishwa kwenda sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Bila ya kuwa na usafiri wa reli wa uhakika hata barabara zetu zitaharibika haraka sana kwa sababu ya mizigo mikubwa inayosafirishwa kwa njia ya barabara.

Kwa maelezo haya ninaunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara nikiamini kwamba mipango yote itakwenda kama ilivyopangwa. Zaidi sana Serikali iongeze fedha zaidi kwenye Wizara hii ili utekelezaji uweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuipongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, Naibu Waziri na Watendaji kwa kazi nzuri na leo kutuletea wanawake wanaofanya kazi katika nafasi nadra (rare occupation) katika sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, natoa mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni usafiri kwa njia ya anga. Napongeza juhudzi za Serikali katika kushawishi mashirika ya ndege ya nchi mbalimbali kwa mkataba wa *Bilateral Air Service Agreement (BASA)* kuja Tanzania. Hata hivyo, bila kuwa na *National Air Line* siyo jambo jema kiuchumi. Kutegemea ndege za nje katika biashara ya utalii hii ni njia ya uvujaji wa mapato ya fedha za nje (*leakage of foreign currency*). *Nashauri Air Tanzania Corporation* iboreshwe kwa ajili ya biashara ya utalii na kusafirisha mboga nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nisuala la reli, bila ya usafiri huu, mizigo inayosafirishwa kwa njia ya barabara huua barabara. *Nashauri Serikali* itafute

Nakala ya Mtando (Online Document)

mkopo ili usafiri wa reli uboreshwe kwa usafirishaji wa mizigo na abiria, reli imilikiye naSerikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ushiriki katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC). Nimeona ushiriki waTanzania katika miradi mingi ya uchukuzi katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki - bandari na reli. Kwa ajili ya usalama (risk) ya kuweza kuyumba mashirikiano ya Afrika ya Mashariki, nashauri Tanzania iwe na mpango wa kuendeleza sekta hizi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, viwanja vya ndege hasa JMK, KIA na Mwanza na Arusha Airport vinahitaji upanuzi na matengenezo ya run way kwa ajili ya ndege kubwa. Nashauri uwanja wa Arusha uwekewe taa ili ndege ziweze kutua nyakati za usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Pili, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kuanza ujenzi wa upanuzi wa kiwanja cha ndege cha JNIA (*Terminal III*) katika Jimbo langu la Segerea. Hata hivyo, inasikitisha kwamba Wizara imeshindwa kufidia wananchi wa Kipunguni ili wahame kupisha upanuzi wa JNIA. Fidia inayotakiwa ni kama shilingi bilioni 20 tu ambazo kama Serikali ingekuwa na dhamira ya kweli isingeshindwa kutoa fedha hizo ili kuondoa usumbufu, kero na maisha ya mashaka kwa wananchi hawa wa Jimbo langu. Kwa miaka mingi sasa wananchi hawa hawajui hatma yao, wanashindwa kuendeleza makazi yao kwa kutojua lini watalipwa na nyumba zao kubomolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama uendelezaji wa JNIA eneo la Kipunguni utachukua miaka kadhaa ijayo, ni vyema wananchi hawa wakafidiwa ili waondoke eneo lile kwani eneo hilo si salama kwa wananchi kuendelea kuishi pale hasa ukizingatia kwamba baada ya *Terminal III* kukamilika, ndege kubwa zaidi kama *Airbus 380* ambazo zitaleta usumbufu na kero kwa wananchi hawa wakati wa kutua na kupaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika kuona kwamba kwenye Hotuba ya Waziri waUchukuzi wala hajagusia au kuahidi chochote kuhusu fidia hii. Namwomba Waziri wakati anahitimisha hoja yake atoe ahadini lini wananchi wa Kipunguni kwenye eneo la JNIA watalipwa fidia yao?

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hotuba yako tu kama nitapata majibu ya kuridhisha na nategemea kuondoa

Nakala ya Mtando (Online Document)

shilingi wakati wa vifungu katika mambo mawili, ujenzi wa Mwanza Airport na ujenzi wa gati Na. 13 na 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza umekuwa wa kusuasua. Kwa mujibu wa mkataba uliokuwa umalizike ndani ya miaka mitatu baada ya kusainiwa Juni 2012, Naibu Waziri, Tizebaaliwakilisha Serikali, wananchi walipewa matumaini makubwa kwamba sasa uwanja huo utakamilika kupanuliwa. Kwa mujibu wa mkataba, uwanja huo ulikuwa ukamilika Juni 2014 lakini cha kushangaza hadi sasa hakuna kinachoendelea. Je, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja huo katika mkataba ulikuwa ujengwe jengo jipyia la kisasa la abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni moja kwa mwaka, upanuzi wa sehemu ya kutua na kurukia kutoka mita 3000 hadi mita 5000 ili ndege kubwa ziweze kuruka na kutua lakini pia ujenzi wa eneo la maegesho katika hali ya usalama zaidi. Zimebaki siku kadhaa za mkataba kumalizika lakini dalili za ujenzi hazionekani. Jengo la abiria halijaanza, maengesho bado na sehemu ya kurukia bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu awali kulikuwa na mgogoro baina ya mkandarasi na Serikali kuhusu michoro lakini hizi danadana za nini, inatia mashaka. Hivi Serikali haijui umuhimu wa uwanja wa ndege wa Mwanza? Ipo minong'ono ya kwamba uwanja wa Mwanza ukimalizika uwanja wa KIA utadorora hasa kwa upande wa watalii hivyo kufanya magari ya kukodi kukosa biashara, naomba hii isiwe sababu. Uwanja wa ndege wa Mwanza una umuhimu mkubwa sana hasa katika Ukanda wa Maziwa Makuu kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa lakini pia itawapunguzia kusafiri kwa umbali watalii wanaotaka kutembelea mbuga za wanyama za Serengeti, Rubondo na Sanane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa uwanja huo kutakuza biashara ya nchi za Maziwa Makuu, Mwanza iko katikati ya Nchi za Maziwa Makuu. Mwanza ni Mkoa wa pili kwa kuingiza pato la Taifa baadaya Dar es Salaam ambapo panajengwa Terminal III, uwanja unaojengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 500. Sitashangaa kuona uwanja wa Dar es Salaam uliopangwa kukamilika 2015 unakamilika kabla ya uwanja wa Mwanza. Gharama za kujenga uwanja huo inakisiwa kufikia shilingi bilioni 105, cha kushangaza, Serikali imekuwa haionyeshi dalili za kuujenga uwanja huo kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012/2013, Serikali ilitenga shilingi bilioni 8.0 lakini pia mwaka 2013/2014 ilitenga shilingi bilioni 8.0 lakini mbaya zaidi hadi leo ni shilingi bilioni 1.6 ndizo zilizotolewa, kwa mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni 12. Huuni mchezo wa kuigiza, gharama ya mradi shilingi bilioni 105,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

unatenga shilingi bilioni 12, huu ni utani, ni kiini macho. Mimi sioni nia thabitii ya kumaliza ujenzi katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni nini? Waziri namjua kwa usimamizi wa mambo, mbona siku hizi amekuwa mzito katika maamuzi tofauti na zamani? Kama huyo mkandarasi ameleta certificate ya shilingi bilioni 15, Mhandisi Mshauri anadai shilingi bilioni 2.5 ambayo jumla yake ni shilingi bilioni 17.5, yeye anatoa shilingi bilioni 1.6 quarter inaisha, watu hawa hawajalipwa, kwa utaratibu huu swalii langu lipo palepale je, Serikali ina nia ya dhati ya ujenzi wa uwanja huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bajeti inayotengwa dusurodusuro mwaka 2012/2013 shilingi bilioni 8.0, mwaka 2013/2014 shilingi bilioni 8.0 na mwaka 2014/2015 shilingi bilioni 12 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 28, ujenzi huo utamalizika baada ya miaka mitano, ni bora pesa zinazotengwa zingekuwa zinatolewa zote. Naungana na Kamati kuitaka Serikali ileze kwa kina na itoe tamko ni kwa nini Serikali (Hazina) isitoe/isitenge pesa za kutosha ili uwanja huo muhimu uweze kujengwa na kukamilika chini ya miaka mitano?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie ujenzi wa gati 13 na 14, kama Kamati ilivyopendekeza, njia pekee ni PPP, utaratibu huu ndio suluhisho pekee litakalomiliza tatizo la ujenzi wa gati 13 na 14. Yapo makampuni makubwa ukitangaza haitachukua muda, yapo makapuni makubwa ya Dubai, Singapore, Hongkong na mengine. Waziri afanye maamuzi ili hata mjinga asimnyooshee kidole, nina uhakiki akifanya vizuri atasifiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema Waziri Mwakyembe ile kasi yake aliyokuwa nayo imepungua, taasisi zilizochini ya Wizara yake haziendani na kasi kufuatana na shughuli zake za kila siku. Ubunifu wa taasisi zake siku hizi haupo, TPA hawamsaidii kupunguza matatizo yaliyopo, ni vizuri TPA wakajipanga vizuri ili kurejesha heshima ya TPA, kila mfanyakazi awajibike mahali alipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAA ilifanya uamuvi wa kukopa fedha CRDB za ujenzi wa upanuzi wa Dar es Salaam Terminal III, ni uamuvi mzuri huo, ndio ubunifu wenye tija. Naupongeza uongozi mzima wa TAA ukiongozwa na CEO wao kwa utaratibu huo uliotumika kukopa pesa CRDB kwa sababu Serikali haina pesa za kutosha. Kwa nini TAA isikope CRDB ili kukamilisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema nitaunga mkono endapo nitajibowi kwa kina kuhusu pesa za uwanja wa ndege wa Mwanza.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri yeye na msaidizi wake kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya. Hakika Watanzania wengi wanajivunia utendaji na utumishi wake uliotukuka katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetumwa na wananchi wa Vunjo kwa niaba ya Mkoa wa Kilimanjaro nimwombe Waziri aangalie uwezekano wa kufufua reli ya Dar es Salaam - Moshi - Arusha - Taveta Kenya. Wananchi wanaona reli hiyo ni muhimu hasa kwa kusafirisha wanafunzi ambao ni wengi sana wanaotoka maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam kwenda kusoma Mkoa wa Kilimanjaro. Wanachi hao wanaamini kwamba reli hiyo ilihujumiwa ili watu wenye malori waweze kufanya biashara nzuri kwa kutumia barabara. Namwombasana Waziri wakati wa ku-wind upanisaidie kufafanua kama kuna uwezekano wa kufufua reli hiyo na hasa ile inayopita kwenye Jimbo langu la VunjoKahe- Himo Sidingi hadi Taveta Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani za awali.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ATCL hongera kwandege ya pili.Napendekeza ziwepo flights Dar es Salaam – Tabora - Mpanda – Kigoma – Bujumbura – Kigali maana wasafiri na mizigo ni wengi hivyo tija na faida ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, gati 13na 14 na reli ya kati. Miaka ya kati ya 1960,Waasisi Hayati Mwalimu Nyerere, Mzee Kaunda na Mao Tse Dung walikubali kujenga reli ya TAZARA. Benki ya Dunia na Marekani walikataa reli isijengwe bali barabara, TAZARA ilijengwa. *World Bank* haitaki tujenge SGR (Standard Gauge Rail) sababu wanasema mizigo haitoshi hivyo tuboreshe hii gauge nyembamba 1000mm.

Hilo pia litafuatia kutojenga gati 13 na 14 kwani tayari TMEA na Serikali ya Kenya wamejenga Gati 17 na 18 Mombasa. CCCC wanajenga fly overs Nairobi na Kampala. Pia Lamu – Ethiopia, Sudan, S. Sudan na Uganda CCCC wanajenga ila sisi PPRA wanasema *World Bank* imetoa black list. Hivi hizi nchi siyo wanachama wa *World Bank* ila sisi tu Tanzania? Tuwe waangalifu bandari na reli ni muhimu hasa SGR. Bandari gati 13 na 14 gharama ni zaidi ya \$523. Magati mawili (2)-\$250m, upanuzi lango la bandari-\$65m, superstructure/cranes reach stackers -\$185m, kuongeza kina cha gati 13 na 14 na kuhamisha bomba 39 KOJ na ku-dredge eneo la kumega Kigamboni ili PAMANAX meli kubwa ya 20–25,000 TEUiweze kuweka nanga ni \$ 200. Ninauzoefu wa magati zaidi ya 70 duniani.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru uwanja wa ndegewa Tabora nilami na nashukuru kwa reli ya ratili 80 ya Igala Jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Serikalikwa kazi nzuri. Naomba kushauri yafuatayo:-

- (i) Ujenzi wa bandari kavu ya Kisarawe uharakishwe ili kupunguza msongamano wa malori Jijini Dar es Salaam.
- (ii) Wizara ishirikiane vyema na Wizara ya Ujenzi kujenga haraka barabara ya lami kutoka Mlandizi hadi Mzenga Wilayani Kisarawe ambapo bandari kavu inatarajiwa kujengwa katika Kijiji cha Vihigo – Mzenga ili kusaidia malori yatakayotoka katika bandari kavu kwenda Mikoani na nje ya nchi kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. CHIRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami nitoe maoni yangu katika sekta hii muhimu ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yoyote ile inayohitaji maendeleo ya kweli, uchukuzi ni sekta ya kipaumbele na utekelezaji wake hufanywa bila mzaha na kushirikisha sekta binafsi ambayo hutekeleza kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya kati imeendelea kupuuzwa na Serikali hii ya CCM. Hakuna asiyejua umuhimu mkubwa kiuchumi wa sekta hii ya reli na hasa reli ya kati. Reli ya kati si tu inategemewa na wananchi wengi wa Tanzania lakini pia nchi jirani za Maziwa Makuu zisizopakana na bahari wanahitaji sana ufanisi wa reli ya kati ili wasafirishe shehena zao. Cha kushangaza ni kuwa Serikali ya CCM ndiyo pekee isiyoona umuhimu wa reli hii katika kukuza uchumi wetu. Kila mwaka Serikali imeshindwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kufufua reli ya kati na hata hizo kidogo zinazotengwa hazitolewi zote.

Hili huenda linafanywa kwa makusudi, ni kwanini sekta ya barabara ndiyo inayopewa kipaumbele zaidi na kupewa fedha nyingi zaidi ya sekta zote za usafirishaji? Ikiwa wote tunajua na kuamini kuwa reli ndiyo mhimilishaji kwanini Serikali inaihujumu reli ya kati na kujenga barabara nyingi zaidi, nani ndiye mmiliki wa malori haya ya usafirishaji? Nani ndiye muuzaji wa mafuta tena yasiyolipiwa kodi? Kodi ya usafirishaji huu mkubwa wa barabara iko wapi? Tukiwa wazalendo wa kweli na kuyapatia majibu sahihi maswali hayo tutaweza kufanya sekta ya reli ikafanya kazi kwa ufanisi kwa ajili ya uchumi wetu.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa barabara wa kusafirisha wananchi na mizigo ambayo sio mizito, pamoja na sekta ya barabara kupewa umuhimu wa juu, barabara hizi kwanza zinajengwa bila kukidhi viwango na huharibika kabla ya muda wake kwa kuwa haziwezi kuhimili uzito wa mizigo. Watanzania wataendelea kutoa fedha za barabara zisizodumu hadi lini? Ni wakati sasa japo kuwa imechelewa sana Serikali ikafufua reli ya katilili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuwapongeza Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni ilituweze kuijadili na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufinyu wa bajeti, pamoja na umuhimu mkubwa wa Wizara hii bado Serikali imekuwa ikiendelea kutenga kiasi kidogo sana cha fedha ya bajeti ukilinganisha na kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii. Licha ya tengeo dogo hilo bado hata hiyo pesa ya maendeleo hawapatiwi kwa wakati hivyo husababisha miradi kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vyaa usafiri sio rafiki na watu wenye ulemavu. Bado Serikali haijaweka utaratibu mzuri wa kuwasaidia watu wenye ulemavu katika vyombo vyaa usafiri ukilinganisha na nchi nyingine. Napenda kujua mkakati wa Serikali kuhusiana na watu wenye ulemavu, mpango wa muda mfupi na mpango wa muda mrefu. Pia napenda kujua kama kuna mpango hata wa kuwa na sheria itakayowalinda walemovu na kuhakikisha vyombo vyote vyaa usafiri hasa mabasi (daladala) yanawawekea mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Viwanja vyaa Ndege. Niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya kwa ujenzi wa viwanja mbalimbali nchini na ahadi ya viwanja 11 kufanyiwa upembuzi yakinifu kikiwemo na kiwanja cha Nduli katika Mkoa wa Iringa. Naomba Serikali itenye pesa kwa ajili ya ukarabati wa hivyo viwanja ambavyo bado havijawa katika mpango wa ujenzi, kwa sababu kiwanja cha Nduli kinatatizo la muda mrefu la ukarabati wa njia ya kurukia (runway) na pia kuna tatizo la mifugo kukatiza katikati ya kiwanja, kinahitaji uzio, kukatiza kwa mifugo kunahatarisha usalama wa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia mamlaka iwe na tengeo maalum kwa ajili ya tahadhari ya kukabiliana na hali ya hewa kwa mfano kama kiwanja

Nakala ya Mtandao (Online Document)

cha Ndege cha Mafia kimekabiliwa na mafuriko na kusababisha korongo linalokwenda kwenye runway.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ndege ya ATCL, inasikitisha nchi kubwa kama Tanzania Shirika lake la ndege linasuasua. Sasa imefika wakati wa Serikali kuboresha Shirika hili na kuliwekea mazingira mazuri ya kibashara yatakayoweza kuvutia mashirika makubwa kuingia ubia, duniani kote biashara hii ndege nyingi hukodishwa. Pengine sasa Serikali iweke wazi kamabado ina nia nzuri na Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ICD – Bandari kavu. Hizi ICD zilianzishwa kwa nia nzuri kabisa ya kupunguza msongamano wa mizigo Bandarini sasa pia zimekuwa ndio chanzo pia cha msongamano wa magari Jijini kwa sababu zimejengwa bila kuwa na eneo kwa ajili ya magari yanayoingia kutoa mizigo hivyo kusababisha msongamano mkubwa sana. Je, mamlaka inayohusika kutoa vibali vya kufunguliwa hizo ICD kwa nini haiangalii kwanza mazingira ya hizo ICD kabla ya kutoa vibali hivyo ili zisisababishe madhara kama hayo? Ili kupunguza msongamano huo, kwa nini ICD hizo zisijengwe nje ya Mji kama Kisarawe, Kibaha nakadhalika? Ni vizuri Mamlaka inayotoa vibali vya ujenzi wa ICD ingezingatia na uwepo wa eneo la kupaki magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iangalie gharama zinazotozwa watumiaji wa ICD hizi wakati mwingine zinakuwa juu sana hivyo kuongeza gharama kwa uagizaji mizigo na mwisho gharama hizo zinahamia kwa walaji. Kwanini mamlaka husika isiweke standars ratekwa gharama zote zinazotakiwa kutozwa mizigo ili kuondoa unyonywaji unaofanywa na ICD zinazomilikiwa na watu binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya kat, niendelee kuipongeza Serikali kwa juhudu ambayo inaendelea kuonyesha katika miradi mbalimbali ya ukarabati na ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni. Naomba niunge mkono ushauri uliotolewa na Kamati, ni kweli ili kuleta ufanisi wa miradi hii ni vema sasa Serikali ikaangalia uwezekano wa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi mikubwa ya ujenzi wa mtandao wa reli na hata kama kuna wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika uendeshaji wa kununua vichwa na mabehewa wapewe nafaili ili mradi tuwe na mikataba mizuri yenyen maslahi na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAZARA, kumekuwepo na changamoto nyingi sana ambazo zimesababisha mgomo wa wafanyakazi na kuleta athari kubwa sana katika jamii na hasa abiria. Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha migogoro hiyo hajitokezi tena na kuleta marekebisho ya Sheria iliyanzisha TAZARA, Sheria Na. 4 ya mwaka 1975 ili ifanyiwe marekebisho. Pia napenda kujua mashirika yanayodaiwa na TAZARA yanadaiwa kiasi gani na

Nakala ya Mtando (Online Document)

mkakati gani unafanywa ili kuhakikisha madeni hayo yanalipika ili kusaidia kuondoa changamoto hizi. Je, ni kiasi gani cha pesa TAZARA inadai?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumtia moyo Mheshimiwa Waziri katika utendaji wa kazi zake. Pili, nimpongeze kwa kuendelea kwake kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuendelea kuimarisha bandari zetu, reli yetu na viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote mazuri ambayo Wizara imekuwa inafanya, ni nafasi yangu kuhakikisha kuwa maendeleo ya pamoja yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia hoja ya Waziri wa Kazi nilibainisha mbele ya Bunge lako Tukufu juu ya fursa ya uwekezaji iliyojitokeza ndani ya Jimbo la Chalinze. Jimbo la Chalinze kwajigrafia yake, ndiyo kiunganishi cha barabara zinazotoka Kaskazini mwa nchi yetu na upande wa Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati na Ziwa. Kwa kifupi, ndicho kituo kinachounganisha eneo kubwa la nchi yetu na Mkoa maarufu na kibiashara wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri muangalie hili kama chachu za kupunguza msongamano wa watu wanaokuja Dar es Salaam kwa madhumuni ya kibiashara kwa kuanzisha bandari kavu, kwa upande mmoja au kuanzisha eneo huru la kibiashara. Kwa maamuzi haya mtakuwa mmeokoa barabara zetu ambazo zimezidiwa na pili kukuza uchumi wa nchi. Pamoja na hoja hiyo lakini pili itasaidia kukuza nchi badala ya kupeleka kila mtu Mkoani Dar es Salaam ambao hata kwa macho unaona Mji umezidiwa na mahitaji muhimu ya kibiashara ikiwemo hewa safi isiyo na ukaa haipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda usiopungua miaka mitatu, wafanyakazi wa Wizara wakishirikiana na wataalam waliiingia katika viji vya Wilaya ya Bagamoyo hasa Yombo, Mateya na kuingia katika makubaliano ya uchukuaaji wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa uwanja mpya wa ndege wa kisasa. Tokea kipindi hicho, hakuna malipo na wananchi wale hawajielewi hasa inapokuja katika shughuli zao za kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa Bandari Bagamoyo. Ujenzi huu umekuwa katika sio tu hali ya kusuasua, lakini pia sintofahamu. Wananchi wa kijiji cha Pande, Zinga walipata ugeni wa wataalam toka Wizarani lakini mpaka sasa hawajielewi na kwamba fidia zao hadi leo hazieleweki. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba huu ni uonevu kwa wananchi wa Bagamoyo? Namuomba

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Waziri atupe maelezo juu ya mipango hii mitatu ya maendeleo ili wananchi wa Wilaya ya Bagamoyo waendelee kujenga imani na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mgogoro wa wafanyakazi wa TAZARA; mgogoro huu wa wafanyakazi wa TAZARA ni mgogoro wa siku nyingi unakwisha halafu unajirudia. Mgogoro huu unasababisha pato la Taifa kushuka, wenzetu upande wa Zambia wananaufaika kwa sababu shughuli zao zinaendelea kama kawaida, kwani wafanyakazi wa TAZARA wanapogoma wenzetu upande wa Zambia huwa wanafanya kazi.

Vile vile wanaingizia Serikali yao mapato lakini huku kwetu wafanyakazi wanagoma na kusababishla hasara Serikali ikiwemo madeni makubwa ya wafanyakazi. Ni lini Serikali italeta muswada Bungeni wa Mabadiliko ya Sheria ya Wafanyakazi wa TAZARA? Ni lini Serikali itawafukuza kazi baadhi ya wafanyakazi ambao wamekuwa ni kikwazo (wanawashauri wenzao wafanye mgomo) kwa wenzao na kuajiri wafanyakazi wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la usafiri wa treni na mabehewa, hata hivyo pamoja na bajeti hii kuongezeka kila mwaka bado kiwango kinachotengwa ni kidogo na hakipatikani kwa wakati muafaka. Hivyo, tunashindwa kukidhi mahitaji kwa nini Serikali isitoe nafasi kwa sekta binafsi kuwekeza, katika usafiri wa reli kama nchi za wenzetu kwa sababu hapa Tanzania kuna wazawa wana uwezo wa kuwekeza kwa mfano, Bakhresa ni mdau mkubwa wa reli, kwa nini hapewi kipaumbele cha kuwekeza katika reli. Kwa sababu yeye ni mzawa, vile vile ana uwezo mkubwa katika kuwekeza kama alivyowekeza usafiri wa majini Dar es Salaam, Zanzibar na Pemba. Naiomba Serikali iache kumpa vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchakavu wa reli na karakana zake, karakana zote za Tanzania majengo yake ni chakavu, kwa mfano karakana ya Morogoro majengo yake ni chakavu, majengo yanavuja ya siku nyingi, vile vile mazingira yake ni machafu. Ni lini Serikali itahakikisha inaboresha karakana zake na vituo vyatia abiria?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Bandari Bubu, Bandari bubi zimekuwa zikitumika vibaya kwa kubeba bidhaa za magendo, kusafirisha wahamiaji haramu, kusafirisha madawa ya kulevyia na kadhalika Tanzania kwa sasa hivi hatuko salama kwani wahamiaji haramu ni wengi wanaingia nchini kwa kupitia Bandari Bubu. Naiomba Serikali hili tatizo la Bandari Bubu liangaliwe kwa macho mawili. Tusipodhibiti Bandari Bubu tunaweza kuvamiwa na Al-

Nakala ya Mtando (Online Document)

shabab kama Kenya. Vile vile Al-shabab bado wapo Kenya na Kenya ni majirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kero za Bandari; kuna kero za Bandari kwa upande wa Zanzibar, suala la bandari ni la Muungano na kumekuwa kuna malalamiko kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara. Kuna malalamiko kuwa wanapofanya vikao viongozi wa Tanzania Bara na Zanzibar taarifa zinakuwa hazifiki kwa wananchi. Vile vile misaada inapotolewa inakuwa haifiki kwa walengwa, ikiwa kuna msaada wowote ule unaotolewa na wafadhili au Wahisani, unaohusu Bandari zetu Tanzania Bara na Zanzibar inabidi misaada inayoletwa Zanzibar ifahamike na habari zake ziwafikie wananchi kama ilivyo bara ili kuepuka malalamiko kwa wananchi wa Zanzibar na kusema Tanzania Bara imevaa koti la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usumbufu wa mizigo itokayo Zanzibar suala hili tumelisema kwa muda mrefu sana, lakini hakuna mabadiliko, tatizo hili linakuwa linajirudia bila ya kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Je, meli zinazosajiliwa Dubai taarifa zake zinafikaje SUMATRA?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwanza nawapa pongezi kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini bado kuna malalamiko kutoka kwa wananchi, kutokana na kucheleweshewa fidia kwa maeneo yao, yalipochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya Ndege. Ni lini Serikali itahakikisha imewalipa fidia zao bila ya kuwazungusha na kuwapa usumbufu usio na sababu?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa kuwashirikisha wajumbe wa Kamati ya Miundombinu katika sekta zote za Wizara ya Uchukuzi.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara hasa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa inayofanywa. Baada ya kuweka ulinzi mzuri wa kubaini madini kama yanatoroshwa katika viwanja vya Ndege, sasa wajanja wameanza kutumia njia ya barabara kupitia hasa mpaka wa Horohoro kuvusha madini. Naiomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara iangalie maeneo ya vivuko vya reli kutokana na ongezeko la Watanzania, kuna maeneo mengi ya reli yanahitaji vivuko tena gharama ya kulipia kuwekewa kivuko ni 4,000,000/=. Kiasi hicho ni kikubwa kwa wananchi wetu kupata Kivuko, lakini tatizo hilo limesababisha maaskari wa TRL wameigeuza kuwa mradi kwani kazi yao ni kuvizia maeneo ya vivuko na kila mabasi au gari ikipita basi hao maaskari

Nakala ya Mtando (Online Document)

wanadai rushwa ili kuruhusu magari au mabasi kupita, ni kero kubwa sana katika Jimbo langu la Uchaguzi la Tabora Kaskazini Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwekewe Vivuko vya magari kwenye njia ya reli katika Kata zifuatazo:-

- (i) Kata ya Ikongolo.
- (ii) Kata ya Ilolangulu.
- (iii) Kata ya Mabama.
- (iv) Kata ya Ibiri.

Inasikitisha sana kuona wananchi wanashindwa kutumia barabara zao kwa sababu vivuko vya reli havipo, naomba sana niwekewe vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na wataalam mbalimbali wanaofanya kazi katika Wizara hii na Taasisi zake kwa Hotuba nzuri na maelezo ya kina yanayojieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mojawapo ya Wizara muhimu sana kwa kukuza uchumi na kuleta Ustawi wa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za Wharfage katika Bandari ya Dar es Salaam ni za juu mno kwamba wafanyabiashara wengi wamekimbia Bandari ya Mombasa Kenya. Naiomba Serikali iliambie Bunge lako Tukufu ni lini Serikali itapunguza gharama hizi ili wafanyabiashara watumie Bandari yetu ya Dar es Salaam na hivyo ilete tija na ipate kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Gati Namba 13 na 14, naomba Serikali haina dhamira ya kweli kujenga Gati hizi. Kenya wamepata mkopo kutoka Serikali ya China kwa nini sisi kila siku tunakuja na hadithi za alinacha. Naomba Serikali itoe kauli hapa ni lini hasa (*Time limit*) Serikali ituambie ni matatizo gani hasa yanayokwamisha gati hizi Namba 13 na 14 zisijengwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, reli zetu hapa nchini ziko katika hali mbaya sana, kutokujengwa kwa reli hizi uchumi wetu utaendelea kushuka mwaka hadi mwaka kwani hela nyingi zinatumika katika ujenzi wa barabara ambazo nazo ubora wake umeharibiwa na malori makubwa yenyewe uzito uliokithiri.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iwekeze katika ujenzi wa reli hizi kutokana na umuhimu wake katika uchumi wa nchi yetu. Ukipitia kitabu *The Central Corridor* maelezo yake yanaonesha fursa za kiuchumi zilizopo kwa kutekeleza mraidi huu kwa uchumi wa Tanzania. Uwepo wa Nchi za Uganda, DRC, Burundi na Rwanda kunaonesha wazi kwamba ujenzi wa reli ya katika kutaharakisha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, Serikali lazima ije na mpango wa dharura wa kujenga reli ya katika ambaao utasaidia kuhakikisha kwamba kabla ya 2025, reli hii itaweza kuwa imejengwa vinginevyo tutaendelea kupeana maneno matamu yasiyo na maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika Tanzania imeshindwa kunufaika na jiografia yake. Reli zetu zitaokoa hela nyingi kwani kilomita moja ya barabara ya lami huligharimu Taifa zaidi ya milioni sita hadi bilioni moja za Kitanzania. Hizi ni hela nyingi kwa Taifa changa kama Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inavyo Viwanja vingi vya Ndege, lakini cha ajabu Shirika la Ndege kuanzia ATCL liko hali mbaya sana. Je, ni lini Serikali itanunua ndege zake au kutafuta wawekezaji binafsi walio makini, wasio na dosari wala mawaa wapate kuwekeza ili kukuza uchumi wetu kupitia usafiri wa anga. Sekta ya Utalii haiwezi kupanuka kwa kuendelea kutumia ndege za Mataifa mengine ili kuleta watalii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iliambie Bunge lako Tukufu ni lini itaondokana na mipango babaifu isiyo na tija kwa nchi yetu, kila siku tunalaumu Matafan Wanachama EAC kwamba wanaitenga nchi yetu. Mipango yetu mibovu ndiyo kikwazo kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja hadi nipewe maelezo ya kina kuhusu mambo niliyohoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. ANNAMARY J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi maana Wizara hii ya Uchukuzi ni Wizara muhimu inayochochea kukua kwa uchumi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na usafiri wa majini hasa katika Ziwa Tanganyika, usafiri wa majini kupitia Ziwa Tanganyika umerahisisha sana adha ya usafiri kwa wananchi wanaoishi katika Mwambao wote wa Ziwa hili kutokea Kigoma kwenda Sumbawanga kupitia Kasanga pia nchi jirani ya Zambia kupitia Mpulungu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado matatizo ni mengi kwa wasafiri kutokamilika kwa baadhi ya Gati, baadhi ya maeneo kama Karema, naomba Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi atueleze ni lini Gati la kivuko cha Karema litaanza kutumika lini ili kuwaondolea wakazi wa Karema adha ya usafiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Viwanja vya Ndege, sina budi kuipongeza Serikali kwa kuona adha ya Mkoa wa Katavi kwa kutujengea uwanja wa ndege. Ninachoiomba Serikali kuboresha ratiba ya usafiri wa ndege ili wafanyabiashara waweze kusafiri kwa haraka na uhakika pia tupate ndege ya abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri Mikoani na Vijiji naiomba SUMATRA iuangalie Mkoa wa Katavi ambao kwa usafiri wa mabasi hasa kutoka Sumbawanga – Mpanda, usafiri ni mgumu sana kwa Sumbawanga - Mpanda sababu hakuna ushindani wa biashara za mabasi zaidi ya basi moja tu la Kampuni ya Sumry. Wananchi wanahangaika sana usafiri, wanajazwa sana kwenye basi na wanakubali hali hiyo kwa sababu hakuna basi lingine. Naomba SUMATRA iangalie suala hili na kutangaza tenda hiyo ya kupata basi kampuni nyingine kama ilivyo kwenye barabara ya Mpanda inayoingia Tabora, mabasi ni mengi na usafiri ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa reli, Serikali ihakikishe inaboresha usafiri huu wa reli Mpanda - Kaliua hasa kwa kuleta injini mpya za treni kwani injini zilizopo zimechoka na zinifikia kuzima njiani na kusababisha usumbufu kwa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba ukarabati wa station ya Mpanda mjini imechakaa sana. Naomba hilo Serikali iliangularie sana Katavi ni Mkoa sasa, tunaomba station hiyo iwe yenye hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. PHILIP G. MTURANO: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni moja ya nguzo muhimu sana ya kuongeza pato kubwa la uchumi wa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na unyeti wa Wizara hii, lakini bado kumekuwepo malalamiko mengi ambayo yanakwamisha juhudu kubwa za kuleta ufanisi ambao ungesaidia sana kuinua pato la Taifa, kinachopatikana ni kidogo sana ukilinganisha na majukumu na uwezo wa Wizara hii kama ingesimamia vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, migomo inayoendelea hivi sasa kuhusu wafanyakazi wa reli ya TAZARA inaitia aibu Taifa na inarudisha nyuma maendeleo ya nchi. Hivi inakuwaje wafanyakazi wanakaa miezi mitatu bila

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kupata mishahara? Tunaitaka Serikali ieleze undani wa tatizo la wafanyakazi wa TAZARA.

Mheshimiwa Naibu Spika, madereva wa treni nao wanalamika stahiki zao, kitu ambacho kimechukua muda mrefu, tunataka kujua kuna tatizo gani hapa? Si hilo tu hata Askari Polisi wanaolinda mizigo, raia na mali za Shirika la Reli bado wanalamikia hayo hayo ya stahiki zao, kuna nini katika Shirika hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kelele nyingi ambazo zimesikika katika Bunge lako Tukufu kuhusu Meli ya MV Liemba, lakini Serikali imeendelea kuziba masikio na hivyo kuwafanya watumiaji wa meli hiyo kuishi maisha ya mashaka pindi wanapoitumia meli hiyo kwa kuwa imechakaa sanam tunataka kujua ni lini Serikali itaikarabati meli hiyo ama kununua nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, malori ya mizigo mbali ya kutoa msaada mkubwa yamekuwa yakiharibu barabara zetu kutokana na uzito wa mizigo iliyobeba tunataka kujua ni kwa nini hali hii ya kuzidisha mizigo imezidi kuendelea ilhali barabara zetu zikizidi kuharibika? Ni nani wa kuwajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ikarabati uwanja wa Ndege wa Lindi kwani ni uwanja mkongwe na unabeba watu wa Masasi, Tunduru, Ruangwa, Liwale, Nachingwea. Hawa wote walikuwa wanapanda Ndege Lindi kuelekea Dar es Salaam. Sasa hivi mpaka waende Mtwara, ni mbali sana kwenda Mtwara, tunaiomba Serikali ikarabati uwanja wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari ya Lindi na Kilwa Bandari hizi ndizo zinazobeba uzito mkubwa wa mazao ya Kusini, mazao kama mbao, ufuta, korosho, chumvi, asali, nta, na kadhalika. Mpaka sasa Bandari ya Lindi imefukiwa na mchanga tu na Bandari ya Kilwa ni majanga tu. Mji Mkongwe Kilwa wa Historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusaidiwe Mikoa ya pembezoni hasa Lindi Mkao mzima. Ahsante.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia suala la Bandari ya Karema, Bandari hii ina mwaka wa nne (4) tangu ianzé kutengenezwa bila kuwa na mafanikio yoyote yale, Wizara ilifanya makosa makubwa sana kwa kumpa tender Mkandarasi asiyekuwa na uwezo wowote ule wa kujenga Bandari hiyo. Mradi umekwama, mbaya zaidi Mkandarasi huyo huyo amepewa tender za Bandari nne (4) kwenye Ziwa Tanganyika.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, najiuliza ni vigezo vipi vilivyotumika kumpa Mkandarasi huyu Bandari zote nne wakati hana uwezo. Ni kwa nini mpaka sasa Mkandarasi huyu hajachukuliwa hatua yoyote ile na Wizara, kwani alishatumia sana fedha za Serikali wakati kazi ya namna yoyote ile haijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu reli, reli ya kati ni kiungo muhimu sana kwa ujenzi wa Taifa letu kwani bila kuunganisha nguvu ya pamoja hatuwezi kukuza uchumi wa nchi yetu. Niiombe Wizara ichukue hatua thabiti na za dharura kuhakikisha tumeimarisha reli ya kati itakayowasaidia sana wanchi wa hali ya chini ambaeo ndio watumiao sana usafiri wa reli. Treni ya Mpanda – Kaliua - Tabora iongezewe mabehewa na kupewa kichwa cha treni kipyia ili iweze kufanya kazi vizuri kwani mpaka sasa treni hii imechakaa sana, behewa zimeharibika na kichwa cha treni ambacho kimechakaa sana. Ni vyema Wizara hii ikashughulikia kuimarisha treni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Meli ya MV Liemba, meli hii imechakaa na ya muda mrefu na leo hii mmetangaza kuisimamisha kazi mbadala wa meli hii ni upi na lini itanza kujenga meli mpya ya Ziwa Tanganyika? Nitahitaji kupata majibu ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa barabara (SUMATRA), Mpanda wasafiri wanapata taabu sana kwa kupandishiwa kwa gherama kubwa sana, SUMATRA inafanya nini? Sijaona wakaingilia kupanga viwango vya nauli wananchi wanaumia sana kwa kulipa nauli kubwa sana. Nikuombe Waziri uiagize SUMATRA waangalie nauli za kutoka Mpanda-Kigoma, Mpanda – Sumbawanga, Mpanda – Tabora na usafiri wa ndani ya Mkoa na Wilaya, nauli zao ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahitaji kupata maelezo ya kina juu ya ujenzi wa Bandari ya Karema, ni kero kubwa na nakusudia kushika shilingi.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwi mbele yetu. Baada ya kuunga mkono hoja, naomba kuchangia baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa uwanja mpya eneo la Kisumba na ujenzi wa uwanja wa Sumbawanga, ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Kimataifa eneo la Kisumba, Sumbawanga ni jambo la muhimu kwa ajili ya kuunganisha wasafiri wa Mkoa wa Rukwa na baadhi ya wasafiri wa kutoka nchi za Zambia na DRC na hasa ukizingatia hali ya jiografia ya Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kauli zinazosikika mitaani kwamba eneo hili la Kisumba halifai kutokana na maoni ya wataalam,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

nimefarijika katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuendelea kutaja ujenzi wa uwanja huu wa Kisumba kwa siku zijazo. Naomba kuhakikishiwa jambo hili linakuwepo na kunakuwa na *commitment* ya Serikali *seriously* maana nimeshawahi kumsikia Naibu Waziri mwenye dhamana akiongea juu ya kutokufaa kwa eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukiendelea kusubiri ujenzi wa kiwanja kipyä eneo la Kisumba ni vizuri hasa ikaongezwa ujenzi wa kiwanja cha Sumbawanga kikajengwa kwa kuwekewa lami ili kiweze kuruhusu ndege kubwa ziweze kutua katika uwanja huu na kusaidia wasafiri kulipa nauli ya ndege nafuu kwa usafiri wa Sumbawanga Dar es Salaam kutoka nauli kubwa inayotozwa sasa ya shilingi laki sita (600,000/=) wakati nauli ya kutoka Mbeya hadi Dar es Salaam ni shilingi laki moja na nusu tu wakati umbali kati ya Mbeya hadi Sumbawanga nauli yake kwa basi ni shilingi elfu kumi na tano na ni kilomita 330 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kwa Wizara kutambua kuwa *location* ya Mkao wa Rukwa kuwa *strategically* kwa nchi ya Congo DRC na nchi ya Zambia kwa mujibu wa taarifa ya *The Central Corridor. A wider concept note figure 1-1 central corridor transit import, Export Destinations source: BRN Transport lab 2013.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kielelezo nilichokitaja ambacho naamini utaikumbusha Serikali juu ya wazo la kutumia fursa ya uwepo wa reli ya TAZARA kwa kuanza ujenzi wake kutoka Tunduma mpaka eneo la Kasanga port na kwa baadaye kuunganisha Mikoa ya Katavi hadi Kigoma ili kuwe na mtandao wenye fursa kwa uchumi wa nchi yetu kwa kuunganisha mikoa mingi.

MHE. DKT. PUDENCIA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu SUMATRA, baadhi ya wafanyabiashara za usafiri hasa mabasi ya abiria wamekuwa kwa kushirikiana na watumishi wasio waaminifu wa SUMATRA kuhodhi njia/barabara za usafiri, kwa mfano, katika Mkao wa Rukwa, mfanyabiashara aitwaye Sumry amekuwa na mpaka sasa anahodhi barabara ya Sumbawanga mpaka Mpanda kwa kuwazuia wafanyabiashara wengine wasipitishe magari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itupatie majibu kwa wananchi ili wajue kuna tatizo gani na kwa nini hali hii inajitokeza? Kwa nini wanawatesa wananchi bila sababu ya msingi? Tunaomba suala hili lishughulikiwe haraka iwezekanavyo.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri mnayofanya. Nawatachia kazi njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, reli ya kati ifanye kazi, ndiyo ukombozi wa wananchi wa Tabora na Mikoa mingine inayoitegemea kwa usafiri na kusafirisha mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatachia kila la heri.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakyembe na Tizeba nyinyi ni majembe chapeni kazi tuko nyuma yenu. Fedha za mradi wa ujenzi wa uwanja wa Ndege Mwanza hazitoshi kwani hata mwaka jana mlitenga fedha shilingi bilioni nane, lakini mkawapa bilioni 1.5 tu. Aidha, Mkandarasi anadai shilingi bilioni 15 na Mhandisi Mshauri anadai shilingi bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii inaonesha kazi ya ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Nyasurura (Mara) ni ndogo sana na maelezo yale yale kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), limekuwa la mgogoro wa muda mrefu usiokwisha. Mimi nikiwa mjumbe wa POAC ya wakati ule niliweza kupata nyaraka mbalimbali ikiwemo mikataba yenye ushahidi kwamba *Simon Group* kwa sasa anamiliki hisa zipatazo 11,511,349 kati ya hisa 15,000,000 sawa na 76.79% wakati Serikali ina hisa 3,488,651 kati ya hisa 15,000,000 sawa na 23.26%. Ninazo nyaraka zote na kwa msingi huo Mheshimiwa Malima alipotosha Bunge kuwa *Simon Group* siyo mmiliki halali wa UDA. Naomba Serikali itoe kauli ya kweli na siyo yenye mwelekeo wa kudhulumu uwekezaji wa *Simon Group*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nawatachia afya njema.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupunguza siku za kutoa mizigo bandarini pamoja na kuongeza mapato yatokanayo na bandari ni hatua nzuri kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili, naishauri Wizara ishirikiane na TRA kudhibiti tabia ya Maafisa kumbambikiza malipo ambayo siyo halali na kupelekea vitendo vya rushwa. Ushauri huu ni vitendo vya rushwa. Ushauri huu ni pamoja na kwenye viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ATC, kuna tabia ya kukatia tiketi watu wengi na kuzidi uwezo wa ndege na kupelekea baadhi ya abiria kuachwa Airpot kutokana na ndege kujaa jambo ambalo litasababisha Shirika kuanguka kutokana na kutokuaminika. Naomba sana suala hili liangaliwe kwa karibu zaidi au umakini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tetesi kwamba bandari ya Mtwara imebin afsishwa kisirisiri. Naomba jambo hili litolewe ufanuzi ili wananchi wapate uelewa wa hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na timu yake kwa kazi nzuri sana waliyoifanya kwa kufufua Sekta hii ya Uchukuzi ili iweze kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanywa ya kuhakikisha kufufua huduma ya usafiri wa reli, Dar – Mwanza, Dar – Kigoma na kadhalika. Baada ya pongezi, naomba kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Serikali itafute fedha hata kama ni za mkopo kwa ajili ya kuongeza vichwa vya treni ili kuongeza uwezo wa kusafirisha abiria ndani na nje ya nchi, hivyo kuongeza uchumi wa Taifa na kupunguza tatizo la uharibifu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuja mchakato wa makubaliano ya ushirikiano wa usafiri wa ndege za China kuja Tanzania umefikia wapi? Ni lini ndege kutoka China zitaaanza safari zake kuja Tanzania? Kwani sasa ni muda mrefu toka nimesikia mipango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuja mipango ya kujenga uwanja mpya wa ndege katika Kata ya Nyakatende Kijiji cha Nyansurura eneo

Nakala ya Mtando (Online Document)

lililotengwa zaidi ya miaka ya 20 iliyopita imefikia wapi? Je, uwanja huu utajengwa au mpango umefutwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege Musoma umechakaa kabisa, na hapa sikuona mpango wowote wa kukarabati uwanja huu ili wananchi wa Musoma na wageni wakiwemo watalii waondokane na adha ya kupitia Mwanza ndiyo waje Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege Serengeti (*International Airport*) unajengwa kwa ubia (*PPP*) Garment Reserve Company Halmashauri na uchukuzi (*RTCAA*).

- Shukrani.
- Shilingi bilioni tano zimeshatolewa na mwekezaji Garment.
- Mazingira – utafiti chini ya *UDSM – NEMC* – kwanini kibali hakitoki?
 - (i) Kurahisisha usafiri;
 - (ii) Kuongezeka kwa usafiri na uchumi;
 - (iii) Kuondoa kuchoka kwa safari ndefu; na
 - (iv) *Western Corridor* ina wanyama wengi kuliko sehemu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua bandari ya Musoma inajengwa wapi na ni lini ujenzi utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli Tanga – Shimiyu – Musoma umefikia wapi na umetengewa kiasi gani fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wakununua meli mpya kwenda Bukoba – Mwanza na kuikarabati meli ya MV. Victoria na MV. Liemba ambayo kwa sasa zimechoka kutokana na kutumika kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu usafiri wa anga Mwanza. Ujenzi ulianza kwa mkataba mwaka 2012/2013 kwa Shilingi bilioni 105. Mwaka 2012/2013 Serikali ilitoa Shilingi bilioni nane tu. Mwaka 2013/2014 Serikali ilitoa Shilingi bilioni 1.6; Mwaka 2014/2015 Serikali imetenga Shilingi bilioni 12 tu na huenda zisitoke na hata hivyo hazitoshi Shilingi bilioni 105.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa hali hii Mwanza tunafanya je? Tutoleeni mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya kati ikiimarika ni mkombozi mkubwa wa barabara za nchi hii zilizotengenezwa kwa lami. Jitihada ziwekwe ili kuziimarisha zikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri na usafirishaji katika reli hii ya kati utainua uchumi katika nchi hii. Nasema ilivyo kwa sababu mizigo mizito na mikubwa yenye tija itabebwa kwa kutumia njia hii kwa goods train. Ongezeni juhudni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inafanya kazi vizuri sana, lakini ina miradi mingi sana. Kila mwaka pesa za miradi zinatoka chache na kwa hiyo, miradi imekuwa haimaliziki mwaka hadi mwaka. Hivyo, napendekeza kuwa Wizara ije na vipaumbele vichache ili pesa wanazopata ziweze kumaliza miradi hiyo michache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu ndege ya ATCL ipepee bendera ya nchi yetu. Ndege hii itaweza kuleta utalii kutoka nje ya nchi. Vile vile watalii watakaoingia nchini watakuwa na uhakika wa kupata usafiri ndani ya nchi, kwani usafiri wa kwenda sehemu nyingi zenye vivutio vya utalii siyo wa uhakika na hili linasaidia kupunguza ujaji wa watalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ichukue hatua kutatua utata uliokuwepo kuhusiana na UDA. Ni aibu kwa nchi yetu.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kazi za Wizara hii kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi wa Taasisi zake zote kwa kazi nzuri. Wanajitahidi ingawa fedha za bajeti hazitoshi kila mwaka. Baada ya pongezi hizi, nashauri yafutayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ikishirkiana na Wizara husika, ihakikishe kuwa vyombo vya aina zote za usafiri vinakuwa rafiki kwa watu wenyewe ulemavu. Kwa mfano, ngazi za kupanda na kushuka wakati wa kupanda kwenye magari, treni, meli na kadhalika. Hata hivyo, nashukuru kwa maendeleo ya jinsi ya kuhudumia abiria wenyewe ulemavu yaliyoko Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu J. Nyerere kwa vile kuna gari maalum lenye ngazi za kupanda na kushuka ili kuwawezesha wasafiri wenyewe ulemavu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni muhimu na ninaamini kwamba Waheshimiwa Viongozi wanayaona haya wanaposafiri nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda sana kumshukuru Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Naibu wake kwa kuiongoza vizuri sana Wizara hii. Nami nawaombea mafanikio tele kwani uchukuzi ni shughuli muhimu na kweli ni kiungo muhimu katika kufanya uchumi wetu ukue kwa kasi tunayoitaka ya kuanzia asilimia 10.

Nimefurahi pia kuona mipango ya ujenzi wa reli katika Jiji la Dar es Salaam. Ombi langu, tutekeleze mambo haya kama tulivyopanga hata kama tunaweza kutumia PPP.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie katika Reli ya Mtwara – Songea – Mbambabay. Naomba Waziri akubali kwamba pawepo na tawi kuelekea kwenye mradi mkubwa wa makaa ya mawe ya Ngaka pale Ruanda na Ntunduwaro. Kwa sasa jamaa wanatumia barabara ambayo hata lami haina. Kwa hiyo, madhara ya afya kwa wananchi ni wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza Tawi lingine lifike mpaka Lituhi au Ndumbi ili iwe rahisi pia kusafirisha makaa ya mawe kwa maji kwenda Mbeya ili kulisha viwanda vya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba commitment ya Serikali juu ya tawi hili tena ya maandishi. Tukumbuke pia maeneo haya ndiyo yenye chakula kingi sana (mahindi) kwa ajili ya kulisha nchi, kama reli itapita pale Lituhi, basi ni rahisi kuweka tawi la kuelekea Ruanda – Ntunduwaro na baadaye Ndembu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maajabu sana sehemu hizi ambazo zina mizigo mingi pamoja na chakula ndiyo ambazo hazina miundombinu imara ya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia baraka tele za Mwenyezi Mungu ili watekeleze hayo yote yaliyo katika bajeti na yale yote ambayo Mungu anataka yafanyike.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uchukuzi inashughulikia sekta muhimu kwa uchumi wa nchi na maisha ya wananchi. Ili

Nakala ya Mtando (Online Document)

Wizara hii itimize wajibu wake kwa ukamilifu, kufanikisha azma hiyo, naomba katika majumuisho Waziri wa Uchukuzi na Taasisi zilizo chini ya Wizara kunipa majibu kuhusu masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari (*TPA*) na Bandari ya Dar es Salaam bado kuna udhaifu ambaao unahitaji hatua za haraka kuchukuliwa na usimamizi wa Kibunge kuongezeka. Ili kuweza kuwianisha maelezo ya maboresho yanayoendelea na mahitaji, niliomba kwa nyakati mbalimbali kupewa nakala ya ripoti ya Kamati ya Uchunguzi ambayo Waziri aliunda *TPA*. Hata hivyo, mpaka sasa sijapewa nakala ya ripoti hiyo. Ni lini Waziri atakuwa tayari kuwasilisha Bungeni taarifa hiyo ili kupata undani wa yaliyobainika na kufuatilia utekelezaji?

Eneo la shughuli za kibandari la muda na kituo cha kupoolea mizigo lililopendekezwa la ekari 132 la *Jitegemee Trading Co. Ltd* lilihofiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani miaka ya nyuma. Je, ni mkakati gani umetumika kupata eneo hilo na ni nani mmiliki wa kampuni hiyo? Je, Wizara ya Uchukuzi ilibaini nini ilipofuatilia juu ya eneo hilo kuwa kwenye ukanda wenye mafuriko (maeneo hatarishi).

Aidha, ni kwanini Wizara ya Uchukuzi na Mamlaka ya Bandari (*TPA*) inaendelea kutenga maeneo katika maeneo ya Dar es Salaam karibu na barabara kuu Mjini badala ya kutenga katika maeneo ya bandari Mkoani Pwani kama Kibaha, Mlandizi na kadhalika ili kupunguza foleni/msongamano wa malori na magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kutegemea Sekta ya Usafiri na Uchukuzi kwa njia ya barabara kwa zaidi ya asilimia 90 ni hatari kwa uchumi wa nchi na maisha ya wananchi. Hivyo Wizara ya Uchukuzi ieleze imepanga Taifa lipunguze utegemezi huu kwa kiwango gani na lini kwa kuboresha njia nyingine za uchukuzi? Hivyo, nguvu zaidi zielekezwe katika usafiri wa reli na majini katika usafirishaji wa mizigo katika kipindi hiki cha mpito ili kupunguza msongamano wa malori katika barabara ya Morogoro.

Wizara ya Uchukuzi na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini na nchi kavu SUMATRA zisimamie kwa karibu mpango wa kuainisha njia za magari makubwa kupita pamoja na muda wa malori kuingia na kutoka Jijini Dar es Salaam kwa kuwa ratiba haizingatiwi. Aidha, Wizara na SUMATRA washirikiane na mamlaka nyingine kuhamasisha magari makubwa kupita njia mbadala ya Msata ili kupunguza msongamano katika barabara ya Morogoro.

Kwa upande mwingine kabla ya majumuisho naomba kupewa nakala ya ripoti ya mwaka 2013, Kamati iliyoundwa kuhusu mipango na mikakati ya kuboresha usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kuitia Wizara hii kwa kuchukua hatua madhubuti ya kuweka mkakati wa kutatua tatizo sugu la kujaa mchanga kwenye makaravati yaliyopo kati ya Stesheni za Gulwe na Godegode kila mara mvua zinaponyesha. Serikali imechukua hatua ya kujenga madaraja sehemu ya Gulwe pamoja na kufanya usanifu na ujenzi wa mabwawa mawili makubwa ya kupunguza kazi ya Maji (PUNGUZA), katika maeneo ya Kimagai na Chiseyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, rejea ahadi ya Mheshimiwa Rais, kwamba kazi kubwa au mradi mkubwa ambao ataufanya kabla ya kuacha Urais ni ujenzi wa Reli ya Kati (*Central line*) mwaka 2015. Je, Serikali kuitia Wizara hii inafanya maandalizi gani ili kutekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais kabla ya kuachia madaraka mwaka 2015?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu kwamba Wizara hii itakapoanza utekelezaji wa kazi hizi zote itashirikisha wadau wote, wakiwemo wananchi wa maeneo husika pamoja na Wabunge wa maeneo hayo kwa michango na ushauri wao, kulingana na jiografia ya maeneo husika pamoja na umiliki wa ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalamu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutekeleza majukumu yao. Wanayo mipango mizuri na wamejipanga vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kuitia Wizara hii kwa kufanya usanifu na ujenzi wa mabwawa mawili makubwa ya kupunguza kasi ya maji ya mvua wakati wa mvua za masika. Mabwawa haya ni sehemu ya Kimagai karibu na Stesheni ya Godegode na bwawa la pili litajengwa karibu na Stesheni ya Msagali eneo la Chiseyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ushauri kwa Wizara ili iweze kuangalia uwezekano wa kupunguza kasi ya maji yatokayo upande wa pili wa Stesheni ya Godegode kutoka Kilosa, kuitia Pwaga kuja hadi kwenye Reli iliyoko Stesheni ya Godegode. Ushauri ninaotaka kutoa ni kuinga maji katika eneo la vilima viwili vya Vibelewewe kwa kuweka banio la maji ambalo litasaidia kuinga maji mengi yatokayo Wilaya ya Kilosa. Banio hili la maji likisaidiana na

Nakala ya Mtando (Online Document)

bwawa kubwa la Kimagai hakika tatizo sugu la Reli ya Kati sehemu ya Godegode - Gulwe litakuwa limepata suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa tunaomba usanifu unaoendelea kufanyika na ujenzi kuendelea baadaye katika mwaka wa fedha 2014/2015 ijumuise maeneo makuu yafuatayo:-

- Bwawa kubwa la kwanza lijengwe sehemu ya Kimagai;
- Bwawa kubwa la pili lijengwe sehemu ya Gulwe (Msagali) katika eneo la Chiseyu; na
- Usanifu na ujenzi wa banio la kukinga maji ya mvua yatokayo Kilosa na kuja kubomoa reli iliyoko Stesheni ya Godegode. Banio hili lijengwe katika eneo la vilima vya Vibelewele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha kwa utekelezaji wa Wizara. Nategemea majibu hata kwa kuandika, ili wananchi wasikie na kujua hatima ya matatizo ya mafuriko haya kila mwaka.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maandishi nichangie hotuba ya Waziri wa Uchukuzi. Wizaraya Uchukuzi na ile ya Ujenzi ni muhimu kwa uchumi wa nchi kama mishipa ya damu ilivyo kwenye mwili wa binadamu. Itoshe kupongeza jitihada za Serikali kuwekeza katika sekta hii, lakini niweke wazi kuwa jitihada zaidi ya kiwango tunachowekeza kinatakiwa ili tupate tija tarajiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaotumia huduma za meli ya MV. Victoria katika Ziwa Victoria hali yao ya usalama iko hatarini. Yapo madai kuwa engine moja ya meli hiyo haina umadhubuti unaotakiwa. Zipo taarifa kuwa mamlaka husika zimekuwa zikitenga fedha lakini fedha hizo hufujwa na kazi ya ukarabati/matengenezo yaliyokusudiwa yasifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa mchango huu kwa njia ya maandishi kama kinga ya uzoefu tulionao katika Ziwa hili. Habari toka ndani ya Shirika ilieleza mapema kuwa meli ya MV. Bukoba ingeweza kuzama kutokana na upungufu uliomo, kimsingi toka kuundwa kwake. Naishauri Serikali sasa kwa umuhimu wa kipekee isimamie matengenezo ya engine zote za meli hiyo na kuhakikisha ina uwezo wa kusafiri salama ziwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na kukumbusha ahadi ya Mheshimiwa Rais J. Kikwete aliyoitoa kwa wananchi wa Muleba kupitia kwa Mheshimiwa Mwakyembe. Nakumbushia ombi la kujengewa gati dogo la kuegeshea boti na mitumbwi mwaloni Kyamkwikwi. Kyamkwikwi ni mwalo muhimu kwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

wananchi na shughuli za Visiwa 33 vya Wilaya ya Muleba katika Ziwa Victoria. Uboreshaji wa gati hili utachangamsha uchumi, kuimarisha usalama kwa kuwezesha boti za kisasa kung'oa na kujenga mahusiano mazuri kati ya wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie juu ya faida ya kiushindani kutokana na mahali nchi yetu iliopo kwa kulinganisha na majirani zetu. Kama nilivyodokeza awali, Sekta za Ujenzi na Uchukuzi ni muhimu ili kutumia fursa tajwa. Ili kupata manufaa tajwa, nashauri pamoja na upanuzi wa bandari, huduma ziboreshwé.

Narudia kushauri kwamba watoa huduma bandarini (*port community*) waitikie kauli mbiu ya Mheshimiwa Mwakyembe kwa kutoa huduma bandarini masaa 24. Serikali isaidie Taasisi ambazo kutokana na sheria au kanuni za utendaji wao wanaweza kuwa wanakwama kufanya kazi masaa 24. Pia kuna kutokuelewa na kusita juu ya mahitaji ya Watendaji zaidi, manufaa ya jumla kutokana na uboreshaji wa huduma za bandari ni makubwa zaidi kwa umbali kuliko gharama za wafanyakazi wa ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri na kupongeza jitihada zinazofanywa na Serikali katika kulinda faida ya kiushindani ya Bandari na nchi yetu. Ushauri wangu ni kuwa jitihada zinapashwa kuwa jitihada za pamoja, yaani Serikali na taasisi zote. Wizara ya Uchukuzi inapashwa kwenda pamoja na Wizara nyingine za ile inayosimamia barabara. Ikumbukwe kuwa utafutaji wa masoko kama ilivyofanyika DR Congo, tuangalie bandari shindani zinatoa nini kwa masoko tunayoyalenga. Msumbiji na hasa bandari yake ya Beira ni mshindani anayechukua soko letu. Pamoja na eneo hilo kutokuwa na faida za kiushindani ndani kwa kuwa na kina kifupi bandarini, lakini bandari yake kuathiriwa kwa kupwa kwa maji. Bado washirika wenzake (fedha na ujenzi za huko) wanatoa huduma na masharti yanayopunguza upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mipango ya muda mrefu kujenga uwanja mkubwa Mkoani Kagera kwa ajili ya ndege. Tunashukuru jitihada za uboreshaji uwanja wa Bukoba hatua iliyowezesha ndege kubwa kidogo kutua. Pamoja na hatua hiyo, bado Mkoa wetu unahitaji uwanja mkubwa utakaowezesha ndege kubwa kutua. Kkama tungekuwa na uwanja wa kutua ndege kubwa za Fast Jet na ikataja na bei, vivutio kama itoavyo kwa viwanja vingine vikubwa, ni dhahiri wananchi wanaotumia siku mbili kutoka Bukoba mpaka Dar es Salaam wangevutiwa na matumizi ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ianze na kwa kuiga nchi nyingine, basi tutumie PPP. Hali hii itafungua Mkoa huu kiuchumi kwa kuweza kusafirisha nyama, samaki na matunda kwenda masoko ya mbali.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na kwamba fedha inayotolewa ni ndogo sana, siyo tu bajeti inayotolewa, lakini hata kiwango halisi wanachopewa. Nasikitika sana kwa Wizara hii kupata asilimia 12.56 tu ya fedha za nje. Ni dhahiri kuwa hii itadumaza miradi ya maendeleo. Natoa wito na ushauri kuwa miradi muhimu ya maendeleo itegeme zaidi fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Mheshimiwa Waziri anaeleza mpango mzuri wa reli, lakini wasiwasi ni kwamba Serikali inahitajika kulipia Shilingi bilioni nane kabla ya mwezi ujao, Juni, 2014 ili mabehewa hayo yaje. Naomba nipate tamko la Serikali kuhusu ulipwaji wa fedha hizo kama inavyohitajika, maana kama siyo hivyo mabehewa hayo hayatapatikana kama Mheshimiwa Waziri alivyosema. Je, nini hatua ya upatikanaji wa mabahewa hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mtoto wa reli, niliyelelewa na reli ambapo baba yangu (Marehemu) alifanya kazi Shirika la Reli. Nina mapenzi makubwa sana na reli yetu na nilikuwa nasikia mipango mingi mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wawekezaji/mwekezaji ambaye alinunua/alikuwa na mabahewa ambayo alikuwa anatumia yeye mwenyewe na kukodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tulipokwenda Malaysia moja ya mafanikio yao katika Sekta hii ya Reli ni ushiriki wa Sekta Binafsi kwa mfumo wa PPP au hata kuwekeza wenyewe, Serikali inafikiriaje wafanyabiashara wakubwa wa uchukuzi kushawishiwa ili sasa waweze kushiriki katika kununua mabehewa ya mizigo, mabehewa ya mafuta na mabehewa yakubebea ng'ombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa nchi inahitaji takriban mabehewa siyo chini ya 2000 na vichwa angalau 60. Nashauri sana Wizara ichukue uamuzi huo ili maendeleo haya ya reli yaende kwa kasi inayohitajika, hasa ukililia maanani na majirani zetu wanawekeza kwa kasi na kwa biashara hiyo hiyo, lakini pia kunusuru barabara zetu na kuleta maisha bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, TAZARA, TRL na ATCL ni mashirika muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Napongeza Wizara kwa jitihada zake za kufufua, lakini mpaka sasa naona wanapewa samaki, badala ya mshipi waende kuvua. Fedha Serikali wanazotoa ni ndogo sana. Serikali tunajua ina mipango mingi lakini ili mashirika hayo yajiendeshe kwa faida yanahitaji mtaji mkubwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikalini kwa nini isiwape taasisi hizi TAZARA na ATCL fedha za kutosha kuleta mageuzi hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anayekaimu siku zote ni mwoga. Viongozi wengi wa Shirika la Bandari wanakaimu na kama Viongozi hawa waliokaa kwa miaka kadhaa wanaweza, basi wathibitishwe ili waweze kufanya kazi bila uwoga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana TPA kwa kuzindua Ofisi yao DRC Lubumbashi. Hii ni hatua muhimu ambayo itasaidia sana TPA kwa mizigo ya DRC. Naomba Ofisi hii iimarishwe ili iweze kuongeza mapato ya TPA na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kupongeza Shirika la Viwanja vya Ndege kwa kazi nzuri, lakini nina wasiwasi wa mradi wa Terminal III maana fedha sioni zikitolewa, labda tupate ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata maelezo ya machache niliyohoji.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Mpango wa Ushirikishwaji Sekta Binafsi katika Miradi Mikubwa ya Ujenzi wa Mtandao wa Reli (PPP), kwani nchi kama Malaysia na Brazil, asilimia tisini ya Miradi ya miundombinu inafanyika kupitia (PPP).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilijengee uwezo Shirika la Reli liweze kusimamia na kuratibu huu mpango, pia Shirika liweze kumudu ushindani na private sector. Hivyo, Shirika litoe mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalam, kuboresha Karakana za Reli hasa ya Morogoro na Tabora na kuongeza Wataalam Chuo cha Reli. Serikali isipofanya hayo, Shirika litashindwa kusimamia hatimaye litakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kupunguza msongamano na muda wa kukaa meli bandarini. Pamoja na pongezi hizi, bado juhudhi za makusudi zinatakiwa na hii itawezekana endapo tutaboresha miundombinu za reli, kwani reli ndiyo zenye uwezo wa kubeba mizigo mingi kwa wakati; hivyo, itasaidia ujenzi wa bandari kavu nje ya Mkoa wa Dar es Salaam, mfano Dodoma, Morogoro na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ieleze ina mpango upi katika uendelezaji wa Bandari ya Kilwa yenyе kina kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itamke nini inakusudia kufanya kwa Uwanja wa Ndege wa Kilwa na Lindi ambapo sasa kuna ukuaji mkubwa wa matumizi kutohana na shughuli za utafiti wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itarejesha meli moja kutoka Ushirika wa China (SINOTA) ili ihudumie Bandari za Tanga, Pemba, Malindi, Dar es Salaam, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi uliokithiri katika Uwanja wa Ndege Dar es Salaam, JKNA na ambapo mwezi Novemba, 2013 nilikuwa mionganii mwa wahanga. Ni lini Serikali itadhibiti vitendo hivi visivyovumilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jitihada ziongezwe kuboresha Reli ya Kati licha ya hatua nzuri za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya TAZARA inasuasua kwa Serikali kuendekeza wachache wahujumu huduma za kuliibia Shirika, ni wakati mwafaka Serikali kuchukua hatua.

MHE. MKIWA A. KIMWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niwape pongezi kubwa Wizara, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kujenga Taifa letu. Pili, naomba kuwaomba wafanye matengenezo makubwa katika Meli ya MV Victoria kwani kwa sasa ni hatari kubwa kwa meli hii. Hiyo siyo siri tena, hatuhitaji vilio tena vya meli mbovu. Tatu, Magati ya Ntama, Lushanga Kyamikwiki na Nyamirembe yatajengwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilichukue deni la ATCL ili iweze kujiendesha kibiashara, kwani shilingi 133 bilioni ni nyingi kwa Shirika kama ATCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni kweli usiopingika kwamba, hautokamilika kwa wakati na ni sababu ipi kubwa ya msingi ambayo inafanya uwanja huu kutoamilika kwa wakati?

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu ya Serikali ni lini wastaaifu wa TAZARA watalipwa haki zao ili waendeshe maisha yao?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka majibu ya Serikali nini hatima ya Wafanyakazi wa TAZARA waliogoma wakidai mishahara yao ya mwezi Machi na sasa mwezi ni Mei na kupelekea Watumishi hao kuwa na madeni yasiyolipika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimama kwa Reli ya TAZARA imeleta adha na maumivu makubwa kwa Wananchi wanaotegemea usafiri huo wa Wilaya kuanzia Mkoa wa Pwani, Kilombero, Wilaya na Kata za Lumumwe, Kimbwe, Kitete na Uchindile. Pia barabara za Kata za kutoka Ifakara - Mlimba hazipitiki na wanategemea treni ya TAZARA tu, hakuna barabara bali ni treni tu. Kibaya zaidi, badala ya kuwalipa wafanyakazi hao stahili zao, Waziri umesikika ukiwaita wafanyakazi wote waliogoma ni wezi bila kubaini wezi hao ili wachukuliwe hatua, huo ni udhalilishaji. Pia Serikali mmpeleka kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kuwatisha wafanyakazi hao kwamba wataondolewa na kuajili vijana wa Kidato cha VI, huo ni udhalilishaji na siyo utawala bora. Sasa napenda Waziri awajibu Wafanyakazi na Wananchi wanaotumia usafiri wa Reli ya TAZARA. Ni lini wafanyakazi hao watalipwa mishahara yao ya mwezi Machi na Mei? Je ni lini wastaifu watalipwa stahili zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Wizara ya Mwaka wa Fedha 2012/2013, Mheshimiwa Waziri alisema TAZARA itaboreshwa kwa mkataba walioingia na China 2012 Machi; je uboreshaji huo umefikia wapi? Je, uboreshaji ulikuwa wa Reli tu bila watumishi? Alikili kuwa, katika mafungu aliyopanga zipo fedha za kulipa wastaifu lakini hadi leo hakuna utekelezaji, ni vyema aueleze umma hali halisi.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuandaa Hotuba hii na kwa kazi nzuri sana wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kuutambua umuhimu wa Reli ya Kati. Mmefikia hatua nzuri katika kuifufua Reli ya Kati kwa kuikarabati, kukarabati vichwa vya treni na kuagiza vipyta. Ili Tanzania iende na wakati inabidi nguvu mpya ziwekwe kwenye kujenga Reli mpya inayoendana na teknolojia ya sasa. Inabidi tufanye hivyo ili tuvutie wafanyabiashara kutoka Congo, Burundi, Rwanda na Uganda. Ni lini Mradi huu wa ujenzi wa Reli mpya ya kisasa unategemewa kuanza na kukamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya mabadiliko ya tabianchi wote tumeshuhudia madhara mbalimbali yanayotokana na mafuriko, vimbunga,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

land slide, upepo mkali, tsunami na kadhalika. Katika hali hii Kitengo kinachowenza kusaidia Wananchi, kuwapa taarifa na tahadhali ni Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Naishukuru Serikali kwa kuendelea kuijengea uwezo Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania. Je, mnawawezeshaje kuweza kutoa tahadhali mapema kabla ya athari; kwa mfano, siku nne, tano, kabla na wanawawezeshaje Wananchi kuelewa taarifa zinazotolewa na Mamlaka hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 49 wa Hotuba, Wizara ilielezea ufinyu wa lango la kuingilia meli bandari. Ni kweli lango hilo linatia mashaka hasa pale meli kubwa zinapotaka kufunga gati na tumshukuru Mungu siku hiyo meli ya Kampuni ya MAERSK Line kuingia bandarini bila ya matatizo. Si jambo jema kubahatisha; hivyo, napenda kuuliza ni lini Wizara itaondoa tatizo hilo ambapo kila muda sehemu hiyo inachimbwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nigosie suala la ujenzi wa Gati Namba 13 na 14. Nimesoma maelezo ya Waziri kuhusu utekelezaji wa mchakato wa Gati hizo. Naomba Wizara itilie mkazo mahususi ili kuona ujenzi unakamilika kwa wakati, kwani inaonekana maelezo yameshakuwa mengi bila ya utekelezaji. Hivyo, kwa maelezo hayo naamini katika bajeti ijayo suala hili litakuwa limeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka hapo awali kulikuwa na wazo zuri la kujenga jengo la car parking eneo la bandari kwa ajili ya kuhifadhiya magari yanayoingia nchini. Hadi leo sijasikia tena suala hilo limefikia wapi. Sasa nataka nijue kama Mradi huo umekufa kabisa na kwa sababu gani? Na je, kuna mbadala wa sehemu ya kuhifadhiya magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inaongozwa na Madaktari wawili mahiri na nawapa hongera, lakini kuna suala la kuharibika mara kwa mara kwa njia ya Reli, eneo la Godegode. Sasa nataka kujua juu ya umahiri wa Viongozi hao suluhisho la eneo limeshindikana? Nataka kujua hatua ambazo Wizara itazichukua.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ione ni kwa namna gani wanaweza kupunguza foleni Dar es Salaam kwa kujenga gati maeneo ya Kunduchi,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Bagamoyo ili kupunguza foleni kama ilivyo kwa Kigamboni na kuwe na maeneo ya ku-park magari katika maeneo hayo ili kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga uwanja wa ndege mkubwa Dodoma nauli za kuja Dodoma kwa ndege ni ghali na hii ni kwa sababu ya ndege zinazokuja hapa ni ndogo, lakini kwa kujenga uwanja mkubwa ndege kubwa nydingi zitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Bajeti ya Wizara imezungumzia kwamba, ina mpango wa kununua ndege mpya. Wasiwasi wangu hivi sasa ATCL ina wafanyakazi wengi wanadai, kuongeza ndege kwa kutumia jina hilo hilo sioni kama ATCL itafanikiwa. Ninashauri Wizara yako imalizane na wadeni wote na ATCL na kuunda Shirika jipya ambalo halina madeni na *management* mpya ambayo watakuwa hapo kibiashara kabisa wakijua kuna ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa kuanzisha safari za treni ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Tizeba, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri za kujenga Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Dodoma walifarijika baada ya Serikali kuonesha nia ya kujenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Mjini Dodoma. Viongozi wa Dodoma tulioneshwa rramani ya majengo mazuri ya kiwanja tarajiwa. Naomba kujua wazo la kujenga uwanja huo limeishia wapi? Wananchi ambao mashamba yao yalichukuliwa kwa ajili ya ujenzi huo walipunjwa malipo ya fidia na mpaka sasa bado wanaidai Serikali; je ni lini watalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania maskini wanaotumia reli kama usafiri kutoka Dar es Salaam, Kigoma, Tabora na Kigoma, wanateseka sana kutokana na gari moshi kutofanya kazi ipasavyo. Pamoja na maelezo ya Waziri, bado mkakati wa haraka wa kuwasaidia Wananchi watumiaji wa reli haujaelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa wazo la kununua ndege mbili kwa ajili ya ATCL. Tunatarajia Uongozi uliopo utasimamia vizuri uendeshaji wa ndege hizo ili kujenga heshima ya nchi yetu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umiliki wa Kampuni ya mabasi ya UDA bado lina utata mkubwa, maelezo ya kueleweka ni nani mmiliki wa UDA kwa sasa kuondoa utata huu yanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuiunga mkono Hotuba hii, ambayo kwa kiasi kikubwa, imesheheni taarifa ambayo imelenga kuboresha Sekta hii ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Rufiji na Mafia, niishukuru Serikali kwa kuazimia kuitengeneza Bandari ya Nyamisati kuwa katika hali bora kabisa. Kiasi cha fedha kilichotengwa cha Tshs. 500,000,000/= kitasaidia kuboresha Bandari hii ili hata boti kubwa za mizigo ziweze kupakia na kuteremsha mizigo kupidia Bandari hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Nyamisati ni kiunganishi baina ya Wananchi wa Mafia na wa Delta ya Mto Rufiji hasa Kata za Salale na Maparoni na eneo la Nyamisati. Bandari hii ambayo inahudumia Wananchi zaidi ya elfu moja kwa siku ni muhimu sana kuimarishwa. Bandari hii ikikamilika, itasaidia pia kuinua uchumi si wa Wananchi wa Nyamisati peke yao, bali pia hata Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuhakikisha kuwa, fedha waliyotenga kwa ujenzi wa Bandari itolewe haraka ili kutimiza ahadi na maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipotembelea Wilaya yetu mwezi wa nane mwaka 2013. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Rais wakati akizungumza na Wananchi wa Nyamisati, aliwathibitishia Wananchi hao kuwa Bandari hii itajengwa katika Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo pia alikuwepo Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, ambaye alinithibitishia kuwa wataingiza katika mwaka wa fedha nilioutaja hapo juu, Mradi huo wa Ujenzi wa Bandari ya Nyamisati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua, kwa kuwa Serikali mmepanga kujenga Bandari hii ya Nyamisati, basi kupanga kwenu kuende sambamba na utekelezaji wa ujenzi wake. Nirudie kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha inajenga bandari hii, ila ujenzi huo ni lazima uende sambamba na ujenzi wa majengo mbalimbali yanayohusiana na upanuzi wa bandari hiyo. Majengo hayo ni pamoja na nyumba ya kupumzikia abiria na jengo la kuhifadhia mizigo ya wananchi au abiria.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, niseme tu naiunga mkono Hotuba hii.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri na Naibu wake, pamoja na Watendaji wao, kwa kazi nzuri yenye matumaini wanayoifanya kutekeleza malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuishukuru Serikali kwa kutoa uamuzi wa kuwataka TPA kuchukua hatua ya kujenga meli mpya na kubwa kwa usafiri katika Ziwa Nyasa kwa mwaka 2014/2015. Nalipongeza Shirika la TPA kwa jitihada za kujinua kiuwezo kuliko hali ya Shirika ilivyokuwa huko nyuma. Pamoja na hatua hiyo, ningependa kushauri ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Nyasa ni Ziwa ambalo liko katika Bonde la Ufa. Ni Ziwa lenye mawimbi makubwa sana kuliko Maziwa mengine hapa nchini, ambayo hayatabiriki kabisa. Meli zinazofanya kazi hivi sasa ambazo ni ndogo zinapata wakati mgumu sana kusafiri wakati wa dhoruba. Ni muhimu sana kabla ya kutengeneza meli hizo, utafiti wa kina ufanyike kujua ni aina gani ya meli kimuundo zitahitajika kuhimili mawimbi ya aina ile. Hata meli ndogo zilizopo ziliundwa maalum kwa Ziwa Nyasa. Kama hatuna wataalam watakaomudu vizuri, ni bora hata Serikali ikaomba utaalam kutoka nje.

Ushauri mwagine ni kuiomba Serikali kupitia TPA, ikarabati meli ndogo ya MV. Iringa ambayo ilikuwa inawasaidia Wananchi wengi kandokando ya Ziwa Nyasa, imeharibika na haijatengenezwa kwa muda sana. Hatua hii, itasaidia huduma wakati Wananchi wanasabiri meli mpya. Kutokana na matatizo makubwa ya usafiri, wafanyabiashara kadhaa wamejitokeza kununua maboti madogo madogo ya usafiri. Tatizo kubwa maboti hayo hayana usalama wa aina yoyote wala hayana vifaa vya uokoaji kama maboya. Hatari zaidi maboti hayo yanajaza watu na mizigo kwa kiwango cha juu sana. Ninaomba SUMATRA Mkoa wa Mbeya, wafuatilie kwa karibu sana kuhusu usafiri wa maboti na meli katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya wasafiri wa Mkoa wa Mbeya na Mikoa na nchi jirani, kuishukuru Serikali kwa kutufungulia usafiri wa ndege kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe. Adha ya kusafiri kwa gari toka Dar es Salaam hadi Mbeya ilikuwa kubwa sana, iliyokuwa inachukua saa 12. Tunaomba jengo jipyga la abiria likamilike haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo mfupi, naunga mkono hoja hii na nawatachia kazi njema.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika uwasilishaji wetu wa Wizara hii muhimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Julius Kambarage Nyerere, umebeba jina kubwa sana kuliko, lakini haupewi heshima inayostahili kwa kuwa umekuwa uchochoro mkubwa wa madawa ya kulevyia. Pamoja na jitihada zinazofanywa, lakini ni dhahiri kuwa kuna tatizo la kimfumo katika Uwanja huu linalofanya wafanyabiashara haramu ya madawa ya kulevyia kuendelea kuutumia uwanja kama route ya biashara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu na inasikitisha sana kuona kuwa uwanja uliopewa jina la Mwasisi wa Taifa, unachafuka kwa usafirishaji wa madawa ya kulevyia. Wizara ina wajibu wa kuhakikisha kuwa kila mwanya uliopo unazibwa ili si tu kulinda jina la Baba wa Taifa, bali pia kulinda hadhi ya uwanja katika Jumuiya za Kimataifa. Namtaka Waziri pia, atueleze toka Mwezi Januari mpaka anapomalizia kuwasilisha hoja yake ni matukio mangapi ya usafirishaji wa madawa ya kulevyia ambayo yamezuiwa katika Uwanja huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la bodaboda limekuwa linaangaliwa kwa jicho la pembedi, lakini ni dhahiri kuwa ujenzi unaosuasua wa barabara za miji mikuu nchini kwa mfano Dar es Salaam, umepelekea kuwepo na foleni zinazokwamisha shughuli zinazohitajika uharaka. Kitendo cha bodaboda kukatazwa kuingia katika maeneo ya mijini si tu unazuia ufanisi, lakini unasababisha ukwamishaji wa shughuli za kimaendeleo ambaao kwa kipindi hiki cha ujenzi wa barabara, bodaboda hazina budi kuruhusiwa katikati ya miji ili kufidia muda ambaao wafanyakazi na wafanyabiashara wanapoteza katika foleni za miji mikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matukio mbalimbali ya ajali za baharini zinazosababishwa na ubovu wa vyombo vyatuhukuzi. Inaelekeea Serikali imeendelea kuwa *reactive* hasa pale ajali zinapotoka. Je, Wizara toka ifanye kaguzi zake za vyombo vyatuhukuzi, ni vingapi vimefungiwa kwa kukosa ama kutokidhi vigezo vinavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali za barabarani nyingi zinazotokea nchini husababishwa pia na hali duni za vyombo vyatuhukuzi ambavyo pia huchangiwa na kuzidisha idadi ya abiria katika mabasi ya abiria. Hili ni janga kwa Taifa kwa kuwa kwa mwaka 2013 pekee takwimu zinaonesha kuwa, kumekuwa na ongezeko la matukio 264 ya ajali za barabarani kwa mwaka jana (2013), ambapo ni sawa na asilimia 1.1, ikilinganishwa na mwaka 2012 ambapo

Nakala ya Mtando (Online Document)

matukio yalikuwa 23,578. Hii ni kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mohamed Mpinga, mwezi Januari mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na sababu nyingi za matukio haya ya ajali zikiwemo ulevi, mwendo kasi na uzembe wa madereva, uchovu wa madereva ambao hutembea umbali mrefu bila kuwa na dereva mbadala na ubovu wa barabara zetu. Wasiwasi wangu ni kwamba, haya yote yanafanyika huku abiria wakiwa hawajapewa kinga za ajali na hivyo kusababisha vifo vingi vinavyoambatana pia na ulemavu kwa majeruhi. Kwa mfano, takwimu zaidi zinaonesha kuwa idadi ya ongezeko la vifo viliviyotokana na pikipiki kwa mwaka 2013 ni 168, sawa na asilimia 18.1, ambapo mwaka 2012 kulikuwa na vifo 930.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa mwaka 2013 kumekuwa na ongezeko la majeruhi 1,046 sawa na asilimia 19, ambapo mwaka 2012 kulikuwa na majeruhi 5,532. Ni wajibu wa Wizara hii kuhakikisha kuwa, abiria na mizigo yao wanakuwa salama muda wote. Napenda kuishauri Wizara kuhakikisha kuwa, kila chombo cha usafiri nchini kinahakikisha usalama wa dereva na abiria wake ili kupunguza ajali hizi. Umuhimu pia uwewe katika kutilia mkazo elimu kwa umma ili kufanikisha juhudini za kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro, inaonesha kuwa imetengewa kiasi cha bilioni 16.1 na kati ya hizo shilingi milioni 100 kati ya hizo sawa na asilimia 0.6 ni fedha za ndani. Hii inaonesha kuwa, mikakati mingi ya Miradi ya Maendeleo inakwamishwa na utegemezi wa bajeti kwa fedha za nje. Lazima Serikali itafute njia nyingine ya kufanya miradi ya Maendeleo bila ya kutegemea fedha za wahisani. Wizara hii ina uwezo wa ku-generate mapato, ni jambo la aibu kuona tunashindwa kuendeleza sekta hii lakini bado tunategemea fedha za wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Marubani hasa wa Kitanzania kutopewa kipaumbele katika masuala ya usafiri limeleta malalamiko makubwa kwa kuwa kuna malalamiko kuwa marubani wa kigeni ambao huja nchini hupewa kazi za Urubani bila ya kuwa na vibali. Sasa Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani, ni lazima waweke mikakati katika kuhakikisha kuwa, suala la usafiri wa anga halipo compromised na wageni wanaofanya kazi bila vibali, kwani hii inapelekea ama inachochea kuwa na *security breach* hasa tukizingatia kuwa tupo katika zama za sayansi na teknolojia, ambapo masuala ya Kigaidi yanayotumia usafiri wa anga yanafanyika mara kwa mara. Tusitoe nafasi hiyo kwa kuhakikisha kuwa kaguzi za mara kwa mara zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kusitishwa kwa mkataba wa Mamlaka ya Bandari Tanzania na Kampuni ya Oceana Advanced Industries Limited mwezi Novemba, 2008 kwa mujibu wa Ripoti ya CAG iliyowasilishwa ya ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka 2012/2013, ulisababishia Mamlaka kulipa

Nakala ya Mtando (Online Document)

kiasi cha shilingi bilioni 2.24 bila kunufaika kwa huduma yoyote baada ya kusitishwa mkataba huo Mei, 2010 ambao ulilenga kukarabati eneo la kutia nanga na kukarabati kituo cha kupakulia mafuta Kurasini. Nitamwomba Waziri, atoe majibu ya kina ni kwa nini mpaka mkandarasi anapewa Mradi huu hakuwa amepewa eneo husika la kazi ambalo ni Gati Namba 7 na kuisababishia Serikali hasara hiyo? Hapo ni lazima nipate majibu la sivyo nitaomba kutoa shilingi ya Waziri kwa uzembe huu wa Mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Tizeba. Tuanze ule muda wa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri yeye atazungumza kwa dakika 20. Mheshimiwa Naibu Waziri Uchukuzi, Dkt. Tizeba, tafadhal!

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai na afya njema kwa kuniwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa ndugu wote waliopoteza wapendwa wao, Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo wa Jimbo la Chalinze. Mheshimiwa William Agustino Mgimwa wa Kalenga. Mwenyezi Mungu awape miyo ya uvumilivu ndugu wote na azilaze mahali pema peponi roho za marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa hivi karibuni, Mheshimiwa Kikwete na Mheshimiwa Mgimwa wa Jimbo la Chalinze na Kalenga karibuni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa ushirikiano anaonipatia katika utendaji wangu katika Wizara yetu ya Uchukuzi. Niwashukuru sana viongozi wengine wa Wizara na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa namna ya pekee sana kwamba, namshukuru Mke wangu mpPENDWA Furaha kwa kunivumilia, maana maneno ya hapa ndani si kidogo, kwa hiyo namshukuru sana kwa kuniLEWA na kunivumilia. Mwisho nitoe shukrani kwa ndugu zangu wana Jimbo la Buchosa kwa mambo mema wanayofanya pamoja na mimi katika kuendeleza Jimbo letu la Buchosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi hii kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Wabunge wakati

Nakala ya Mtando (Online Document)

wa kuchangia tangu asubuhi ya leo. Nitasema kwa kifupi sana kwa hivyo, niombe pale patakapohitaji ufanuzi labda tutakuwatana kwenye vifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maoni yaliyotolewa na mchango wa Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah. Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah amezungumzia korongo lilipo katika uwanja wa ndege wa Mafia na akatoa ushauri ambao kwa kweli niseme tu kwamba ushauri ule ulikwisha, mawazo yake yalikwishajulikana na Mamlaka yetu ya Viwanda vya Ndene kwa kushirikiana na Millennium Challenge Account ambao wanajipanga kufanya hicho hicho ambacho Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah amesema. Kwamba itajengwa mifereji ambayo itafika moja kwa moja Ziwan badala ya kukomea pale barabarani kama wale Wakandarasi walivyokuwa wamefanya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la Nyamisati, pesa imetengwa shilingi milioni 500 kurekebisha gati hilo na kwa hiyo, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa ataona kwamba sasa, gati lile la Nyamisati litaboreshwa na kwa hiyo, Usafiri wa Mafia na Nyamisati utakuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lile la Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, suala lile la watu kupita kwenye Korongo ameomba tusogeze uwanja kidogo ili watu waweze kupita kwa sababu kuzunguka kule uwanja ni mbali sana kwa wagonjwa na wengine wakati huu ambapo barabara imelika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, naagiza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wawasiliane na Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, atakapokuwa yupo Jimboni kwake, waende waangalie uwezekano wa kutafuta eneo ili kuweza kutoa huduma hiyo kwa wananchi. Siyo jambo gumu, nadhani litawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Amina Amour, yeye amesema Marubani wa kike wawe *trained* wengi zaidi. Nataka niseme kwa kifupi tu kwamba wazo la Mheshimiwa Amina ni zuri, lakini linaendelea kutekelezwa, baadhi ya hawa uliowaona hapa wamepatikana kwa utaratibu ambao upo. Tunao Mfuko wa Kufundishia Marubani, sasa hivi tuseme tu kwamba kipaumbele kitatolewa kwa wanadada wenye sifa. Wanadada wenye sifa jitokezeni Mfuko wa Kufundishia Marubani unaendelea kuchangiwa pesa, mwaka huu tumepeleka watano na tutaendelea kupeleka wengi zaidi kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi inayoendeshwa na Wizara kupitia PPP. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Uwezesajji kwa maelezo ya msingi ya Sheria yenye aliyojatoa na niseme tu kwamba, Wizara inayo miradi

Nakala ya Mtando (Online Document)

mingi sana, tumekuwa tukiitangaza. Mamlaka ya Bandari wametangaza miradi mingi ya bandari kuanzia Mwambani Tanga, Bagamoyo, Lushungi, Lindi yote hii watu wenye nia walikuwa huko juu kwenda kuangalia waeleze wanachotaka kufanya, watengeneze *proposal*, halafu mamlaka itapitia na kumpa yule ambaye ataonekana maelezo yake yanashabihiana na mawazo ambayo mamlaka yenyewe wanayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye viwanja vya ndege tunakaribisha pia watu wenye uwezo wao wawekeze katika viwanja vya ndege kwa makubaliano ambayo tutaona yana maslahi kwa Taifa. Viwanja viko vingi ambavyo vinaweza kuwekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hata PPP kwenye reli yenyewe. Hivi sasa mfanyabiashara mmoja mkubwa nchini Said Bakhresa anayo mabehewa mengi sana ya kwake binafsi yanayovuta mizigo kwenye reli yetu ya kati. Kwa hiyo, hauzuiliwi mtu mwenye uwezo kununua treni, *locomotive* ya kwake akanunua mabehewa ya kwake, akaingia makubaliano na Kampuni ya RAHCO namna ya kutumia reli iliyopo sasa hivi. Kwa hiyo, siyo kwamba PPP inazuiliwa, hapana. Watu wanakaribisha waingie kwenye hii miradi kama wanayo mitaji wawekeze, masharti yameelezwa hapa na Mheshimiwa Mary Nagu, yanaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Amina pia alizungumzia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kubakiza pesa wanazokusanya. Ni kweli tuliiomba Serikali katika bajeti ya mwaka uliopita, wakatukubalia kwamba sasa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itakuwa inabakiza pesa zote wanazokusanya. Mwaka jana walikuwa na Bajeti ya shilingi bilioni 31, waliyokuwa wameruhusiwa kubakiza na wanaendelea kukusanya hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, fedha ambayo wanaruhusiwa kubakiza ilikuwa ina mipango yake, lakini juu ya hiyo walikuwa na fedha iliyokuwa imeombwa kutoka bajeti ya Serikali na hiyo ndiyo ambayo ingegharamia miradi mikubwa kama wa Mwanza ambao unaendelea kujengwa sasa hivi na miradi ya Kigoma, Tabora, Bukoba na kwingine ambayo ile ilikuwa na *component* ya Serikali kuweka fedha pale penye fedha ya ufadhili. Kwa hiyo, hizo pesa zinahitajika kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sambamba na ile ambayo walikuwa wanapata wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa James Mbatia amezungumzia PPP projects nimeshasema. Pia akazungumzia mapato ya TPA ya bilioni 165 mwaka 2007 na yalivyoongezeka kufikia sasa hivi na kusema kwamba bado hayatoshi. Ni kweli, ukitazama fedha wanazokusanya TPA wenyewe unaweza kuona kwamba ni bilioni hizo 417, lakini ziko idara za Serikali nyingi zinazopata mapato mengi pia kuitia pale pale Bandarini.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA wanakusanya fedha nyingi sana kupitia Bandari, sijui Mionzi, Maliasili na kadhalika wengi tu wanakusanya pesa kupitia Bandarini. Kwa hiyo, hizi zikijumulishwa ni fedha nyingi sana na siyo hiki kiasi kidogo tu ambacho wanasema ni cha TPA peke yao kukusanya bilioni 417.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya maegesho Mjini Dar es Salaam. Maeneo ya maegesho kwenye hotuba ya Waziri amesema kwamba sasa hivi kuna maeneo kama matatu ambayo yamebuniwa ya kufanya maegesho kwa ajili ya magari makubwa. Moja kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, lingine eneo la TAZARA na Kampuni ya Jitegemee Enterprises ambako sasa hivi mazungumzo yanaendelea. Maeneo yote haya matatu yatatumika kwa ajili ya kujenga amegesho kwa magari makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, yeye amezungumzia suala la Dar es Salaam kubaki Mji wa biashara na Makao Mkuu kuhamia Dodoma. Mheshimiwa Mchungaji sijui umri wako kwa sasa, lakini nadhani hili wazo lilishasemwa na kuanza kufanyiwa kazi miaka zaidi ya umri wako.

Sasa sijui kwa nini leo umeliibua leo hapa. Tupo Dodoma mimi na wewe sasa hivi, kwa sababu ya hilo wazo, ndiyo maana tupo hapa vinginevyo Bunge lilikuwa linakaa Karimjee Dar es Salaam, lakini kwa sababu ya wazo hilo ndiyo Bunge limehamia hapa, TAMISEMI iko hapa na wengine watafuata. Kwa hiyo, siyo wazo jipya, nakukumbusha tu kwamba ni wazo lipo siku nyingi na linatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Msalato, upembuzi yakinifu na usanifu umekamilika na hili naomba wote waliozungumza kuhusu uwanja wa ndege wa Msalato watuelewe vizuri. Uwanja wa ndege wa Msalato upembuzi yakinifu na usanifu umekamilika, sasa hivi andiko hilo limepelekwa Hazina kwa ajili ya kuanza kutafutiwa pesa. Kwa hiyo, suala la Msalato linaendelea na Wizara inalipa umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msalato na viwanja vingine 11 ni awamu ya pili ya pili ya ujenzi wa viwanja vya Mikoa hapa nchini. Tulianza awamu ya kwanza na ujenzi wa viwanja saba vinaendelea kukamilika sasa hivi; Tabora, Kigoma, Bukoba na vinginevyo, Mpanda sijui na wapi. Sasa hivi tunaingia awamu ya pili ya viwanja 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa aina ya kiwanja na ilivyo vitatafutiwa pesa vingine kwa njia ya ubia na watu binafsi na vingine kwa bajeti ya Serikali na vingine kwa kuomba wafadhili, lakini awamu ya viwanja 11 ndiyo inayofuata. Hii ni pamoja na hicho cha Nduli Mheshimiwa Msigwa ulichokiongelea, kiko katika awamu hii ya viwanja kumi na moja.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la viwanja vya ndege, sasa uzuri tu ni kwamba Bunge lenyewe kupitia Kamati ya Miundombinu limekwishaona kasi iliyonayo Serikali. Mwisho, wanatumbia fungeni break kidogo, maana ni ushauri wa Kamati kwamba tusifanye miradi mingi sana kwa sababu tukiendesha miradi mingi sana inaweza ikafika mahali tukawa tunagusagusa kila mahali halafu mambo yakawa hayaendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeshauriwa tu-concentrate na viwanja vichache, tuvitengeneze vikamiliike, tuhamie kwenye viwanja vingine. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuvute subira. Kama Mkoani kwako kwa mfano pale Babati, Babati na viwanja vingine hivi ambavyo vitaingia kwenye awamu ya tatu, tuombe muwe na subira kwa sababu kiukweli hatuwezi tukajenga viwanja vyote vya ndege nchini kwa mara moja. Hatua za kwanza zitafanyika, za upembuzi yakinifu, usanifu na kadhalika, lakini phase ya ujengaji ni lazima iendane na mahitaji pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko viwanja vingine ambavyo vinahitaji matengenezo ambayo siyo makubwa sana, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wamekwishaelekezwa, wavifanyie matengenezo kuvizezesha kuanza kutumika. Kiwanja cha Musoma lazima kifanyiwe matengenezo ili kiendelee kutumika. Sasa hivi waendeshaji ndege wanakikimbia kwa sababu ya kokoto zile zilizoko pale, zinarukia kwenye ndege kwa hiyo haziendi. Mamlaka ya Viwanja vya ndege wanayo maelekezo mazuri ya namna gani ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe amezungumzia Mabehewa ambayo wachangiaji wengi wameyasema, mabehewa ya mizigo 274 ambayo bado hiyo bilioni nane na ushee karibu bilioni tisa, ikipatikana ikalipwa, basi yatafika nchini hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba, mwaka wa fedha wa Serikali haujawkisha tuna matumanu makubwa kwamba hadi kufika Juni, fedha hii itakuwa imepatikana, watengenezaji watakuwa wamelipwa na kwa hiyo mabehewa yetu yale tutayapata kwa wakati. Naomba niseme tu kwamba, katika bajeti hii kwa waliosoma na kumsikiliza Mheshimiwa Waziri tunao mpango wa kununua tena Mabehewa mengine ya mizigo 204, lakini mwaka kesho tutaomba mabehewa mengine 900 na kadhaa. Kwa hiyo, ni program endelevu hii ya kupata mabehewa na kupata vichwa vya treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe ameomba ile *halt* ya Kambuzi kuwa *station*. Hili ni wazo tunalichukua kwa sababu umuhimu wa treni kusimama pale ulishaonekana siku nyingi, sasa wataangalia kama idadi ya abiria wanayopatikana kwenye eneo hilo inatosha, basi TRL watafanya huo uwamuzi wa kusimama pale kama kituo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, gati la Kalema, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, liko katika mpango wa matengenezo, zabuni imekwishatangazwa ya Gati hilo, nadhani wako kwenye mchakato wa evaluation wakishampata Mkandarasi ujenzi utaanza. Nimesikitika tu Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, kwamba bado mabehewa yetu yana panya wakubwa kama panya buku. Naomba niseme kwamba si kweli mabehewa yetu, hii hadithi na ile picha ambayo amezungumza Mheshimiwa Mbunge, ni picha ya Jerry Muro ya mwaka 2012, miaka mitatu iliyopita. Sasa hivi Mabehewa yetu siyo mabaya namna hiyo, yanafanyiwa fumigation mara kwa mara, hakuna mapanya wanatembea katika mabehewa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, MV Liemba mbadala wake ni nini? MV Liemba mbadala wake ni meli mpya mbili zitakazojengwa ndani ya Ziwa Tanganyika kama hotuba ya Waziri ilivyosema. Kile kitabu ukikipitia vizuri utakuta takwimu yote ya namba gani tunajipanga kujenga hizo meli kwenye Maziwa yetu haya matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukarabati wa station za Reli unaendelea. Nitoe taarifa kwamba ukarabati wa station ya Kigoma umekamilika, station ya Mwanza umekamilika, station ya Kaliua umekamilika na tunaendelea kufanya hata matengenezo kwa awamu. Kwa hiyo, fedha siyo nydingi huko TRL, lakini hizo wanazopata wanafanya ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumizie kwa haraka suala la flow meter kwa sababu limehojiwa na watu wengi hapa. Suala la flow meter lilianza siku nydingi na genesis yake ni kwamba kulikuwa na wizi wa aina mbili ulikuwa unaendelea pale bandarini. Mafuta yalikuwa yakiibiwa KOJ, lakini mafuta yalikuwa yakiibiwa kwenye bomba kuu linalotoka Baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubaini upungufu huu wa wizi na kadhalika mamlaka ikachukua jukumu la kununua flow meters na kuzifunga pale. Kilichokuja kubainika ni kwamba, waingizaji wa mafuta walikuwa wanalamika kwamba wanatozwa kodi isiyolingana na mafuta yanayoingizwa. Wakati huo huo TRA na wao wanalamika kwamba waagizaji wanaongopa kiasi cha mafuta wanachotakiwa kulipia kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikaenda namna hiyo malalamishi haya yakawalazimisha Wakala wa Vipimo kusimamisha matumizi ya hizo flow meters. Baada ya kusimamisha matumizi ya hizo flow meters kutokana na malalamiko ya pande zote mbili ndiyo mazungumzo yakaanza kubaini tatizo liko wapi. Suala hili limeendelea kwa muda mrefu na mwisho kilichobainika ni kwamba kwanza

Nakala ya Mtando (Online Document)

mfumo wa ushushaji wa mafuta na kuyapeleka kwenye hifadhi si mzuri sana katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Mafuta yanayotakiwa kupimwa ili yatozwe kodi yanapaswa yawe ni mafuta ambayo yamekwisha tulia na siyo yale mafuta yanayosukumwa moja kwa moja kutoka kwenye meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaratibu sasa unafanyika na ndiyo maana Mamlaka ya Bandari wanao mradi mkubwa wa kujenga matenki ya kuhifadhia mafuta ili mafuta yakishashushwa kutoka kwenye Meli yasiende moja kwa moja kwenye Makampuni ya Mafuta. Yakae mahali yatulie, baada ya hapo yakiwa yanatoka kwenda kwenye makampuni ndiyo yapimwe kwa uhakika kujua kiasi cha mafuta ambacho sasa kinapaswa kitozwe kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari wanataka kujiwekea *control mechanism* kwamba, watafunga mita nyingine kabla ya matenki ili kujua angalau kujiridhisha kwamba ni kaisi gani yameingia na watu wa mapato watakapokuwa wanatoza wajue kwamba ni mafuta kiasi gani wanamtoza mwenye mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunazungumzia hili jambo, Mamlaka ya Bandari wanajipanga kununua hizo mita kama Mheshimiwa Mbarouk alivyosema. Mita za zamani sasa hivi hatuwezi kuzifunga kwenye mfumo kwa sababu kuu mbili.

Kwanza, mfumo wa mabomba yenyewe, hauko sawasawa kutupa vipimo tunavyovihitaji, lakini uwezo wa hizo mita, ni mdogo kulinganisha na uwezo mkubwa wa bomba letu la kusukuma mafuta, ambalo sasa ni kati ya mita za ujazo 2000 mpaka 3000 kwa saa. Mita zile zilinunuliwa wakati uwezo wa kusukuma mafuta ulikuwa kati ya mita za ujazo 500 mpaka 700. Tukizifunga zile, tutaanza tena kuona msururu wa meli za mafuta pale baharini zikisubiri kushusha mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana zile mita zilinunuliwa, bahati mbaya wakati ule na sasa hatuwezi kuzifunga wa sababu tukizifunga tutashusha tena chini uwezo wa bandari yetu kushusha mafuta.

Kwa hiyo, liko wazo kwamba *Tipper*, ikibidi labda tuangalie mkataba uliopo sasa hivi wa uendeshaji wa *Tipper* na bandari yenyewe kujenga maeneo mengine. Nimemwona Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ameuliza lile swalii, haya yote ni katika kuangalia utaratibu sahihi wa kuhifadhi mafuta na kuyapima kwa ajili ya kutoza ushuru na kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuunga mkono hoja.

Nakala ya Mtando (Online Document)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Tizeba kwa maelezo yako mazuri na ufanuzi mzuri sana. (*Makofii*)

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwakyembe, Waziri wa Uchukuzi ili na yeye aweze kufafanua na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri una dakika 40, karibu tafadhal!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa jioni ya leo, kwa lengo la kuhitimisha bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Miundombinu ya Bunge, kwa mchango wao mkubwa kwa Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuihakikishia Kamati, kuwa tutazingatia kwa kina ushauri wote waliota. Tumepokea pia hoja za Waheshimiwa Wabunge, kuhusu namna bora ya kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Wabunge wote waliochangia kwa kusema na waliochangia kwa njia ya maandishi wakati wa hoja yangu na kwenye hoja ya Waziri Mkuu na Wizara zingine. Kazi yangu sasa ni kutoa maelezo na majibu kuhusu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Mheshimiwa Dokta Tizeba, Mbunge wa Buchosa na Naibu Waziri wa Uchukuzi, ameshatoa maelezo kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Naona na mimi niendelee kutoa ufanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa.

Nitaanza kwanza kwa kutoa maelezo ya ujumla, yakifuatiwa na yale ya Kamati ya Miundombinu, kisha Kambi ya Upinzani na kuhitimisha na ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa kifupi, nisipopata muda wa kutosha, basi naomba nikuhakikishie tu kuwa taratibu zote za Bunge zitafuatwa ili niweze kuwapatia majibu yote kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu pamoja na hoja ninayohitimisha leo, michango ya Waheshimiwa Wabunge, iligusia zaidi maeneo makuu matano kwenye sekta hii ya uchukuzi.

- (i) Ufufuaji wa huduma za reli ya kat;
- (ii) Uendelezaji wa Bandari zetu hususan ujenzi wa gati namba 13 na 14 na uboreshaji wa huduma za kibandari;
- (iii) Urekebishaji wa Sheria ya TAZARA;

Nakala ya Mtando (Online Document)

(iv) Uboreshaji wa viwanja vya ndege hususan kiwanja cha ndege cha Mwanza; na

(v) Mradi wa reli katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nihitimishe utangulizi wangu kwa kusema kwamba, bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2014/2015, ni bajeti ya kuendeleza na kuimarisha sekta ya uchukuzi ili sasa ianze kukimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge waniamini, mwaka wa fedha wa 2012/2013, bajeti yangu kwa kweli ilikuwa ni ya kuitoa sekta ya uchukuzi kwenye chumba cha wagonjwa mahututi na wote mnajua hilo, ilikuwa hakuna reli hapa. Mwaka huu wa fedha, ni mwaka wa 2013/2014, ulikuwa ni mwaka kwa kweli wa kuiwezesha sekta hii kuanza kutembea. Nawahakikishia, mwaka wa fedha 2014/2015, kutakuwa na mabadiliko makubwa katika sekta, reli itakuwa katika nguvu ya kukimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza, tutakuwa na vichwa vya treni vipyta vya uhakika 51, haijapata kutokea katika historia ya nchi yetu. (Makofii)

Sasa hivi tunavyo vinane tu vya kusuasua na maana yake ni nini, kwa hesabu za kiuchukuzi, ina maana tunaweza kusafirisha tani milioni 1.5 za mizigo, kulinganisha na mizigo wa sasa hivi wa tani laki mbili na mara nyingine chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vichwa vya treni ambavyo TRL inaanza kuvipokea muda siyo mrefu ni vya gharama kubwa sana, vinahitaji kutunzwa ili viweze kutoa huduma katika muda amba vinatakiwa kuishi. Lazima kwa kweli naona tutoe motisha ya kutosha kwa madereva wetu wa treni na tumeshaanza mazungumzo na Kampuni ya Japan, Toshiba, ambayo itawezesha karakana yetu ya Morogoro kufanya matengenezo muhimu ya treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo langu kwa Bodi na Management ya TRL, ni kuhakikisha kuwa vichwa hivyo vinafanyiwa matengenezo hayo muhimu kila muda unapofika. Sitakuwa na subira ya aina yoyote kwa ambaye atafanya kinyume na mahitaji haya ya lazima ya matengenezo ya vichwa vya treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulihakikishia Bunge hili Tukufu kuwa sekta ya uchukuzi itakuwa na uwezo mkubwa wa kuwezesha sekta zingine kufanya majukumu yake ndani ya mwaka ujao wa fedha 2014/2015 hasa kuanzia Januari, baada ya kuwasili vifaa vyote.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe maelezo kwenye masuala ya kijumla ambayo yalijitokeza wakati wa majadiliano ya hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ambayo mawazo, hoja hiyo ililetwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati. Kwanza Kamati imetushauri sisi tuharakishe kukamilisha utekelezaji wa Mradi ya Malipo kwa Njia ya Mtandao, *Electronic Payment System*. Tuharakishe kuwaunganisha pamoja Watoa Huduma kwa Njia ya Mtandao, *Electronic Single Window System*, sambamba na kuhakikisha bandari, pamoja na Mamlaka ya Mapato TRA zinafanya kazi kwa saa 24 kwa siku saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu kwa kweli sisi tumeuzingatia, na hatua za utekelezaji nimeshazieleza, lakini naomba nizurudie tu kwamba, mradi wa kuwaunganisha pamoja watoa huduma kwa njia ya mtandao, yaani *Electronic Single Window System* umeshaanza mwezi Aprili, 2014 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekaji yaani *installation* ya mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao, *electronic payment system*, unatarajiwa kuanza ifikapo mwezi Juni, 2014 na kukamilika mwezi Novemba, 2014. Aidha, mwezi Februari, 2014, mkataba wa wadau wote wa bandari ya Dar es Salaam wa kufanya kazi kwa saa 24 kwa siku zote ulisainiwa na Mamlaka ya Bandari tayari inatekeleza utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vilevile ili kuboresha huduma za bandari, Mamlaka inatekeleza mradi wa ujenzi wa jengo refu la ghorofa 35, One Stop Center Building, ili kuwaweka wadau wote kwa pamoja. Tuna wadau wamesambaa kila sehemu na ndiyo wanaofanya kwa kweli ucheleweshaji mkubwa utokee wa mizigo bandarini. Tuna uhakika jengo letu litakamilika mwaka kesho na kuwajumuisha watu wote pale wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasilitiza kuwa TPA kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji, tujaribu kujenga haraka maegesho ya maroli. Hili ni wazo zuri na nimeshueleza kwamba mamlaka imeshapata maeneo kadhaa mjini kwa ajili ya kuweka mizigo kutoka nchi jirani za DR Congo na kuingiza maroli yao pale, Burundi, Rwanda na Zambia, Malawi wana sehemu zao, ndiyo maana siwataji. Vile vile Mamlaka kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, inaanishiwa mradi wa maegesho ya magari makubwa ya mizigo eneo la Kurasini, linalomilikiwa na Manispaa ya Temeke, lina ukubwa wa ekari 7.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, makububaliano ya mwisho na utekelezaji wa mradi huu yanatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, kuanzia mwezi Julai, sitaki kusikia tena kuna mazungumzo, nataka kuona

Nakala ya Mtandao (Online Document)

vitendo vinafanyika. Vilevile, Kamati imetushauri Serikali kwamba, itoe maelezo kuhusu maendeleo ya bandari za Mwambani, Tanga, Mtwara, Kigoma na Itungi Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka imekamilisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya kukamilisha maandalizi ya kuanza ujenzi wa bandari za Mwambani na Mtwara, ambapo zabuni zilitangazwa tarehe 27 Machi, mwaka huu na zitafunguliwa tarehe 26 Juni, mwaka huu. Kazi zinatakiwa kuanza ifikapo Septemba, 2014 na kukamilika mwishoni mwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bandari ya Kigoma, mamlaka imetekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ilioainishwa kwenye BRN. miradi hiyo ni pamoja na ukarabati wa cherezo, (*sleepway*) kwa shilingi milioni 200. Ukarabati unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, mwaka huu. Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa Crane, ile Crane kubwa, RMJ ya kupakua na kupakia mizigo, amepatikana kwa gharama ya shilingi milioni 592 na ataanza kazi mwezi ujao na ukarabati utakamilika mwezi Septemba, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile TPA inaendelea kukamilisha malipo ya fidia ili kupisha ujenzi wa gati eneo la Kibirizi. Vile vile mamlaka inakamilisha tathimini kwa ajili ya malipo ya fidia eneo la Katosho, ili kujenga bandari kavu ambapo mamlaka imetenga fedha za malipo katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari ya Itungi, mamlaka imekamilisha utaratibu wa kuhamisha chelezo kutoka Mwanza, chelezo moja ndogo, *floating dock*, kwenda *Itungi port* kwa ajili ya maandalizi ya matengenezo ya meli. Sambamba na hilo, bandari hii itafanyiwa ukarabati katika mwaka wa fedha 2014/2015 ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati imetushauri kwamba, sasa hebu waone tunakwenda kwa kasi kuhusu gati namba 13 na 14. Ushauri wa Kamati umezingatiwa. Vile vile Kamati ilikuwa inashangaa, tunataka kuondoa miundombinu KOJ ya mafuta. Kamati inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kama watalam wa bandari waliofanya uamuzi wa kujenga boyo katikati ya magati walikuwa na utalaam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, gati la mafuta KOJ tunaloliona Dar es Salaam sasa hivi, lilijengwa mwaka 1958, kwa ajili ya kupakua shehena ya mafuta. Wakati wa ujenzi wake, gati hilo kwa kweli lilikuwa limejengwa mbali kabisa na gati za kuhudumia shehena nyingine miaka hiyo. Ilikuwa bandari ndogo na hivyo kukidhi matakwa ya kiusalama na meli wakati huo. Vilevile,

Nakala ya Mtando (Online Document)

zitakapo jengwa gati namba 13 na 14, sasa ndipo KOJ itakuwa katikati kabisa ya magati ambayo siyo sahihi kabisa kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasema mpango wa ujenzi wa meli tatu katika Ziwa Tanganyika, Victoria, umefikia wapi! Tumeelezea vizuri kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 44.

Kamati vile vile imefarijika kusikia mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya TAZARA, na mimi naturahi kwamba rasimu ya marekebisho ya sheria ya TAZARA imepatikana kutoka nchi zote mbili. Kinachosubiriwa sasa hivi ni Bodi ya Wakurugenzi kukaa na Baraza la Mawaziri, tuketi tumalizie hilo suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kwa kweli nichukue machache tu Kamati imeongea vitu vingi vya msingi. Serikali izipe kipaumbele na kuwiwezesha karakana zetu za ndani kama vile karakara ya treni ya Morogoro ambayo ina wataalam wanaoweza kutengeneza ama kukarabati treni kama ambavyo inafanyika Malaysia. Pia kuimarisha Chuo cha Reli Tabora ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uundwaji upya wa vichwa ninane vya treni unaofanywa na Wamalaysia katika karakana ya reli ya Morogoro, unashirikisha pia mafundi wazawa walioko hapo na wengine kutoka karakana za Dar es Salaam na karakana ya Tabora, kwa nia ya kuwawezesha kujifunza na kuitumia teknolojia hiyo hata hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Chuo cha Reli, tawi la Morogoro kina jumla ya wanafunzi 60 waliopatiwa mafunzo ya ufundi wa kutengeneza vichwa vya treni. Kati ya mafunzo hayo ni pamoja na kujifunza teknolojia mpya kutoka Malaysia ya kuunda upya vichwa vya treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa treni kusafirisha abiria Jijini Dar es Salaam (*city train*). Kwa kifupi ninaweza kusema tu kwamba, Serikali imeamua kutumia utaratibu wa kushirikisha sekta ya umma na binafsi PPP na kampuni kadhaa za ndani na nje ya nchi zimeshaonesha *interest* na nia ya kutosha kushiriki katika mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwa hatua ya kuchukua mkopo katika Benki ya Biashara na kuanza ujenzi wa *terminal three*. Napokea pongezi hizo kwa niaba ya TAA, huo ndiyo ubunifu unoaoendelea na tutaendelea kuhakikisha kwamba hicho kiwanja kwa kweli kinajengwa na kinakuwa ndiyo kioo sahihi cha Tanzania.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inataka Serikali kutoa tamko rasmi kuhusu nia thabiti ya utekelezaji wa muda kukamilisha mradi wa upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. Serikali ina nia thabiti kabisa ya kutekeleza mradi wa upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. Mradi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza, unahusisha upanuzi na ujenzi kwa maana ya kuboresha kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za upanuzi na ujenzi zinahusisha urefushaji wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita zingine 500 kutoka mita 3,200 na kukifanya kiwanja cha Mwanza kuwa na run way ndefu kupita viwanja vyote nchini na pengine Afrika Mashariki, sija-check na viwanja vya Uganda na Kenya, lakini kwa hapa Tanzania kitakuwa ndiyo kiwanja chenye run way ndefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maegesho ya ndege za abiria, jengo la mizigo, maegesho ya ndege za mizigo, barabara za kiungo, jengo la kuongozea ndege na jengo la abiria na miundombinu yake. Kazi zinazoendelea sasa hivi, katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, ni pamoja na kuchimba eneo la kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa nguzo za jengo la mizigo na jengo la kuongozea ndege na ujenzi wa karavati la kutolea maji ya mvua kutoka upande mmoja wa barabara ya kutua ndege na kuruka ndege kwenda upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu unahitaji fedha nyingi katika kipindi kifupi ili kukamilisha kazi zilipangwa. Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeanza mazungumzo na Exim Bank ya China ili kuziba pengo la fedha zinazohitajika. Tumeliona hilo tatizo na sisi, kwa sababu sehemu kubwa ya fedha katika mradi huu inatoka Serikali ya Tanzania, siyo kwa wafadhili. Wafadhili ni 20 bilioni, sisi tunatakiwa tutoe 89 bilioni. Kwa sababu kwa upande wetu hakuna hiyo kasi sahihi, tumeona tutafute hiyo njia, mazungumzo yanaendelea vizuri na kwa kasi nzuri ya kutekeleza mradi huu, kwa kweli tukipata fedha hiyo, kiwanja cha ndege cha mwanzo kinawezekukamilika kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Kamati inasema, baada ya ugunduzi wa gesi na ujenzi wa viwanda kama vile Kiwanda cha Cement cha Dangote, ni dhahiri kuna umuhimu wa kujenga Kiwanja cha Mtwara. Kwa kweli ushauri tumeupokea, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka taasisi mbalimbali duniani kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huu mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya ukarabati wa njia ya kuruka na kutua

Nakala ya Mtando (Online Document)

ndege. Hiyo lazima tu-maintain kwa muda kabla ya ujenzi halisia. Naomba, maeneo mengine ambayo Kamati imegusa, tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nielekee kwenye maoni ya Kambi ya Upinzani, nitayatolea maelezo masuala machache tu, kwa vile mengi yameshajibiwa kwenye hotuba yangu. Mengine yanahusu maeneo ambayo hayako chini ya Wizara ya Uchukuzi, siwezi kumlaumu sana mdogo wangu Mheshimiwa Machali, kwani ni mgeni katika nafasi hiyo, kwa hiyo, hata mipaka ya ofisi yake haijawa bayana kabisa. Kwa mfano, suala la UDA analiongelea ukurasa wa 38 mpaka 40 wa hotuba yake, hilo lina Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa DART anaouongelea kwa kirefu 17 na 18, Kituo cha Mabasi cha Ubungo, ukurasa wa 15 mpaka wa 18. Kwa kweli namshukuru Mungu tu kwamba hakuniuliza kuhusu matokeo ya mtihani wa darasa la saba maana haya hayako kwangu, ila mengine ameyaongea mazuri tu, masuala ya uchukuzi Japan, China na Spain, hayo sitayagusia kwa sababu nadhani Waziri Kivuli anayajua zaidi, mimi kwa kweli huko sijawahi kuishi. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kifupi, hoja ya kwanza ya Mheshimiwa Joseph Machali ni kuhusu hatua iliyofikiwa kwenye malengo ya BRN kuhusiana na sekta ya bandari. Hilo nimelielezea vizuri sana katika hotuba yangu ukurasa wa kwanza mpaka 11 na ukurasa wa 47 mpaka wa 67.

Mheshimiwa Naibu Spika, anahoji kwa nini siku za meli kusubiri isipungue kufika siku moja au siku mbili, ni hoja nzuri, lakini shughuli za Bandari zinawahusu wadau wengi sana. Tuna TRA, EWURA, TASAA hawa ni wamiliki wa meli, TAFFA hawa ni Chama cha Clearing and Forwarding Agency, TBS, Uhamiaji, Kilimo, Mifugo, mionzi, atomic energy wako Arusha, Afya, TDFA, wote hao meli ikija wanahusika kwa njia moja au nyingine na nyaraka, ndiyo maana kuna ucheleweshaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sasa hivi tunajenga jengo la ghorofa 35 Bandarini na linakwenda kwa kasi. Namwomba Mheshimiwa Waziri Kivuli atembelee Bandari aone, jengo lilipofikia, vijana watampokea vizuri. Naomba nisisitize hapa kwamba Waziri Kivuli ni an essential component ya Parliamentary democracy, ni muhimu, tunamheshimu, kwa hiyo, njoo uangalie mwenyewe kasi ilipofikia. Tukishamaliza jengo hilo mwaka wa kesho hawa players wote tutawaingiza kwenye jengo moja tuweze kupunguza muda wa urasimu katika kupakua na kusafirisha mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa nini container dwelling time imekuwa siku tisa nukta tatu badala ya siku saba au siku tisa kama ilivyokuwa mwaka 2012. Muda wa makasha kukaa bandarini kuwa siku tisa nukta tatu kwa kweli

Nakala ya Mtando (Online Document)

ulichangiwa na mgomo wa wenyewe malori kuchukua mizigo bandarini. Ilitumiza sana ile kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, anauliza, Waziri, Wabunge, watendaji wa Mamlaka ya Bandari kutumia fedha nyingi kwa safari za nje na mafunzo yasiyo na tija. Kwa kweli taarifa hii si sahihi, maana mimi sijawahi kufanya ziara yoyote ya mafunzo kama Waziri nikiambatana na Wabunge na watendaji wa TPA kwa kozi ya mafunzo.

Sasa mimi Waziri, Mwanasheria nikajifunze ufundi mchundo wa meli yananihusu nini mimi sijawahi kwenda huko. Namwomba Mheshimiwa Waziri Kivuli, akiona kuna hoja ameletewa huko pemberi anilize tu nitampa kila kitu, yeye ni sehemu muhimu ya uendeshaji wa Wizara hii. Sijakwenda Singapore, sijakwenda Hong Kong kujifunza, ila vijana wangu wa TPA lazima waende kujifunza, lazima wa-remain current na maendeleo mbalimbali ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa magati katika Ziwa Tanganyika umegubikwa na utata katika maeneo yafuatayo:-

Gharama za ujenzi kupanda, ucheleweshwaji wa miradi. Kwa kweli miradi hii ilishasababisha Mhandisi Mkuu wa TPA na wenzake kuwajibishwa pamoja na menejimenti nzima. Kwa sababu hili ni suala la nyuma, maelezo ya kina kuhusu ujenzi wa magati katika Ziwa Tanganyika yamo katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 50 – 52 aya ya 83 kuhusu hatua ya ziada tulizozichukua sasa kwa Makandarasi. Tumeleza kuhusu kuwanyang'anya Makandarasi hao kazi zao, kuwashtaki makandarasi hao kwa PPRA, kuwashtaki kwa CRB ili wanyang'anywe usajili wa kampuni zao na mwingine tumependekeza afunguliwe mashtaka ya jinai kwa sababu ya kughushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua gani zimechukuliwa na Serikali dhidi ya menejimenti ya TPA na Bodi yake kutokana na Mheshimiwa anasema kushindwa kusimamia mkataba wa ukarabati wa gati namba moja (1) – 11 kati yake na Kampuni ya Osheana. Haya yalitokea 2010, tulishayachukulia hatua haya, sisi tunasonga na yaliyopo na yajayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Wizara ya Uchukuzi inatumia fedha za TPA kwa ajili ya shughuli za Wizara. Kwa kweli Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Uchukuzi. Baadhi ya shughuli zake hufanywa kwa kushirikiana na Wizara, ina Bodi yake ya Wakurugenzi. Nitoe mfano tu kama wa promotion ya Lubumbashi na kuanzisha *liaison office*. Waliona waende na Waziri na Wabunge kwa sababu ya kulifanya suala liwe kubwa na viongozi wa Congo wawepo. Sasa pale hutegemei Wizara ianze kujilipia wakati ni wazo la TPA. Kwa kweli mambo haya naomba tu yaeleweke kwamba hakuna mahali

Nakala ya Mtando (Online Document)

ambapo Wizara imetumia pesa ya TPA bila TPA wenyewe kuhusika na mchakato huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Wizara inahamishia watumishi wake kwenda TPA. Hili ni suala la uelewa tu. Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, mtumishi wa umma, anaweza kuhamishwa au kushikizwa katika Shirika la Umma au Taasisi nyingine za Umma kwa manufaa ya umma kwa kibali cha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, ni kitu cha kawaida kabisa.

Mheshimiwa Waziri Kivuli anadai Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, Bandari ya Dar es Salaam kwamba ni kihyo, hana sifa. Mheshimiwa Machali, nikuombe tena, acha kupata taarifa tu hata kama ni CAG, wewe una nafasi ya kuniona, yeye anapitia bila kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba, mtu huyo anayeongelewa na ambaye mwenzangu akinukuu chochote lazima akinukuu hata kama ni cha miaka mitatu iliyopita. Huyo mtu ametoka Wizara ya Ulinzi, alikuwa ni Mkuu wa Procurement kule, ameshakuwa TANROADS, Mkuu wa Procurement. Tusipake matope watu hivi hivi, tujaribu kufuata taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani anasema injini za meli MV Liemba ni mbovu, zinazimika ikiwa safarini, nafikiri pia ni kusimuliwa, si kweli. Naomba mnielewe, kwa taarifa yako mheshimiwa MV Liemba ilijengwa as a steamship ilipokuja kutoka Ujeruman. Sisi tumekuja kuikarabati upya mwaka 1993, kuondoa kabisa mashine za steam na kuweka mashine za diesel electric mwaka 1993 kama nilivyosema na kuanzia hapo lazima kila miaka kumi ifanyiwe overhaul.

Mheshimiwa Naibu Spika, overhaul ya kwanza imefika mwaka 2004, overhaul ya pili imefanyaika 2010, injini ni nzima, tatizo meli hii ina jenereta nne za kufua umeme. Jenereta moja iliharibika na SUMATRA hawawezi kuruhusu chombo hata kama inapokwenda meli inatumia jenereta moja tu, lakini ikitokea ikazimika baharini, ikazimika na ya pili na ya tatu itatokeaje, ndiyo maana ikasimamishwa. Hata hiyo Kamati ya Ulinzi unayozungumzia ilipitia pale wakati imeshasimamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vimefika, hizo jenereta zimeanza kutengenezwa na SUMATRA watakwenda kujiridhisha kama kweli meli hiyo itafaa kurudi tena baharini. Meli nyingine zitakuja lini, nimeeleza vizuri ukurasa wa 44 na 45 wa hotuba yangu. Tunaanza ujenzi wa meli hizi mwakani kwa Ziwa Victoria, halifu Ziwa Tanganyika; ambalo kutokana na mahitaji ya pale lazima Ziwa Tanganyika pekee lipate meli mbili mpya.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa *ticket fake*, sasa hii ni ngumu, tunaomba tu ushirikiano na wananchi wanaotumia huduma hii. Tukipata taarifa tunachukua hatua. Kati ya Desemba mwaka wa jana na Mwezi Januari tumefukuza vijana wanne kwa ajili ya mambo ya *ticket*, sasa Mheshimiwa naye amekaa na hizo *ticket* badala ya kupeleka Polisi. Sasa uniletee mimi hapa nitajuaje kuzitengeneza mwenyewe. Kwa hiyo naomba tu, ukiona kitu kinatokea chukua hatua hatua hapo hapo, kwanza wewe ndiye Waziri Kivuli wa mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumpatia mfanyabiashara mmoja mjini Arusha eneo la reli. Mimi mwenyewe nimekwenda Arusha, baada ya Mbunge wa Arusha kunishinikiza kweli kweli. Mheshimiwa Lema kanishinikiza sana, nikaenda Arusha, nimeliangalia vizuri suala lile. Ni kweli kuna mtu pale ambaye amepewa kwa mkataba very strict wa miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni eneo ambalo halitumiki, lakini vile vile amesaidia lisije likaporwa na watu wengine na tumekubaliana naye, nikianza kupeleka treni kesho mkataba unakufa. Huo ndio mkataba tuliokuwa nao. Kwa hiyo, haujabinafishwa, haiwezekani chini ya uongozi wangu wa Wizara hii, siwezi kufanya kitu cha klipuuzi kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitoi fedha kwa ajili ya injini za treni mpya na mabehewa, hiyo si kweli. Nimeshaeleza vizuri sana ukurasa wa 14 na 15 kuhusu injini mpya zinazokuja, tunazipokea vizuri tu na nina uhakika mwaka wa kesho tutakuwa na vichwa 51, vitatufanya tuweze kubeba mzigo wa tani milioni moja nukta tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi wanaofanya kazi *TRL* hawalipwi mishahara yao na posho za safari. Nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri aligusia kidogo, lakini naomba tu niseme kwamba si askari peke yao, ni wafanyakazi wote wa *TRL* ambao wamepitia kipindi kigumu kidogo katika muda huu ambao *TRL* imekuwa ikisuasua. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana wafanyakazi wa *TRL* kwa uvumilivu wao, kwa moyo wao wa uzalendo, wamefanya kazi katika mazingira magumu sana, lakini wakiwa na matumaini kwamba hali itabadilika na sasa hivi hali itabadilika; mimi kama Waziri wao nawaahidi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Machali ana taarifa ya kuwepo kwa mvutano kati ya RAHCO na *TRL* kiutendaji, mimi kwa kweli taarifa hizo sina, naomba tu aje na mifano halisi ya mvutano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu, maana yako mengi ambayo yameongelewa, mengine Mheshimiwa Waziri kivuli nitahakikisha unayapata kwa maandishi.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Andrew Chenge, meli kukaa sana outer anchorage, lakini ningependa tu kusema kwamba kwa kweli sasa hivi meli kukaa outer anchorage, ni wastani wa siku moja nukta nane ndiyo imekaa sana, lakini mara nyingi meli inaingia *straight* kwenye berth, efficiency imeongezeka, lakini zipo sababu nyingi zinazosababisha meli kukaa outer anchorage, si kwa ajili tu ya Mamlaka ya Bandari, lakini mara nyingi inakuwa tu kwamba *Shipping Agent* hajakamilisha nyaraka zake husika kuhusu meli kutia nanga, au hajakamilisha malipo ya TRA na TPA na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile upande wa mbele kabisa kule meli nyingi zinakaa pale kwa ajili ya usalama wao tu, wanaogopa kwenda mbali, wakae karibu na nchi iliyo salama na bandari salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia pia Wharfage ni kubwa kupita ya Mombasa, tumelisikiliza hilo kwa makini, ningependa tu kumwambia Mheshimiwa kaka yangu Chenge kwamba kwa hilo tutakaa tena na wataalam wetu tuangalie, wapi sisi ni gharama sana. Tatizo ni kwamba ukiliangalia kwa ujumla la Mombasa wenzetu wana *hidden cost* ambazo zinaifanya Mombasa *to be even more expensive*. Sisi wharfage yetu inategemea CIF value ambayo imekuwa approved na TRA, lakini Mombasa wao ni *flat rate*, ni Dola nane kwa tani moja, inaonekana ni *very cheap*. Lakini wana kitu kinaitwa *terminal charge* ya Dola 70 kwa container, *terminal charge* sisi hatuna. Kwa hiyo ukipiga hesabu sisi tuko *cheaper*. Kwa hiyo may be tu-adopt ya wenzetu ambapo hii ya wenzetu ya kufichaficha ni nzuri zaidi kuliko ya kwetu. Kwa hiyo, tutaliangalia tena tuone *which one is the best method*.

Mheshimiwa Naibu Spika, gati namba 13 na 14 anasema mradi umechelewa sana, miaka 13 tunaongelea. Naomba tu nisisitize kitu kimoja kuhusu gati namba 13 na 14. Wote wakiongea hapa utadhani huu mradi ni wa miaka 13, miaka 20, mimi ninavyojua mradi huu umeibuliwa na TPA 2009/2010 ndipo ulipoanza utekelezaji wake.

Ndugu zangu mara nyingine sisi Watanzania tunajijaji so *harshly*, utafikiri kwamba tumekaa miaka kumi, kumi na tatu, hapana, ni juzi; lakini naelewa kwamba kweli tumechelewa. Tatizo liliojitokeza hapa ni dhamira ya uongozi wa Wizara imetushinda kuendelea na mpango huo. Haiwezekani ukajenga berths mbili kwa Dola milioni ishirini na tano point tatu. haiwezekani, kwa sababu sasa hivi sisi tuko kwenye PPP negotiations na kampuni moja kubwa duniani itakayojenga berths mbili, special berths palepale, special berths sehemu ambayo haikuwa kwenye master plan. Anafanya dredging ya mita 15 kwenda chini na analeta vifaa vyaa kisasa kwa Dola 160,000,000; sina uchungu na hilo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu airport ya Mwanza nimeeleza. Sasa nashindwa kuelewa nianze na lipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdulkarim Shah nafikiri Mheshimiwa Tizeba amemjibu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rita Mlaki, naomba tu nimhakikishie kwamba deni la sh. 133,000,000,000 ndilo linalotusumbua sisi. Serikali inalishughulikia suala hili sasa hivi kwa lengo la kulichukua ili kusafisha mizania ya ATCL, tayari tumeandaa waraka ambao utajadiliwa kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hapa si kununua ndege, wengi hapa, mpaka mwingine anasema tuelewe, hatuoni unanunua ndege. Hakuna anayenunua ndege kama baiskeli, gari au pikipiki. Ndege nikiwa na milioni mbili hapa nitaleta Embraer mpya, ndio utaratibu huo, ndiyo maana nasema, nikiondolewa kiwingu tu cha deni la ATC, deni ambalo lilipatikana kwa njia za ajabu ajabu, deni hilo tu likiondolewa, nitaleta ndege hapa hata tano. Suala si ndege, ukileta leo ndege zitakamatwa na court order.

Ndugu zangu, Mheshimiwa Mbatia anasema tuwe na miradi ya PPP, nasema miradi ya PPP tunayo jamani. Mwambani Port, Bagamoyo Port, Rushungi, Lindi, Kilwa, Dry Port ya Kisarawe, yote hiyo iko kwenye pipeline ni PPP projects.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari mna earn kiasi kiasi gani, ameuliza Mheshimiwa Mbatia. Nimwambie tu kidogo, 2007/2008 Bandari ilikuwa inapata bilioni 165.2 kwa mwaka. Leo hii, niseme 2012/2013 tunapata bilioni 417.4 kwa mwaka, ni ongezeko la asilimia 150.8. Mapato haya hayahusu TICTS, TICTS ni separate, ni TPA tu, TICTS nao wanalipa ile corporate tax independent. Kwa hiyo, tumekuwa vizuri kabisa na tukumbuke mapato ya bandari yanafaidisha watu wengi, sehemu kubwa ya mapato ya TRA yanatokana na efficiency ya bandari. Yameongezeka kwa sababu bandari ni efficient.

Mheshimiwa Naibu Spika, Road Funds. Road Funds kabla hatujaleta mabadiliko pale bandarini walikuwa wanapata bilioni 18 kwa mwezi. Leo ni kati ya bilioni 42 na 50, ni two years. Bandari imefanya vizuri, jamani, mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa maji, hili ni suala ambalo Mheshimiwa Magufuli analifanya kazi vizuri tu kuanzia Bagamoyo, lakini sisi Wizara ya Uchukuzi tuko kwenye PPP projects pamoja na Kampuni ya SS Bakhresa, tunafanya dredging ya kile ki-stretch kinachotoka baada ya daraja hili linalojengwa kuelekea mpaka kule mtoni. Tunafanya dgedging, tutakuwa

Nakala ya Mtando (Online Document)

na meli pale ambayo inachukua abiria kupita chini ya lile daraja. Subirini, mambo mengi ni mazuri tu, lakini yote yanahitaji muda na mipango mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie tu kuhusu Pauline Gekul, Mheshimiwa anatutaka tuweke vipaumbele. Tatizo ni kwamba, Mheshimiwa hakuwepo jana wakati tunasoma hotuba, ndiyo ameingia leo, vipaumbele tunavyo, tuna BRN, ndiyo priority yetu. Ndiyo maana anasema hata reli haipewi fedha, inapewa fedha Mheshimiwa, ndiyo maana nimesema kuna vichwa vingi vinakuja safari hii, utavipanda unavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema Waziri ni mwongo, atatuhadaa, mtanunuaje ndege wakati mnadaiwa. Hapana, wewe nifutie madeni uone ndege nitakazokuwa nazo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Bajaji, zinatozwa sh. 100,000/= huko Babati, nataka nikuhakikishie kwamba hayo ni makosa. Lakini, natanguliza lakini, ya kwamba kijana mwenye pikipiki yake moja kumtoza mapato ni kumuonea, tukafuta, lakini kuna watu nimewagundua huko kwako Babati ana pikipiki 15. Lazima atozwe, ana kipato kikubwa kupita hata mtu mwenye hoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisije nikagongewa kengele ya mwisho. Mengine Waheshimiwa Wabunge tutayajibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makof)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwanyembe, kwa ufanuzi wa maswali mbalimbali yaliyokuwa yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Najua muda hautoshi, lakini tutapata ufanuzi wa ziada kama vile Mheshimiwa Waziri alivyoahidi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza, nitoe ufanuzi kidogo wa Kanuni kuhusiana na matumizi yetu ya utoaji wa shilingi kwenye Mshahara wa Waziri, ambavyo tumekuwa tunakwenda, tunakwenda vizuri, lakini sidhani kama wote tunaelewa nini maana hasa ya neno kutoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri. Kwa sababu kimahesabu, katika mshahara wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

Waziri ukitoa shilingi moja, umetoa nini. Hakuna ulichokitoa, zero point zero sijui ngapi. Haina maana.

Lile neno kutoa shilingi ni neno la Kibunge lenye maana Fulani, lenye ujumbe fulani. Katika Bunge fulani lililopita tuliwahi kufanya ziara mimi, Mheshimiwa Mwakyembe na baadhi ya Wabunge wengine. Tukaenda baadhi ya nchi za Commonwealth tukakuta hiki kitu.

Kutoa shilingi na ndiyo maana inakuwa kwenye mshahara wa Waziri, wakati huu wa Bajeti ni kwa jambo la kisera. Kwa jambo kubwa, siyo nafasi ya kubishana ili upate nafasi ya kusikika. Kurudia tena kusema na kusema. Huwa ni kwa jambo kubwa, ni demokrasia, unawesa ukaitumia hilo kutaka kusema na kusema ili usikike, lakini nataka kusema matumizi ya neno hilo hasa maana yake ni nini.

Ni kwa jambo kubwa la Kisera, jambo ambalo lina msisitizo wa kipekee na ikitokea Wabunge wote wakakukubalia wewe Mbunge mmoja. Maelezo yako, wakatoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri. Mantiki yake ni kwamba katika baadhi ya nchi, Waziri huyo anapaswa kujuzulu. Kwa sababu hiyo maana yake ni kwamba Bunge halina imani na huyo Waziri. Hiyo ndiyo falsafa yenyewe ya neno kutoa snilingi. Kwa hiyo, hata tunapopiga kura, kuna ile kupiga kwa kuhoji, Ndiyo, Siyo. Yaani bila kujua, halafu yaktokea mambo fulani fulani baadaye, mtu anaanza kusema mimi sikuwemo na kutoa visingizio mbalimbali.

Kwa hiyo, kutoa shilingi ni jambo zito, hukazwi Mbunge ye yote yule, lakini ni jambo la msingi sana na tujue repercussion zake, maaana yake hata katika historia ya Bunge letu, inaingia kwamba wakati fulani kwenye shilingi ili wahi kutolewa katika mshahara wa Waziri fulani.

Baada ya maelezo hayo, naomba tuendelee.

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi

Kif 1001 – Administration and Human
Resource Management... ... Sh. 3,379,433,400/=

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nijadili hoja ambayo nilizungumza katika mchango wangu wa maandishi na nilizungumza katika mchango wangu wa kuzungumza, lakini Mheshimiwa hajanipatia majibu yoyote wala Naibu Waziri. Kwa hiyo, niombe basi kupata ufanuzi wa kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusiana na mgogoro, uliondelea kwa muda wa miaka 17, kati ya wananchi wa Vijiji vya

Nakala ya Mtando (Online Document)

Sanya Station, Tindigani, Hundugai, Mtakuja, Chemka na Chekimaji, katika Kata ya Masama Hundugai, na Kata ya Kia katika Wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro, kuhusiana na mgogoro wa ardhi. Ardhi ambayo ilikuwa imepimwa na kuwa ardhi ya vijiji nilivivotaja mahali hapa, ikiwa inahusisha wananchi zaidi ya 10,000. Ardhi yenye kilomita za mraba 101, ambazo zilisemekana zilitengwa kwa sababu ya kuuendeleza Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo limekuwa ni tatizo kubwa mno ambalo linaleta usumbufu sana kwa utawala wa Serikali ndani ya Wilaya ya Hai na hata katika Mkoa wa Kilimanjaro. Tumekaa vikao vingi ili kujaribu kutatua hili tatizo. Mheshimiwa Waziri nimezungumza naye kwa muda mrefu na wako Mawaziri wengine kadhaa wa awamu zilizopita, ambao walishughulikia suala hili na hawakulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi nimwombe Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, ambaye nina hakika analifahamu suala hili, atoe basi kauli yake ya Kiserikali ili tujue tunamaliza vipi mgogoro huu ambao kweli umedumu kwa muda mrefu sana. Nina hakika kama akitaka tulifanyie kazi ya ziada na tukalimaliza na tukaleta amani kwa wananchi wale ambao wanakwazika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie na kama sitaridhika nitawaomba Wabunge wenzangu wanisaidie tujadili jambo hili, kwa sababu ni jambo ambalo linawagusa wananchi wengi bila sababu ya msingi. Hili ni jambo ambalo nina hakika tunaweza tukalimaliza kama Serikali ikiwa na nia ya dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu ya msingi, nilitoa hata mifano nikasema, kwa uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, unachukua eneo ambalo halifiki kilomita nne za mraba, lakini kwa uwanja ya KIA, kutengewa kilomita 101 za mraba ni rekodi ya dunia. Hakuna *Airport* yoyote duniani ambayo imetengewa eneo kubwa kama hilo la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matokeo yake ni kwamba, kama ile ardhi, ingekuwa haina kazi sawa, matokeo yake wananchi wanafukuzwa, hawaruhusiwi kuijiendeleza, wala kuendeleza eneo lile na awali hilo eneo lilishapimwa kwa ajili ya matumizi ya vijiji na wananchi walikuwa wanalima katika maeneo ikiwa ni pamoja na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi alitolee kauli. Ahsante. (Makofij)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili, ilinilazimu niende mpaka Mkoa wa Kilimanjaro, bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge hakuwepo, alikuwa na shughuli zingine, ikanikalisha pale siku mbili. Nilielewa vizuri sana, ikapelekea mpaka Wizara ya Uchukuzi ikaunda Kikosi Kazi (Taskforce), kwa ajili ya kuhakiki mipaka na kuelewa source ya tatizo na kum-advice Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tumeshakamilisha zoezi hilo, Mheshimiwa Mbunge nafikiri na wananchi pale, ikatokea tena process ya pili ambapo ilihusisha hata Uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro, ambao nao umeunda Tume nydingine, nao wamefanya hiyo kazi. Tumeona sasa badala ya kuleta confusion, mimi natoa tamko na uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro unatoa mengine. Niliona siyo vizuri, kwa hiyo, nimewaomba Mkoa wa Kilimanjaro wakikamilisha zoezi lao ndani ya mwezi huu ujao, wanitaarifu niweze kukaa chini na uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro, akiwepo Mheshimiwa Mbunge, ili tulimalize hili suala, kwa sababu hakuna haja ya kuendelea kuvutana na wananchi kwenye suala ambalo linaleweka.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maeleo yake. Wakati tunaendelea na Bunge Maalum la Katiba, tulipata ujumbe wa wananchi zaidi ya 40 waliokuja kutoka Wilayani Hai na walipata fursa ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Lukuvi, waliokuwa wamekuja hapa wakiwa na kilio chao cha kwamba tatizo lao linashindwa kutatuliwa katika ngazi ya mkoa. Nina hakika Serikali, kupitia kwa Mheshimiwa Lukuvi, walifanya mawasiliano na huo Uongozi wa Mkoa na Serikali ikatoa ahadi kwamba itatoa majibu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anachokizungumza Mheshimiwa Mwakyembe, sina hakika ndicho hicho alichokizungumza Mheshimiwa Lukuvi kwa niaba ya Waziri Mkuu, ambaye ndiye alikuwa ameombwa asikilize kile kilio cha wananchi wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mvutano ambao ulionekana dhahiri ulikuwa unapelekea kuchochera, kukamata lile eneo la wananchi na katika mazingira ambayo haikujulikana ni nani anayetakiwa apewe ile ardhi ya kilomita 101 za mraba. Sasa naomba Mheshimiwa Mwakyembe au pengine Mheshimiwa Lukuvi atawezu kunisaidia hapo, tunalimaliza lini hili tatizo? Kwa sababu kama nilivyosema limekwenda kwa miaka 17 bila sababu zozote za msingi. Ni jambo ambalo nina haki kwamba Serikali ingekuwa na nia njema tungelimaliza mapema tu, wala sioni kwamba kuna sababu ya kuwataabisha wale wananchi kwa kiwango kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa sana kuingia kwenye kushika shilingi za Mheshimiwa Waziri, kwa sababu sijakosa imani na Waziri wa Uchukuzi.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Nina hakika yeye na wengine wakiamua kulimaliza hili tatizo wataweza kulimaliza. Kwa kweli sielewi ni kwa nini kunakuwa na delay kama hizi ambazo hazina sababu ya msingi. Kwa kuwa sijaona sababu yake kwa uwanja kutengewa kilomita 101 za mraba, dunia nzima hicho kitu hakuna. Sasa kwa nini tunataka kuweka record za dunia katika sehemu hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA URATIBU NA BUNGE):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli aliyosema Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Kamati ya Wizara ilikwisha jitahidi ikaenda mpaka Mkoani na Mkoani walikwenda mpaka kwenye site wakachukua hatua, ambazo wale wananchi hawakuzielewa na hawakuzipenda.

Baadaye hiyo delegation ikiongozwa na Madiwani wa Chama cha Mapinduzi, walikuja hapa kumwona Waziri Mkoo na Waziri Mkoo, ni kweli alinipa fursa nikakutana nao. Bahati mbaya wakati nakutana nao, Mheshimiwa Waziri mwenye sekta alikuwa nje ya nchi, lakini tuliwasiliana na Katibu Mkoo na kwa ufupi naomba niseme kwamba, tunayo taarifa ya awali kutoka Wizarani ambayo Katibu Mkoo alimwandikia Katibu Mkoo wetu. Lakinimaelekezo ya Waziri Mkoo, maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkoo, ndiyo yaliyochelewesha hii Timu. Maana yake hii Timu ingekuwa imeshamaliza kazi mpaka mwezi huu wa Mei, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waziri Mkoo alielekeza katika ile Timu ni lazima awepo mtumishi wa CHFC na lazima awepo Msajili wa Hazina na mimi mwenyewe nilizungumza wakati ule na Msajili wa Hazina, alikuwa Malawi, tukakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa Wizara ya Uchukuzi chini ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, imebidi waunde timu mpya ya kuwaunganisha mtumishi wa CHFC na Msajili wa Hazina. Nina uhakika wa maandisi kwamba timu hii imeundwa sasa iko tayari kwenda kufanya kazi ili kutatua ule mgogoro. Hatua ambazo Mkoo wa Mkoa alikuwa anataka kuzichukua za kuweka mapipa katika maeneo hayo, tulimsimamisha ili tuwe na timu moja tu. Kwa hiyo, timu inayokwenda ni ya Wizara ya Fedha ambayo itaunganisha Wizara ya Fedha kwa maana ya CHFC na Msajili na kwa sababu sasa walikuwa wameagizwa na Waziri Mkoo, baada ya hapo watatoa taarifa kwa Mheshimiwa Waziri Mkoo juu ya mapendekezo ya hatua ya kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumshawishi Mheshimiwa Mboge kwamba Serikali ni moja, jambo hili limeshapanda ngazi liko kwa Mheshimiwa Waziri Mkoo, anashirikiana na Wizara zote ndani ya Serikali,

Nakala ya Mtando (Online Document)

ambazo zinahusika na jambo hili, maana yake alijua kwamba mwenye mali ni Msajili, ukimuacha nyuma Msajili jambo hili kwa Wizara peke yake itakuwa tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka aendelee kumwamini Waziri Mkuu kama alivyomwamini kwamba jambo hili litakwisha.

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Mheshimiwa Andrew Chenge!

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Wakati nachangia asubuhi ya leo kuhusiana na eneo la upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, nilisema nasikitishwa kidogo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Kiwanja hiki muhimu katika ukanda huo, lakini kubwa zaidi kwa sababu ndiyo tunategemea katika ukanda wa Maziwa Makuu, kama kitovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema, iwapo sitapata maelezo ya kutosha kutoka Serikalini, nitatoa shilingi. Nimemsikilzia kwa heshima sana Mheshimiwa Mwakyembe, yeye kalielezea vizuri tu, lakini ninapoongea hapa naongea kuhoji dhamira ya Serikali, kwa Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu una historia, Benki ya BADEA, ambayo iliji-commit ina component ndogo ya Dola za Marekani milioni 12, lakini Serikali ilifahamu kwamba ina mchango mkubwa wa takriban bilioni kama shilingi bilioni kama 85, kugharamia kiwanja hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi 2012/2013, Serikali imeweka saini na Mkandarasi wa ujenzi kwa kipindi cha miaka mitatu. Tulisikia taarifa ya Kamati ya kisekta, ikielezea mtiririko wa utoaji wa fedha hadi sasa, kusema kweli ni kama vichekesho tu. Ni kama Serikali haitaki mradi huu utekelezwe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu, Serikali ilikuwa imeahidi sh. 8,000,000,000/=, lakini mpaka sasa hivi Serikali imetoa shilingi bilioni 1.6. Sasa tunajiulizia, hivi Serikali wanataka tuseme nini zaidi, kwamba ukanda huo tunafanyiwa hivyo kwa sababu, kwa sababu, kwa sababu...

MBUNGE FULANI: Hakusikika.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo fulani, nadhani kama tunaanzisha miradi kwa nia njema, kwa kweli dhamira yetu ioneshe kwamba tunataka kutekeleza Miradi hii. Sasa napenda sana Serikali hasa kupitia Wizara ya Fedha, watueleze kigugumizi cha kutoa fedha kwa mradi huu, ni kipi au kiko wapi?

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki sana kumwonea Mheshimiwa Waziri Mwakyembe kwani kile anachoomba ndicho anachopewa. Sasa wale ambao wanaona hawakuwa na sababu ya msingi ya kuanza kutafuta fedha kama Tanzania mchango wake kwa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza basi watueleze, nasema Serikali ni moja na naamini watasikiliza, kwa hiyo, kama sipati maelezo ya kutosheleza kusudio langu la kutoa shilingi bado lipo palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Dkt. Tizeba!

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uwanja wa ndege wa Mwanza una historia mpaka hapa tulipofikia, usanifu wa kwanza wa huo uwanja ulifanyika mwaka 2002 na miaka ile ndipo makadirio ya gharama ya ujenzi yalipotolewa, wakati ule Mwanza abiria walikuwa wachache sana na kwa hiyo hata usanifu uliokuwa umefanyika ulikuwa kwa abiria wachache hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BADEA na OFID walikuwa wame-offer msaada wa dola milioni 12 wakiwa wamegawana lakini OFID wakasema wao management ya huo mchango wao wanawaachia BADEA. Sasa ikatokea mradi hauanzi kwa sababu bajeti ilikuwa haitoshelezi kwa local component kuanzisha ujenzi. Miaka mingi imepita mpaka mwaka 2012 tulipofikia uamuzi kwamba, sasa ni lazima tuanze, kwa sababu tukikaa mpaka fedha yote ya kujenga uwanja ipatikane uwanja usingeanza kujengwa, tukafanya tu uamuzi mgumu kwamba tuingie mkataba tuanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzenetu wakatoa fedha kidogo, lakini kwa sababu ya muda mrefu kupita, tangu usanifu wa awali ufanyike, kwa hiyo, gharama na kila kitu vilikuwa vimebadilika. Wakandarasi walivyokuja kuomba hiyo kazi, Mkandarasi wa chini aliyepatikana ndiye huyo akafikia kiwango cha bilioni 105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anajibu hoja Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba kati ya hizo dola hizi bilioni 12 au 14 ni sawa na shilingi bilioni 20 tu kati ya shilingi bilioni 105 ambazo zingehitajika kwa mchoro ule kutekeleza yale yaliyokuwa yanatakiwa pale. Kwa hiyo, Serikali ikawa na wajibu wa kuchangia katika ujenzi shilingi bilioni karibu 89. Mkandarasi alipewa advance akaanza kazi.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu zilikuwa zimetengwa bilioni nane, ni sahihi kabisa anavyosema Mheshimiwa Chenge na mpaka sasa imetolewa shilingi bilioni 1.6, mwaka haujafika mwisho, mwaka wa fedha wa Serikali haujafika mwisho. Hivyo, namwomba sana Mheshimiwa Chenge atuelewe, nadhani ni mdau namba sifuri kama namba moja anapatikana atakuwa ananifuatia mimi kwa suala la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunachosema ni kwamba, mwisho wa bajeti hiyo ya bilioni nane ni tarehe 31 Juni, Serikali hii kama alivyosema ni moja, Wabunge wengi wamechangia hapa wakizungumzia uwanja wa ndege wa Mwanza, ni concern ya kila mtu *including the Government itself*.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba *by that time* tutakuwa tumeona kwa sababu *chunk* ya mwisho ya *displacement* kutoka Hazina kwenda kwenye Wizara haijatolewa na tunatarajia kwamba tutapata fedha hizi zilizokua zimesalia kwa mwaka huu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge!

MHE. ANDREW J. CHENG: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelezo ya Mheshimiwa Dkt. Tizeba, lakini hayajanitosheleza na kwa maana hiyo natoa shilingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba Serikali ni moja, Wizara ya Uchukuzi ni chombo tu cha Serikali katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Serikali imesema bado leo tupo mwisho mwisho wa mwezi wa Tano mwaka wa fedha unakwisha mwezi ujao tarehe 30, Juni. Nilitegemea kwamba Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kama wana nia njema, angalau wangesema kwa fedha iliyobaki basi kwa mwaka huu wa fedha na kwa kutambua uzito wa suala hili kwamba inatoa *commitment* ya kuzitoa fedha zote shilingi bilioni 6.4, nadhani tungekuwa tunaanza mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inataka kunipaka mafuta kwa kutumia mgongo wa chupa, hilo kidogo nalionia ni gumu kwangu na naomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa hili hasa Wabunge tunaotoka ukanda huo tuelewe, ni vizuri kabisa kwa sababu mengine sikutaka kuyasema, kwa sababu nasema nimekuwa katika Wizara hiyo katika kipindi fulani. Ni vizuri tu Serikali ikatuambia katika mpango wake kwa sababu tangu mwanzo tulijua kwamba *commitment* ya BADEA ilikuwa ni ndogo na tulitegemea kwamba kufika sasa tulipochukua uamuzi wa kuanza ujenzi wa upanuzi wa kiwanja hiki, tungekuwa sasa tumeona maeneo mengine ambapo tumekwenda kupiga hodi, kuweza kupata fedha za upanuzi wa uwanja huu muhimu, lakini hatuoni dalili hiyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema hivyo ni kwamba, katika kipindi hiki ambacho tunacho, tuna miradi mingi ambayo Serikali isipojipanga vizuri, tutakuwa tunapoteza nguvu za walipa kodi wa nchi hii na jasho lao bila miradi hiyo kukamilika na mmojawapo ni huu mradi wa Mwanza na sisi tusingependa tulione hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini baada ya kusimama na kuiomba Serikali kwa heshima zote kabisa na wanani fahamu, mara nyingi huwa sipendi sana kusimama na nikisimama nina sababu. Kwa hiyo, nawaomba sana tufike mahali pazuri na suala hili, Serikali angalau, nasema angalau itupati commitment kwa mwaka huu ili ziweze kupatikana zile shilingi bilioni 6.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuuru!

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Serukamba!

WABUNGE FULANI: Ichangiwe kwanza.

MWENYEKITI: Ichangiwe kwanza halafu Waziri, halafu inarudi tena kwa mto a hoja.

Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Lolesia, nadhani wanne hao wametosha, kwani orodha ni kubwa sana, kipekee Mzee Cheyo!

Mheshimiwa Serukamba, dakika moja moja itasaidia!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na tumeisema kama Kamati, mkataba huu ni wa bilioni 105. Katika bilioni 105, tuna bilioni 20 za BADEA maana yake zilizobaki ni bilioni 85.

Mwaka wa kwanza tulitoa bilioni nane maana yake zimebakia 78, mwaka wa pili zimetoka 1.6, lakini mkataba huu ni wa miaka mitatu na mwaka kesho bilioni 12 . Kwa hiyo, maana yake hapa huu uwanja wa Mwanza unakwisha baada ya miaka 10 ijayo na kama ni baada ya miaka 10 ijayo nani atalipa hizo interest?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba angalau hizo bilioni 6.5 zilizobaki zitoke na nadhani Mheshimiwa Dkt. Tizeba amesema zitatoka mpaka tarehe 30, ni matumaini yetu litafanyika hilo, lakini tukubaliane kwamba za mwaka kesho hizo tunamaliza lini kwa sababu tunataka kazi hii iishe baada ya miaka mitatu.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Ndassa!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, katika maelezo yake anasema, wanafanya mazungumzo na Exim Bank, wanafanya mazungumzo, halafu akasema tukipata pesa, isipopatikana hakuna uwanja? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi aliyeko site sasa amesha-raise certificate nne, anadai bilioni 15, Mhandisi Mshauri anadai bilioni 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Chenge, shilingi tuondoke nayo, lakini tunataka uwanja wa Mwanza ujengwe haraka pesa zitoke. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Wenje!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Contract period mradi huu ulivyoanza mwaka 2012/2013 ilikuwa ni miaka mitatu, tunapoendelea kuchelewa maana yake ghamama ya contract inaongezeka. Sasa kama mwaka wa fedha 2013/2014 zilitengwa shilingi bilioni nane mpaka sasa zimeshalipwa shilingi bilioni 1.6 ni asilimia ndogo sana, halafu mwaka wa fedha ndiyo unakwisha hivi, halafu Mheshimiwa Waziri anatuambia hizi wiki tatu zilizobaki ndiyo atapeleka percentage kubwa iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji commitment ya Serikali, watuambie hapa kwamba, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza utakwisha lini? Yaani watupe specific time kwamba ni lini mradi huu utakwisha, *that is what we want!* Tunahitaji commitment ya Serikali!

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba!

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Uwanja wa Mwanza ni kwa kipindi kirefu sana tumekuwa tukizungumzia kupanua uwanja huu. Mimi binafsi nilikuwa kwenye Kamati ya Miundombinu kuanzia mwaka 2010 mpaka 2013 na mara kwa mara tulikuwa tunazungumzia suala hili, lakini mpaka sasa naona hakuna mwelekeo wowote kwa suala hili la upanuzi wa kiwanja cha Mwanza.

Kwa hiyo, naungana sana na Mheshimiwa Chenge kwa jinsi alivyosema, tuombe commitment ya Serikali katika suala hili kwa sababu ni muda mrefu sana suala hili kwa kweli halitekelezeki. Pia kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ni kweli kabisa kwamba utoaji wa hizi fedha hauendi sawasawa.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Kwa hiyo, naomba suala hili lipelekwe kwenye Kamati ya Bajeti ili waone namna ya kuweza kurekebisha ili tuweze kupata fedha zaidi kwa ajili ya kuweza kujenga kiwanja hiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na sasa ni Mheshimiwa John Cheyo, mchangiaji wa mwisho!

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namuunga mkono Mheshimiwa Chenge, najua alikuwa amekasirika na ameshindwa kusema ni kwa nini mnafanya hivyo, ni kwa sababu sisi ni Sasa akashindwa kumalizia, ni kwa sababu sisi ni Wasukuma ndiyo tunajua, ndiyo mnafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili najua halina msingi kwa sababu hatugawi fedha ya maendeleo kwa misingi ya Makabila, lakini hisia ukiona mambo yanayokwenda kwa uwanja wa Mwanza unapata hisia za namna hiyo. Ukiona unajenga barabara Mwigumbi mpaka Lamadi miaka 10 unapata hisia za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kama mradi ni 105, kwanza za mwaka unaomalizika bilioni sita, ni aibu hata kuzungumza juu ya bilioni sita, kwa mradi wa bilioni 105. Pili, kama mradi ni wa miaka mitatu, 105 lazima ziwe also referred katika bajeti, bajeti sasa imeweka bilioni 12, ndiyo kusema mwanzoni Waziri hana nia ya kuonesha kwamba mwaka kesho atajenga huo mradi. Nafikiri labda hata hiyo bajeti yenyewe mngeileta tuizungumze hata kwenye Kamati ya Bajeti pamoja na ku-declare interest kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo, lakini niwatoe wasiwasi watani zangu Wasukuma kwamba, kama Dodoma tungkuwa tumepewa fedha za kujenga uwanja wa ndege mngelalamika, lakini sasa ndiyo hatuna kabisa, sasa ninyi mnalalamika kitu gani?

Mheshimiwa Waziri wa Fedha!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kuonesha uchungu wa suala hili na naelewa how he feels!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kumhakikisha kwamba Serikali nia ya kujenga uwanja wa ndege wa Mwanza na pengine *the best proposal* ambayo tungefanya kwa sasa hivi ni kwamba, labda kesho tu, tukae pamoja na Wizara yaani sisi Hazina pamoja na Wizara ya Fedha, lakini kwa kumshirikisha

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mwenyekiti mwenyewe wa Kamati ya Bajeti kuangalia possibility ya kumaliza hii *6.4 billion before the end of this financial year*, lakini vilevile tu kumpa proposal nyingine ambazo tutaweza kuendelea kutekeleza miradi hii katika miradi yetu ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili tulifanye *immediate*, nimeona karibu Waheshimiwa wote wamesimama na wameonesha uchungu. Hatuna nia mbaya hii ni nchi yetu wote na Mwanza ni kiwanja ambacho nadhani kimepata *statistics za watu karibu one-third of the population, it is very important*.

Kwa hiyo, nataka kutoa hiyo *commitment kwamba, tutakaa pamoja sisi na Wizara ya Uchukuzi pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili kupitia mafungu na kuona tuta-disburse* *vipi hizi 6.4 billion.* (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chenge, kwa kifupi!

MHE. ANDREW J. CHENG: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa maeleo yake na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamesimama na kuunga mkono hoja hii ya kutoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeleo ya Mheshimiwa Waziri yanatoa matumaini, nasema mawili; la kwanza, pendekezo la kukutana Serikali na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ni zuri, lakini nasema tukutane na Serikali na Kamati ya Bajeti, tuone kama tunaweza tukafika mahali pazuri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni vema Serikali ikaanza kuangalia tuwe na mpango mzuri baada ya mwaka ujao wa fedha pamoja na gharama ambazo Serikali itabidi igharamie, tunakwendaje mbele ya safari katika kukamilisha *financing* ya mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru wewe, niwashukuru Wabunge wenzangu Wajumbe wa Kamati ya Matumizi kwa kunisikiliza na natamka kwamba narejesha shilingi katika fungu hili.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla!

MHE. DKT. HAMIS ANDREA KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesimama hapa kuzungumzia suala la uchukuzi kwenye Jiji la Dar es Salaam hususani migogoro iliyopo kwenye Shirika la Usafiri Dar es Salaam yaani UDA na namna ambavyo imekuwa ikiathiri utekelezaji wa shughuli za usafirishaji unaofanywa na Shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu kumekuwa na kauli tata mara nyingi na Kamati yangu kwa kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina *interest* kwenye shirika hili ya 24.21% ilifanya kazi ya kulisikiliza kwa kina, ikawaita CHC, ikamwita Msajili wa Hazina, ikawaita Jiji, ikawaita Wabunge wa Dar es Salaam na tukakaa kwa pamoja hapa Dodoma. Pia na washauri kama KPMG wakawepo na CAG akawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukalizungumza suala hili na tukatoa mapendekezo ambayo tulidhani yana maslahi mapana kwa Taifa letu na Shirika kwa ujumla wake. Tulitoa mapendekezo mbalimbali yakaletwa ndani ya Bunge, yakajadiliwa na hatimaye ikabainika kwamba, mwekezaji aliyeingia katika Shirika hili ana haki ya kuendelea kuendesha Shirika hilo na kutumia assets mbalimbali ili kuweza kuliendeleza Shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa majibu yanayoendelea hapa yanaonesha kwamba hata yale maazimio yaliyotolewa na Kamati ya TAMISEMI yakapitishwa na Bunge zima, sasa yanaanza kudharaulika na hayatekelezeki kutokana na kauli iliyotolewa hapa na Naibu Waziri wa Fedha kwamba, Shirika lile halimilikiwi na huyo mwekezaji ambaye amelinunua kwa kiasi kikubwa, zaidi ya asilimia 76. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipatiwe ufanuzi, hii ni mikakati...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, Manaibu Waziri wa Fedha ni wawili; sijui ni yupi unayem-refer hasa!

MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA: Alikuwa ni Ndugu Adam Kigoma Malima, siku ya Mei 15.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina lengo la kutoa Shilingi, lakini nimesimama ili tu kupata ufanuzi: Je, usafirishaji katika jiji la Dar es Salaam siyo jukumu la Uchukuzi ambalo linapaswa kusimamiwa na kuwezeshwa na Serikali yetu? Ama ni kwa vile huyu mwekezaji ni mtu mweusi ndiyo maana ananyanyasika? Au kuna sababu gani nyingine ambazo zimejificha? (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kigwangala, ahsante sana. Muda hauko upande wetu. Mheshimiwa Malima naona unataka kusimama!

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Kigwangalla, amezungumza mambo mengi sana, lakini kimsingi alivyoanza kujenga hoja ni jambo ambalo halihusu Wizara ya Uchukuzi. Habari ya umiliki wa UDA ni suala kati ya CHC, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na huyo bwana mwingine. Sisi shughuli yetu ni service yenyeche ya uchukuzi, yaani huduma ya uchukuzi. Nani anamiliki yale mabasi, ni suala la wenyewe hisa katika hiyo Kampuni. (Makofii)

Kwa hiyo, kama swali ni: Tunashughulikia vipi usafiri na uchukuzi ndani ya Jiji? Wizara ina-co-ordinate, inaratibu juhudhi za Taasisi na Wizara mbalimbali namna bora ya kuendesha shughuli za uchukuzi na usafirishaji katika Jiji la Dar es Salaam. Ndiyo maana tuliiingia hata katika kuwaambia TRL waanzishe usafiri wa treni kati ya Stesheni na Ubungo Maziwa; TAZARA waanzishe usafiri kati ya Mwakanga na TAZARA. Hizo zote ni jitihada za Wizara kuhakikisha kwamba usafiri mjini Dar es Salaam unakuwa mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ipo Kamati ambayo mimi ni Mwenyekiti wa kuangalia Taasisi mbalimbali na wadau mbalimbali wa uchukuzi Jijini Dar es Salaam wanafanya kazi. Kwa kweli niseme Serikali kwa maana ya habari ya uchukuzi Dar es Salaam, inasaidia, inawezesha, yenyeche inaingiza fedha ili kuhakikisha kwamba usafiri Dar es Salaam unakuwa mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la UDA kwamba nani anamiliki? Namwomba tu Mheshimiwa Kigwangalla asubirie Wizara husika itakapofika aweke hilo suala mbele ye Wizara yenyeche.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Nilivyomwelewa Mheshimiwa Kigwangalla, suala lake hakulitupa kwenu as such, lakini kwa vile Serikali ni moja, alimlenga zaidi Naibu Waziri wa Fedha na amemtaja kwa jina. Sijui kama unakumbuka hilo jibu ambalo linaleta hii confusion! Tafadhali, kama una cha kusema Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wa Fedha!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mheshimiwa Kigwangalla, lakini nadhani siku ile hakuelewa majibu tuliyoyasema. Tulichosema siku ile ni kwamba UDA ni Taasisi ambayo ilikuwa inamiliikiwa na Serikali na katika hisa zake zilikuwa za makundi mawili. Kulikuwa na *allotted shares* ambazo zilikuwa ni hisa zinazomilikiwa na Serikali kwa maana ya Msajili wa Hazina, kwa nafasi nyingine zilikuwa zinamiliikiwa na Halmashauri ya Jiji. Zipo hisa nyingine ambazo zilikuwa hazina mwenye hisa, zilikuwa ni *unallotted shares*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulichosema ni kwamba, baada ya muda, akatokea mtu pale anasema na yeye ana hisa za UDA. Serikali inasema wewe upo katika taratibu hii, kakuleta nani? Unasema nimeuziwa hisa na Halmashauri ya Jiji. Serikali inasema, hizo hisa ulizouziwa, *mind you!* Wanasema, katika hisa hizo nilizokuwanzo mimi, sasa nina asilimia 76 wakati umiliki wetu sisi Serikali na Halmashauri ya Jiji ilikuwa asilimia 49 kwa 51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali linakuja, mwenzetu umepenyapenya huko, kakuingiza nani? Maana jambo hili ni la watu wawili, wanahisa wawili; sisi hatukushiriki kwenye kukuingiza wewe kwenye hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye historia hii, pamoja na kwamba naheshimu kwamba Kamati yako ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imefanya kazi, iko Kamati nyingine ya Fedha, iko nyingine ya LAAC; zote ni Kamati za Bunge na zote zimekaa hivi sasa kufanya tathmini suala hili. Kwa sababu suala linakuja kwamba, wewe unamiliiki hisa za Serikali, hisa za Serikali hazitoki isipokuwa Msajili wa Hazina azitoe na Baraza la Mawaziri liridhie. Hisa za Serikali hazitoki kwa kusema tu kwamba nimetoa hisa kama sambusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichosema ni kwamba, kwa sababu hatuna maelezo ya wapi Serikali na lini iliridhia kutoa hisa hizi, lakini kwa sababu kwenye maelezo yale, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Msajili wa Hazina, wote wawili hawana kumbukumbu ya lini mimi nilitoa hisa kukukabidhi wewe; nasema kwa sasa hivi, mpaka utakaponiletea ushahidi. Hisa za Serikali zinabaki kama zilivyokuwa na hisa za wananchi kwa maana ya zile za Jiji zinabaki kama zilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ndilo jibu letu nilivyosema siku ile. Lakini kama Mheshimiwa Kigwangalla kwa niaba ya Simon Group, ana ushahidi wa kuonesha kwamba hisa za Serikali zilitoka, basi nazo ziletwe, halafu tutaendelea na utaratibu, kwa sababu Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi haina nia ya kumnyima mtu haki yake. (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! Naomba nitoe taarifa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kangi Lugola, taarifa ya nini?

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba ku-declare *interest* kwamba mimi nimefanya kazi kwenye Wizara ya Uchukuzi, nilikuwa Mkuu wa Usalama wa Viwanja vya Ndege nchi nzima. (Makofij)

MBUNGE FULANI: Kweli! (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Tizeba na Mheshimiwa Mwakyembe ninayemheshimu sana, ni Mwalimu wangu wa Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kusema kwamba Wizara yake haihusiki na jambo la UDA, nataka nimpe taarifa fupi tu; na ninasikitika kwamba kama leo asubuhi amewatambulisha madereva wa malori makubwa, lakini hapa anasema hahusiki na mwekezaji anayeshughulika na usafiri Dar es Salaam, mimi nasikitika. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisome barua hii ili kuonesha kuna mahusiano gani ya Wizara ya Uchukuzi na Shirika la UDA. Kuna barua ya tarehe 11 Mei, 2010 ambayo iliandikwa kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, iliyandoikwa na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, kwenda kwa Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa, wakati ule akiwa ni Waziri wa Miundombinu ambapo Wizara ya Uchukuzi ilikuwa.

Anamwambia hivi, yahusu Mapendelekezo ya Bodi ya UDA juu ya uuzwaji wa hisa asilimia 49 za Serikali inazomiliki UDA kwa mwekezaji Simon Group Ltd.

Nimepokea barua Kumb. Na. UDA/T20/3 ya tarehe 10 Mei, 2010 ambayo yajieleza yenyewe. Anamwambia Uchukuzi; kama Wizara yako haina matatizo na mapendelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi wa UDA na kama nia ni kuiinusuru Kampuni ya UDA na kuleta nafuu katika usafiri wa mabasi ndani ya Jiji la Dar es Salaam, Wizara ya Fedha na Uchumi, haitakuwa na kipingamizi na mpango unaopendekezwa na Bodi hiyo. (Makofij)

Nashauri Wizara yako, (yaani anaishauri Wizara ya Uchukuzi) iandae Waraka wa Baraza la Mawaziri ili kupata kibali cha Serikali cha kutekeleza azma hiyo (yaani azma ya kuza hisa). Wataalamu wa Wizara yangu wanaweza kutoa *inputs* zozote zitakazohitajika katika maandalizi ya Waraka huo.

MWENYEKITI: Ahsante, naomba umalizie taarifa iwe fupi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya Simon Group anakwenda TAMISEMI, anatoka; anakwenda Kamati ya Kudumu Bunge ya TAMISEMI, anatoka; anakwenda Uchukuzi anaambiwa hatukujui; wanamchezeshesha kama Joyce wowowo kwa wimbo ule wa Indemoni. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Simon Group hana namna ya kufika hapa na yeye akasema, naomba jambo hili, kwa sababu kuna nyaraka; mimi nilizipata nikiwa bado mjumbe wa POAC, tukamaliza jambo hili, lakini baadaye Mheshimiwa Adam Malima ninayemheshimu sana, nadhani alipotoshwa au alishauriwa vibaya ndiyo akasema kwamba Simon Group siyo mmiliki halali wa Kampuni ya UDA wakati anamiliki hisa ambazo kuna mikataba hapa tuliyokutana nayo, ambayo imesainiwa na Wanasheria na Wizara zinazohusika, akina Musera, akina Mwakibinga wanajua jambo hili. Sasa nashangaa kwamba taarifa muhimu kama hii wanasema Simon Group hatumjui.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kangi Lugola.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kigwangalla, tafadhali tuendelee na utaratibu. Mheshimiwa Kigwangalla, kidogo, halafu Mheshimiwa Waziri nitakupa nafasi.

MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kutokana na mkanganyiko huu na kutokana na uwepo wa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hii ya Matumizi, kuwa na taarifa mbalimbali kama ilivyodhihirika kwa Ndugu Kangi Lugola, naomba nitumie fursa ya kikanuni kutoa hoja ya kuondoa Shilingi kwenye Mshahara wa Waziri ili tupate fursa kwa Wabunge wengi zaidi kulijadili jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja hiyo kwa misingi tu kwamba taarifa alizonazo Mheshimiwa Malima, nachelea kutumia neno zimepotoshwa; nafikiri siyo sahihi sana. Kwa sababu hata mgawanyiko wa shares tu kadri anavyoutaja, siyo sahihi. Mimi hapa nalinda maazimio ya Kamati yangu ya TAMISEMI ambayo naiongoza, pia nalinda maazimio ya Bunge hili Tukufu kwamba tulileta mapendekezo ya maazimio ya Kamati yetu ndani ya Bunge hili mwezi Novemba, 2013, yakajadiliwa kwa kina, na Bunge hili likagonga muhuri kwamba haya ni maazimio sahihi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo mimi kama Mbunge, lakini pia kama Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI, naomba niyalinde maazimio hayo kwa sababu la sivyo yanachezewa chezewa tu. Tulichokisema sisi ni kwamba, badala ya Simon Group kununua hisa kwa bei ya kutupwa ya Sh. 145/=, sasa

Nakala ya Mtando (Online Document)

anunue kwa bei ya soko ambayo ilikuwa kati ya Sh. 1,600/= na Sh. 2,200/=. Tathmini hii ilifanywa kwa maelekezo ya CHC na Shirika la KPMG ambao ni wataalam. Hilo ilikuwa ni pendeleko la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendeleko la pili, tulisema kwamba Shirika la Simon Group linanyanyaswa kwa sababu ambazo hatuzielewi. Lakini sababu kubwa inayosemwa pale ni kwamba, liko katika mashirika ambayo yalikuwa specified kwa mujibu wa Sheria Na. 19 ya mwaka 2002. Tukasema, kama hivyo ndivyo; uzuri na Mwanasheria Mkuu alikuwepo, tukamwomba atupe ushauri; akasema kama hivyo ndivyo, hili Shirika haliangukii katika sheria ile kwa sababu lenyewe ni private company, linaongozwa na Articles of Association ambayo inaliongoza Shirika la UDA lenyewe.

Kwa hiyo, hata mauzo yaliyofanywa yalikuwa halali kwa kuwa halikuwa specified kwa mujibu wa sheria hiyo niliyoitaja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na sababu hizo nyingine zote, tukasema ili kuongeza efficiency, UDA iruhusiwe kufanya kazi, lakini pia Baraza la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam walikuwa wameshakaa na wameazimia kuza hisa zao, kwa hiyo, tukasema, kama Baraza limeshaamua, sisi Kamati ya Bunge hatuwezi kutengua maamuzi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Treasury Registrar naye alikuwa ameshakaa na ameshaandika waraka kwa maelekezo ya barua, nafikiri ndiyo hiyo anayoisema Mheshimiwa Kangi Lugola; naye alikuwa ameshakaa na ameshapeleka waraka kwa Makatibu Wakuu na wanapeleka kwenye Baraza la Mawaziri. Tukasema sasa sisi Kamati ya Bunge tutaliampela vipi suala hili wakati wao wenyewe wenyewe hisa zao wameshaamua kuza! Sisi tunazuia nini? Kwa hiyo, sisi kama Kamati ya Bunge pamoja na uchungu tuliokuwa nao, tukasema kwa kuwa Simon Group anakubali kulipa hisa kwa bei ya soko...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kigwangalla malizia kwa kifupi sana.

MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA: Kwa kuwa Simon Group anakubali kulipa hisa kwa bei ya soko, basi na aachiwe anunue hisa hizo ili aweze kufanya kazi yake kwa ufanisi. Sasa leo nashangaa, maelezo ya Serikali ile ile yanakengeuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni moja. Naomba leo hapa tupate kauli mahususi kwamba wanaheshimu maamuzi ya Bunge ambayo yaliletwa kama mapendeleko na Kamati yangu ama, la! Kama hayaheshimiki, mimi niko tayari hata kuachia hii nafasi ya Uenyekiti wa Kamati ili wao waweze kufurahi na kuendelea na mambo yao.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Shilingi.

MWENYEKITI: Haya tuanze na Mheshimiwa Machali, halafu Mheshimiwa Mangungu, Mheshimiwa Mbewe na Mheshimiwa Lukuvi. Haya Mheshimiwa Machali anza kwa kifupi sana.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naomba ku-declare *interest* kwamba nami pia ni Mjumbe wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ukijaribu kuangalia, maelezo ya Serikali yanajikanganya. Naomba tu pengine niseme kwamba kauli aliyoitoa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Adam Kigoma Malima siku ile, na tulimnukuu kwenye taarifa yangu kama Waziri Kivuli, ni tofauti na maelezo ambayo anatupatia hapa. (Makofii)

Ukijaribu kuangalia ukweli, inaonekana kabisa hii *Simon Group Company Ltd.* ni kama kuna kitu ambacho kimejificha kwa baadhi ya watu nyuma ya pazia. Ifike mahali hebu waangalie huyu bwana kama aliiuziwa hata hizo hisa pengine kwa bei ambayo inaonekana ni ndogo na ya kutupa, nani alaumiwe? Yeye au yule aliyeuza hisa ndiye alaumiwe na aulizwe? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it is likely* labda wewe una duka lako, unauza mashati; shati ambalo lilitakiwa liuzwe kwa Sh. 10,000/=, ukaamua kuniuzia kwa Sh. 5,000/=: Je, mimi niliyenunua shati la Sh. 10,000/= kwa Sh. 5,000/= kwako ndiye nilaumiwe au wewe ndiye ulaumiwe? Sasa kuna shida kidogo!

SAsa kama Jiji wameuza hisa zao zilizokuwa zimesalia, leo Naibu Waziri wa Fedha anasema kwamba zile hisa hazijauzwa, bado ziko Serikalini, hii *statement* inatokana na nini? Wao wameuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri *best practice* labda Naibu Waziri pamoja na Wizara ya Fedha au Serikali kwa ujumla wangeenda kuwaliza Jiji kwamba hizi hisa mmeziua namna gani? Lakini so far kwa sababu wameshamuuzia huyu *Simon Group*, sidhani kama watakuwa wanamtendea haki. Naona kama kutakuwa kuna kitu, sasa hebu wakiweke hapa ili kusudi iweze kujulikana kwani hili suala ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Machali, nakushukuru. Mheshimiwa Mangungu!

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunip fursa niweze kuchangia. Nilitaka nimkumbushe Mheshimiwa Kangi Lugola ambaye tulikuwa naye kwenye Kamati hiyo ya POAC, mimi ndiye nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo iliyoundwa na Kamati ile kwa ajili ya kushughulikia suala hili la UDA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, documents ambazo yuko nazo nakubaliana nazo kwamba ziko sahihi, lakini kwa kiasi fulani tuipe Serikali sasa iweze kuzifanya kazi ili kuweza kupata ufumbuzi wa hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika hili la UDA lilianzishwa kwa CAP 212 kwa maana kwamba, ni kama vile kampuni binafsi ambayo ilikuwa inamilikiwa kama ilivyosemwa asilimia 59 kwa 49. Uuzwaji wa hili Shirika mpaka sasa bado una utata, kwa sababu Hazina yenyewe ambayo ndio mmiliki na anayeshikiria share za Serikali, kwa muda wa zaidi ya miaka 15 hawakuteua Wajumbe wa Bodi kwenda kuwakilisha kwenye UDA. Hii inamaanisha kwamba kusita huku ilikuwa tayari wameweka mfumo ambao utasaidia wachache ambao watateuliwa upande wa UDA ndio washiriki kwenye zile unallotted shares.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni swali ambalo Serikali lazima mtupe majibu kwamba, nia yenu ni nini? Huyu mwekezaji kama aliuziwa kimakosa, mlipeni fidia atoke ili shirika hili lirudi kwenye umiliki wenu, muuuuzie mtu mwingine ambaye anakubalika. Kwa hiyo, ili kutuondoa katika majibu ya utata, ripoti ya CAG ipo ambayo inaonesha mfumo na mwenendo mzima wa uuzwaji na mpaka leo bado Hazina mnapiga mpira wa kuzungusha kwamba tunaenda wapi, tunaenda wapi; haiwezekani Shirika la Umma kama hili likawa kama mpira wa kona kwamba kila mtu anahangaika nao ili kuuingiza wavuni. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zaidi ya tano za Bunge hili, kila moja inatoa maelezo na maneno yake. Hivi Serikali mnataka kitokee kitu gani ili kuweza kufikia ufumbuzi wa suala hili? Kwa hakika na mwono uliopo, wanaotetea Simon Group wana maslahi yao na wanaotetea upande mwingine kwamba Simon Group haijanunua kihalali, wana maslahi yao. Tuondoe huu utata kwa maana kwamba uuzwaji na utaratibu wote ufutwe na uanze upya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbewe!

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo ambalo Serikali hii ya CCM inastahili kupata kupata aibu ni kwenye jambo hili. Maana yake kinachotokea hapa ni kwamba Serikali hii hii inajivua nguo, Serikali hii hii Wizara moja haielewi Wizara nyingine imefanya nini. Wanazungumza hawamtambui mwekezaji wa Simon Group, huyu mtu ameingiza magari 300

Nakala ya Mtando (Online Document)

Dar es Salaam, yanatembea kwenye barabara za Dar es Salaam, Serikali inasema haitamtambui! Mbona ni mambo ya aibu mnazungumza mahali hapa? Kamati mbalimbali zinagongana! Mambo haya ndio yanayokatisha tamaa wawekezaji katika nchi hii, kwasababu maamuzi hayafikiwi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati maamuzi yanalazimika kufikiwa hata kama siyo maamuzi ambayo ni popular. Haiwezekani watu wamewekeza fedha zao; kundi hili linauza, kundi hili linasema hatujauza, utata mtupu! Kamati mbalimbali za Bunge zinagongana katika kutoa matamko na kauli, Mawaziri wanagongana katika kauli, Wizara inadai haihusiki, ni Serikali moja hii hii! Ni Serikali moja siku hii hii! Halafu inataka sisi tuishauri; tuishauri nini? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishauri Serikali, tunahitaji usafiri Dar es Salaam. Ninyi kama Serikali, kaeni chini, tafuteni ufumbuzi wa kumaliza tatizo hili. Mna uwezo wa kumaliza tatizo hili, mkatuondolea aibu ya kuvuana nguo wenyewe kwa wenyewe hapa ndani! Kama Serikali yenu imefanya uzembe ikashindwa ku-privatize UDA ikawa na ufanisi mzuri, ni tatizo ya Serikali yenu. Sasa mnashindwa kuzungumza Serikalini huko, mmeshindwa kuyamaliza kwenye Baraza la Mawaziri, mnakuja kuanza kuvuana nguo hadharani hapa, mnataka sisi na wananchi wa kawaida tuzungumze nini katika jambo hili? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona Serikali ya CCM ikiwa *low* kuliko leo. Mnashindwa kutafuta ufumbuzi wa kumaliza tatizo, mnakuja hapa na kuanza kudanganyana kwamba oh, hawa waliamua hivi na wale waliamua hivi. Tunachohitaji, tunataka Dar es Salaam ipate usafiri mzuri, wananchi wa Dar es Salaam waweze kupata usafiri wa uhakika.

Sasa kama kama kuna makosa mlifanya nyuma, kakaeni chini mmalize matatizo haya kwasababu mnaweza kuyamaliza haya matatizo, na siyo kuja kulumbana Bungeni mambo ambayo hayana maana, mkamaliza hili suala ili watu waende mbele katika hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio ushauri ambao nilitaka kuutoa kwa Serikali kwasababu inavuana nguo bila sababu za msingi mahali hapa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mboge. Mheshimiwa Kangi Lugola, tutakuomba hiyo barua uliyoisoma uiweke Mezani hapa. Namwita Mheshimiwa Lukuvi halafu tutakuja kwako Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo siyo ya leo, ni la siku nyingi na wala hakuna nguo ya Serikali itakayochomoka kwa hili; hatujavuliana nguo hapa; na hakuna mtu anayepingana na mwenzake. (Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokuwa anakisema Mheshimiwa Adamu ni kwamba, mnakumbuka wakati fulani tulikuja hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa taarifa kwamba atamwagiza CAG akachunguze na ripoti ya CAG ipo na bila shaka taarifa mbalimbali mmezipata. Haya aliyokuwa anasema Mheshimiwa Adamu, yako katika ripoti ya CAG, ni ya Serikali na mnajua mpaka sasa jambo hili Serikali imewatupia TAKUKURU. Mnalifahamu hilo, Kwamba TAKUKURU bado wanahangaika na hili kwa kushirikiana na DPP. Kwa hiyo, Serikali bado tunalo, siyo kwamba limetuvua nguo au namna gani, lakini tunaendelea nalo.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema kwamba kama Serikali, tunaendelea nalo hili jambo kupitia TAKUKURU kwa namna ya kutafuta uhalali wa mauzo wa mauzo na utaratibu wa handing over na utaratibu wote uliofanywa ndani ya UDA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ndani ya Bunge hili wiki iliyopita, Mheshimiwa Mnyika hapa alitoa hoja, jambo hili tena limechukuliwa na sisi kwa upande mwingine. Mheshimiwa Spika alitoa *ruling* kwamba hoja hizi zinazozungumzwa, maana Mheshimiwa Mnyika aliuliza uhalali wa yule mmiliki kutangaza kule na kuwatuhumu baadhi ya Wabunge. Mheshimiwa Spika, *rule out* kwamba aje kwenye Kamati ya Maadili, aseme alipataje na hivi, athibitishe.

Kwa hiyo, Serikali tunaendelea nalo. Nilitaka kukukumbusha tu Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba Serikali tunaendelea nalo, lakini na wewe na Kiti chako unaendelea nalo kwa *ruling* uliofanya wiki iliyopita, kwamba umeagiza aje atoe maelezo kama alivyotoa maelezo kule nje, atoe maelezo ndani ya Kamati ile, athibitishe, lakini pia athibitishe na zile tuhuma alizozitoa kule nje.

Kwa hiyo, nafikiri ni wakati mzuri kwetu sisi Wabunge kupitia ile hoja ya Mheshimiwa Mnyika, kupitia Kamati yetu ya Maadili, tutaupata ukweli. Lakini wakati huo huo Serikali siyo kwamba tumeliacha hili jambo, tunaendelea nalo kupitia TAKUKURU.

MWENYEKITI: Kipekee kabisa, kwasababu Kamati ya Miundombinu pia iligusa jambo hili, kwa dakika chache sana Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla ni kuhusu umiliki. Hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla siyo hoja ya watu kutukanana, lakini naomba nitoe taarifa kuwa magari 300 yaliyoingia nchini, Serikali iliwapa exemption ambayo ndiyo Serikali hii leo inasema haimfahamu huyu mtu. (Kicheko/Makofi)

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala hili limekuja kwenye Kamati yetu miaka mitatu iliyopita, tukawaita watu wote tukajadiliana nao, wakasema tatizo kubwa lililoonekana pale, ni suala la bei kwamba ilikuwa ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nitoe taarifa kwamba hili suala limekwenda mpaka Mahakamani. Aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo kapelekwa Mahakamani kwamba alikula rushwa kwa uuzaji wa Shirika hili. Mahakama imemfanya yuko free, ameshinda kesi. Pia alichanganywa Simon Group kwenye hiyo kesi! Kesi haipo, imeondoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu, hili jambo tuangalie watu wa Dar es Salaam, tatizo letu ni usafiri Dar es Salaam, naomba tulitatu. Habari ya kwamba nani kamsema nani; nani kamuuzia nani; haitusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, huyo mwekezaji ni ngozi nyeusi mwenzetu. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, ni zamu yako Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu niwasilishe maoni yangu ambayo ningependa yaingie kwenye kumbukumbu za Hansard kwamba kwa kweli sijaridhika jinsi Kamati yako ilivyoruhusu suala hili kuingia kwenye majadiliano ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imenisikitisha kwa sababu, naona hata aibu kwamba mimi ni Mwalimu wa Mheshimiwa Lugola. Huwezi kuleta barua iliyokuwa imeandikwa wakati Wizara hii ilikuwa inaitwa Wizara ya Miundombinu na wakati *UDA* haijawa specified. It was that time a state company ambapo Serikali 100% shares zinakuwa owned na state. Ilipokuwa Specified, iliondoka as a legal entity chini ya usimamizi wa Wizara, ikaenda chini ya PSRC. Sijawahi kuona chombo ambacho kiko chini ya PSRC kikaongozwa na Wizara. Ndiyo maana mimi sijawahi wala Katibu wangu Mkuu wala Naibu Waziri, kuona *UDA* ikija juu ya meza yetu tufanye maamuzi. Sasa mimi nashangaa, inakujaje sasa kwenye bajeti yangu hapa hiyo *UDA*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini umeiruhusu? (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nitoe masikitiko yangu kumshangaa kabisa Dkt. Mwakyembe. Suala hili ni suala la uchukuzi! (Kicheko/Makofi)

WABUNGE FULANI: Ndiyoo!

Nakala ya Mtando (Online Document)

MWENYEKITI: Serikali ni moja! Uchukuzi, Dar es Salaam. Hata kama liko upande wa kushoto, hata kama liko upande wa kulia, lina athari katika masuala ya uchukuzi. Kwa hiyo, ni sawa tu.

Kilichokuwa kinanipa taabu ni namna gani inaweza ikahusishwa hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla na kutolewa kwa Shilingi kwenye mshahara wako wewe, kwa sababu yeye alikuwa amelielekeza zaidi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, lakini mada ya suala lenyewe ni uchukuzi.

Kwa hiyo, kwa mada nzima, hatuwezi kulikimbia, lakini alikuwa hajalielekeza kwenye Wizara yako na bahati nzuri aliyekuwa ameeliyekezewa yupo na ndiyo maana mnaona na sisi wengine ambao hatujashiriki katika mijadala hiyo, kwa kweli leo tumejifunza, kumbe kuna kitu ambacho kiko namna hiyo. Kamati yako yenyewe ya Miundombinu na Mwenyekiti wake amesimama hapa na kukiri kwamba hata wao kama Kamati, wameliona jambo hili na exemptions zimetoka, na wametueleza hapa kwamba kuna 49 sijui 59 shares, si ndiyo? Kwamba 51 ilikuwa ni private eh! 49 ndiyo Serikali. Unalipelekaje PSRC? (Makofii)

Kwa hiyo, haya mambo yana mkanganyiko maalumu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe haya ni yetu wote, tusiayakimbie. Ni yetu wote, tufike mahali tuyatatue tu. Tusilaumiane kwamba Mwenyekiti umefanya hivi na hivi. (Makofii)

Baada ya maelezo hayo, nikuombe Mheshimiwa Kigwangalla umalizie kwa kifupi sana, lakini uirudishe hiyo Shilingi kwasababu ya mkanganyiko tuliosema, tupate namna fulani ya kuwaomba Serikali ili jambo hili liondoke kwenye utaratibu. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kwamba kwanza Dkt. Mwakyembe hakuwa sahihi. Shirika la UDA halijawahi kuwa specified kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma, Sheria Na. 16 ya mwaka 1993. Halijawahi kuwa specified na halijawahi kuwa chini ya PSRC. Mgogoro huo ulipoibuka, walienda Mahakamani na UDA alishinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hili suala sisi tumefuatilia kwa muda mrefu sana, nikikuonyesha nondo nilizonazo hapa, ni makabrasha ya nyaraka, ni makubwa! Tumefuatilia kila kitu, judgments zote, kwasababu tulisaidiwa na CAG, tulisaidiwa na Mwanasheria Mkuu, tulisaidiwa na watu wa CHC, tuliwaita KPMG, wadau wote walikuwepo hapa. Kwa hiyo, taarifa ninazozitoa ni za uhakika na huu muda mchache tulionao hapa hauwezi kutosha kuwapa ufahamu wa kutosha Wajumbe wa Kamati yako hii ya Matumizi.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe kusema kwamba maelezo ya Serikali yaliyotolewa na Mheshimiwa Lukvi pia nadhani na yenyewe hayawezi kuwa mna msingi, kwasababu kesi ya rushwa tayari ilishafika Mahakamani, na Ndugu Idd Simba akiwa ameshitakiwa na Serikali kwa tuhuma za rushwa akashinda kesi. (Makofii)

Pia hao hao waliiondoa kwasababu alikuwa anaelekeaa kushinda, Serikali ikarudi, ikakaa vikao na mihtasari ya vikao vyote tunayo kama Kamati, tukaisoma ile mihtasari tukaona Serikali ilikubali kwamba ni bora wamuuzie huyu Bwana hili Shirika ili liwe lina tija na ufanisi. (minong'ono)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, malizia ili tuondoke hapo.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mtu akiibuka hapa akasema kuwa limeuzwa kinyemela, siyo sahihi kwasababu Serikali hao hao waliruhusu likauzwa *in the first place*. Kwa nini leo tena wakatae? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti ukisoma taarifa za uendeshaji wa Shirika hilo, wanaita Memorandum and Articles of Association, liloanzisha UDA mwaka 1974, wakati linaanzishwa, utaona kwamba ndugu yangu, mtani wangu Mheshimiwa Mangungu haja isoma MEMARTS ile na haelewi utaratibu wa kuuza hisa ulio ndani ya MEMARTS ukoje.

Saimon Group amefuata utaratibu huo, kapelekwa Mahakamani, kawashinda zaidi ya mara tatu. Sasa mtu wa namna hiyo unasemaje humtambui? Kila akienda Mahakamani anawashinda! Sisi tukasema, kwa kuwa ana mpango wa kuleta mabasi 300u na ameshayaleta na kwa kuwa ana mpango wa kuleta mabasi mengine 500, ili kuwanusuru wananchi wa Dar es Salaam na matatizo ya Uchukuzi, ni bora huyu Bwana apewe hili Shirika aliendeshe, aweke mabasi barabarani watu wapate huduma ya usafiri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tulisema, angalizo ni moja ambalo amelisema Mheshimiwa Serukamba kwamba UDA ilikuwa na tatizo. Wakati wanauzu share waliuza kwa bei ya kutupwa ya Sh. 145/=, Sisi tukasema, kama hili ndilo lilikuwa tatizo, ni kwa nini sasa asiuziwe hisa zilezile kwa bei ya soko?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malizia.

MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo tukasema sasa yale mapendekezo ya Shirika la Ushauri la KPMG ya kwamba hisa ziko katika value ya kati ya Sh. 1,600/= na Sh. 2,200/= yazingatiwe.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Ndiyo maana sisi kama Kamati yetu tukanawa mikono na kuachai UDA sasa ikauzwe.

Serikali hawa wanasema hapa leo hii kuwa nyaraka za kuuza zile hisa asilimia 23 zilizokuwa chini ya *Treasury Registrar* zipo kwenye Baraza la Mawaziri, muda siyo mrefu watajadili na watapitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niirudishe tu Shilingi ya Dkt. Mwakyembe kwasababu ni kaka yangu. Kwa heshima yake, nairudisha lakini Serikali wajipange, watoe statement hapa Bungeni ya kufuta maelekezo yaliyosemwa hapa na Mheshimiwa Malima kwamba *Simon Group* hatambuliki na wala hana hisa yoyote ili huyu mtu apate haki yake, afanye kazi yake kwa uhuru kama Mtanzania ye yote ambaye amemua kuwekerza katika Shirika lile.

MWENYEKITI: Nakushukuru Sana kwa kurudisha hiyo Shilingi. Nakushukuru sana. Mheshimiwa MKiwa Kimwanga, kwa upande wa CUF!

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kupata ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 44 wa hotuba yake, ameongelea kuandaa, yaani kutengeneza meli nne katika Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, lakini vilevile katika ukurasa huu wa 44 unaonyesha wazi kwamba katika Ziwa Victoria MV. Victoria imechoka na inahitaji matengenezo makubwa ambayo yalikuwa yafanyike mwaka wa fedha mwaka 2013/2014 na sasa anaisogeza mbele utafanyika mwaka 2015/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli hii huwa inatoka Mwanza ikielekea Kemondo mpaka Bukoba Mjini. Lakini katika Ziwa hilo Victoria pia kuna meli ya Serengeti ambayo imechoka. Sasa nataka kujua Mheshimiwa Waziri anaposema meli hii itafanyiwa ukarabati Julai, 2015; hivi tunahitaji kaburi lingine kwa watu wanaosafiri na meli hizi katika Ziwa Victoria hasa MV. Victoria? Ama tunahitaji tena kuja kujenga minara ya kumbukumbu kama huzuni na kuweza kumalizia pesa kwenye minara? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika asilimia 47 ya pesa aliyopewa, na ametuambia muda bado anaweza kuongezwa pesa nyingine; ningombaa Serikali mwongeze pesa kabla ya kumaliza mwaka huu wa fedha ili aweze kufanya marekebisho makubwa ya meli ya MV. Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri hatanipa majibu ya kuniridhisha mimi na wananchi wa Kanda ya Ziwa kwa Ujumla...

MWENYEKITI: Iweke vizuri. Hoja yako hasa ni nini unachotaka kijibewe?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivi, mwaka 2013/2014 aliahidi kufanya matengenezo makubwa ya MV. Victoria ambayo inahudumia Kanda ya Ziwa na sasa amesema kwamba meli hii itakarabatiwa 2015/2018 katika ukurasa wake huo huo wa 44. Sasa ninachohitaji, meli hii imechoka, tunahitaji makubwa na ya haraka ili kunusuru maisha ya wasafiri wa Ziwa Victoria.

MWENYEKITI: Ah, unataka matengenezo yawe hivi sasa eh?

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Yawe hivi sasa. Kama Mheshimiwa Waziri hatanipa majibu ya kuridhisha nitaondoa Shilingi katika matengenezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Kicheko)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika bajeti yetu ya mwaka uliopita tulikuwa tumedhamiria kufanya matengenezo katika meli ya MV. Victoria, lakini kwasababu za ufinyu wa bajeti, maeneo mengi ikiwamo pia Marine Services Company Limited hawakupa fedha yoyote kama walivyotarajia.

Kwa hiyo, fedha kidogo waliyopata ilitosha kufanya marekebisho ya msingi ya kuifanya MV. Victoria iendelee kutoa huduma bila ya kuhatarisha usalama wa wasafiri.

Sasa hivi suala ambalo limebaki la matengenezo makubwa katika hiyo meli ya MV. Victoria ni ile crane ya kubeba mizigo. Ile crane ndiyo imeharibika ndiyo maana sasa hivi MV. Victoria haiwezi kubeba magari kutoka Mwanza kwenda Bukoba au kutoka Bukoba kuja Mwanza. Lakini matengenezo ya injini pamoja na kuweka katika hali nzuri vyumba na maeneo ya kukaa abiria, haya yalifanyika na ninadhani wananchi wanaotumia meli hiyo, wanaweza kutoa ushahidi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkiwa, rudisha Shilingi.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayaniridhishi. Tarehe 21 Mei tumefunga miaka 18 kwa kuzama kwa meli ya MV. Bukoba. Tulianza kusema hivi hivi, kwasababu mimi nilikuwa ni mtumiaji wa meli hiyo, na siku ilipozama meli hiyo ilikuwa ni siku ya kutoka Uganda kuja Tanzania. Lakini siku hiyo kwa uhaba wa meli, ilikuwa inatoka Bukoba kuja Mwanza. Ilizama na tulikuwa tunasema mambo haya tukiwaeleza Viongozi na wakawa wakisema kwamba meli ile iko salama.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba Meli ya MV. Victoria haiko salama kama anavyoongea Mheshimiwa Naibu Waziri. Wasafiri wanaosafiri na Meli ya MV. Victoria wanasema, mimi mwenyewe nimeshasafiri. Kurekebisha viti vyatukalia ni suala moja, lakini je, hiyo meli Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mmeisafiria mkaiona hali ilivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunusuru maisha ya wananchi wa Kanda ya Ziwa na wafanyabiashara wengine wanaotoka maeneo tofauti, nawaomba Wabunge wenzangu waweze kuniunga mkono tuweze kujadili meli hii ya MV. Victoria kwa kuiomba Serikali iikague na kufanya matengenezo makubwa sasa, kwa sababu meli zote mbili zina matatizo. MV. Serengeti ina matatizo, lakini kubwa nimesimamia hapa ni MV. Victoria. Nawaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono tuweze kulijadili hili kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makof)

MWENYEKITI: Mimi sidhani jambo kama hili kwa kweli linahitaji hata malumbano sana. Yaani maana yangu ni kwamba, kama alivyotoa wito Mheshimiwa Mkiwa, iko tu haja ya Serikali kutazama suala zima la usalama wa meli hiyo, kwa sababu ni jambo ambalo halina ubishi. Kuna ambaye hataki itengenezwe? Haya tuendeleel! (Kicheko)

Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Rwamlaza. Kwa kifupi sana kwa sababu muda ni mdogo sana!

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ilipokuja kuzama MV. Bukoba wananchi wote wa Kanda ya Ziwa walijua kabla haijazama kwamba hii meli itazama. Walisema Serikali haikusikia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wote wa Kanda ya Ziwa leo wanajua kwamba hata pesa zilizopelekwa kufanya yale matengenezo ya kupaka paka zimeliwa. Ni maneno yaliyopo Mtaani; mitandao yote ya watu wa Kagera wana-communicate na kuzungumza hatari iliyomo. Wafanyakazi wa meli ile wanazungumza hatari ikayowapata kwa sababu ya matengenezo duni yaliyofanyika.

Katika maelezo yangu ya maandishi nimemweleza Mheshimiwa Waziri na mwende kwenye maandishi muangalie. Meli ile itazama, mtakimbilia wapi? Ndugu zangu wote walizama, hawajarudi. Hao wakizama itakuaje? Serikali ilikuwa ikijua kwamba meli ile itazama, kuna evidence na hakuna fidia iliyolipwa kwa watu waliozama.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hatuwezi kukubali kurudia hili. Hili suala ni muhimu, afadhali meli ifungiwe isifanye kazi. Tumechoka kuomboleza! (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakoso!

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mtoa hoja kwa sababu eneo la Ziwa Victoria ni sambamba na eneo la Ziwa Tanganyika ambako kuna meli ya MV. Liemba inayofanana na mazingira kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba, lazima Serikali ichukue commitment kubwa sana kuhakikisha maeneo yote ya majini ambako vyombo vina hali ya kuhtarisha usalama ichukuliwe hatua ipasavyo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso, nakushukuru sana kwa kuongea kwa kifupi. Mheshimiwa Rwamlaza!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda kuungana na mawazo ya Mheshimiwa Adam Mkiwa Kiwanga kwamba Serikali itueleze maana yake ahadi imekuwa ya muda mrefu. Sasa hivi ni miaka 18 tangu MV. Bukoba imezama ndani ya Ziwa Victoria. Sasa hivi kwa ushahidi mkubwa, mimi natumia sana ile meli ya MV. Victoria kusafiri kati ya Mwanza – Bukoba, lakini nimeshapewa warning na wafanyakazi kwamba wewe mwanamke, vipi na hii meli?

MBUNGE FULANI: Mbunge mzima...!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Kwa hiyo, Mbunge mzima! Nikasema bwana mimi napenda kusafiri kwa sababu sipotezi muda. Nikitoka Bukoba saa 2.00 usiku, nafika Mwanza nafanya shughuli halafu jioni narudi Bukoba. Kwa hiyo, sina nafasi ya kupoteza pale, ndiyo maana naipenda meli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli tupo katika riski kubwa, tunaomba Serikali itengeneze ile meli au iifungie. Maana yake mlituhaidi tangu enzi za Mheshimiwa Benjamin Mkapa mpaka leo, kwamba tutapata meli mpya. Hakuna meli mpya! Mnataka tuzame watu wa Bukoba tufe mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtupe meli au muifingie basi tujue kwamba hakuna meli katika Ziwa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy ni wa mwisho katika uchangiaji wa Wabunge.

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi mkono hoja kwa sababu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ameahidi kuikarabati meli zote, naamini zitakarabatiwa pamoja na Liemba.

Meli ya MV. Bukoba ni kweli ziliundwa pamoja pacha na MV. Muongozo. Zilikuwa na matatizo kwa sababu zilikuwa zinayumba na Mwongozo mpaka leo imesimama, ipo Kigoma, haifanyi kazi. Kwa hiyo, Victoria ni kuifanyia matengenezo ambayo tumeahidiwa ni meli nzuri na Liemba ikitengenezwa ni meli nzuri, itafnaya kazi zake kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. (Kicheko)

TAARIFA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, taarifa ya kuhusu nini? Wewe ni Waziri Kivuli, haya sema bwana!

MHE. MOSES J. MACHALI: Ndiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Unajua wakati Mheshimiwa Waziri ana-wind-up amezungumza kwamba meli ya MV. Liemba kidogo kama lugha haikuwa nzuri. Lakini taarifa ninazompa zimetoka kwenye source ambayo ni sahihi kwamba hata Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kigoma walitaka kuisimamisha hii meli ya MV. Liemba.

Leo anapozungumza hapa kwamba meli hii iko safi, sijui kuna ma-generator mangapi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, kinachozungumza hapa ni MV. Victoria.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu ku-link tatizo lile kwa sababu Mheshimiwa Kakoso pia amezungumzia meli ya MV. Liemba ina matatizo yanayofanana na meli ya MV. Victoria.

Niombe Serikali wa-take serious note juu ya matatizo haya. Tusingubiri mpaka majanga yatokee halafu ndiyo wanakuja kujifanya kwamba wanakuwa kwanza kwenda kuhani watu, wanapenda watu ambao pengine wana misiba. Haya mambo hayatusaidii. Wa-take serious note waache kutuambia mambo ambayo wakati wataalamu wanaozihudumia hizo meli wanahangaika kila siku wanalamika. (Kicheko/Makofii)

Nakala ya Mtando (Online Document)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Machali. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Waziri kwani muda umekwisha kwa upande wa Wabunge. Mheshimiwa Waziri, MV. Victoria!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasikia Waheshimiwa Wabunge wakitumia assessment tu ya kukaa kwenye meli wakaelezea technical problems za meli. Mimi nitakachofanya, nitawatuma tena wataalamu wangu wa SUMATRA ambao ndio wamebobea katika masuala hayo na ndiyo ambao wameisimamisha meli ya MV. Liemba waende na Lake Victoria wakakague.

Tulipopata tatizo la vyombo viwili vya meli, Skagit na Spice Islander Zanzibar hapo katikati wataalamu wetu wa meli walipitia meli zote kwa ukaguzi. Lakini wenzetu hapa Waheshimiwa wanasema wao ndio wanapanda, hivyo wanaelewa zaidi matatizo; tutawatuma tena wataalamu wetu wa SUMATRA. Kama kuna umuhimu wa kusimamisha, tutazisimamisha hizo meli.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge mnikubalie kwamba tuongeze nusu saa ili tusogee kidogo. Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kuna masuala mengine yanayoshangaza sana, kipindi Mheshimiwa Mwakyembe anafanya wind-up, alisema kwamba katika development vote, hawajaweka pesa hata kidogo ya kununua ndege kwa sababu nchi inadaiwa na Shirika linadaiwa, na ndege zikiletwa maana yake ni kwamba hizo ndege zitakamatwa.

Waliosababisha haya madeni makubwa, wapo kwenye nchi hii na wamesababisha haya madeni makubwa kwa ubadhirifu alivyosema Mheshimiwa Waziri, kwenye macho ya Serikali ya CCM inaangalia kwamba Shirika linakufa kwa sababu ya ubadhirifu. Sasa najiuliza, maana yake ni kwamba tunajenga viwanja vya ndege vingi sana, lakini hatuwezi tukanunua ndege hata moja kwa sababu tuna madeni na tukileta ndege zitakamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo serious. Nataka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, waliosababisha hasara hii na kusababisha haya madeni ni akina nani na wamechukuliwa hatua gani? Hili deni litalipwa lini ili ndege ziletwe tuwe na ndege? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata majibu ya kutosha, natoa Shilingi. Hili suala ni kubwa kwa Taifa, tunahitaji ndege ya Taifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

Nakala ya Mtando (Online Document)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipeleka hili suala kwenye vyombo vinavyohusika, TAKUKURU na Polisi. Uchunguzi umefanyika, baadhi ya watu waliohusika wako Mahakamani sasa hivi na Mheshimiwa Mbunge anajua. Sisi tulichokifanya ni kuiomba Serikali itofautishe kati ya *Criminal Act* au hiyo *liability* iliyotuletea madeni na ATC operations zake. Ndiyo maana tumetengeneza andiko, linaenda Cabinet sasa ili Serikali iweze ku-take over hayo madeni, tupate a clean balance sheet ya ATCL, na ATCL ianze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la watu kuchukuliwa hatua, hao watu wako Mahakamani, nisingependa kuliongelea kwa sababu lipo Mahakamani. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wenje!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti nzima aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri, hakuna *item* hata moja inayoonyesha kwamba haya madeni yanaenda kulipwa na yanalipwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hakuna *item* hata moja, haionyeshi seriousness na commitment ya Serikali ili haya madeni yalipwe ili tuwe na ndege. Ni aibu kwamba leo hakuna hata ndege ya Serikali inayotoka Dar es Salaam kwenda Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa Shilingi, naomba Wabunge wenzangu tujadili hii hoja, ni hoja muhimu ili tujue specifically haya madeni yanaenda kulipwa lini ili tuwe na national carrier? Ni aibu nchi kubwa kama hii hatuna ndege! Shirika linayumba! *There is nothing kwenye hili Shirika!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa Shilingi tujadili hili suala nipate commitment ya Serikali, ndege hizi wanaenda kulipa madeni lini ili tuwe na ndege?

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona hukunipa nafasi ya kufunga hoja yangu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkiwa, wanapeleka walaalamu ambao wao wata-assess sasa kuona kama kuna umuhimu wa kuzifungia hizo meli au kama ni matengenezo ni kiasi gani na kadhalika.

Mimi nafikiri tumefika pazuri. Kwa sababu tuking'ang'ania kama sisi Wabunge kwamba meli ile ni mbovu kama sisi ni wataalamu, ile commitment waliyoitoa Serikali nafikiri imetufikisha pazuri.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Lakini ulipaswa uniuilize na mimi ndiyo naona mjadala unavyokwenda. Kwa sababu ukitoka tu kwangu ukarukia tu kule hujaniambia chochote ili nini?

MWENYEKITI: Niliona kwa busara zote za Kiti, hapa tulipofika ni pazuri. Ahsante Mheshimiwa Mkiwa. Tunaendelea.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Hapana, na utaratibu pia ni muhimu!

MWENYEKITI: Angalizo la Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ili mjadala huu uwe na manufaa, Waheshimiwa Wabunge watofautishe kati ya Serikali kuchukua madeni na Serikali kulipa madeni. Nitashukuru sana.

MWENYEKITI: Siyo ungefafanua tofauti yake, maana tupo wengi hapa. Siyo lazima wote tuwe tumekuelewa. (*Minong'ono*)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimetoa angalizo kwamba... (*Minong'ono*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewaruhusu waongee kwanza hao!

MWENYEKITI: Nimekuruhusu wewe Mheshimiwa Waziri. Hebu kaeni kidogo halafu nitachukua majina yenu. (*Kicheko*)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tumeanza mchakato kuiomba Serikali iyabebe haya madeni ya ATC na iangalie namna ya kuyalipa. Kwa hiyo, hayawezi ku-appear kwenye bajeti ya Wizara kwa sababu ni suala la kuchukua yale madeni kwanza ili ku-clean up balance sheet ya ATCL. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokuwa anasema Mheshimiwa Mbunge ni vizuri tu kwamba yeye alitaka aone namna tunavyolipa kwenye bajeti yetu hapa hayo madeni. Hapana, siyo hilo. Sisi tunataka Serikali i-take over hayo madeni na tumejenga hoja na hiyo hoja inaenda cabinet, ndiyo hicho tu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wenje, umeelewa mazungumzo hayo ili kama kuna wachangiaji uendelee!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Mwakyembe. Ninachojaribu kusema, kwa sababu anasema kuna mchakato. Sasa nchi hii michakato ni mingi mno.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Tunachohitaji ni commitment ya Serikali sasa kwamba huo mchakato wenu wa ku-take over hayo madeni yanaenda kukoma lini ili muweze kununua ndege? That is what I want! Time frame! Tupe commitment!

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ametoa Shilingi tangu mwanzo. Tuanze na Mheshimiwa Mbowe halafu atafuata Mheshimiwa Lema.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba ni-declare interest kwamba katika watu wanaoidai Air Tanzania mojawapo ya Kampuni yangu inaidai Air Tanzania hela nyingi karibu Dola 200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwa na *national carrier* mbali ya suala la uchumi ni suala ya prestige kwa nchi. Mheshimiwa Rais ameshawahi kutoa ahadi mara nyingi sana kwamba hataruhusu Air Tanzania ife na Serikali wakati wote imekuwa inatoa kauli kwamba haitaruhusu Air Tanzania ife. Lakini matendo ya Serikali na muda inaotumia kutengeneza azma hii hayaendani na ahadi ambayo wameitoa.

Kwa hiyo, ambacho naungana mkono na Mheshimiwa Wenje ni kwamba whether ni kuchukua madeni ama kuendesha Shirika; Shirika la Air Tanzania linamiliwi na Serikali kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, Serikali haiwezi kujivua madeni ya Air Tanzania, haiwezi ikajivua uzembe wa Menejimenti ya Air Tanzania, haiwezi ikajivua wajibu wake kulifufua Shirika la Air Tanzania kama kweli tunahitaji kuwa na *national carrier*. Kama tunaona utalii ni jambo la msingi, basi hivyo hivyo na *national carrier* ni jambo la msingi, na ni prestige kwa nchi.

Sasa tunachokiomba sisi, Serikali itoe commitment. Haya madeni yanavyozidi kuchukua muda mrefu, ndiyo sasa tunaanza kuingia hofu ya watu kukamata ndege, magari na sio heshima! Msifikiri ni Air Tanzania inapata aibu, ni nchi! (Makofij)

Serikali itoe commitment! Waziri wa Fedha ametoa commitment hapa kuhusu mambo mengine ambayo Wabunge wameyasimamia hapa. Kwa hiyo, siyo suala la kumbana Waziri peke yake, hata Serikali nzima iko hapa, itoe commitment, italipa lini haya madeni ili Air Tanzania iweze kufufuliwa? Ndio hilo tu!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hawa ndugu zangu wanawaonea sana. Serikali ambayo imeshindwa kununua madawati shulen, wanapowapa wajibu wa kuendesha Airline, kimsingi wanawaonea sana. Nami niwatake radhi kwa ajili ya jambo hilo. (Kicheko/Makofij)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa unayoiona hapa ni kuwa na Viongozi ambao ni *negative thinkers*. Kwamba Taifa la tatu kwa dhahabu, lenye madini ya Tanzanite, mbuga za wanyama nyingi, gesi, makaa ya mawe, *uranium*, ardhi, hamna ndege! Ndio sababu nasema wanawaonea! Mmeshindwa madawati, mmeshindwa vitanda hospitalini, eti wanataka mnunue ndege!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kwenye hotuba yangu ya Wizara ya Mambo ya Ndani niliomba Watanzania wafanye maombi hii Serikali itoke madarakani, na huo ndiyo msingi mkuu Watanzania lazima wafanye. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, unapanua wigo? Hapa kuna jambo specific sana.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ime-run kwa muda mrefu sana kwa Shirika la ndege ambalo linaongozwa na watu binafsi. Ukiangalia pesa ambayo inatakiwa kulipwa deni ni *commitment* ya kikao cha Serikali *positive* cha masaa matano kama mko *serious*. Hamwezi kuniambia kwamba Baraza la Mawaziri likae mbele ya Rais kwenye nchi ya utajiri kama hii kwamba mnaweza mkakosa hizo fedha za kulipa madeni na nchi hii ikaanza ku-run *airline*. Hamko *serious*!

Hamko *serious* kwa sababu moja. Mlitegemea sana vyeti na majina Maprofesa kutafuta Mawaziri badala ya kuangalia *commitment* na *attitude* katika *thinking positively*. Ndiyo maana leo nchi hii mambo mengi hayaendi. Leo mnasema kwamba pesa hiyo ikishalipwa ndiyo tutanunua ndege. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo deni linaweza likabaki *pending* na ndege zikaletwa. Haya ni mambo yakukaa mezani na kujadili deal. Ni nani anaweza kukataa kuikopesha nchi?

TAARIFA

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Taarifa Mwenyekiti!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Wee mama kaa chini!

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mie mama yako? Mch! (Kicheko)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema naomba uzime chombo chake. Mheshimiwa Faida samahani sikuwa nimekuona. taarifa fupi! (Kicheko)

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukupa taarifa na kumpa taarifa huyo anayeongea, huyo Lema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unawapa watu muda mrefu sana kikanuni haueleweki; mtu ana hotuba! Wakati wa kutoa hatuba alikuwa wapi? Sasa hivi tunaenda kifungu kwa kifungu kwanini Lema anachukua muda mrefu mpaka anatoa mahotuba makubwa makubwa inahusu nini? Hiyo ndiyo taarifa! (Makofi/Kicheko)

Muda wote wanapoteza wao tu! (Makofi)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo nimepewa mimi Mheshimiwa Lema haukupewa wewe. Kwa hiyo, muda wako unatosha. Mheshimiwa Kakoso!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitampigia simu, nitamweleza nje habari niliyokuwa naongea. Nilikuwa nasema,...

MWENYEKITI: Nimeshavuka kwako, ahsante Mheshimiwa Lema, kwa heshima zote.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema umeshaeleweka, ahsante. Mheshimiwa Aliko Kibona samahani Mheshimiwa Kakoso.

MHE. ALIKO KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani kwamba...

MWENYEKITI: Naomba tujaribu kufuata ushauri tuliopewa na Mheshimiwa Faida kuongea kifupi. Waheshimiwa!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashawishi Wabunge wenzangu, nilidhani kwamba siyo sahihi kwamba Waziri wa Uchukuzi atoe tamko ndani ya Bunge hili sasa hivi kwamba madeni ya ATCL yangeonyeshwa kwenye kitabu hiki, kwa sababu madeni ya ATCL yapo kwenye vitabu vyatua ATCL na wajibu wa kupeleka maombi ili madeni yale yachukuliwe na Serikali ni ATCL yenye.

Mimi nilidhani kwamba, kila Mjumbe anayechangia kwanza awe ameja kwanza utaratibu wa madeni hayo ni namna gani yanachukuliwa na Serikali.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mimi nadhani pia kwamba siyo busara kila tutakapoona kwenye Shirika kuna tatizo la madeni, tuanze kumshinikiza Waziri anayehusika kwamba Serikali ichukue yale madeni. Mwisho wa siku tutakosa madawa mahospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wajumbe wamesema tuna gesi, tuna nini; hayo nayo yana utaratibu wake. Ile gesi kuigeuza ikawa pesa ni process ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuunga hoja ya Mjumbe kwamba madeni haya yachukuliwe au Mheshimiwa Waziri atoe tamko sasa hivi katika hili. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kufufua Shirika hili. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Shirika hili kwa kweli lilikuwa mahututi kwamba hata leo bado wanaweza wakaruka wakaenda Kigoma, wakaenda Mbeya, wakaenda Bujumbura, wakaenda Comoro, ni jambo ambalo nasema nawapongeza kwa juhudhi hiyo kubwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri hiyo ambayo Shirika limeanza kufanya na Wizara kuisimamia, haiondoi responsibility yetu kama Serikali kutatua tatizo la Shirika letu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ATC linaanzia zamani sana. Mnakumbuka historia yake ambayo ni ndefu sana, hapa ndani tunaifahamu. Kama nchi, umefika wakati tuamue. Mbia wa Shirika hili kwa maana ya shareholder ni Serikali.

Kwa hiyo, tuwaombe watu wa ATC waende wamwandikie Mwanahisa wao, waiambie hali halisi, Mheshimiwa Waziri amesema wanaandika waraka wa Baraza la Mawaziri. Naiomba Serikali kwamba waraka huo uende haraka, maamuzi yafanyike haraka ili Shirika hili liweze kurudi barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, Serikali mnafanya juhudhi kubwa sana kujenga viwanja vya ndege. Unaweza kuona tunajenga viwanja vingi sana vya ndege. Kama tutakuwa hatuna ndege, hivi viwanja tunavyovijenga vitakuwa white elephant.

Kwa hiyo, ninachoomba Serikali ilione hili pamoja na juhudhi inayofanyika, maamuzi ya haraka yanahitajika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Shirika letu la Ndege la Tanzania ni asset na asset yake kubwa ni routes. Kwa hiyo, kwenye biashara hii, biashara

Nakala ya Mtandao (Online Document)

namba moja ni routes kwa sababu routes tunazo nyingi sana, umefika wakati tuzifanyie kazi.

Mheshimwia Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba tukishamaliza kusafisha hiyo mizania, watu wa kuwekeza wapo wengi, lakini umuhimu wa kuwa na National Carrier ni muhimu sana. Naomba Serikali ifanyie juhudhi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba waraka niliokuwa nauongelea ulishaandaliliwa, umepita ngazi mbalimbali za Serikali, ni suala tu la kuupeleka kwenye Baraza la Mawaziri.

Hilo andiko lina maeneo mawili. Kwanza kuiomba Serikali i-take over, ichukue madeni ya ATCL, lakini upande wa pili unapendekeza fedha. Tumefanya utafiti, ni fedha kiasi gani zitahitajika ku-recapitalize ATCL kuweza kuifufua ATCL? Ndiyo andiko hiko. Nami nina mategemeo ndani ya pengine wiki chache au mwezi mmoja Baraza linaweza likakaa kusikiliza hilo andiko letu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wenje!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nimwambie rafiki yangu Mheshimiwa Kibona kwamba Wazungu wanasema: “*is better to be quiet to be thought a fool than to speak and clear the doubt.*” (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba gharama za usafiri wa anga nchi hii iko very expensive kwa sababu competition iko very low kwa maana kwamba ndege hazitoshi. Majibu ya Waziri sasa hivi ni kweli inaonesha kwamba kuna agency ya kufanya hili suala.

Mheshimiwa Waziri narudisha Shilingi lakini naamini kwamba kwa commitment hiyo uliyoitoa kwamba kwa muda mfupi ujao Baraza la Mawaziri litakaa na waraka umeshaandika, tafadhali jitahidi sana ili tuwe na National Carrier ambayo ina nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudisha Shilingi.

MWENYEKITI: Namkushukuru sana Mheshimiwa Wenye kwa gesture hiyo. Mheshimiwa Kibona hukutaka hata kusimama kidogo, lakini nakushukuru. Nakushukuru sana Mheshimiwa Wenje. (Kicheko)

Twende kule kusini kabisa jamani Waheshimiwa!

Nakala ya Mtando (Online Document)

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mwakyembe kwa kazi zake nzuri. Usipate taabu, usiwasilizile sana hawa. Hawa hata Ofisi yao hawana, wanakaa tu kwenye kishimo tu cha ndege pale Kinondoni. Wasikupe shida. Sisi tumefanya mambo mengi sana katika nchi hii! Tumejenga vitu vingi! Hawa hata Ofisi hawana, watakuwa watu gani hawa? Wewe chapa kazi tu bwana! (Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komba rudi kwenye mada tafadhali.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye mada. Pana shida gani? Mna Ofisi nyie? (Minong'ono)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni hivi, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 46 unakanganya na ukurasa wa 61 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 46 inasema, TPA wanaangalia uwezekano wa kujenga meli moja katika Ziwa Nyasa kwa ajili ya kuimarisha uchukuzi wa mizigo. Ukifika ukurasa wa 61 kuna statement inayosema TPA itaanza mradi wake wa kwanza mwaka wa fedha 2014/2015 katika Ziwa Nyasa ambako usafiri wa majini ni wa mashaka. Huku inasema, inaangalia uwezekano, huku inasema itaanza mradi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lipi nishike kama Mbunge wa huko nikiwakilisha mpaka kwako Kyela kule mpaka kwa Mheshimiwa Filikunjombé kule Ludewa, wananchi wa kando kando ya Ziwa na wanaokaa Ziwa Nyasa? Nataka tu maelekezo. (Kicheko)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kapteni Komba. Mheshimiwa Waziri, ufanuzi tafadhali.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Kapteni Komba kwa kupigania sana kuhusu suala la uchukuzi ndani ya Ziwa Nyasa. Wapo Waheshimiwa wawili wengine; Mheshimiwa Cynthia Ngoye na Mheshimiwa Filikunjombé ndiyo wameshikilia sana hilo bango na kwa kweli nawashukuru, mmetufanya sisi Wizara tufikirie hilo suala kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 46 timesema MSL, yaani Shirika letu la Meli kwenye Maziwa kwa kushirikiana na TPA, kwa pamoja wamekuwa na mchakato wa mazingumzo. Lakini TPA walishaamua kabisa kwamba mchakato ukilegalega, wao tayari wameshaji-commit kwa pesa yao ndiyo maana tunasema sasa ukurasa wa 60 ni wao peke yao TPA siyo kwa kushirikiana tena na MSL. Wakichelewa MSL, TPA tayari wameweuka fungu kwa sababu wamefanyakazi nzuri, wamepata pesa ya kutosha na siyo tu kwa upande wa

Nakala ya Mtando (Online Document)

meli na siyo ziwa Nyasa tu, wakimaliza wataingia Tanganyika na Lake Victoria, lakini siyo hivyo tu; wamenunua vichwa vyatreni vitatu na mabehewa kwa ajili ya mizigo kwenda Mwanza na mizigo kwenda Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chiligati!

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina nia ya kuondoa mshahara wa Waziri, ningekuwa na uwezo kwa kweli ningemwongezea kwa sababu anafanya kazi nzuri. Ila nimesimama kuomba ufanuzi kuhusu reli ya Dodoma, Manyoni, Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu cha Waziri cha hotuba reli karibu zote zimetajwa zitashughulikiwa na zile ambazo hazipo lakini zipo katika mpango zimetajwa. Hii ambayo ipo tayari ya Dodoma, Manyoni, Singida nimerudia kusoma mara mbili labda kama nimesoma vibaya atanielekeza baadaye, haimo kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Singida, hatuna usafiri wa maji kwa sababu hatuna ziwa wala bahari, hatuna usafiri wa anga kwa sababu kiwanja chetu bado kipo kwenye upembuzi yakinifu, usafiri wa treni umesimama, sasa huu mwaka wa nne; tumebaki na barabara tu.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika mwaka unaokuja, hii reli ambayo ndiyo tegemeo letu sisi kubeba mizigo yetu na abiria, kwanini Wizara haikutaja kabisa? Ni mwaka wa nne haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ilipotengezwa reli ile miaka ya 1980 kwa kweli ilikuwa isiishie tu Singida, ilikuwa iende mpaka maeneo ya Kateshi kule kwenye mashamba ya ngano ili ibebe mzigo mkubwa zaidi. Badala ya kwenda mbele mpaka Katesh ambako ndiko ilitegemewa, ni mwaka wa nne sasa haifanyi kazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Capt. John Chiligati. Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Tizeba, ufanuzi!

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika vitabu hivi reli ya Singida haionekani kwanza kwa sababu kipande hicho cha Manyoni - Singida kiliacha kutumika siyo kwa ubovu wa reli. Ni pale tu Shirika lenyewe lilipokwenda chini na baada ya wale wabia walioingia na kampuni ya TRL, wao waliamua kuacha safari katika baadhi ya maeneo ambako mwanzo

Nakala ya Mtando (Online Document)

huduma zilikuwa zinatolewa na TRC. Hivyo wakaacha kwenda Singida, Moshi na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwepo Singida; naomba nitumie tena nafasi hii ya Bunge kuagiza TRL watekeleze nilizoliagiza jana Singida. Wakafanye ukaguzi wa hicho kipande cha Manyoni - Singida kujiridhisha tu na hali ya reli kwa sasa baada ya kutotumika kwa kipindi hiki cha miaka minne. Kwa sababu tunatarajia kupatikana kwa vichwa vya treni sasa ambavyo limekuwa tatizo, mara hivyo vichwa vitakapopatikana na mabehewa yale 22 ya abiria yatakapokuwa yamepatikana, tunatarajia kwamba tutaanza safari za kuelekea Singida.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia nilzungumzia suala la PPP na Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Nagu na Mheshimiwa Waziri walieleza kwamba PPP ipo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Mipango tuliwaita kwenye Kamati ya Bajeti tukawaomba watusaidie orodha ya miradi yote ambayo itakwenda kwenye PPP, majibu waliyotupa ni kwamba wana tatizo la *proper feasibility study* ya miradi na kwa maana hiyo wanashindwa kutangaza kusema mradi huu na huu umekamilika ili kujua *stake* ya Serikali itakuwa ipi na *stake* ya private sector itakuwa ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha Mheshimiwa Waziri hapa, miradi yote iliyopo katika page ya 15 mpaka 20 hakuna hata mradi mmoja wa PPP. Kitabu cha *planning* hiki hapa chote hakuna mradi wa PPP; na Wizara zote zinakuja hapa zinalalamika kwamba hazikupata fedha kwa sababu bado Serikali ndiyo ina-finance miradi yote. Mheshimiwa Waziri anasema kila kitu kipo sawasawa, sheria ipo na kadhalika.

Tumeomba kwenye Kamati, tunataka orodha ya miradi ya PPP mpaka leo haijaletw. Serikali ituambie, miradi ya PPP ipo wapi? Imetangazwa lini, ina thamani gani? Waliotaka kuwekeza ni nani na nani? Kwa sababu hata Sheria ya *Investment* inatoa muda wa siku 60 tu mtu apate majibu. Hakuna mtu anayepata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya Serikali kabla sijachukua hatua nyingine.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: PPP, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mary Nagu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge akiwepo Mheshimiwa Hamad Rashid kufuatilia miradi ya PPP.

Kwa mujibu wa Sheria ya 2010 ya PPP Wizara ndizo zinazopaswa kufanya feasibility study na hatimaye wanaleta kwenye Kitengo cha Uratibu ambacho kipo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na Kitengo cha uratibu ambacho kipo Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuja kufuatilia na nilieleza kwenye maelezo yangu ya awali na ndiyo maana nilisimama hapa, kwamba utekelezaji wa ile sheria umekutana kwanza na urasimu kwamba kuna vitengo viwili na pili, ni kwamba Wizara ambazo zinapaswa kufanya feasibility study zingepaswa kuwa na hela za kufanya feasibility study. Tukagundua kutokuwa na Mfuko wa PPP ni moja ya changamoto ambazo kwenye marekebisho ya sheria ambayo tunaleta, miradi ipo, lakini haikukamilika.

Miradi ambayo ipo naweza nikamwonyesha Mbunge baadaye lakini kwa kweli feasibility study haitoshelezi; na kwa sababu miradi ya PPP ni lazima ionyeshe jukumu la wabia ni lipi na mafao au manufaa yatakayopatikana na ule ubia ni ipi ili baadaye tusiingie kwenye mgogoro na mradi uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ipo isipokuwa feasibility study haijafanywa vizuri tukagundua changamoto hii na ndiyo maana sasa tunaleta sheria na wakati huo huo tunaendelea vile vile na feasibility study ili zitosheleze.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kujazia majibu hayo!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana kutoka kwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Mary Nagu, nilikuwa naomba niongezee kwa kusema, kwa upande wa Wizara ya Uchukuzi tuna miradi mingi kweli ya PPP. Study zote zimekamilika!

Kwa mfano nichukulie central line ambapo tunajenga standard gauge railway kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka; na kutoka Isaka mpaka Kigali; na kutoka Isaka mpaka Msongati. Huu ni mradi wa nchi tatu na Wakuu wetu wa Nchi walishaweka sharti la kwamba uwekezaji wa PPP tumeshamaliza studies zote. Mwezi wa Pili mwaka huu, 2014 ndiyo tumepata a detailed study ambayo imefanywa na CANARAIL.

Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wizara ya Uchukuzi tumeiuza Central Corridor kwa nguvu sana. Kati ya miradi 51 Barani Afrika iliyokuwa inaangaliwa na World Economic Forum kama ni suitable for PPP Investment Participation ya Private sector na Public, mradi wetu ume-emerge the best, ndiyo maana tumekuja na kitu kinaitwa a wider concept note ambayo nimeigawa kwa kila Mbunge hapa. Hiyo yote ni ku-attract private sector tuweze kuwekeza kwenye hiyo reli ambayo itatugharimu kiasi cha Dola bilioni 7.6 yote kwa pamoja, pamoja na network ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili miradi yetu mingi, zaidi ya asilimia 80 ya bandari ni miradi ya PPP na studies zimefanyika, zimekamilika. Kinachoendelea sasa hivi ni wale ambao tuliwapa expressions of interest wameturudishia majibu, tunaona mazuri; tunataka sasa watuletee proposal, zimekuja zipo chini ya evaluation tumwone ni nani ambaye anafaa kwenda na sisi. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikubali tu kwa sababu ya kukubali tu. Kwa sababu hamjafanya kitu chochote cha maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha maana kilichosemwa na Bunge hili, kumbukeni maagizo ya Spika. Tulilisema ndani ya Bunge, Spika akasema mlete orodha ya miradi yote ya PPP, hamjatekeleza hilo agizo. Tumeagiza kwenye Kamati mlete, hamjaleta! Tumewaita watu wa planning, wamesema bado study hazijafanywa.

Sasa kama Serikali hamna kauli moja, mtaiyumbisha nchi. Ndiyo maana leo tumekuja hapa katika bajeti ya Planning, Wizara zote ni 50 percent only. Kama kweli miradi ya PPP ingekuwepo, bajeti ingekuwepo hapa ni ya kusaidia Polisi, Majeshi na kadhalika; mambo ya utawala tu. Haya mengine ya miradi yanefanywa na private sector.

Nimeonyesha mfano wa nchi ambazo zinafanya hivyo. 80 percent of the project zinakwenda kwenye PPP. Leo bado tunalalamikia sungura mdogo kwa sababu bado private sector, study zimekaa kwenye shelves, hazijulikani wala hatujui chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kutoa Shilingi naomba uagize watuletee kwenye Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uchumi na Fedha miradi yote ambayo inatakiwa kwenye PPP ili tujue ni kitu gani kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Natumaini kila mtu amesikia. Muda sasa hauturuhusu, tunaingia kwenye utaratibu wa guillotine. Katibu.

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 62 - WIZARA YA UCHUKUZI

Kif. 1001 - Administration and HR Mgnt.....Tshs. 3,379,433,400/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts..... Tshs. 635,571,000/=
Kif. 1003 - Policy and Planning.....Tshs. 1,264,464,400/=
Kif. 1004 - Government Comm. UnitTshs. 322,716,000/=
Kif. 1005 - Procurement Mgnt Unit.....Tshs. 350,089,600/=
Kif. 1006 - Internal Audit Unit.....Tshs. 339,422,000/=
Kif. 1007 - Legal Services Unit.....Tshs. 337,769,000/=
Kif. 1008 - Inform. & Comm. Techn. Unit.....Tshs. 315,128,000/=
Kif. 2005 - Trans. Infrastructure Div.....Tshs. 472,878,000/=
Kif. 2006 - Transport Services Div.....TShs. 85,192,042,300/=
Kif. 5002 - Trans. Safety & Envirnt Div.....TShs. 696,877,300/=

(Vifungu vilivyo tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 62 - WIZARA YA UCHUKUZI

Kif. 1003 - Policy and Planning.....Tshs. 24,690,000,000/=
Kif. 2005 - Trans. Infrastructure Div.....Tshs. 261,720,399,000/=
Kif. 2006 - Transport Service Div.....TShs.148,217,000,000/=

(Vifungu vilivyo tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae, Waziri taarifa!

TAARIFA

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kupitia Makadirio na

Nakala ya Mtando (Online Document)

Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi - Fungu 62, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 mafungu kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa
Mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa ushirikiano mliotoa kwa meza na kwetu sote katika wakati huu wa kujadili makadirio na matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Kwa niaba yenu nampongeza sana Waziri wa Uchukuzi - Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, Mheshimiwa Naibu Waziri - Dkt. Tizeba, Katibu Mkuu - Dkt. Shabaan Mwinjaka na Watumishi wengine wote wa Wizara hii.

Tunajua kabisa kwamba fedha tulizowapatia kwa kweli ni ndogo ukilinganisha na kiasi halisi mnachohitaji kufanya maisha yetu Watanzania kuwa rahisi, lakini tunaamini kabisa kwamba kiasi hicho mllichopata kitawasaidia na kutusaidia sote kuboresha hali ili iwe bora zaidi mwakani.

Waheshimiwa Wabunge, wengi mlikuwa mmeomba kuchangia Wizara hii, siyo wote mlipata nafasi, naomba mtuwie radhi meza, lakini wengi vilevile militaka muwe na maswali kwenye mshahara wa Waziri, vilevile haikuwezekana. Waliopata nafasi wametuwalisha, naomba tukubaliane na hali hiyo kutokana na muda wetu kwamba ni mdogo.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho kabisa, karibu tuko nusu sasa ya safari yetu ya kushughulikia bajeti ya Serikali nzima. Ukiangalia toka tulipotoka mpaka sasa yapo mambo mengi sana ambayo kama yatapita kwenye Baraza la Mawaziri yatasaidia sana mambo kwenda.

Kwa hiyo, Baraza la Mawaziri wenzetu kwa kweli ipo kazi ya kufanya. Iko backlog kubwa ya mambo mengi. Ukichukua Wizara moja moja ukayajumlisha yale ukayaorodhesha, ni mengi sana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hivyo, tunawaomba wenzetu waangalie hili jambo huko mbele ya safari ili haya yote ambayo yanahitaji baraka ya Baraza la Mawaziri yaweze kupata Baraka hizo tuweze kusogea kama nchi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, kwa kuwa shughuli zilizoandaliwa leo kwenye Order Paper zimekamilika, naomba sasa kwa nafasi hii nahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.25 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 27 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*